Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

**HUDUMA YA KUWAIMARISHA VIONGOZI WA KANISA AFRIKA MASHARIKI**

# UWAKILI WA KIBIBLIA

**na**

**Jonathan M. Menn**

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974**
**J.D., Cornell Law School, 1977**
**M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders-East Africa**
**3701 N. Gillett St., Appleton, WI 54914**
**(920) 731-5523**
**jonathanmenn@yahoo.com**
**www.eclea.net**

Septemba 2008; imepitiwa upya Julai 2014

Mafafanuzi na matumizi ya Neno la Mungu kuhusu uwakili wa kibibilia, katika maeneo yote kuanzia maana, uumbaji, na asili ya uwakili wa kibibilia, majukumu na wajibu wetu kama mawakili katika maeneo makuu ya maisha yetu. Uangalizi maalum umetolewa katika uwakili wa mazingira, nia zetu, muda, miili, mahusiano, fedha na mali, na kanisa: utume na kusudi la msingi la kanisa; kanisa na fedha, na wajibu wa kanisa kwa maskini na wenye uhitaji.

# YALIYOMO

**WITO WETU KAMA MAWAKIL** ……………………………………………………………......4

**I. Maana ya "Mawakili"**……………………………………………………………........4
**A.** ***Mawakili Katika Agano la Kale***……………………………………………………………4
**B.** ***Mawakili Katika Agano Jipya***…………………………………………………………...4

**II. Uumbaji na Tabia ya Uwakili wa Mwanadamu**……………………………………...4
**A.** ***Tangu Mungu alipomuumba mwanadamu kwa mara ya kwanza, alimfanya awe ndiye wakili wa uumbaji wote***……………………………………………………………......4
**B.** ***Wajibu wetu wa kwanza kama mawakili wa Mungu ni kuwa na mahusiano yaliyo sahihi na Mungu mwenyewe***……………………………………………...............5
**C.** ***Yesu anaelezea uwakili wetu kwa mifano mitatu***……………………………….....6

**UWAKILI WA MAZINGIRA**……………………………………………………………..8

**I. Ulimwengu na Vyote Vilivyomo Ndani Yake ni Mali ya Mungu**...…………………..8
**A.** ***Mungu ndiye muumba wa dunia na vyote vilivyomo***…………………………….8
**B.** ***Mungu humiliki dunia na vyote vilivomo ndani yake***…………………………..8

**II. Ulimwengu na Vyote Vilivyomo Ndani Yake Humdhihirisha Mungu na Utukufu Wake**………....8
**A.** ***Kila kitu ambacho Mungu alikiumba kina umuhimu wa ndani na uthamani, kwa sababu Mungu alikiumba***……………………………………………………………..8
**B.** ***Kila kitu humfunua Mungu***……………………………………………………...8

**III. Matokeo ya Uumbaji na Uwakili wa Mwanadamu Juu ya Uumbaji Huo**…….............................9
**A.** ***Sisi tunatakiwa kumwabudu Mungu peke yake; hatupaswi kuabudu nyota, dunia, mimea, wanyama, au kitu chochote kilichoumbwa***……………………………….9
**B.** ***Mungu alimpa mwanadamu mamlaka juu ya dunia yote "kumiliki" na "kuilima" na "kuitunza" dunia nzima na viumbe vyote vilivyomo ndani yake (Mwa 1:28; 2:15***……….........9
**C.** ***Hatutakiwi kudhulumu, kuangamiza, au kuharibu uasili ulioumbwa, bali tunapaswa kuuhudumia vizuri***…………………………………………………….....10
**D.** ***Tunapaswa kutenda kwa makini na kwa busara katika kuonyesha umiliki wetu wa maumbile***…….11
**E.** ***Tunapaswa kuleta uponyaji wa kweli wa maumbile au uasili***……………….....12
**F.** ***Tunapaswa kujibidisha kuongeza uzuri wa uumbaji***……………………………..13

**UWAKILI WA BINAFSI NA KWA WENGINE**…….................................………......13

**I. Utangulizi**…………………………………………………………………….........13
**A.** ***Maisha ya Ukristo ni safari, na siyo tukio***……………………………………....13
**B.** ***Wakristo wote ni mawakili wa miili yao na nafsi zao***………………………….13

**II. Uwakili wa Nia**……………………………………………....................................14
**A.** ***Kila moja, katika kila desturi, anao mtazamo wa dunia unaomfanya aishi maisha anayoyaishi***……………………………………………………………………...14
**B.** ***Biblia Takatifu ni Ufumaalum wa Mungu kwa wanadamu***……………………….....14
**C.** ***Mtazamo wa mtu wa dunia unahitaji kuchukua umbo na uongozi wa Maandiko***…………………...14
**D.** ***Tabia maalum za nia iliyofanywa upya***………………………………………...15
**E.** ***Kwa vile mtazamo wetu mpya wa dunia umesimamia Biblia, ni lazima tuitafsiri vizuri***……………...17

**III. Uwakili wa Muda au Wakati**……..............................................................................19
**A.** ***Wakati ni Uhai***…………………………………………………………………..19
**B.** ***Wapi na vipi tutaishi milele, hutegemeana na jinsi tunavyoishi na maisha yetu ya sasa***…………......20
**C.** ***Kanuni za msingi za kusimamia muda***………………………………………....20
**D.** ***Kukabidhi madaraka na majukum***……………………………………………..23

**E.** ***Mambo mengine ya kuzingatia kuhusu uwakili wa muda au wakati*……………………………...24**

**IV. <u>Uwakili wa Mwili</u>……………………………………...…………..…................................26**
**A.** ***Miili yetu ni ya muhimu na ni zawadi ya ajabu kutoka kwa Mungu*………………………….……26**
**B.** ***Miili yetu ni ya kipekee kwa vile tuliumbwa kwa mfano wa Mungu, na miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu*……………………………………………………………………………...27**
**C.** ***Kuna uhusiano wa dhahiri kati ya hali yetu ya kimwili na hali yetu ya kiakili, kihisia, na kiroho*……………………………………………………………………………………......27**
**D.** ***Tunawajibika kwa Mungu kwa uwakili wetu wa miili aliyotupatia*……………………………..28**

**V. <u>Uwakili wa Mahusiano</u>……………………………………………………………………...30**
**A.** ***Mahusiano ya nipe nikupe dhidi ya mahusiano ya neema*………………………………………...30**
**B.** ***Tumeitiwa kuonyesha upendo katika maeneo yote ya mahusiano*…………………………......31**
**C.** ***Jinsi tunavyowatendea watu huonyesha kikamilifu jinsi tunavyomfikiria Mungu*...…….................32**
**D.** ***Tuyafanyayo katika maisha haya—hasa jinsi tunavyowafanyia watu wengine—kutakuwa ndicho kipimo tutakachohukumiwa nacho katika hukumu ya mwisho*………………………......33**
**E.** ***Orodha ya vipaumbele vya msingi katika maeneo muhimu ya maisha*……………………….…34**
**F.** ***Njia ya kimatendo ya kudhihirisha upendo: lugha tano za upendo*  ……………...……………..36**

**<u>UWAKILI WA FEDHA NA MALI</u>………………………………... …………………...............38**

**I. <u>Mtazamo wa Ki-Biblia wa Fedha na Mali</u>……………………………...……………..38**
**A.** ***Mungu ndiye Mkuu juu ya vyote, zikiwako fedha na mali*……………………………………....38**
**B.** ***Chochote tulicho nacho si "mali yetu" hasa—yote tumekabidhiwa tu na Mungu; sisi tu mawakili wake (m.y, waangalizi wa mali zake) na tutatakiwa tutoe hesabu ya uwakili wetu*………………………………………………………………………………………..38**
**C.** ***Mungu anaweza kutubariki kwa fedha na mali, lakini jinsi atakavyotubariki ni ikiwa tutafanya kazi vizuri, tukimweka Yeye na maswala yake nafasi ya kwanza maishani mwetu*……………39**
**D.** ***Kitu muhimu kuliko vyote kwetu ni kuwa na mtazamo na vipaumbele sahihi kwa Mungu, fedha, na mali*……………………………………………………………………………..39**
**E.** ***Uwakili mzuri wa fedha na mali unahusika na yafuatayo*……………………………………...40**
**F.** ***Kwenye kitovu kabisa cha uwakili wetu wa fedha na mali, ni utoaji*……………………………………40**
**G.** ***Mungu hubariki na hutoa thawabu kwa matumizi na uaminifu wa fedha na mali*……………………40**
**H.** ***Kwa sababu ni uwakili utokao kwa Mungu, matumizi yetu ya fedha na mali kusema kweli ni swala la kiroho la umuhimu mkubwa rohoni*……………………………………………………40**
**I.** ***Uwakili wa kiMdoo unaohusu fedha na mali*…………………………………………………..41**

**II. <u>Kutoa</u>…………………………………………………………………...….............................43**
**A.** ***Mungu ni mtoaji*………………………………………………………………………………43**
**B.** ***Utoaji chini ya Agano la Kale: sheria ya zaka*……………………………………………………..44**
**C.** ***Utoaji katika Agano Jipya: kwa hiari, kwa ukarimu, na utoaji wa mlingano kukidhi haja halisi*…..51**
**D.** ***Utoaji kulingana na Yesu*…………………………………………………………………………55**
**E.** ***Kutoa kulingana na Mitume*…………………………………………………………………...59**

**III. <u>Upotofu wa Injili ya Mafanikio</u>...……………………………………………...................64**
**A.** ***"Injili ya Mafanikio" ni nini*……………………………………………………………………...64**
**B.** ***"Injili ya mafanikio" ina mtazamo wa makosa wa Mungu, mpango wa Mungu , na Injili*…………65**
**C.** ***"Injili ya mafanikio" ina mtazamo wa makosa kuhusu imani na maombi*……………………….…..69**
**D.** ***"Injili ya mafanikio" inamtazamo wa kimakosa wa fedha na mafanikio*…………………….......72**
**E.** ***"Injili ya mafanikio" inamtazamo wenye makosa kuhusu utoaji*……………………………..........75**
**F.** ***"Injili ya mafanikio" ina ufinyu wa uelewa*………………………………………………….........75**
**G.** ***"Injili ya mafanikio" ina tafsiri mbaya za vifungu vya Biblia ambavyo inasimamia*……………..78**
**H.** ***Hoja za nyongeza kuhusiana na injili ya mafanikio*…………………………………………………83**

**<u>HITIMISHO</u>—Mahubiri ya Mafanikio: Ya Udanganyifu na Yenye Kuua.......................................84**

**UWAKILI WA KANISA …………………………………………………………………………….86**

**I. Utume na Kusudi la Kanisa…………………………………………………………………………86**
**A.** ***Kanisa lipo kwa ajili ya neema ya Mungu na utukufu wa Mungu…………………………………...86***
**B.** ***Neema ya Mungu imedhihirishwa kwetu, naye anatukuzwa nasi, kupitia imani yetu kwake……….86***
**C.** ***KUABUDU—utume na kusudi la kanisa linapatikana katika kumwabudu Mungu………………...86***
**D.** ***KUIMARIKA (MALEZI)—utume na makusudi ya kanisa yanapatikana katika kuwakamilisha watakatifu kwa kazi ya huduma……………………………………………………………………88***
**E.** ***HUDUMA (KUWAFIKIA WENGINE)—utume na kusudi la kanisa unapatikana katika kuwahudumia wengine, na kuwafikia wale ambao wako nje ya kanisa………………………..89***
**F.** ***UMOJA (MSHIKAMANO)—utume na kusudi la kanisa unaonekana katika umoja na mshikamano………………………………………………………………………………………...91***

**II. Kanisa na Fedha…………………………………………………………………………………94**
**A.** ***Kanisa linatakiwa kuonyesha uwajibikaji wake wa fedha………………………………………...94***
**B.** ***Kanisa linatakiwa kuelekeza fedha na rasilimali zake kufuatana na bajeti iliyoandikwa…………..96***
**C.** ***Kanisa linatakiwa kumlipa Mchungaji wao………………………………………………………….98***
**D.** ***Usimamizi wa fedha moja kwa moja unahusiana na utume wa kiroho na kufanikiwa vizuri kwa kanisa…………………………………………………………………………………………..99***

**III. Wajibu wa`Kanisa kwa Masikini na Wahitaji………………………………………………101**
**A.** ***Kila mahali katika Biblia, kuwahudumia masikini na wahitaji kumesisitizwa……………………101***
**B.** ***Kifungu kikuu kinachoshughulikia kanisa kuwahudumia masikini na wahitaji ni 1 Tim 5:3-16……………………………………………………………………………………..101***
**C.** ***Paulo anajadili kanuni kadhaa za kuamnua yupi kanisa limsaidie……………………………...101***
**D.** ***Mambo mengine ya kutafakari kuhusu 1 Tim 5:3-16 na kuwasaidia masikini na wahitaji……….102***
**E.** ***Matokeo yanayoweza kuja wakati kanisa linatimiza wajibu wake kuwahudumia masikini na wahitaji……………………………………………………………………………………………104***

**NUKUU ZILIZOTOLEWA……………………………………………………………………104**

**KUHUSU MWANDISHI………………………………………………………………………107**

# WITO WETU KAMA MAWAKILI

## I. Maana ya "Mawakili"

**A.** ***Mawakili Katika Agano la Kale***

1. Usemi wa Kiebrania ambao ulielezea vizuri zaidi Wakili ni *Ha ish asher al bayit*, "ni mtu [au, yeye] asimamiaye nyumba [au, kaya]" (ona **Mwa 3:16, 19; 44:1, 4**, ambayo yote huzungumzia usimamizi wa Yusufu kwa nyumba ile].
2. Ingawaje maneno mengine yametumika, maana hiyo hiyo imenenwa kwa Eliezeri, msimamizi wa nyumba ya Ibrahimu (ona **Mwa 15:2**).
3. Wakili hapa ni mtu asimamiaye nyumba ya mtu mwingine. Yeye huteuliwa na kuaminiwa kwa mamlaka na kuwajibika kwa bwana wake kwa uangalizi wa mambo yote ya nyumba hiyo. Msimamizi huyo aliwajibika kwa familia ya bwana wake na kwa mali zake. Hilo linaonekana wazi kabisa kwa Eliezeri, ambaye hata alipewa jukumu la kumpatia mke Isaka.

**B.** ***Mawakili Katika Agano Jipya***

Lile wazo kwamba Wakili ni mtu aliyepewa mamlaka juu ya nyumba ya bwana na kwamba anawajibika kwa bwana wake kwa usimamizi wa maswala yake unapatikana pia katika Agano Jipya.

1. Maneno mawili ya Kiyunani yaliyotumika katika Agano Jipya kuonyesha nafasi ya wakili ni:
   a. *Epitropos*—Mwangalizi mkuu, kiongozi, wakili, mlinzi (ona **Math 20:8; Luka 8:3; Wagal 4:2**); na
   b. *Oikonomos*—Mwangalizi wa nyumba au shamba, wakili, mwangalizi (ona **Luka 12:42; 16:1, 3, 8; Wagal 4:2**). Katika **Rum 16:23** neno hilo hapa linamwakilisha mweka hazina wa mji.
2. Maneno yote mawili yametajwa katika **Wagal 4:2**, ambapo yametafsiriwa "walinzi na wasimamizi walindao" (NASB), au "walinzi na wale wadhamini" (NIV), au "wakufunzi na watawala" (KJV), ambayo yanaonyesha kwamba kimsingi ni maneno yanayoshabihiana.
3. Katika Agano Jipya *oikonomos* pia limepewa maana ya mtu moja aliyeaminiwa kwa maswala ya kiroho.
   a. *Wakristo wote wanaitwa "Mawakili"katika Agano Jipya.* **1 Wakor 4:1-2** panasema: "*[1] Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu. [2] Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu."*
   **1 Pet 4:10** vivyo hivyo panasema : "*kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbali mbali za Mungu."*
   b. *Viongozi wa kanisa ndio hasa huitwa "Mawakili": "Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno kwa kuwa ni wakili wa Mungu."* (**Tito 1:7**).

## II. Uumbaji na Tabia ya Uwakili wa Mwanadamu

**A.** ***Tangu Mungu alipomuumba mwanadamu kwa mara ya kwanza, alimfanya awe ndiye wakili wa uumbaji wote.***

1. **Mwa 1:26-28** panaonyesha mwanzo wa uwakili wa mwanadamu juu ya uumbaji wote. *[26] Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya ya nchi. [27] Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. [28] Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendancho juu ya nchi.*
   a. Agizo la Mungu kwa Adamu na Hawa siku zote huitwa "Wajibu wa Mamlaka ya Kumiliki" (kwa sababu mwanadamu anaambiwa kutawala au kuusimamia uumbaji wote), au "Mamlaka ya Umilikaji wa Uasili" (kwa sababu mwanadamu ameambiwa kuitawala na kuitiisha dunia yote).
   b. Uwakili juu ya uasili wote ambao Mungu alimpa mwanadamu ulitolewa sawa sawa kwa mwanamume na mwanamke (**Mwa 1:28**).
   c. *"Kuitiisha dunia" na ukweli kwamba jukumu la kiwakili lilitolewa kwa wote wawili, mwanamume na mwanamke, kunatoa kigezo cha kimahusiano kwa uwakili wetu.* Kwa maneno mengine, sisi siyo tu ni mawakili juu ya "vitu" vya dunia, lakini pia mawakili juu ya watu

tunaohusiana nao na mahusiano yetu juu ya watu hao.

d. *Katika **Mwa 1:28** neno la Kiebrania "Kutiisha" ni kahvash.* Linamaanisha kutumia nguvu ambazo zimedhibitiwa, na zilizofikiriwa.

2. **Mwa 2:15-17** panaonyesha masharti na maelekezo ya ziada ya uwakili wetu. [15] *BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza.* [16] *BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula,* [17] *walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.*

a. *Katika **Mwa 2:15** Mungu anamwambia Adamu "uilime" na "uitunze" bustani* (ona pia **Mwa 2:5**; **3:23**).

(1) "Kuilima" (*abad*) maana yake "kufanya kazi," "kulima," "kutumikia." Kuna pande mbili za "kuilima," kama ilivyotolewa katika agizo la uasili au mamlaka:

(A) Kulima au kufanya kazi ni kuletesha kitu kilicho kizuri na cha thamani.

(B) Neno la Kiebrania kwa ajili ya "kulima" au "fanya kazi" (abad) pia linamaanisha "tumikia" na pia "fanya kazi."

(C) Kwa hiyo, uwakili wetu juu ya uumbaji unahusu kufanya kazi kiubunifu kwa uzuri, tukiwa na mtazamo kwamba tu watumishi wa Muumba wetu katika kuwatumikia wengine.

(2) "Kuitunza" (*shamar*) maana yake "kutunza" "kusimamia," "kukiangalia," "kuhifadhi," "kulinda," "kufanya kitu kwa uangalifu," "kuchunga." Hiyo inamaanisha tunao wajibu wa kutunza na kulinda kile ambacho kiko katika mamlaka na uwakili wetu.

b. Utendaji mzuri wa umiliki wa mwanadamu kwa uumbaji unaonekana katika **Mwa 2:19-20.** Mfano ulio dhahiri wa mwanadamu kuhusu umiliki wake juu ya uumbaji unapatikana **Mwa 2:19-20,** ambapo Mungu alimpa Adamu jukumu la kuwapa wanyama majina yao. Kukipa jina kitu ni ishara ya kuonyesha madaraka. Kunahusisha kuvitambua vitu, kuvipanga katika makundi, na kuviainisha. Mambo hayo yote yanategema kuchunguza, kuelewa, na kufikiria. Hii inaonyesha Adamu alitumia madaraka yake kwa umakini mzuri.

3. Katika **Mwa 2:15-17** Mungu anausimamia udhibiti wa umiliki na mamlaka juu ya uumbaji.

a. Mungu alimpa mamlaka mwanadamu na wajibu wake, lakini Mungu anaweka sheria na mipaka ya mamlaka ya mwanadamu, kwani Mungu ndiye mmiliki wa vitu vyote.

b. Mungu anamtazamia mwanadamu kwa jinsi anavyopaswa kuutekeleza uwakili wake (ona **Mwa 3:14-19**).

c. Hata baada ya anguko la mwanadamu katika dhambi, ingawa Mungu aliwafukuza Adamu na Hawa kutoka bustanini, hakuuondoa uwakili aliowapa juu ya dunia na viumbe vyake (**Mwa 3:14-24; Zab 8:4-8**).

d. Kama mawakili wa Mungu, tutawajibishwa mbele za Mungu tutawajibishwa mbele za Mungu kwa kile tukifanyiacho kuhusiana na uwakili wetu (ona **Math 25:14-46; Luka 12:35-48; 16:1-13; Waeb 9:27-28; 2 Pet 3:7; Ufu 20:11-15**).

**B.** ***Wajibu wetu wa kwanza kama mawakili wa Mungu ni kuwa na mahusiano yaliyo sahihi na Mungu mwenyewe.***

Ikiwa tunatakiwa tuwe mawakili waaminifu, ni lazima tuwe katika uhusiano ulio sahihi na Bwana wetu badala ya kuwa katika uasi naye. Njia pekee ya hilo kuwezekana ni kupitia Yesu Kristo. Kitovu cha kuimarisha mahusiano sahihi na Mungu kupitia Kristo ni kama ifuatavyo:

1. Mungu ni mkamilifu. Ndani yake hakuna dhambi kabisa. Ameweka sheria kamilifu kwa mwanadamu. Mungu ni upendo **(1 Yoh 4:8).** Hapendi mtu awaye yote apotee **(2 Pet 3:9).** Mungu pia ni Mtakatifu **(Isa 6:3; Hab 1:13)** na wa haki, na kwa hiyo ni lazima aihukumu dhambi **(Rum 6:23).**

2. Wanadamu hutenda dhambi katika mawazo, hisia, maneno na Mdo, kwa kutimiza na kutokutimiza wajibu. Watu wote wana uwezo wa kutenda dhambi ndani yao. Wanadamu hutenda dhambi kwa asili yao na kwa kuamua. Huchagua kwa makusudi kumkataa Mungu na njia zake. Wamepotea katika dhambi, wako katika kufa na wanaikabili hukumu, na hivyo wanaweza ama kuamua kujisafisha, au kujiokoa (**Rum 1:18-32; 3:10-18, 23; 6:23a; 14:23; Yak 2:10; 4:17**).

3. Yesu Kristo ni Mungu - Mtu kamili. Alikufa msalabani na kufufuka kutoka kwa wafu kulipia gharama ya dhambi zetu na kutupatia nafasi mbinguni, alijiitoa kama kipawa cha bure (**Isa 9:6; 53:6; Yoh 1:1-14; 1 Wakor 15: 3-4; 2 Wakor 5:21; 1 Pet 2:24**)

4. Ni kwa neema yake pekee, Mungu anatoa wokovu kama kipawa cha bure; si kitu ambacho watu waasi, na wadhambi wanaweza kukipata au kustahili **(Isa 9:6; 53:3-11; Yoh 1:14; 1 Wakor 15:3-4; 2 Wakor 5:17-21; Waef 1:3-14; 1 Pet 2:24**). Wokovu anaoutoa Mungu kwa neema yake unachanganya uzima wa milele, kuhesabiwa haki kwetu (kuhesabiwa haki mbele za Mungu), uzima mpya, utakaso (tabia njema mbele za Mungu), kipawa cha Roho Mtakatifu, anayekuja ndani yetu kutuongoza katika njia ya uzima mpya, na kuitukuza miili yetu mipya ambayo tutaishi ndani yake katika nchi mpya na dunia mpya (**Yoh 10:10; 14:1-20; Rum 6:3-6; 8:9-17, 26-39; 1 Wakor 15:35-57; Waef 2:8-9**).
5. Tunaipokea neema ya Mungu kwa kutubia maisha yetu yasiyofaa ya utu wa kale, na kumpokea Yesu Kristo kama Bwana wetu kwa imani. Imani ni kumtumaini Yesu Kristo peke yake kwa ajili ya uzima wa milele (**Yoh 1:12; 3:16; Mdo 16:29-31; 17:30-31; Rum 10:8-13; 2 Wakor 7:10; Waef 2: 8-9**). Imani yetu inadhihirika tunapokuwa kama Kristo tunapoishi kwa ajili yake na kutii kile anachotuambia, kupitia Neno linavyotuagiza kufanya (**Yoh 14:21-24; Waef 2:10**).

**C. *Yesu anaelezea uwakili wetu kwa mifano mitatu.***

1. Mfano wa mtumishi mwaminifu na asiye mwaminifu (**Math 24:45-51; Luka 12:42-48**).

a. *Katika mfano huu Yesu anatumia kazi ya kawaida tu* (kugawa chakula—**Math 24:45; Luka 12:42**), thawabu kwa ajili ya uaminifu (kusimamia mali ya bwana wao—**Math 24:47; Luka 12:44**), na maovu (Mdo mabaya na ulevi—**Math 24:49; Luka 12:45**) kwa mawakili wa karne ya kwanza.
b. *Zile thawabu na adhabu kwa watumishi waamnifu na wasio waaminifu* (**Math 24:50-51; Luka 12:46-48**) zinawakilisha matukio ya Siku ya Hukumu ya Mwisho wa ulimwengu, kwa vile Yesu alinenea "Kulia na kusaga meno" kwenye mfano huo katika **Math 24:51.** Ni lugha ambayo mahali pengine hutumika rasmi kwa ajili ya adhabu ya jehanamu (ona **Math 25:30; Luka 13:28**).
c. *Maana kamili ya mfano huo ni:* "(1) Mungu atawapa thawabu na kuwaadhibu watu katika hukumu ya mwisho kwa misingi ya uwakili wao, yaani kazi walizopewa. (2) Uwakili wa uaminifu unahitaji uvumilivu na saburi, kwani ule mwisho unaweza kuja wakati wowote. (3) Wale wanaoyaacha majukumu yao na kutenda uovu wakati huo watakuja kujikuta kwamba wamechelewa mno kufanya marekebisho kwa makosa yao." (Blomberg 1990: 193)

2. Mfano wa wakili asiye haki (**Luka 16:1-13**).

a. *Yesu aliutoa mfano huu katika kuwafundisha wanafunzi wake.* Hakuwa anasema kwamba wale wasiodhamiria, watumie fedha kuupata wokovu. Pia haagizi kwamba watu waseme uongo au wafanye uzembe. Badala yake, ingawaje mtu hawezi kutumikia pande zote; yaani Mungu na mali (**Luka 16:13**), Wale ambao tayari ni wafuasi wake lazima waonyeshe matunda ya kujitoa kwao katika maeneo ya mali za kidunia, kwani hicho ndicho kipimo kizuri cha uanafunzi.
b. *Hoja muhimu za mifano hii ni:* (1) Watu wote wa Mungu wataitwa kutoa ripoti ya utumishi wao kwake. (2) Maandalizi ya taarifa hizo yanapaswa yahusishe matumizi sahihi ya rasilimali zetu zote, hasa katika maswala ya kifedha. (3) Kama mwenye mali, Mungu anayo haki-hata katika maisha haya—kuondoa kwenye uwakili wetu manufaa au majukumu ,ikiwa hatuyatekelezi kikamilifu. Kwa hiyo, tunahitaji kutumia rasilimali zetu za kidunia kuujenga ufalme wa Mungui. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunajizatiti wenyewe kwa siku zetu za mbeleni.
c. *MacDonald anaongezea yafuatayo kuhusiana na mistari ya **8-9**:* "Kiko kitu kimoja tu cha kilicho kizuri kwa upande wa wakili asiye na haki, nacho ni, kule kujiandaa mambo kwa ajili ya siku za mbeleni. Alichukua hatua kuhakikisha kwamba bado atakuwa na marafiki baada ya uwakili wake kwisha. Alihudumu kwa ajili yao katika siku za "baadaye" badala ya "sasa" .

Kwa maana hii, wakili asiye haki alikuwa na busara zaidi kuliko Wakristo. Hata hivyo, ili kuelewa sababu, ni lazima tuelewe kwamba siku za mbeleni za Mkristo haziko katika dunia hii, bali ni mbinguni. Hii ni hoja muhimu. Siku za mbeleni za asiyeamini humaanisha kati ya sasa na kaburini. Hatima ya mwana wa Mungu humaanisha uzima wa milele na Kristo. Mfano huu basi unafundisha kwamba wana wa ulimwengu huu wana busara na bidii zaidi katika kujiandaa kwa ajili ya maisha yao ya mbeleni hapa duniani kuliko Wakristo wanavyojiandaa kwa ajili ya nafasi zao mbinguni.

Kitu muhimu kwa asiye haki ni fedha au kitu kingine chochote cha jinsi ya mali. Tunaweza kuvitumia vitu hivi kuvunia roho kwa ajili ya Kristo. Watu waliovunwa kwa kupitia matumizi mazuri ya fedha hapa huitwa "marafiki." Siku inakuja ambapo tutafikia mwisho, (ama

kufa au kuchukuliwa mbinguni na Kristo wakati wa kunyakuliwa kanisa). Marafiki waliovunwa kupitia matumizi ya uaminifu wa mali zetu ndio watatumika kama kamati ya kutupokea katika makao yetu ya milele.

Hii ndiyo njia ambayo mawakili wenye hekima hupangilia kwa ajili ya siku zao za mbeleni—si kwa kutumia maisha yao madogo kwa kujihangaikia tu kidunia; bali kwa juhudi yenye shauku ili wazungukwe mbinguni na marafiki waliopatikana katika Kristo kupitia fedha zao." (MacDonald 1975: 25-26)

3. Mfano wa Talanta (**Math 25:14-30**).

a. *Kwa siku za zamani, Talanta ilikuwa ndiyo kipimo kikubwa zaidi cha uzito katika Agano la Kale kilichoendana na mtu kuweza kubeba (kinakadiriwa kuwa kati ya kg 26-56 au [60-125 lbs.]).* Kikawa kipimo cha kupimia kikiwa sawa na shekeli 3000 (Katika Agano la Kale) na angalau Dinari 6000 hivi (katika Agano Jipya). Dinari moja ilikuwa ndiyo wastani wa mshahara wa mtu kwa siku moja (hivyo, talanta moja = inakaribia kuwa mshahara wa mtu wa miaka 20 hivi). Matumizi ya "talanta" kuonyesha "uwezo wa mtu" unajitokeza sana kinamna katika mfano huu.

*b. Hoja muhimu za mfano huu ni kama zifuatavyo:* "(1) Kama vile Bwana Mungu, alivyogawanya kwa watu wote sehemu ya rasilimali zake, akiwategemea watende kama mawakili wema wa hizo. (2) Kama wale watumishi wawili, watu wa Mungu watapongezwa na kupewa thawabu watakapokuwa wametekeleza kiuaminifu utume huo. (3) Na kama vile yule mtumishi mwovu, wale ambao watashindwa kutumia vipawa ambavyo Mungu amewapa kwa utumishi wake wataadhibiwa kwa kutengwa na Mungu na mambo yote yaliyo mema." (Blomberg 1990: 214)

c. *Maswala ya nyongeza na matumizi kuhusu mifano hii:*

(1) Katika mifano hiyo, yule bwana aliwakabidhi watumishi wake viwango tofauti vya talanta zake *"kulingana na uwezo wa kila moja"* (**Math 25:15**). Mungu hakutupatia kitu chochote ambacho hatuna uwezo wa kukifanyia kazi, wala si mali yetu wenyewe (**Math 25:20, 22**), au kupitia wengine (k.m, Benki—**Math 25:27**). Kwa hiyo, Mungu hututegemea kabisa sisi kutumia kwa uaminifu vile tulivyokabidhiwa.

(2) Kama vile wale watumishi katika mifano ile walivyokuwa mawakili juu ya kila kitu ambacho bwana alikuwa amekiweka juu yao, vivyo hivyo sisi nasi tu mawakili juu ya kila kitu ambacho Mungu amekiweka juu yetu, ikiwa ni pamoja na vile tulivyo navyo, yale tuyafanyayo, yale tuyasemayo, yale tunayoyafikiria, na jinsi tulivyo (**1 Wakor 10:31; Wakol 3:17**).

(3) Ikiwa hatutumii kikamilifu chochote tulichopewa kama wakili, kwa vile Mungu bado ndiye mwenye kumiliki yote hayo aliyoyaweka kwetu, anayo haki ya kuchukua "talanta" zake kutoka kwetu (**Math 25:28-29**).

(4) Kimsingi Mungu anaangalia juu ya mtazamo wetu na uaminifu wa yale tuliyo nayo, na siyo ukubwa hasa wa kile tulicho nacho. Pongezi zake kwa mtumishi aliyepewa talanta tano zililingana tu na za yule aliyekuwa amepewa talanta mbili, *"Vema, mtumwa mwema na uaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako"* (**Math 25:21, 23**).

(5) Kwa vile *"BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo, maana wanadamu huitazama sura ya nje mbali na Bwana, BWANA huutazama moyo"* (**1 Sam 16:7**), tukichukulia kwamba talanta hapo mwanzoni ilikuwa ni kipimo cha uzito, inaweza ikawa kwamba wale ambao hapa duniani wana "mzigo mzito zaidi," mazingira magumu zaidi, wenye fedha chache zaidi, na walio na mali chache zaidi, kusema kweli wanafanana na yule aliyepewa talanta tano, na siyo yule mtumishi aliyepewa talanta moja. Mungu anaweza pia kuwa amemweka yule mtu katika mazingira magumu, akijua kwamba mtu huyo anao uwezo kiuaminifu kabisa kumudu mazingira hayo magumu. Kama akidumu kuwa mwaminifu, thawabu yake itakuwa kuu, kama vile alivyokuwa mtumishi yule mwaminifu aliyeaminiwa kwa kupewa talanta tano.

# UWAKILI WA MAZINGIRA

## I. Ulimwengu na Vyote Vijazavyo Ndani Yake ni Mali ya Mungu.

**A.** ***Mungu ndiye muumba wa dunia na vyote vilivyomo.***

1. Mungu aliumba dunia na kila kitu kilichomo ndani yake. (**Mwa 1:1-2:3; Kut 20:11; Mdo 14:15; Ufu 4:11**).
2. Wanadamu ni *viumbe,* vilivyoumbwa na Mungu (**Mwa 1:26-27; 2:7, 18-22**).
3. Mungu hakuamua tu kuwaumba wale watu wawili wa kwanza (Adamu and Hawa), na kisha kutuacha peke yetu. Badala yake, Mungu kamuumba *kila mtu* (**Kut 4:11; Ayu 10:8; 31:15; Zab 33:13-15; 100:3; 119:73; 139:13-16; Isa 44:24; Yer 1:4-5; 27:5**).

**B.** ***Mungu humiliki dunia na vyote vilivomo ndani yake.***

1. Kuna uhusiano kati ya uumbaji na umiliki: Mungu hubakia kuwa ndiye mmiliki na mkuu na mwenye mamlaka juu ya dunia na kila kitu ndani yaket (**Ayu 12:7-10; Zab 24:1; 50:10-12; 104:1-30; Isa 66:1-2a; Math 5:34-35; Mdo7:49-50**).
2. Kwa vile Mungu aliwaumba wanadamu, sisi ni wake tangu kuzaliwa hadi kufa (**Kum 10:14; Zab 24:1; 50:10-12; 95:6-7; 100:3; Isa 17:7; 29:19; 44:24; 45:9; 64:8; Yer 18:1-10; Eze 24:15-18; Rum 9:20**).
3. Mungu hasa hasa huwamiliki Wakristo wote **(Rum 14:7-8; 1 Wakor 6:19-20; 7:23; 1 Pet 1:17-19; 2 Pet 2:1).**

## II. Ulimwengu na Vyote Vilivyomo Ndani Yake Humdhihirisha Mungu na Utukufu Wake.

**A.** ***Kila kitu ambacho Mungu alikiumba kina umuhimu wa ndani na uthamani, kwa sababu Mungu alikiumba.***

1. Kila kitu Mungu alikiumba, alikiumba "chema kabisa" (**Mwa 1:4, 10, 12, 18, 21, 25, 31**).
2. Anguko la mwanadamu katika dhambi, na hukumu ya Mungu kwa dhambi ile, limeiathiri dunia, wanyama, na wanadamu wenyewe (**Mwa 3:14-24**).
3. <u>Licha ya dhambi ya mwanadamu na hukumu yake, Mungu anadumisha mahusiano maalum na dunia na vitu duniani.</u>
    a. Mungu ameanzisha Agano kati yake mwenyewe na dunia na viumbe wote duniani kwamba, kipindi chote dunia ingalipo na vizazi vyake, hataangamiza tena viumbe hai vilivyomo duniani kama alivyofanya wakati wa gharika kuu (**Mwa:9:8-17**).
    b. Anaishikamanisha dunia pamoja na kuvihifadhi kikamilifu viumbe vilivyomo (**Ayu 38-39; Zab 104:1-32; Mdo 17:28; Wakol 1:16-17; Waeb 1:2-3; 2 Pet 3:5-7**).
    c. Anao mpango na makusudi kwa dunia (**Ayu 23:13-14; Zab 33:8-11; 135:5-6; Isa 14:24-27; 46:9-11; Waef 1:8-12**).
    d. Anatawala vitu vyote na watu wote, na yuko kazini ili kuukamilisha mpango wake (**Ayu 12:13-25; Isa 10:5-16; 40:21-26; Hab 1:1-11; Mdo 2:22-24; 4:27-28; Rum 8:28-30; 9:14-24; Ufu 17:14-17**).
    e. Mungu hutumia vitu vya asili kufanya mambo muhimu anapojifunua mwenyewe na mpango wake kwa dunia, ikiwamo milima (**Mwa 22:1-19**; **Kut 19:9-25; Mdo :9-12**); uwingi wa maji (**Kut 14:5-31; Yos 3:1-17; Math 3:13-17; Marko 6:45-51**); mimea (**Kut 3:1-6; Yos 24:26**); na wanyama (**Hes 22:21-33**).
    f. Kristo atakapokuja tena mwisho wa nyakati hizi, uumbaji wenyewe utafanyishwa upya (**Rum 8:18-25**).

**B.** ***Kila kitu humfunua Mungu.***

Mungu ni nje ya ulimwengu aliouumba. Hata hivyo, ulimwengu ni muhimu Hata uumbaji una umuhimu wa kiroho kwa vile unasaidia kufunua nyanja mbali mbali za tabia na sifa za Mungu. Kwa hiyo:

1. Uumbaji humfunua Mungu (**Rum 1:18-20**).
2. Mbingu humfunua Mungu (**Zab19:1-2**).
3. Viumbe hai humfunua Mungu (**Ayu 12:7-9**).
4. Watu ndio rasmi humfunua Mungu kwa sababu wanadamu ni viumbe pekee walioumbwa kwa mfano wa Mungu na waliumbwa rasmi kwa ajili ya kumtukuza Mungu (**Mwa 1:26-27; 5:1-3; 9:6; Isa 43:7;**

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

**Rum 8:29; 9:23; 2 Wakor 3:18; Waef 4:22-24; Wakol 3:9-10; Yak 3:9-10**; **Ufu 4:11;** ona pia **Rum 11:36; 1 Wakor 10:31**).

5. Ingawaje si kila kitu kilichoumbwa ni cha kiungu, vitu vyote vilivyoumbwa vinamwakilisha Mungu.

a. *Biblia inamlinganisha Mungu ki-wanadamu kama:*

(1) Mfalme—**1 Sam 8:7.** (3) Mwenye shamba—**Math 21:33.**
(2) Baba—**Math 6:9.** (4) Kuhani—**Waeb 7:24.**

b. *Biblia inamlinganisha Mungu ki-wanyama kama:*

(1) Simba—**Isa 31:4.** (3) Kuku—**Math 23:37.**
(2) Tai—**Kum 32:11.** (4) Mwana kondoo—**Ufu 5:6.**

c. *Biblia inamlinganisha Mungu ki-viumbe visivyo na uhai kama:*

(1) Mwamba—**Kum 32:4.** (5) Mwenge au mwanga—**Ufu 21:23.**
(2) Jua—**Zab 84:11.** (6) Moto—**Waeb 12:29.**
(3) Chemchemi—**Zab 36:9.** (7) Nyota ya asubuhi—**Ufu 22:16.**
(4) Kivuli—**Zab 91:1; 121:5.** (8) Nuru—**Zab 27:1.**

## III. Matokeo ya Uumbaji na Uwakili wa Mwanadamu Juu ya Uumbaji Huo

**A. S*isi tunatakiwa kumwabudu Mungu peke yake; hatupaswi kuabudu nyota, dunia, mimea, wanyama, au kitu chochote kilichoumbwa.***

1. Mafundisho ya viumbe, Utofauti mkuu kati ya Mungu na kitu kingine chochote. "*Vitu vyote* viliumbwa kutoka utupu. *Vitu vyote, changanya na mwanadamu, vinatokana na asili moja , kwa msingi wa kiuumbaji*. . . . Yeye [Mungu] aliumba vitu vyote, na ni Yeye pekee ndiye Muumba. Kitu kingine chochote kile kiliumbwa. Ni Yeye tu ndiye Wa milele Asiye na Mwanzo, na ni Yeye tu ndiye Muumba; na kila kitu kingine humtegemea Yeye. Hivyo mwanadamu, mnyama, maua, na mashine, kwa mtazamo wa Ki-Biblia, vyote ni tofauti kabisa na Mungu kwa vile Yeye ndiye aliyevifanya hivyo vyote. Kwa maana ya uungu, mwanadamu ni tofauti na Mungu kama ilivyo mashine." (Schaeffer 1982, vol. 5: 28)

2. Kwa sababu ya utofauti wa msingi kati ya Muumba na uumbaji, basi kuabudu au kukipa nafasi ya kwanza kitu chochote kilichoumbwa ni dhambi; na kutasababisha hukumu ya Mungu (**Kut 20:1-6; 23:24; Kum 5:6-10**). Kukatazwa kuabudu sanamu (yaani, chochote nje ya Mungu Mwenyewe) kunahusisha kuabudu malaika (**Wakol 2:18; Ufu 19:10; 22:8-9**); wanadamu (**Dan 3; Mdo 10:25-26; 14:8-18**); wanyama (**Rum 1:18-32**); miti (**Yer 2:20; 3:6, 13; Hos 4:13**); vitu visivyo hai, vya duniani, au mbinguni (**Ayu 31:24-28**); au kitu chochote kilichotengenezwa na watu (**Kut 32; 2 Fal 18:4; Yer 10:1-15**).

**B.** ***Mungu alimpa mwanadamu mamlaka juu ya dunia yote "kumiliki" na "kuilima" na "kuitunza" dunia nzima na viumbe vyote vilivyomo ndani yake (Mwa 1:28; 2:15).***

1. Kuhusiana na swala la mazingira, kuna maswala mawili kuhusu "kumiliki":

a. *Kumiliki matumizi ya nguvu zilizodhibitiwa, na zilizofikiriwa.* "Ni nguvu, kwa mfano, kama zinavyotumika kukatia mti na kisha kuuchonga, na nguvu hiyo inatawalika; kwa vile kuna mategemeo yake katika akili, na kuna kitu kimepangwa kitakachotengenezwa; kati ya vitu vingi vinavyoweza kutengenezwa. Hii inamaanisha kwamba "kutiisha" kunahusisha kutumia mali ghafi ili kutengeneza kulingana na kile kilichoko kichwani. Hali hii ni tofauti kabisa na wanyama wanavyotumia hisia zao. Mwanadamu ana muundo wa kitu kichwani, kitu anachokikusudia kuunda, lengo, kitakavyokuwa akilini mwake, na hutumia nguvu zilizodhibitiwa ili kukamilisha lengo hilo." (Peck na Strohmer 2000: 156-57)

b. K*ulingana na Agizo la Mamlaka, kumiliki hakufanyiki peke yake.* "Kuna ushirika (wahusika wawili). Mawazo ya "Hawa" na msaada wake—yeye ni aina ya yule aliye makini na mtahadharishaji kwa Adamu—katika picha nzima. Hivyo kutiisha hakufanyiki na mtu peke yake. Kunaendelea mpaka kwa jamii na kundi zima. Hii inamaanisha kwamba mawazo ya jumuiya yanachangia aina ya utiishaji unaofanyika. Chukua mfano, huko Marekani, meza zake ni tofauti na meza nyingine, kwa mfano, na zile za Japani, ambako meza zake ni fupi sana (inchi chache kutoka sakafuni) kwa sababu huko watu hawakai katika viti wanapozitumia." (Ibid.: 157)

2. Pia kuna pande mbili za "kulima" mazingira.

a. *Kulima au kufanya kazi ni kuzalisha kile kilicho chema na cha thamani.* "Unaishughulikia ardhi iwe shamba, mbegu iwe mhindi au tunda fulani, mbegu kuwa chakula au kiungo. Kipande

cha dhahabu kinachimbuliwa na kisha 'kufanyiwa kazi' kutoa kwa mfano pete ya arusi, na kuendelea. Kwa hatua hizi, watu hutoa 'kutokana na mali ghafi' siyo tu vitendea kazi vya kiMdoo, lakini pia bidhaa za thamani. . . . uumbaji, ndipo, unakuwa wa thamani kadiri watu 'wanavyoutiisha'. Nao unakuwa wa thamani siyo tu kiuchumi, lakini pia kimtazamo, kijamii, kiitikadi, na kadhalika." (Peck na Strohmer 2000: 157)

b. *Neno la Kiebrania la "kuilima" au "fanya kazi" pia linabeba maana ya "kutumika"—abad ambayo kimsingi inamaanisha "tumikia" kama vile "fanya kazi."* Kwa vile maana ya msingi ya "kulima" au "kufanya kazi" ni "kutumika," kutiisha kwetu na kufanya kazi duniani "siyo kwa kujinufaisha" (Ibid.).

3. <u>"Kuyatunza" mazingira yaliyofanyiwa kazi au kulimwa. Mazingira lazima yatunzwe na yalindwe.</u> Sababu moja kwa nini hili ni lazima, ni kwa vile jinsi tutakavyotunza mazingira kutaathiri kiuzuri, au kiubaya kizazi kilichopo na kijacho cha watu wanaobeba sura ya Mungu. Jinsi tunavyopahudumia *"Mahali pa kuwekea miguu ya Mungu"* (**Isa 66:1; Math 5:35; Mdo 7:49**) na sura yake mwenyewe unaonyesha hasa jinsi tunavyomwazia yeye.

**C. *Hatutakiwi kudhulumu, kuangamiza, au kuharibu uasili ulioumbwa, bali tunapaswa kuuhudumia vizuri.***

1. <u>Mtazamo wa Ki-Biblia kwa Uasili unaupatia thamani yake fulani *kivyake , kwa sababu Mungu ndiye aliyeufanya.*</u> Kile alichokifanya Mungu, sipaswi kukidharau (hasa kwa vile mimi nami nimeumbwa na Mungu). Kama asemavyo Dallas Willard, "Mungu Mwenyewe anaipenda dunia sana kiasi kwamba hauondoi mkono wake chini yake. Na kwa vile anaipenda na ni nzuri, kuitunza kwake pia ni kazi ya kiungu na ni sehemu ya uzima wa milele" (Willard 1997: 205). Watu mara zote wametumia ile hali ya umiliki juu ya Uasili vibaya—kwa kuharibu viumbe na uasili kama vile si kitu chochote. Francis Schaeffer anaonyesha kwamba: "Mkristo ni mtu ambaye anayo sababu ya kushughulikia kitu kilichoumbwa kwa heshima ya hali ya juu zaidi. . . . na kwa sababu ya juu kabisa: kwa sababu nampenda Mungu—Nampenda Yeye aliyevifanya vyote! Katika kumpenda Yeye Aliyevifanya hivyo, Ninaheshimu kile alichokifanya" (Schaeffer 1982, vol. 5: 32-33). Kusema ukweli, kwa sababu tunampenda Mungu kuliko tunavyoipenda dunia hii, tunapaswa tuitunze dunia hii vizuri zaidi kuliko wale wanaofikiria kwamba dunia hii ndiyo "kila kitu kwao."

2. <u>Tunapaswa pia kuuhudumia uasili kwa heshima kwa sababu Mungu *ndiye anayeumiliki.*</u> Mtazamo wetu kwa dunia hii ya asili lazima uwe kwamba: "ni mali ya Mungu, na ni lazima tuutumie umiliki wetu juu ya vitu hivi si kama vile tumepewa kuviangamiza, lakini kama vitu tulivyoviazima au tulivyovimiliki kwa kuaminiwa. Tunapaswa kuvitumia tukijua kwamba si vyetu kimsingi. Umiliki wa mwanadamu uko chini ya umiliki wa Mungu" (Schaeffer 1982, vol. 5: 40).

3. A<u>fya ya Mwanadamu, maisha, na heshima yake huathirika wakati mazingira yake yanapokuwa mabaya na yanapoharibiwa.</u> Kuharibu mazingira kunadhuru afya za watu, maisha, na thamani ya maisha yao. Yesu ametupatia amri "amri ya upendo" (Mpende Mungu, na umpende jirani Yak kama nafsi Yak—**Math 22:34-40;** ona pia **Yoh 13:34-35**) kama kipimo ambacho tunatumia kufanyia katika jambo lolote. Tumepewa wito au utume wa kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi dunia yote (ona **Math 28:18-20; Yoh 17:17:18; 20:21**). Ikiwa Wakristo wanaharibu na kuyachafua mazingira, tunaonyesha kwamba hatumpendi Mungu, kwa sababu hatuthamini kile ambacho amekiumba. Ikiwa Mdo yetu yanaathiri afya za watu, maisha yao, au thamani ya maisha, tunaonyesha kwamba hatumpendi jirani yetu kama tunavyojipenda sisi wenyewe.

4. <u>Mifano ya kutoharibu Uasili au maumbile ni pamoja na:</u>

a. *Vijiji vingi ni vichafu sana.*

(1) <u>Malundo makubwa ya takataka na uchafu huwa yanalundikana kila mahali, mifuko ya maplastiki, hutupwa popote tu na kuachwa hapo ambapo watu wanaishi.</u> Hii haipendezi kwa macho, na huonyesha ukosefu wa heshima ya mwanadamu na thamani ya maisha yake. Madimbwi machafu ni mahali pa kuzalishia mbu waletao Malaria, nzi,vijidudu mbali mbali, na vimelea vya maradhi. Femi Adeleye anaelezea mkasa aliokutana nao kuonyesha jinsi ilivyo si ya Ki-Biblia: "Ninaijua nyumba moja ya wageni ya Mkristo fulani katika nchi zetu za Bara la Afrika, iliyozungukwa na uchafu wa kila aina. Niliwaona watu wa nyumba hiyo na wale wa ujirani wakitupa takataka na uchafu zaidi na zaidi hapo na kufanya chuguu kubwa. Harufu ilikuwa mbaya kiasi kwamba ilikuja madirishani mwetu na kuingia ndani. Nikaamua kuulizia ni jukumu la nani kuondoa zile takataka. Nikaambiwa "Serikali ndiyo inatakiwa ifanye hivyo lakini hao jamaa hawajaja kwa muda mrefu sasa". Nikatazama pande zote na nikagundua

kulikuwa na marundo mengi ya takataka mitaani, na nyingine ni karibu sana na mlango wa gesti yetu. Ilionekana kama raia wengi tu walikuwa wanaingojea Serikali iondoe ule uchafu. . . . Mtazamo wa namna hii unatokana na kuchora mstari wa kubagua kati ya kipi ni kitakatifu na kipi ni cha kidunia au kati ya kipi sisi tunakiita cha kiroho, na kipi cha kidunia. Tunafikiria kwamba kuondosha uchafu ule, na usafi wa mazingira na uwakili mzuri wa rasilimali za Serikali ni "Maswala ya kidunia"au ni kuwajibika tu, hivyo hatushughuliki nayo. Huwa tunajiwekea uwigo kwa kushughulikia mambo ambayo tunayaita ni matakatifu au ya kiroho. . . . Tunahitaji kurudi kwenye mtazamo wa Ki-Biblia. Kwa mtazamo wa Ki-Biblia, mambo yote ya maisha ni matakatifu." (Adeleye 1999: 127)

(2) <u>Makanisa yangeweza kufanya utume wenye thamani kwa kuelimisha watu kuhusu mazingira kwa kufanya usafi wa vijiji kuondoa uchafu na takataka zlizolundikana.</u> Kwa kufanya mambo haya, makanisa yangelikuwa yanawaambia watu kuwa: "Afya yenu, maisha, na thamani ya maisha yenu yana umuhimu kwetu. Mna umuhimu mno na hamstahili kuishi katika dimbwi la uchafu. Tunawajali, na tunajali thamani ya kijiji hiki." Serikali ya Rwanda ina sheria ambayo imeleta tofauti kubwa kuhusiana na hili. Inawaamuru watu wasafishe maeneo yao mara kwa mara. Na matokeo yake, Rwanda ni nchi safi zaidi kuliko nchi nyingine za Afrika Mashariki. Wakristo wasingepaswa kutegemea serikali iwasimamie kwa sheria kutekeleza yale ambayo tunaweza na tunapaswa tuwe tunayafanya wenyewe.

b. *Kutoyachafua maji.* Kutupa vitu vyenye sumu katika maji (kwa mfano, Karatasi za nailoni [*kaveras*], miili ya viumbe vilivyokufa, vinyesi vya watu au vya wanyama) huharibu afya zetu na mazingira pia.

c. *Usiondoshe au kukata vitu kwa sababu ya unajisikia tu.* "Ikiwa ni lazima uondoe jiwe au mwamba ili kujenga msingi wa nyumba, basi hapo kwa vyovyote uliondoe. Lakini kama uko katika matembezi msituni, basi usiukwanyue mmea wowote pasipo sababu yoyote, mfano kukwanyua kuvumwani na kisha unauacha hapo unyauke. Hata huo mmea unayo haki ya kuishi" (Schaeffer 1982, vol. 5: 43-44). Tunaweza kukata miti kwa ajili ya matumizi ya ujenzi, au kwa matumizi mengine ikiwa mibichi, lakini si kukata miti ati kwa sababu tu ya kuamua kuikata. (ona **Kum 20:19-20**).

d. *Kutokuvua samaki kupita kiasi.* Upatikanaji wa samaki lazima uwe endelevu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

e. *Kufungulia redio kwa nguvu bila kujali wanaokuzunguka, au kugeuzia spika nje kwa watu, ili maeneo ya watu yapigizwe na sauti kali ya redio Yak.* Hilo hufanyika kila mahali Afrika na India. Ni aina ya "uchafuzi kwa njia ya sauti" utumiwao na watu wasio na fahamu za kuwajali wengine. Ni kutowafikiria wengine na hakuendani na uzuri wa asili wa Afrika wala India.

**D.** ***Tunapaswa kutenda kwa makini na kwa busara katika kuonyesha umiliki wetu wa maumbile.***

1. <u>Tunapaswa kujua sisi ni nani na matokeo ya Mdo yetu ili tupate kutenda kwa uwajibifu.</u> "Zipo kanuni ambazo zimeanzishwa na Mungu au sheria ambazo zinaweza tu kujulikana kwa kuchunguza utaratibu wa vitu vilivyoumbwa na Mungu. . . . [Francis] Bacon [1561-1626] na akasema tunapaswa kuzitumia sheria za maumbile katika namna ya "utakatifu"wakati tunainua ujuzi wa sayansi zetu. Kwa hili, alimaanisha ulimwengu ulioumbwa lazima utendewe kwa mtazamo wa Kikristo na unyenyekevu na kwamba Mdo yanayotokana na sheria za maumbile ni lazima yasukumwe na misingi ya Ukristo. Maarifa yanayopatikana, Bacon alisema, yanapaswa yatumiwe kuwahudumia wengine kwa kuondosha matatizo yanayowakabili watu wengine ana kuongeza "hali njema ya maisha" (Peck na Strohmer 2000: 155). Kwa mfano, Mungu ameumba mimea mingi yenye uwezo wa kutibu magonjwa, na kurutubisha afya. Twaweza kupanda mimea hiyo kwenye bustani zetu, tunapoitumia katika uasilia wake, twaweza kujikinga tusipatwe na maradhi, na hivyo kuokoa fedha nyingi kwa kutokununua madaya ya viwandani, yaliyotengenezwa kwa mchanganyiko wa kikemikali Tunahitaji kuzitumia rasilimali hizo kwa shule zetu, Mashirika ya Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika Binafsi, na yale Ya Kujitolea, na maktaba ili kuongeza maarifa na ujuzi wetu; ili kwamba tuweze kutenda kwa umakini na kwa busara zaidi.

2. <u>Kutenda kwa umakini na kwa busara kunahitaji maamuzi yanayohitaji gharama na muda pia.</u> Hugharimu fedha nyingi zaidi, hasa pale mwanzoni, kuihudumia ardhi ipasavyo. Pia, kikawaida huchukua muda mrefu kutengeneza ardhi. Kama Francis Schaeffer asemavyo, "Hivi ni vitu viwili

vinavyoongoza katika uharibifu wa mazingira yetu: fedha na wakati —au kwa maneno mengine, tamaa na kukimbizana. Swali ni kwamba, au linaonekana kuwa, je tutakwenda kuwa na faida ya mara moja na kukimbizana na wakati, au tutakwenda kufanya kama watoto wa Mungu wapasavyo?" (Schaeffer 1982, vol. 5: 49) Kuhusiana na mfano kwa hili, Schaeffer anasema: "Makatapila makubwa yamekuwa yakibomoa ardhi na kuangusha miti kabla nyumba hazijajengwa. Mwisho wa kazi hiyo huwa hapapendezi tena. Ingegharimu maelfu ya dola nyingi kuyarudishia mazingira *kuzungukia* miti hiyo, lakini badala yake huwa inafyekwa tu bila maswali yoyote. Na kisha twajiuliza, baada ya kuona matokeo, jinsi watu watakavyoishi pale. Ni upungufu wa uanadamu panapokuwa jangwa, na hata kiuchumi ni hali ya umasikini zaidi pale ule udongo wa juu unapoondolewa na kupotea. Hivyo wakati mwanadamu anapovunja kule kuaminiwa na Mungu, kiuhalisi huwa yuko katika kutaabika." (Ibid.: 44)

3. Kutenda kwa uangalifu na kwa busara kunahitaji sisi tutumie ufahamu wa Nia ya Kristo na kuzitumia kanuni za Kikristo. Tunayo "nia ya Kristo" (**1 Wakor 2:16**). Swali ni kama tutaitumia hiyo tunapoutenda uwakili wetu juu ya uasili au maumbile. Tunahitaji kutumia uthamani wa Kikristo wa Ki-Biblia katika Mdo yetu kuhusiana na maumbile, ambayo ni sehemu ya umiliki wetu. Katika kufanya hivyo, tunatakiwa kujiuliza wenyewe mara kwa mara mambo kama vile: Kwa nini tunafanya hili tulifanyalo? Je kule kutiisha uasili kunafanyika katika haki au bila haki? Je kunafanyika kwa utukufu wa Mungu au kwa sababu za ubinafsi?

4. Mifano ya utendaji makini na wa kibusara juu ya Umiliki wetu kwa Maumbile:

a. *Kupumzisha ardhi, kubadilisha uoto au mimea, kumwagilia vizuri, na pia kuhifadhi vyote; ardhi na uwezo wake wa kuzalisha* (ona **Law 25:1-7**).

b. *Kupanda miti na mimea mingine.* Hili linaweza kuzuia kumomonyoka kwa udongo, huleta hewa safi, kivuli, kuni, na kupendeza. Na huu ufuatao ni mfano mojawapo wa ujinga wa *kutokufanya* hivyo: "[Kwenye kijiji kimoja kidogo cha Tanzania] mti moja uliota, Mwembe wa kimo cha kadiri tu lakini wenye majani mengi sana. Pakawa na kivuli kizuri chini yake. Chini ya kivuli kile walikuwepo watu Thelathini waliokuwa wanasukumana ili kupata nafasi ya kivuli kile, wakiangaliwa na mbuzi aliyekuwa amefungwa kamba kwenye jua pembeni mwao. Kile kilichoonekana kama ni mchezo fulani wa kuigiza wa lile kundi, kilikuwa dhahiri ndiyo mtindo wa maisha ifikapo mchana kila siku ili kujiokoa. Kilichonishangaza zaidi mimi kwa kundi hili kubwa la watu waliobanana pamoja wa kijiji hiki chini ya mti moja pekee, ni kwamba hakukuwa na mtu yeyote kati yao aliyekuwa na wazo la kupanda miti ya maembe mingine ili kupata kivuli zaidi. Ilikuwa ni rahisi zaidi kupanda mti—kwani, mwembe huu ulikuwa na mbegu maelfu—ajabu hakuna yeyote aliyeamua kupanda hata moja, au kama yeyote alipanda, basi huo mti ulikatwa. Picha ya Waafrika hawa chini ya mti ule moja katika kile kijiji kidogo cha Tanzania mikoa ya Kati wakigongana kujaribu kujibana chini ya ule mti moja, ilikaa nami kama mfano dhahiri wa kupanga mipango ya mbeleni, au kupungukiwa nao." (Theroux 2003: 248)

c. *Kutoa usalama kwa wanyama.* Hili linaweza kuhusisha: kutowachoma nyuki wakati wa kuvuna asali; kutowapiga ng'ombe wakati wa kulima, kuwalinda wanyama pori kwani hutupatia nyama, maziwa, na ushirika mzuri; na kuleta utofauti wa mazingira yetu (k.m, gorila wa Rwanda). Kufanya hivyo kunaongeza thamani ya maisha na huweza kuongeza thamani ya kiuchumi kwani watu huvutwa ili kuona mimea hiyo isiyo ya kawaida na wanyama pia.

d. *Kutengeneza barabara kiustadi.* Katika maeneo fulani, wanakijiji wanatimuliwa na mavumbi kwa miaka kadhaa wakati barabara zao zinaporekebishwa. Hilo hudhuru afya yao kwa kiwango kikubwa na hushusha thamani ya maisha yao. Kupitisha njia za mkato vijijini kwa ajili ya malori, badala ya kufanya magari yote kupitia njia moja kati kati ya kijiji, na kufanya njia za lami kwenye vijiji, kungeboresha thamani ya maisha na afya. Kufanya njia kuu zipitishe magari matatu au manne badala ya mawili, kungeboresha uwezo wa usafirishaji na uchumi.

**E. *Tunapaswa kuleta uponyaji wa kweli wa maumbile au uasili.***

1. Kristo alitangaza kwamba wakati umetimia, ufalme wa Mungu umekaribia, na sasa upo (**Math 21:31; Marko 1:14-15; Luka 17:20-21;** ona **Wakol 1:13**). Ingawa kutakuwa na utimilifu wa Ufalme hapo Kristo atakapokuja tena, ufalme upo hata sasa katika hali isiyo wazi. Hata sasa tumepewa: uzima mpya; uzima wa milele; nia ya Kristo; na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo: "Wakristo waiaminio Biblia siyo tu wameitwa kusema "siku moja" kutakuwa na uponyaji, lakini kwamba kwa neema ya Mungu, kwa msingi wa kazi iliyomalizika ya Kristo, uponyaji kamili unaweza kuwapo hapa na sasa. . . . Tunapoyachukua mawazo haya sehemu ambazo tunahusiana nazo kimaumbile na kiuasili, panakuwepo

na uwiano mzuri. Kwa msingi wa ukweli kwamba kutakuwepo na ukombozi kamili baadaye, siyo tu wa mwanadamu, bali kwa viumbe vyote. Mkristo anayeiamini Biblia anapaswa kuwa ni mtu—kwa msaada wa Mungu na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu—kuutendea uumbaji sasa katika uelekeo utakavyokuwa wakati huo. Siyo kwamba utakamilika kabisa kwa sasa, lakini kunapaswa kuwe na kitu fulani cha dhahiril au basi tutakuwa hatujafanikiwa katika wito wetu." (Schaeffer 1982, vol. 5: 39)

2. Mifano ya kuleta uponyaji kwa maumbile au uasili:

a. *Kurudishia udongo wa juu mahali ambapo palikwnguliwa na kuchimbuliwa.* "Kama hao wanaokwangua udongo wangeliyachukua makatapila yao wauchimbe udongo na kisha kuurudishia ule udongo wa juu tena mahali pale, miaka kumi tu baada ya uchimbaji wao pangekuwa na shamba kubwa, na katika miaka Hamsini patakuwa na msitu kabisa. Lakini bahati mbaya, kama ambavyo siku zote amekuwa akifanya; mwanadamu amekuwa akigeuza ardhi kuwa jangwa na kisha analia kwamba udongo wa juu umeondoka, majani hayaoti, na hakuna njia ya kufanya miti iote hata kwa miaka Mia kadhaa"! (Ibid.: 48)

b. *Kuondosha matakataka yanayochafua ardhi; kuziba mashimo barabarani, na pia kuboresha miundo mbinu yao.*

**F.** ***Tunapaswa kujibidisha kuongeza uzuri wa uumbaji.***

1. Uwakili wa maumbile au uasili unahusisha pia uzuri wa asili. Katika kusema kwake kwamba *"hata Sulemani katika utukufu wake wote hakujivika kama mojawapo ya maua haya"* (**Math 6:28-29**), Yesu alikuwa anautambua uzuri wa asilia. Schaeffer anasema hivi kuhusu hili: "Wakati kanisa linaweka imani katika utendaji, kuhusiana na mwanadamu *na kwa uasili au maumbile, kuna uponyaji wa kutosha.* Moja ya matunda ya awali katika uponyaji huo, ni ufahamu mpya wa hali ya kuvutia. Uthamani wa wale wanaopenda mambo ya uzuri kwamba yasipuuzwe. Mungu amemuumba mwanadamu na ufahamu wa uzuri ambao wanyama hawana. Hakuna mnyama yeyote aliyewahi kutengeneza au kuchora kitu chochote kutokana na sanaa. Mwanadamu, akiwa ameumbwa katika mfano wa Mungu, ana sifa ya kupenda uzuri, na mara aanzapo kujihusisha na uasili au maumbile kama anavyotakiwa, uzuri wa maumbile huwa unahifadhika. Lakini pia, uthamani wa kiuchumi na kiutu unapoongezeka, kwa matatizo ya utegemeano wa viumbe tulio nao sasa utapotea." (Schaeffer 1982, vol. 5: 42)

2. Mifano ya kuongezeka uzuri ni pamoja na kupanda miti, vichaka, mimea ya kingo, na maua kuzunguka nyumba zetu, au hata pembeni mwa barabara, kuhifadhi uzuri wa mahali. Mimea huongeza upatikanaji wa Oksijeni (hewa safi), na kwa kando ya barabara, hupunguza vumbi, moshi wa magari, na sauti zinazotokana na matumizi ya barabara. Kupanda maua na miti ya matunda kama vile maembe kando ya barabara kuu, siyo tu hufanya zipendeze, lakini pia huwapatia watoto wa shule na watu wengine matunda ambayo ni mazuri kwa ajili ya miili yao na kuwapa kivuli pia.

## UWAKILI WA BINAFSI NA KWA WENGINE

## I. Utangulizi

**A.** ***Maisha ya Ukristo ni safari, na siyo tukio.***

Maisha ya Ukristo siyo kusafiri tu, bali ni safari ya mapambano inayihitaji nidhamu, hasa nidhamu ya kujitawala. Msimamo wetu wa msingi unapaswa umlenge Mungu kwanza na wenye msingi wa neema ya Yesu. Utumishi kwa Kristo usichukue nafasi ya kumtafuta, au kujitoa kwake Kristo. Lazima mara kwa mara tuwe walinzi kinyume na dhambi—mitazamo isiyofaa, mawazo, maneno, na mtendo. Lazima daima tuwe makini juu ya "Umuhimu wa maswala" (m.y., matukio yote ya maisha yetu ambayo yanatumia muda wetu na usikivu wetu na kugeuza uelekeo wetu mbali na mambo ambayo ni ya umuhimu mkubwa zaidi). Kuishi maisha mazuri si swala la "kujitahidi zaidi," lakini la "kujitahidi kwa busara zaidi."

**B.** ***Wakristo wote ni mawakili wa miili yao na nafsi zao.***

Uwakili wa binafsi unapaswa ushughulikie nyanja zote sita zinazomfanya mtu (my. kiroho, kimwili, kijamii, Kiakili, kitabia, na kihisia). Kwa kufanya hili kutaondoa matatizo mengi ya binafsi, na kuboresha jhali ya mtu na utoshelevu wa maisha, na kuweza kuongeza utendaji bora zaidi wa huduma ya mtu.

## II. Uwakili wa Nia

**A.** ***Kila moja, katika kila desturi, anao mtazamo wa dunia unaomfanya aishi maisha anayoyaishi.***

1. Mtazamo wa mtu kuhusu dunia au ulimwengu kwa kiwango kikubwa hurithiwa kutokana na familia zilivyo na desturi au mila zao.

2. Mtazamo wa mtu kwa dunia unatoa jawabu la maswali makuu ya maisha, kama vile:

a. *Kwa nini dunia ipo?* Je kipi ni halisi? (Ontolojia; metafizikia; mada na roho).
b. *Je Mungu yuko?* Je yukoje? Je kuna uhai baada ya kifo? (theolojia).
c. *Je nawezaje kujua kipi ni kweli?* (Epistemolojia; Mamlaka na kweli).
d. *Mimi ni nani? Kwa nini nipo?* Je lipi ni lengo na kusudi la maisha? (umuhimu)
e. *Kwa nini kuna uovu?* Je nini kifanyike ili yawe sawa? (thamani na wokovu)
f. *Je kipi ni sahihi na kipi ni makosa?* Je niwe na tabia gani? (maadili

**B.** ***Biblia Takatifu ni Ufumaalum wa Mungu kwa wanadamu.***

1. Waandishi wa Maandiko wanathibitisha kwamba Biblia ndiyo Ufumaalum wa Mungu ambao wameunena na kuuandika (ona mfano, **Kut 17:14; 20:1; 24:4, 7; 34:27; Neh 9:13-14; Yer 1:4, 9; Luka 3:2-4; 1 Wakor 7:10; 11:23; 1 Wathes 2:2-9; 2 Tim 3:16-17; 2 Pet 1:20-21; 3:14-16**).

2. Kutoiamini Biblia huleta hali ya kutomwamini Kristo; kutoielewa vizuri Biblia huleta kushindwa kumwelewa vizuri Kristo.

a. *Kristo mwenyewe aliyaamini Maandiko yote (**Yoh 10:35**).* Aliyaamini matukio ya kihistoria ya Agano la Kale na wale wahusika wake kama matukio ya kweli na siyo ya kutunga. (**Math 12:39-41; 19:4-5; 24:37; 24:37-39; Luka 10:12; Yoh 3:14**). Aliiamini miujiza ya Agano la Kale (**Math 12:39-40; Luka 4:25-27; Yoh 6:49).** Alifundisha ujumbe wa Unabii wa Agano la Kale kuwa ulitoka kwa Mungu (**Math 24:15; Luka 24:25-27, 44-45; Yoh 5: 39**).

b. *Yesu aliiona Biblia akama yenye mamlaka (**Math 4:1-11; Luka 4:1-13; Yoh 17:17**).* Alithibitisha kwamba Biblia ilivuviwa kwa kila moja ya maneno yake na nyakati zake za Mdo hayo. (**Math 5:17-19; 22:31-32, 43- 45; Luka 16:17**). Alithibitisha kwamba Mungu alinena kupitia watu. (**Math 22:43; 24:15**); wakati huo huo aliitofautisha Biblia na desturi za watu (**Math 15:6; Yoh 5:46-47**).

c. *Alisema kila neno alilolisema mwenyewe lilikuwa ni neno la Mungu (**Yoh 8:28-29; 12:44-50**).* Alisema kwamba Biblia (Maandiko) lazima yatimizwe ndani yake (**Math 5:17; 26:56; Luka 4:21; 22:37**).

d. *Aliwakemea watu kwa kushindwa kuielewa Biblia (**Math 22:29; Luka 24:25; Yoh 3:10**).*

**C.** ***Mtazamo wa mtu wa dunia unahitaji kuchukua umbo na uongozi wa Maandiko.***

1. Neno la Mungu Msingi wa ufahamu wa kweli. Kuanzia mwanzo kabisa, wanadamu walikuwa wameumbwa kwa kumtegemea Mungu, kwa yote mawili: kwa kuweko au kuishi kwao na ufahamu wao.

a. *Kabla ya anguko, Adamu na Hawa walijua kila kitu kumhusu Mungu.*

(1) Walifanya ushirika na Mungu uso kwa uso (**Mwa 3:8-10**).
(2) Waliweza kujifunza kwa kuangalia mazingira yao, lakini uwezo wao wote wa kuelewa ulimtegemea Mungu.
(3) Adamu na Hawa walitakiwa kutegemea kikamilifu, na kutii, ufumuo maalum wa Mungu (Neno lake)—m.y., ufunuo kuhusiana na mti uliokatazwa na madhara yake (**Mwa 2:16-17**).

b. *Kushindwa kutegemea Neno la Mungu, Ufuwake maalumn, na kuutii, ndiko kulileta dhambi kamili.*

(1) Anguko la mwanadamu lilileta kifo cha roho. Baada ya dhambi kuingia duniani, akili za wanadamu zikapotoshwa, na watu wakaanza kutafsiri mambo kwa makusudi yao badala ya kumtegemea Mungu na Neno lake.
(2) Watu wanaweza kujifunza kiasi kikubwa kwa kujifunza uasili au maumbile, lakini ufahamu unakuwa ni kidogo tu kwa sababu haueleweki kwa uelewa wa mahusiano yatokayo kwa Mungu kama Muumba. Mengi tunayojifunza kutoka kwa wengine si sahihi kwa vile wao nao ni wadhambi tu.

c. *Imani inayookoa inahitajika ili kuielewa Biblia kama Neno la Mungu, na Yesu Kristo kama "njia, kweli na uzima"* (**Yoh 14:6**).

(1) Uhalisi wa kiroho na kweli haviwezi kuonekana mpaka Mungu aihuishe nafsi iwe hai (**Waef 2:1-4**). Neema ya Mungu ya kuokoa (**Waef 2:8-10**) inatufanyizia njia sisi ili tuwe na ufahamu wa kweli na kuimarisha uelewa wa Ki-Biblia, na wenye shina katika Neno.

(2) Wokovu huturejesha mahali ambapo tunajifunza kulitumaini Neno la Mungu juu ya mawazo yetu wenyewe. Hata hivyo, uelewa na mtazamo huu mpya, haujitokezi hivi hivi tu wenyewe wakati wa kuokoka—ni lazima nia zetu zifanyishwe upya kwa Maandiko (**Rum 12:1-2**).

2. Biblia imetolewa kwetu kama njia ya kuyabadilisha maisha yetu. **Rum 12:1-2** panasema: *[1] Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. [2] Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*

a. *Biblia hufunua mengi zaidi ya njia ya wokovu.* Inao mtazamo kamili wa dunia yote, na kutufundisha kuhusu uhalisi, kweli, mawazo, na Mdo.

b. *Katika **Rum 12:1-2** Paulo anaonyesha mahusiano kati ya kile tunachokiamini (mtazamo wetu wenyewe) na jinsi tunavyoishi,* pale anapowaasa Wakristo *"itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."*

c. *Kwa sababu "kufananishwa na dunia hii" huanzia akilini (nia), "kufanywa upya nia" kunamaanisha ni lazima tujifunze kufikiri kwa njia ambayo ni tofauti na jinsi tulivyofikiri kabla hatujaamini.* Nia zetu zinapofanyishwa upya kwa Maandiko, nasi pia twatakiwa kuleta mienendo na tabia zetu zote chini ya ubwana wa Kristo. Tunamtukuza Mungu kwa kuishi maisha matakatifu ambayo, kwa mara nyingine yanadhihirisha tabia ya Mungu kwa vile sisi tunawakilisha sura ya Mungu (**1 Wakor 10:31; Wakol 3:17; 1 Pet 1:15-16**).

**D. *Tabia maalum za nia iliyofanywa upya***

1. Biblia inavyotumia maneno kama "moyo" (Kiyunani, *kardia*) na "nia" (Kiyunani, *nous*) kimsingi ni maneno yanayofanana.

a. *"Moyo" ni "kiti cha maisha ya kimwili, kiroho, na akili"; kisha "ni katikati ya kiini cha maisha ya utu wa ndani, pamoja na fikira zake, hisia zake na ridhaa zake"* (Danker 2000: *"kardia,"* 508: ona pia Zodihiates 1992: *"kardia,"* 819-20). Ni "kiini cha uanadamu wetu ambako uhai unabubujika. Ndicho kinachotupa mweleko wa maisha kuhusiana na kila kitu tunachokifanya" (Willard 1997: 206).

b. "Nia" ni "Ile sehemu ya juu zaidi, sehemu ya kiakili ya mwanadamu ikiwa ndiyo inayosimamia mawazo na mipango"; na inaweza pia kuonyesha "ile jumla ya ufahamu wa akili na hisia za mhusika" (Danker 2000: *"nous,"* 680; ona pia Zodhiates 1992: *"nous,"* 1017-18).

c. Kwa hiyo, Biblia inaweza kumzungumzia mtu "sawa kama alivyo *"kusudia moyoni mwake"* (**2 Wakor 9:7**), na huwazungumzia watu jinsi *"bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza"* (**Rum 1:21**).

2. Kama matokeo ya wokovu, tumepewa mioyo mipya, tukapewa Roho Mtakatifu ndani yetu, na sasa *"tuna nia ya Kristo"* (**1 Wakor 2:16**).

3. Kuwa na nia ya Kristo hakumaanishi tunafikiri kama Kristo kimkato tu.

a. Ni lazima tutambue kwamba kuna vita vikali ndani yetu kati ya nguvu ya dhambi ikaayo ndani yetu na moyo uliofanywa upya na nia (Rum **7:23-25; 8:7;** ona pia **Math 16:23; Wafil 3:17-19**).

b. Tunalo jukumu la kuanza kwa juhudi kamili hatua ya *"tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo "* (**2 Wakor 10:5**).

4. Kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; kunahitaji kuandaa nia zetu, kujaza nia zetu na, kujitoa kwa vitu vya Kiungu na njia za Mungu (**Math 16:23; Luka 16:15; Rum 8:5-8; Wafil 4:8; Wakol 3:1-3; 1 Pet 4:1-2**).

5. Tunaweza kujifunza na kuwa tumejitoa kwa njia za Mungu kwa kufanya yafuatayo:

a. Kujifunza Neno la Mungu ili kujua, kuelewa, na kushaurika kikamilifu juu ya mambo ya Mungu (**Rum 14:5; 2 Wakor 13:5-8; 2 Tim 2:15; 3:16-17; 1 Pet 1:13**).

b. Kuchunguza na kuyapima mambo ambayo watu wanayasema, kulingana na Neno la Mungu, ili kujua kama Yak sahihi au hapana (**Mdo 17:11; 1 Wakor 14:29; 1 Wathes 5:21; 1 Yoh 4:1**).

c. *Kuishi kiimani yetu* -Neno la Mungu lisemavyo katika kila eneo la maisha yetu (**Yoh 14:21; 2 Wakor 8:8-12; 9:7; Waef 4:17-32; Wafil 4:9; Jas 1:22-25; 2:14-26; 1 Pet 3:1-3, 15**).

6. Kwa kupitia kujifunza na kulitenda Neno la Mungu, nia zetu zinavyogeuzwa maisha yetu yanachukua tabia mpya *"tunafanyishwa kwa mfano wa Mwana wake"* (**Rum 8:29**). Tabia au asili hiyo mpya inachanganya yafuatayo:

a. Tunaanza kumpenda Mungu kwa mioyo yetu yote, nafsi, akili, na nguvu zetu (**Math 22:37-38; Marko 12:30; Luka 10:25-28**).

b. Hatuhangaiki tena juu ya vitu na mambo ya dunia hii, na kutumainia uwezo wa ukuu wa Mungu na kumtegemea kwa utulivu na utoshelevu (**Luka 12:29; Wafil 4: 6-7, 10-13; 1 Tim 6:6; Waeb 13:5**).

c. Tunatafuta ushirika na waamini wenzetu (**1 Wakor 1:10; 2 Wakor 13:11; Rum 15:5-6; Wafil 1:27; 2:2; Wakol 3:14; 1 Pet 3:18**).

d. Hatujifikirii wenyewe kuwa bora zaidi ya tunavyopaswa, lakini tunawapenda majirani kama nafsi zetu (**Math 22:39; Marko 12:31; Luka 10:25-28; Rum 12:10; 13:8-10; 14:10; 1 Wakor 12:31b-13:13; Wagal 5:13-14; Waef 5:21; Wafil 2:3-8; Wakol 3:12-13; 1 Tim 1:5; Yak 2:8**).

7. Hatua nyingine zinazotusaidia kugeuza nia zetu ili zimfananie Kristo ni pamoja na :

a. *Usomaji wa Ukombozi. Tunatakiwa kutawala na kusimamia kile kiingiacho akilini mwetu.* Watu wengi ambao wana mafanikio ni wasomaji. Je tunasoma vitabu vinavyofaa na kutafuta habari zilizo nzuri au njema? Siyo tu Biblia, lakini vitabu vizuri hutupatia habari muhimu na shauku ya kuishi maisha yenye mafanikio na mazuri.

b. *Ibada ya Ukombozi.* Kumwabudu Mungu kwetu kunaonyesha uhusiano tulio nao na msimamo wetu na Mungu. Tunahitaji kuwa katika utendaji wa kweli tukishirikiana na kanisa zuri linalompenda Bwana, na waamini, wahubiri, na linalofundisha Neno lake. Kuabudu ni tendo la kutoa heshima na kumpenda Mungu katika maisha ya mtu. Kwa hiyo, haliishii ibada za Jumapili, lakini linapaswa kuwa swala la kila siku. Tunapaswa kumwomba Mungu aikague mioyo yetu kila siku kwa ajili ya dhambi na kwa mwenendo usiofaa.

c. *Urafiki wa Ukombozi.* Tunahitaji kujenga uhusiano na kundi dogo la marafiki ambao ni wacha Mungu ambao tunaweza kushirikisha mambo yetu wazi bila kuwa katika hatari. Tunahitaji kulea tabia ya kuwasikiliza wengine wanachosema, na kumsikia Mungu akisema nasi kuwapitia wao. Marafiki wacha Mungu wanaweza kutiana moyo, kusahihishana, kufarijiana, kusaidiana, kuonyeshana upendo, kufundishana, kujengeana maisha ya Ukristo katika maisha ya kila moja, na kujengana kiimani.

d. *Maombi ya Ukombozi.* Maombi yanapaswa kuwa ni sehemu yetu ya kawaida kila siku (ilikuwa tabia ya Yesu). Kadiri mawasiliano yanavyoendelea, ndivyo uhusiano mzuri unavyokolea. Hilo ni kweli kwa pande zote; na Mungu na mahusiano yetu na watu wengine. Tunahitaji kuyachunguza mambo katika maisha yetu ambayo ni kizuizi cha maombi (k.m, dhambi, mashaka, ubinafsi, kushindwa kuonyesha upendo kwa mwenzi wa ndoa, nk. ) Tunatakiwa kutenga muda wa kuomba. Zaidi ni kuwa, maombi ni kudumisha mlango ulio wazi wa mawasiliano na Mungu. Na matokeo yake, ni lazima tusiyachukulie maombi yetu kama ni kuongea na Mungu tu, bali tunatakiwa kumsikiliza Mungu anasema nini wakati tunaomba. Kisha tunatakiwa kutendea kazi kile tunachoelezwa ili kumtii Mungu.

e. *Kutafakari kwa ukombozi. Tunaposoma Neno la Mungu,* tunapaswa tuwe tunajiuliza maswali kama vile: Mungu anasema nami nini katika kifungu hiki? Je ananionya nini katika kifungu hiki? Je nawezaje kukitumia kifungu hiki katika maisha yangu? Na zaidi ya hapo, tunapaswa kuwa wanafunzi wenye bidii maishani. Tunahitaji kujichunga wenyewe katika maisha yetu, kuangalia vipau mbele vyetu, mahusiano yetu, na kisha kufanya mabadiliko yanayotakiwa ili kuleta maisha yetu katika kuendana na Neno la Mungu..

f. *Mipango ya Ukombozi. Watu wengi hawana mipango ya kuwaongoza.* Imewahi kunenwa kikweli kwamba "mtu anayeshindwa kupanga mambo, anajipangia kushindwa." Watu wote wana muda kiasi sawa katika kila siku. Hata hivyo, ikiwa hatuiendeshi hiyo siku, basi hiyo siku itatuendesha sisi. Ikiwa hatuzitawali fedha zetu, fedha zetu zitatuendesha. Ikiwa hatuupangilii muda wetu, tutajikuta tuko chini ya rehema za matukio ya watu wengine. Tunapaswa kujifunza kusema "hapana" kwa baadhi ya watu, na vitu fulani ambavyo vinatubana. Muda muhimu, na sehemu kubwa ya fedha, isitumiwe katika mambo yasiyo muhimu. Kupanga na kuweka malengo ni muhimu. Watu wenye mafanikio (wale wenye mafanikio katika kila uwanja,

zikiwemo biashara na kazi, na wale wenye mafanikio ya kiroho, kimahusiano, na kimwili) wana mipango, kisha huweka malengo, na kisha kwa umakini kabisa huitendea kazi hiyo na kuitumikia. Tunapofanya hilo, tunaona kwamba litie nguvu. Kadiri tunavyochukua hatua kusimamia maisha yetu, tunaona kwamba kila eneo la maisha yetu liwe bora zaidi.

g. *Uvumilivu na dhiki za Ukombozi.* Ni nchi za Magharibi tu ndiko watu wanakosea na kuwazia kwamba maisha yanapaswa kuwa ya raha, yenye kufurahisha, yaliyojaa furaha, na bila dhiki. Maandiko hayatoi ahadi za namna hiyo, na historia hushuhudia tena na tena kinyume na wazo hilo. Tunahitaji kuutafuta mkono wa Mungu katika dhiki zetu, tujifunze katika hizo, na tumfananie "Kristo" kama matokeo yake. Kwa kufanya vile, tutaweza kuwahusisha vizuri zaidi, kuwahudumia, kuwatia nguvu, na kuwafariji wengine wanaoteseka. Watu wote huwa na mategemeo na hutegea kuona mabadiliko mazuri kwa wenzi wa ndoa zao, watoto, na kwa wale wanaotumia muda kukaa nao. Hata hivyo, tunapaswa kutoruhusu matumaini na matarajio yetu kuwa ndiyo masharti ya mabadiliko. Mungu ndiye aletaye mabadiliko, kwa wakati wake, si kwa wakati wetu.

h. *Msamaha wa ukombozi.* Kristo ametusamehe deni la dhambi na uasi kinyume na yeye ambao tusingeweza kuwa na uwezekano wa kulipa. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa watu wa msamaha na wa mapatano. Tunapaswa kuwa wepesi kuomba msamaha na kurekebisha mambo tunapokosea, au kuwakwaza watu. Kwa kufanya hivyo, majeraha madogo hayatageuka kuwa madonda makubwa, nasi tutadumisha mahusiano yenye afya kijamii, kibinafsi, na kihisia. Kama hatuwi watu wa kusamehe, akili zetu na maisha yetu hayawezi kuwekwa huru na mambo yaliyopita, tutakuwa na mchungu, na hatutaweza kukua na kuwa aina ya watu ambao Kristo alitukusudia tuwe.

i. *Pumziko la kiukombozi na kurudishia nguvu za ujana.* Pumziko, kustarehe, na maburudiko, ni ya lazima kwa ajili ya afya ya akili na mwili. Tunapokuwa tumechoka na kuishiwa nguvu kimwili, akili zetu huwa si makini tena. Zaidi ya hapo,ikiwa tunatumia muda wetu wote kwenye kazi zetu, maisha yetu yanakuwa hayana uwiano; na mahusiano yetu na familia zetu na marafiki zetu huathirika. Kudumisha uhusiano thabiti na watu walio karibu nasi, na kupanga muda wa "kutia nguvu betri zetu upya" na kupangilia upya vipaumbele vyetu, ni muhimu ikiwa tunataka kuwa na akili zilizo makini, zinazofanya kazi yake vizuri, na maisha mazuri.

**E. *Kwa vile mtazamo wetu mpya wa dunia umesimamia Biblia, ni lazima tuitafsiri vizuri.***

Biblia hujieleza yenyewe. Biblia ni mkusanyiko unaofunua mpango wa wokovu kwa njia ya imani katika Kristo (ona **Luka 24:27, 44-47; Yoh 5:39**); hata hivyo, ufunuo wa Mungu ni *wa hatua kwa hatua*—hujifunua kila mahali katika Biblia. Kanuni muhimu kadhaa hujitokeza kutokana na kweli hizi:

1. <u>Njia pekee ya kudhibiti tafsiri ya andiko ni kupata maana ya andiko hilo katika lugha ile yake ya asili.</u> Ili kuielewa kwa usahihi Biblia—au ujumbe wowote ulioandikwa popote au nukuu yoyote ya kifasihi popote — swali la kwanza la kuuliza ni hili "Je *mwandishi* alimaanisha nini alipoandika kifungu hiki?" Zaidi ya hapo, kwa vile vitabu vya Biblia hapo awali viliwakusudia watu fulani maalum na katika mazingira maalum, ni lazima tujiulize "Je andiko hili lilikusudiwa nini kwa wale waliolengwa nyakati hizo?" Kisha tunaweza kuuliuza, "Je andiko hili linanihusuje mimi?" Labda muhimu kuliko yote, tuulize, "Je andiko hili linasema nini *cha kunionya*? "

2. <u>Andiko haliwezi kwenda kinyume na Andiko jingine.</u> Biblia inakubaliana yote. Kwa hiyo, vifungu viwili vinavyoonekana kupingana vyenyewe, vitakuja kuonekana kuwa havipingani pale vitakapoangaliwa vizuri zaidi. Kifungu kimoja kinaweza kuongeza kitu fulani au kukihalalisha kingine, lakini hakitapingana.

3. <u>Yote mawili historia ya ukombozi na "ushauri wote wa Mungu" (**Mdo 20:27**) lazima uzingatiwe kikamilifu ili kuelewa vizuri kifungu chochote.</u>

a. *Mafundisho ya "ufuwa hatua kwa hatua" hutuambia kwamba historia ya ukombozi ni lazima izingatiwe wakati wa kutafakari kifungu chochote.* Biblia ni jumla ya maelezo yanayoelezea jambo moja. Hata hivyo, kweli za Biblia hazifunuliwi zote kwa mkupuo moja, bali hujifunua hatua kwa hatua. Kwa hiyo, Agano la Kale ni maandalizi ya ya Injili; Zile Injili ni udhihirisho wa Injili yenyewe; Kitabu cha Mdo ya Mitume ni upanuzi wa Injili; zile Nyaraka ni maelezo ya zile Injili; na Kitabu cha Ufuni utimilifu wa Injili. Maana kamili ya kifungu chochote kile au mafundisho yoyote ya Ki-Biblia yanaweza yasiwe wazi mpaka Biblia yote inapokuwa imeheshimiwa na kutopuuzwa.

b. *Agano Jipya linatafsiri Agano la Kale.* Inasemekana kwamba "Agano Jipya limefichika

katika Agano la Kale." Sheria za Agano la Kale, zile sikukuu zake, na desturi zake zimetimilizwa na kujumlishwa katika Kristo (**Math 5:17; 2 Wakor 3:12-16; Wagal 3:23-4:7**). Ingawaje walikuweko kiukweli, Waisrael wa Agano la Kale na sheria zao, sikukuu zao, na desturi zao nyinginezo, walikuwa "vielelzo," "vivuli," au "mifano" ya uhalisi wa Agano Jipya (**1 Wakor 10:1-6; Wakol 2:16-17; Waeb 8; 10:1**). Kuna yote mawili, mwendelezo na kukatika kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Agano Jipya hujijenga lenyewe juu ya hoja za Agano la Kale, mara nyingi katika nia za kushangaza. Kwa hiyo, "Mara zote soma maandiko ya Agano la Kale kupitia miwani ya Agano Jipya." (Lehrer 2006: 177).

4. Maandiko yaliyo wazi yatoe tafsiri ya Maandiko yaliyojificha au ambayo hayaeleweki vizuri.

a. *Vifungu vingine vina ugumu wa kueleweka, haviko wazi au ni vigumu kuvielewa na vinahitaji vifungu vingine ili kuvielezea.* Katika hali kama hizi tunatakiwa:

(1) Kuangalia vifungu vingine ambavyo hutoa mwanga mwingi zaidi kuhusiana na somo au jambo hilo "hutoa maelezo ya nyongeza" kuhusu sehemu iliyobakia ya kitabu, wosia au agano, au Biblia kwa ujumla. Jaribu kulinganisha vifungu visivyoeleweka viendane na vile vinavyoeleweka. Vifungu vinavyoeleweka vinaweza angalau vikatuelezea kuhusu yale ambayo vifungu vile vigumu havimaanishi.

(2) Jali mtiririko "wa fikira" na kusudio la msingi la "yaliyonenwa hapo katika kifungu hicho." Mazingira ya ujumbe ambapo kifungu hicho kisichoeleweka ulikuwa unazungumzia; unaweza ukajitetea wenyewe kuhusu kile ambacho kinawezwa kumaanishwa au kutokumaanishwa.

b. *Vifungu vingine vinaonekana virahisi kwa kuonekana kwake, lakini havijitoshelezi; vifungu vingine vinahitajika ili kukamilisha maana.*

5. Jumuiko la maana ya maelezo yote ni muhimu sana kwa kuelewa kifungu chochote cha Maandiko. Kwa Maana hicho ndicho "kile kinachoendana na kifungu hicho." Zipo, kusema ukweli, *pande mbili za maana* zinazogusa kila kifungu: Ile *maana ya kimaandishi* na *maana ya kihistoria.* Maana ya kimaandishi inaweza kueleweka katika Biblia yenyewe. Maana ya kihistoria huhitaji maelezo mengine yaliyoko nje ya Biblia.

a. *Maana ya kimaandishi*—m.y, "maneno, sentensi, vifungu, au sura za maandiko zinazozungukia na kuhusiana na maelezo ya kifungu hicho" (Doriani 1996: 31). Maana ya maandishi hutuonyesha kifungu hicho au kifungu kingine cha Maandiko ambacho kinaweza kujitosheleza zaidi, na kutupatia mwangaza wa nyongeza kuhusu maana ikusudiwayo, hata kama hatujui lolote kumhusu mwandishi wake au asili yake au walengwa.

b. *Maana ya kihistoria*—m.y., "Ile mila, desturi, lugha, imani zao, na historia ya mwandishi na lile kundi alilokuwa analilenga wakati huo" (Doriani 1996: 31). Maana ya kihistoria hutupatia mwangaza juu ya sehemu hiyo ya Biblia inavyohusika na dunia ya sasa. Inatupatia sisi taarifa ya jinsi mambo yalivyokuwa yanayoelezea umuhimu wa maneno, kauli, desturi, watu, mahali, na matukio ambayo mwandishi huyo wa Biblia anayazungumzia.

c. "*Vipengele vya mawazo" katika Biblia ni vifungu, na siyo mistari.* Mistari pekee hutupa mkanganyiko mbaya wa fikira unaotufanya tuwazie kana kwamba kila mstari "unajitegemea" wenyewe kwa maana. Hiyo si kweli.

(1) "Ufunguo wa maana kwa mstari wowote unatokana na kifungu kizima, na siyo tu kwa maneno binafsi." (Koukl 2001: n.p.). Sababu ya hili ni kwamba "Ile maana inayozungumziwa katika kifungu kile, ndiyo inayounda mistari, na kuipa maana maalum. . . . Hii inatenda kazi kwa sababu ya kanuni ya msingi inayohusu mawasiliano: Maana siku zote huwa inamiminika kutokea juu kuja chini, kutokea vifungu vikubwa kuja vifungu vidogo zaidi, na siyo kinyume cha hapo" (Ibid.).

(2) Kwa hiyo, maneno yanapaswa kueleweka kwa tafsiri za vifungu ambavyo hutokea; vifungu navyo vinatakiwa kutafsiriwa kulingana na vifungu vinavyovizunguka mbele na nyuma. Mambo haya yote yanahitaji kueleweka kwa uelewa wa lengo au malengo makuu la Sura husika, sehemu zake, na kitabu kwa ujumla.

(3) Hili ni muhimu sana kiasi kwamba ile "sheria ya msingi" ni: "*Kamwe usiusome mstari wa Biblia.* Badala yake, soma kile kifungu chote, angalau. Siku zote hakikisha kinachozungumziwa. Zingatia mtiririko wa mawazo yake. Kisha kazia macho kwenye mstari huo. . . . Ni somo la muhimu kuliko yote la utendaji nililowahi kujifunza . . . na kitu kimoja pekee niwezacho kukufundisha" (Ibid.).

6. Tafsiri lazima iendane na vipengele vya maandishi na aina ya mkondo wa kifungu

a. *"Aina ya mkondo" ni mweleko unaojitokeza`au mtindo wa uandishi maalum wa kitabu au kazi. Hutambulika kwa aina maalum ya utaratibu au mfumo (mtindo, ladha yake, mtindo wa maneno yanavyotumiwa, yaliyomo, nk).* Biblia ina aina nyingi za kujieleza (k.m, historia, mashairi, mithali, unabii, kauli, nyaraka [barua], hekima, fasihi, historia ya vizazi , Ufuuliopo). Kila aina ya mkondo wa uandishi una makubaliano yake. Kwa hiyo, kulitafsiri shairi, kama kwa sheria za ushairi za kawaida, kunaweza kukaleta kosa kubwa la kimaandiko.

b. *Waandishi wa Biblia pia hutumia mara nyingi lugha za mbinu mbali mbali (k.m, sitiari, mlinganisho, makadirio, lahaja, au nahau, lugha ya kufananishia kitu fulani, kutia chumvi katika maelezo, kejeli au kinyume).* Kutoka na hayo, mtu ni lazima awe anajua aina mbali mbali za mitindo ya uandishi wa Ki-Biblia, na atumie ufahamu katika kuyaendea maandiko na kutafsiri.

7. <u>Tambua kusudi la mwandishi na ujumuishe wazo kuu la kitabu hicho, imla yake, na kifungu hicho.</u> Kabla hujakazia macho kwenye kifungu kimoja au mstari, unahitaji kuelewa jinsi kifungu hicho kinavyoendana na wazo kuu la kitabu hicho kiujumla na mwenendo wa kitabu hicho ambacho linatokea. Kumbuka: Jumuisho la maana ya maneno yote na mistari. Kule kuweza kulieleza kikamilifu wazo kuu kwa maneno Yak mwenyewe kutakusaidia kukielewa. Kutokuweza kuliona wazo kuu kunaonyesha kwamba bado hujakielewa, na hii inaonyesha kuwa unahitaji kukisoma, kujifunza, kupata picha kutoka kitabu hicho, sehemu yake, au kifungu hicho zaidi. *Kufupisha kitabu, sura, au kifungu ni zana inayosaidia sana kuelewa mtiririko wa mawazo na maana.*

8. <u>Maelezo yanavyotofautiana na Maelekezo.</u> *Maelezo* ni mfano au kauli au taarifa kumhusu mtu fulani, kitu, au tukio lililotokea. *Maelekezo* ni agizo (ni "elekezo") linalotuagiza nini tunatakiwa kufanya au jinsi tunavyotakiwa kuishi. Mifano ya Ki-Biblia kikawaida *haiagizi* kama amri, mpaka iwe inaambatana na agizo au amri fulani. Kosa la kawaida ni kugeuza maelezo kuwa maelekezo, au kudai kwamba mfano wa Ki-Biblia au utaratibu fulani uliofanyika ni lazima ufuatwe kwa ajili ya kanisa la leo.

9. <u>Fasihi ya Kimaandiko na uelewa sahihi wa kifungu chochote cha Biblia unategemea vipengele vitatu vilivyomo—uchunguzi; tafsiri; na matumizi.</u> Uchunguzi, tafsiri, na matumizi yanatazamwa kama sehemu tatu muhimu za Fasihi ya Kimaandiko. Uchunguzi ni *mtazamo kabla* ya tafsiri na matumizi; hata hivyo, kiutendaji vipengele hivi vitatu huingiliana kwa kiwango kikubwa.

a. *Uchunguzi hutoa majibu ya swali "Je kifungu hiki kinasemaje?"* Uchunguzi ni msingi ambao ni lazima uuweke kwanza ikiwa unataka kutafsiri kwa usahihi na kuitumia Biblia. *Tafsiri sahihi na matumizi hutegemea uchunguzi sahihi.*

b. *Tafsiri sahihi hujibu swali "Je kifungu hiki kinamaanisha nini?"* Tafsiri ya kutosha itakuwa ni dhahiri na itatosheleza mtiririko wa kiasili ikiwa mtu *atachunguza* maandishi kuhusu kinachozungumziwa ili kujua *kinachomaanishwa.* Huwezi kuelezea andishi linamaanisha nini mpaka kwanza ulielewe vizuri. Kadiri unavyolielezea andiko, ni lazima uhakikishe kwamba maelezo yanaendana na uchnguzi.

c. *Matumizi yanajibu swali kwamba "Je maana ya kifunu hiki inanihusuje mimi (na kwa wengine) leo?"* Matumizi yake "yatafanyika pale unapokabiliwa na kweli na kutakiwa kutekeleza kiutiifu kabisa kulingana na kweli ile" (Arthur 1994: 11)[1]

## III. <u>Uwakili wa Muda au Wakati</u>

### A. *Wakati ni Uhai.*

"Wakati ni Uhai. Ni maneno yasiyorudi kinyume wala hayawezi kubadilika. Kupoteza muda wako ni kupoteza uhai wako, lakini kuudhibiti muda wako, ni kuyatawala maisha Yak na kupata faida iliyo kubwa zaidi ya maisha." (Lakein 1989: 11)

1. <u>Kila moja duniani anao muda kiwango sawa.</u> Kila mtu anao "muda wote uliopo"—saa 24 kwa siku; saa 168 kwa juma; na saa 8736 kwa mwaka. Jinsi tunavyotumia muda wetu ndivyo tunavyotumia maisha yetu.

2. <u>Muda unakimbia.</u> Biblia inasisitiza jinsi muda wetu ulivyo mchache wa kukaa hapa duniani. Siku zetu hufananishwa na mvuke au pumzi (**Ayu 7:7; Zab 39:5, 11; 144:4; Yak 4:14**); Kama uvuli tu (**Zab 39:5**); kama kivuli kipitacho (**Ayu 8:9; 14:2; Zab 102:11; 109:23; 144:4**); kama ua, au majani yanayonyong'onyea haraka (**Ayu 14:2; Zab 90:5-6; 102:11; 103:15-16; Isa 40:6-8; Yak 1:10-11; 1 Pet 1:24**).

[1] Mafundisho ya kina kuhusuTafsiri ya Biblia yanapatikana kwenye mtandao wa ECLEA: www.eclea.net.

3. Tunaishi katika "siku za mwisho." Yesu anarudi tena duniani. Hakuna anayejua atarudi lini (**Math 24:36, 42; 25:13**). Hata hivyo, tunajua kuwa tayari tuko kwenye "siku za mwisho" (**Mdo 2:15-17; 1 Wakor 10:11; 1 Tim 4:1; Waeb 1:2; Yak 5:3; 1 Pet 1:20; 1 Yoh 2:18**). Siku hizi zitaishia wakati ambapo "hatutegemei kabisa" (**Math 24:36-25:13**).

**B.** ***Wapi na vipi tutaishi milele, hutegemeana na jinsi tunavyoishi na maisha yetu ya sasa.***

1. Ingawaje muda hapa duniani unakimbia, tutaishi milele; ama katika dunia mpya (mbingu) au jehanamu. C.S. Lewis aliliweka namna hii: "Hakuna watu wa *kawaida*. Hujawahi kuongea na mtu asiye lolote. Mataifa, desturi, sanaa, ustaarabu—hivi huharibika, na uhai wao, kwetu sisi ni kama uhai wa jambo dogo linaloudhi; lakini siyo wa uharibifu pale tunapoamua kufanya kazi nayo, kuoa, dharau, ama kujinufaisha kwayo—kusababisha vitisho vya uharibifu (mambo yasiyokubalika) au burudiko lidumulo fahari ya kudumu." (Lewis 1980: 19)

2. Sisi sote tunakabiliwa na hukumu ya Mungu juu ya maisha yetu tutakapokufa (**Math 10:15; Waeb 9:27; 1 Yoh 4:17**).

a. Wokovu wetu unategemea uhusiano wetu na Yesu Kristo (**Yoh 3:16, 36; 1 Yoh 5:11-12**).

b. Mungu atatuhukumu na kutupa thawabu, iwe ni kwa mema au kwa mabaya, kulingana na kile tulichokifanya au kutokufanya wakati tunaishi duniani (**Math 16:27; Rum 2:5-10; 1 Wakor 3:12-15; 2 Wakor 5:10; Waef 6:8; Wakol 3:23-25; Ufu 2:23; 20:11-15**).

3. Kwa vile wakati katika dunia hii ni mfupi, kwa vile tutakwenda kuhukumiwa kulingana na Mdo yetu, na kwa vile Mdo yetu yanaathiri jinsi tutakavyoishi milele ijayo, Biblia inatuambia "tuukomboe wakati wetu" sasa.

a. ***Waef 5:15-16*** *panatuambia, "[15] Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; [16] mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu.* [kimsingi, *mkiukomboa wakati*], *kwa maana hizi ni siku za uovu."* **Wakol 4:5** pia husema, *"Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati* [kiuhalisia, *kuukomboa muda*]*."*

b. *Neno la Kiyunani katika mistari hii ni exagorazō ambalo "kiujumla linamaanisha kununua, kununua kila kilichopo mahali popote uwezapo, na kutoruhusu muda wowote unaofaa kupotea bila kutumika, bali kuudaka na kuumiliki kama wa kwako."* (Zodhiates 1993: 597). Ni neno hilo hilo lililotumiwa katika **Wagal 3:13** na **4:5** pakizungumzia Kristo kutukomboa sisi kutokana na dhambi na mauti. Kwa hiyo panaonyesha umuhimu mkubwa wa kuutumia wakati wetu kwa busara (ona pia **Rum 13:11; 1 Wakor 7:29; 2 Wakor 6:2; 1 Tim 6:18-19; 1 Pet 1:17; 4:1-3, 7**).

**C.** ***Kanuni za msingi za kusimamia muda***

"Kupata mafanikio hakukufanti uweze kuusimamia muda wako vizuri; bali kuutumia muda vizuri kunakufanya mwenye mafanikiol."

"Swala si 'Ni muda gani nimebakiza?' bali 'Ninafanya nini na muda niliobakiwa nao?'"

1. Kuukomboa wakati wetu na kuutumia kwa busara kwa kiwango kikubwa kunahusiana na kupangilia na kusimamia kwa dhati vipaumbele tuviwekavyo kuhusu matumizi ya wakati wetu. Wasimamizi wazuri wa muda hujua kwamba tatizo la jinsi tunavyoweza kufanya kile tunachopaswa kufanya kwa wakati uliopo kwetu "linazama zaidi ya upungufu wa muda; kimsingi ni tatizo la mipangilio ya vipaumbele" (Hummel 1967: 4). Hatupaswi kutumia muda mwingi kwa ajili ya mambo madogo madogo.

a. *Kulingana na mahitaji yetu ya msingi maishani, tunahitaji kujiuliza wenyewe maswali ya msingi kama vile:* (1) Ni kitu gani kimoja ningekifanya, kama ningelikifanya mara kwa mara, kingeleta badiliko kubwa katika maisha maisha yangu binafsi? (2) Ni kitu gani katika huduma yangu mwenyewe, biashara, au taaluma yangu ambacho kingeleta matokeo hayo hayo? (3) Ni kitu gani katika maisha yangu ya kiroho kingeleta matokeo hayo hayo? (4) Je natakiwa nianze kufanya nini kuhusiana na mazoea yangu ya zamani, mazingira niliyo nayo, na mategemeo ya baadaye na ndoto? (5) Je natakiwa niache nini kuhusiana na mazoea yangu ya zamani, mazingira niliyo nayo, na mategemeo ya baadaye na ndoto?

b. *Kuhusiana na shughuli zetu zozote, tunahitaji kujiuliza maswali kama vile:* (1) Kwa nini ninafanya hili? Lengo ni nini? (2) Nini kitatokea kama nitaamua kutolifanya hili? (3) Hivi ni jambo sahihi la kifanya? [Kazia kufanya mambo yaliyo sahihi kikamilifu ] (4) Ni nini jambo la busara kwangu kufanya kuhusiana na mazoea yangu ya zamani, mazingira niliyo nayo, na

mategemeo ya baadaye na ndoto?

2. Ni lazima TUPANGE jinsi tutakavyotumia muda wetu ("kushindwa kupanga ni kupanga kushindwa").

a. *Anza ukiwazia mwisho wake.* "Kuanza ukiwa na mawazo juu ya mwisho wake maana yake anza ukiwa na uelewa kamili wa hatima yake. Ni kujua unakwenda wapi ili ujue vizuri zaidi sasa uko wapi na hatua unazozichukua siku zote zinakuwa katika uelekeo unaostahili. . . . Kila sehemu ya maisha Yak—tabia Yak ya leo,, tabia ya kesho, tabia ya siku zijazo, tabia ya mwezi ujao—inaweza ikaangaliwa katika dhana nzima, ya nini ambacho unakiona kuwa cha muhimu zaidi kwako, kipi ambacho unakijali zaidi. Kwa kuzingatia hatima hiyo, unaweza kuwa na uhakika kwamba lolote ulifanyalo siku yoyote ile, halipingani na vigezo fulani muhimu ulivyojiwekea kuwa ndivyo vya muhimu mkubwa, na kwamba kila siku ya maisha Yak inachangia kwa namna ambayo ni ya maana kuelekea kwenye maono uliyo nayo maishani mwako kiujumla. . . . Ni rahisi mno kushikika kwenye mtego wa shughuli,katika pilika-pilika za maisha, ukifanya juhudi nyingi ili kupanda ngazi ya kimafanikio, na kuja kugundua kumbe inaegemea kwenye ukuta ambao si sahihi. Inawezekana kuwa na pilika pilika—kuwa na pilikapilika sana—lakini utendaji ukawa haufai. . . . Ni tofauti kiasi gani maisha yetu yanakuwa pale tunapojua lipi ni la muhimu mno kwetu, na, tukiwa na picha hiyo kichwani, tunajisimamia vizuri kila siku ili kuwa, na kufanya kile chenye umuhimu mzito zaidi." (Covey 1989: 98)

b. *Fanya la kwanza kuwa la kwanza—pangilia na kuzingatia vipaumbele.* "Dhana ya usimamizi mzuri na mahili wa muda na maisha ni kujizatiti kuzingatia maswala yanayowiana ya vipaumbele . . . . Nauliza swali hili: kama ungejikuta katika kosa mojawapo ya maeneo haya matatu, ambayo yangekuwa: (1) kukosa uwezo wa kupanga vipaumbele; (2) kukosa uwezo au shauku ya kupangilia mambo kuzungikia vipaumbele hivyo; au (3) kukosekana nidhamu ya utekelezaji kuhusiana na hayo, kubakia na vipaumbele vyako na mpangilio wako?

Watu wengi wanasema kwamba kosa lao ni kukosa nidhamu. Nikifikiria zaidi, naamini hivyo sivyo ilivyo. Tatizo la msingi ni kuwa vipaumbele vyao havijaoteshwa kwa dhati mioyoni mwao na akilini mwao." (Covey 1989: 157-58)

c. *Upangaji mipango lazima ufanyike kimsingi angalau kila juma (kwa kiwango kikubwa zaidi), pia kila siku.*

(1) Njia bora zaidi ya kupangilia maisha Yak ili kudumisha mambo yale ya kwanza kuwa ya kwanza, na kuhakikisha kwamba unatumia muda wa kutosha kutekeleza vipaumbele vyako, ni kuwa na mipango ya muda mrefu zaidi pamoja na kuwa na mipango ya muda mfupi kwa matumizi ya muda wako. Kujua nini unataka kukamilisha kwa mwaka, au mwezi, au muhula wa shule, au kipindi kingine kikubwa cha muda kunatusaidia tulenge kwenye mambo muhimu.

(2) Ufunguo kwa usimamizi wenye manufaa wa muda ni kupangilia maisha Yak kwa msingi wa kila juma. "Unaweza pia kujipanga na kuweka vipaumbele kwa msingi wa kila siku, lakini msukumo wa kuegemea zaidi ni mpangilio wa juma zima. Kupangilia kwa msingi wa juma zima hutoa uwiano mkubwa zaidi na dhana zaidi kuliko wa mpango wa kila siku. Kunaonekana kuna mwelekeo wa kidesturi wa kulitambua juma kama kipimo kimoja, kilichotimilika cha muda. Biashara, elimu, na mitazamo mingine mingi ya jamii hutenda kazi kwa mipango ya juma, kuzipangia siku fulani kuwa rasmi kwa uwekezaji , na nyingine kwa kupumzika au kuvuviwa . . . . Watu wengi hufikiri kwa mwelekeo wa majuma. . . . Wakati [mipango ya kila siku]inaweza ikakusaidia kupangilia kipaumbele cha shughuli zako, kimsingi zinakusaidia kupangilia msongamano au kazi nyingi zikitokea. Ufunguo si kuweka vipaumbele yale yaliyo kwenye ratiba zako, bali kupangilia vipaumbele vyako. Na hili linaweza kufanywa kiubora kabisa lilifanywa kimpangilio wa juma." (Covey 1989: 161)

(3) Kumbuka: Siku zote unaweza kubadili mpango wako, lakini ni mpaka uwe nao kwanza.

3. Ni lazima tutofautishe kati ya YA MUHIMU na DHARURA, na tutumie muda mwingi zaidi kwa mambo yale ambayo ni MUHIMU.

a. *Hatari kubwa katika kusimamia muda ni kuruhusu mambo ya dharura, yaongezeke na kuyazidi mambo muhimu.* "Tunaishi katika mvutano mkubwa kati ya mambo ya dharura, na ya muhimu. Tatizo ni kwamba, jukumu la muhimu ni lazima lifanyike leo, au hata wiki hii. . . . lakini kazi za dharura zinatutaka tuzifanye sasa hivi—na uhitaji usiokoma hutubana kila saa na

kila siku. . . . Visingizio vya kitambo vya majukumu haya huonekana kutozuilika na na huwa ya muhimu, na kutuchukulia nguvu zetu. Lakini kwa mtazamo kuhusu msimamo wa wakati, udanganyifu wake unaojitokeza hufifia; pamoja na hisia ya hasara twakumbuka majukumu muhimu tuliyoyasukuma pembeni. Tunatambua tumekuwa watumwa wa mtego (au jaribio ) wa dharura." (Hummel 1967: 4-5).

b. *Kanuni zifuatazo zinasaidia kutofautisha mambo ya dharura kutoka mambo ya muhimu:*

(1) Dharura au haraka huendana na uelewa wetu wa muda:, wakati umuhimu huendana na thamani au ubora. "*Dharura* maana yake kinahitaji kushughulikiwa haraka. Ni cha 'Sasa!' Mambo ya dharura hutuparamia. Simu inayolia ni kitu cha haraka.Watu wengi hawawezi kulipokea wazo la kuiacha tu simu iwe inaita . . . . Vitu vya dharura kikawaida huonekana kwa macho. Huwa vinatukandamiza; vinasisitiza kufanyiwa kazi. Mara nyingi huwa vinajulikana na watu wengine. Mara nyingi huwa vimetukabili mbele yetu. Na mara nyingi huvutia, rahisi, vinapendeza kuvifanya. Lakini mara nyingi si vya muhimu!

*Umuhimu,* kwa upande mwingine, huhusiana na matokeo. Kama kitu ni cha muhimu, kinachangia kwenye huduma Yak, uthamani wako, vipaumbele vyako vya juu." (Covey 1989: 150-51)

(2) kutendea kazi; tofauti na: Kuonyesha mwitikio. "Lazima tuonyeshe mwitikio kwa maswala ya dharura. Maswala muhimu ambayo si ya dharura huhitaji kujituma zaidi, utendaji zaidi. Lazima tutende ili tuinyakue nafasi au fursa, ili kufanya mambo yatokee. . . . Ikiwa hatuna wazo lililo wazi kuhusu kipi ni cha muhimu, cha matokeo ambayo tunayataka msishani, tunapotoshwa kiurahisi sana kuelekea kuhusika na yale ya dharura." (Covey 1989: 151)

4. JEDWALI LA USIMAMIZI WA MUDA (Covey 1989: 151):

| | **DHARURA** | **SI YA DHARURA** |
|---|---|---|
| **MUHIMU** | **I**<br>Majanga<br>Matatizo shinikizi<br>Jukumu lenye masharti ya muda | **II**<br>Mipango; kujenga mahusiano<br>Kuweka malengo na mipango<br>Kuzuia matatizo<br>Kutambua fursa mpya<br>Shuguli za ukarabati, mapumziko |
| **SI MUHIMU** | **III**<br>Muingiliano wa matukio;<br>Baadhi ya simu,<br>Baadhi ya barua; baadhi ya vikao,<br>Mashinikizo<br>Shughuli zilizozoeleka | **IV**<br>Upuuzi, kazi nyingi; baadhi ya barua,<br>Baadhi ya simu;<br>Shughuli zinazopendeza;<br>Vipoteza muda |

5. Kuelewa na kutekeleza Jedwali la Usimamizi wa Muda:

a. *Watu wote huelewa kwamba* ***Kifungu I*** *ni cha muhimu zaidi,* ***Kifungu IV*** *ni cha umuhimu mdogo zaidi.* Hata hivyo, watu wengi kimakosahukazia **Kifungu III** kama kipaumbele kifuatacho baada ya kushughulika na **Kifungu I**. Hilo ni kosa.

b. *Ufunguo kwa usimamizi wenye kufaa wa muda ni kuzidisha muda wako kwenye shughuli za* ***Kifungu II***. Kwa kufanya hivyo kiuhalisi utakuwa unapunguza ukubwa wa **Kifungu I** kwa kuzuia hali ya hatari, na matatizo kutokea. Zaidi ya hapo, kibano kikubwa hutokana na kuchelewa na kungojea mpaka muda kufikia mwisho ndipo kazi za miradi huanza. Kwa kuusimamia muda vizuri, na kumaliza miradi kabla ya muda kufikia mwisho, utaondokana na mikandamizo mingi maishani mwako.

c. *Stephen Covey, ambaye alitengeneza Jedwali la Usimamizi wa Muda, analielezea:*
"Kifungu I ni yote mawili dharura na muhimu. Kinashughulikia matokeo ya muhimu yanayohitaji kuhudumiwa haraka. Kikawaida tunaziita shughuli za Kifungu I 'hali ya hatari' au 'matatizo.' Sote tuna shughuli za fungu katika maisha yetu. Lakini Kifungu I huwashika watu wengi. Wapo wasimamizi wa hali za hatari, watu wenye mtazamo wa ki-matatizo, wazalishaji wanaoongozwa na muda wa mwisho.

Kadri unavyokazia Kifungu I, kinaendelea kuwa kikubwa zaidi na zaidi mpaka kinakutawala. . . . Baadhi ya watu kimsingi wamepigika na matatizo siku nzima kila siku

Ahueni pekee wanakuwa nayo wakati wanakwepea kwenye yale mambo yasiyo ya muhimu, yale yasiyo ya dharura ya Kifungu IV. Kwa hiyo unapoangalia jumla ya jedwali hilo, asilimia 90 ya muda wao uko kwenye Kifungu I na sehemu kubwa iliyobakia asilimia 10 iko Kifungu IV, kukiwa na mkazo mdogo sana kwa Kifungu II na III. Hivyo ndivyo watu wanaosimamia muda wao kwa hali ya hatari wanavyoishi.

Wako watu wengine wanaotumia muda wao mwingi kwenye 'dharura, lakini siyo katika ya muhimu' Kifungu cha II, twakidhania wako Kifungu I. Huutumia muda wao mwingi wakionyesha mwitikio wa kushughulikia mambo ambayo ni ya dharura, wakidhania kuwa ni ya muhimu. Lakini kiuhalisi ni kuwa udharura wa mambo hahyo mara zote hutokana na vipaumbele na matarajio ya watu wengine.

Watu wanaotumia muda kikamilifu kwenye Kifungu III na IV kimsingi huishi maisha ya kutowajibika.

Watu wenye utendaji mzuri hawawi kwenye Kifungu III and IV kwa sababu, iwe ni dharura au hapana, kwao hayo sio muhimu. Pia huminya ukubwa wa Kifungu I kwa kutumia muda mwingi kwenye Kifungu II.

Kifungu II ni moyo wa kujisimamia mwenyewe kwenye ufanisi. Hushughulikia mambo ambayo siyo ya dharura, bali ni ya muhimu. Hushughulikia mambo kama kujenga mahusiano, kuandika tamko rasmi la utume wako binafsi, kupanga mipango ya muda mrefu, kutekeleza, matengenezo ya kukinga, maandalizi—mambo hayo yote tunajua tunahitaji kuyafanya, lakini ni mara chache tunajikuta tunayafanya, kwa sababu siyo ya dharurat." (Covey 1989: 152-54)

d. *Kumbuka ile sheria ya 80/20:* Karibu 20% ya mambo tunayoyafanya yana uthamani wa karibu 80%. Thayo ndiyo mambo muhimu. Kwa hiyo, tunatakiwa kukazia muda wetu na nguvu zetu kwenye hiyo 20%.

**D.** ***Kukabidhi madaraka na majukum***

1. <u>Hakuna mtu yeyote kwenye nafasi ya uongozi ana, ama muda au uwezo wa kufanya kila kitu peke yake.</u> Kwa hiyo, ili shirika lolote liweze kwenda vizuri—iwe ni kanisa, biashara au kazi, au nyumba—majukumu na kazi za miradi lazima zikabidhiwe kwa wengine kuzifanya.

2. <u>Waajiriwa wengi au watu walio kwenye nafasi za chini hutaka majukumu yaje kwao, ili waweze kuthibisha jinsi walivyo na uwezo mzuri.</u> Bahati mbaya, viongozi wengi ni si watoa madaraka wazuri: hawatoi kazi zinazoeleweka vizuri au zenye maana; wanasema wanakabidhi kazi fulani, lakini hujaribu "kuipangilia kinamna" kazi nzima; au huwa hawatoi rasilimali zitakiwazo kumwezesha mtu ambaye kazi imekabidhiwa kwake ili aweze kuifanya vizuri.

3. <u>Ziko kanuni za msingi za "kukabidhi uwakili" ambazo zitaletesha kukabidhi kazi na madaraka kwa wengine.</u> "Kukabidhi uwakili kunakazia matokeo badala ya mbinu au njia. Huwapa watu uchaguzi wa njia na kuwafanya wawajibike na matokeo" (Covey 1989: 173-74). Kuwa mtendaji wa kufaa, kukabidhi uwakili kunahitaji uelewa wa wazi, na ulio mbele kabisa wa kimanufaa na kukubaliana katika maeneo manne:

a. *Matokeo yatamaniwayo.* "Umba maelewano yaliyo wazi na ya kunufaisha ya kile kinachotakiwa kukamilishwa, kwa kuzingatia matokeo gani, na siyo jinsi wala mbinu za matokeo" (Covey 1989: 174). Eleza kiufasaha matarajio Yak. Unahitajika kumpa mtu unayempa majukumu kazi maalum,na onyesha tarehe maalum na wakati ambapo inatakiwa kukamilishwa. Ufasaha unatiwa nguvu kwa kuweka jambo katika maandishi. Tumia muda, uwe mvumilivu, na ujibu maswali yote vizuri. Kama unakabidhi kazi mbali mbali kwa wakati moja, mweleze huyo mtu umuhimu wa kila kazi. Kamwe usichukulie kivyepesi kuhusiana na kupanga malengo. Kukabidhi kiholela ni sababu mojawapo ya vyanzo vikubwa vya mafadhaiko.

b. *Maelekezo.* Tambua mipaka au uwezo wa mtu huyo kuweza kutenda kazi yake. Hivi vinapaswa kuwa vichache iwezekanavyo, kwa sababu sababu mojawapo ya kukabidhi ni kwamba wewe, ambaye unayekabidhi kazi au mradi huo, huna haja ya kuendelea "kumsimamia mtu huyo begani" ili kuhakikisha kwamba anaifanya hiyo kazi. Pia, hakikisha unaonyesha maeneo muhimu ambayo huenda mtu huyo atakumbana na matatizo. Wahudumie watu wako vizuri. Kumbuka: Mpe mtu uhuru wa kufanya kazi hiyo kwa njia aionayo inamfaa—unachotaka wewe ni matokeot, siyo kumwambia mtu huyo hatua anazotakiwa kuzifuata ili kupata mafanikio la lengo kuu. Unaweza kushangazwa kwa ubunifu wa mtu huyo uliyekabidhi madaraka kwake.

c. *Rasilimali.* Ni lazima umpatie mtu unayemkabidhi majukumu rasilimali za kutosha ili kazi

ifanyike. Hii nipamoja na kuhakikisha kwamba anao muda wa kutosha, fedha, msaada wa kitaaluma, na mamlaka ya kufanya ili aweze kukamilisha kiufasaha matokeo yanayotarajiwa. Hakikisha unamwonyesha rasilimali za watu, fedha, taaluma, na rasilimali za shirika hilo awezazo kutumia ili aweze kukamilisha kazi hiyo. Kushindwa kumpatia rasilimali za kutosha kuifanya kazi hiyo ni ni sababu nyingine ya mafadhaiko katika kazi zilizokabidhiwa.

d. *Kuwajibika na matokeo yake.* Panga viwango vya utendajiambavyo vitatumika kupimia matokeo, na muda maalum ambao utoaji taarifa na tathmini itafanyika. Elezea kabisa nini kitatokea, kwa yote mazuri na mabaya, kama matokeo ya tathmini hiyo. Pawe na kivutio fulani kwa mtu huyo ambaye unamkabidhi jukumu. Mweleze mtu huyo mapema kwamba utamjulisha mambo atakayofanya, yaliyo mazuri na mabaya. Watu wafanyapo vitu vizuri, uwapongeze mara moja—wajulishe yale mazuri waliyoyafanya, na uyataje kabisa; wafanye wajue jinsi unavyojisikia kuhusu kile walichokifanya na jinsi kilivyo cha muhimu. Watu wafanyapo mambo mabaya, uwakaripie mara moja—waeleze kile walichokikosea, nautaje moja kwa moja; wafanye wajue jinsi unavyojisikia kuhusu kile walichokifanya na jinsi kilivyo cha muhimu. Hata hivyo, usiachie karipio hilo jinsi hiyo tu. Badala yake, baada ya karipio hiloa, uwakumbushe jinsi gani unavyowathamini; wafanye wajue kwamba uko upande wao, hata kama hufurahishwi na utendaji wao katika jambo hilo. Kisha kumbuka, wakati karipio limekwisha, iwe imekwisha. (Blanchard and Johnson 1982: 44, 59)

**E. *Mambo mengine ya kuzingatia kuhusu uwakili wa muda au wakati***

1. <u>Tunahitaji kuzuia “vipoteza muda.”</u> Kipoteza muda ni kitu chochote kinachotuondosha kwenye namna ya kuutumia wakati vizuri—kitu ambacho kinatuvurugia vipaumbele vyetu. Mara nyingi, vipoteza muda huwa ni vitu vizuri tu kwa mtazamo, lakini tunavikalia au hutupeleka kwenye kuzidi. Vile vipoteza muda vya kawaida ni pamoja na:

| | | |
|---|---|---|
| a. Televisheni | c. kuongea na simu | e. “Kushughulika na Internet” |
| b. Michezo na burudani. | d. Kusoma magazeti | f. Kuhangaika au kufikiri |

2. <u>Tumia vipanga muda vya kila siku, au orodha iliyo katika maandishi ilikukusaidia kupanga muda wako.</u>

a. *Saa za ukutani, saa za mkono, kalenda, na ratiba za siku; vyote hutusaidia ili kupangilia na kuitumia siku vizuri zaidi.* Hii ni muhimu kwa vile sisi tu mawakili juu ya muda wetu, na siyo watumwa wake.

b. *Fuatilia muda wako. Watu wengi hawajui jinsi wanavyoutumia muda wao mwingi.* Wanaweza kukosea sana kuhusiana na makadirio ya kiasi cha muda wanaoutumia katika nyanja tofauti katika maisha yao. Mbinu mojawapo ni kufuatilia kiasi gani cha muda unatumia katika kila shughuli, ni kwa kuandika kuandika hilokimaandishi kila baaba ya dakika 30 hivi. Orodhesha kila jambo, kuchanganya na kuongea kwenye simu, kuvinjari ndoto za mchana, kutafuta vitu, kujisomea, kuomba, kuzungumza, nk. Fanya hivyo kwa juma moja. Unaweza ukashangazwa kwa kuona kiasi gani cha muda unakipoteza katika mambo ambayo si ya muhimu. Njia pekee ya kufanya mabadiliko yatakiwayo ili kutumia muda zaidi ukifanya mambo yaliyo muhimu (Kifungu II), ni kwa kujua jinsi unavyoutumia muda wako sasa. Kuandika matumizi ya muda wako si jambo gumu kulifanya. Kimsingi, ni tabia unayoweza kujijengea. Wanasheria na watu wengine walio wataalamu ambao hutoza gharama za huduma zao kwa masaa, hufanya hili mara kwa mara.

3. <u>Lazima ujifunze kusema “hapana” kwa “uhitaji” wa watu kuhusu muda wako.</u> Wachungaji haswa hupaswa kusema “ndiyo” kwa kila hitaji la muda wao. Bahati mbaya, hilo linamaanisha kwamba wachungaji— ambao wana majukumu mengi makubwa—hawawezi tena kujipangia vipaumbele vipasavyo. Hawako tena katika udhibiti wa muda wao, bali wanakuwa watumwa wa vipaumbele vya watu wengine wote. Mengi ya mahitaji hayo si ya msingi. Mara nyingi, muda mwingi wa wachungaji hutumiwa na mambo ambayo si ya muhimu. Zaidi ya hayo, wachungaji wengi wanatakiwa watoe chakula na malazi kwa kila mtu anayewajia—hata kama mchungaji hana chakula cha kutosha, au kitanda kingine, na kanisa likawa halimpatii fedha za ukarimu kukabili gharama za ugeni wa jinsi hiyo. Matokeo ni kuwa, kwa kule kujitolea kwa kila hitaji linalokuja kwake, mchungaji huwa, kiukweli, hafanyi kazi yake mwenyewe vizuri. Anakuwa ana mafadhaiko, na watu watu hawahudumiwi kama inavyopaswa.

a. *Wachungaji, viongozi wa kanisa, na washirika, wanapaswa kulijadili jambo hili muhimu.* Panapaswa pawe na matarajio yal wazi na ya kimsingi kuhusiana na muda wa mchungaji. Watu

wengine katika washirika wanaweza, na wanapaswa wajitolee kiukarimu, zaidi ya mchungaji. Ikiwa kanisa litadai kwamba mchungaji atoe chakula na malazi, kanisa linao uchaguzi wa kutoa pia rasilimali zinazohitajika kufanya hivyo. Ikiwa kanisa linatambua tatizo hilo, kanisa linaweza likajianzishia huduma lenyewe kukidhi haja hizo, na kwa kufanya hivyo, kuupunguza mzigo wa mchungaji.

b. *Swala la kuitikia msukumo wa haja za watu wengine kwenye muda wako ni dhana ya ukipaumbele, ambayo wewe hatimaye utakuja kuwajibishwa.* Covey anataja kuwa, "Simaanishi usijihusishe na miradi au kazi muhimu za kiibada. Mambo hayo ni ya muhimu. Lakini lazima uamue ni nini vipaumbele vyako vya juu kabisa, na uwe na ujasiri—kwa furaha, ukitabasamu, bila kuomba msamaha—kusema 'hapana' kwa mambo mengine. Na niia ya kufanya hivyo, ni kwa kuwa na 'ndiyo' kubwa zaidi ikiungua ndani Yak. Adui wa 'bora kabisa' huwa ni 'inatosha'.

Kumbuka daima unasema 'hapana' kwa kitu fulani. Ikiwa si kwa vitu vionekanavyo kuwa vya haraka na dharura maishani mwako, huenda ni kwa vitu ambavyo ni vya msingi, na vya muhimu sana. Hata kama hicho cha dharura na haraka ni kizuri, huo uzuri unaweza ukakunyima kile bora kabisa, kikakunyima mchango wako wa kipekee, kama utakiruhusu." (Covey 1989: 156-57)

4. <u>Kupangilia muda, zamu za huduma, na kushughulikia mambo yaliyojiingiza.</u>

a. *Unapaswa upangilie muda wako na zamu za huduma kwa kiwango ambacho una uwezo nacho.* Kila moja ana nyakati za siku ambazo akili zao huwa zimechangamka zaidi na kuzaa matunda. Kwa upande mwingine, kila moja ana nyakati ambazo huwa kimsingi huzalisha kidogo sana. Unatakiwa kutumia muda wako bora kabisa kiuzalishaji kukazia kwenye mambo ambayo ni ya muhimu zaidi (Kifungu I na II). Panga zamu ambazo si za muhimu sana, mikutano, nk. Kwenye muda ambao si wa kiuzalishaji sana. Mikutano yenyewe inapaswa iwe na agenda maalum. Mikutano mingi hujiburuta na kupoteza muda kwa sababu agenda haikupangwa na lengo la mkutano halijazingatiwa.

b. *Kama mchungaji, unahitaji muda wa kusoma na maombi usiovurugwa.* Moja ya majukumu muhimu ya mchungaji ni kufundisha na kuhubiri Neno la Mungu (ona k.m., **1 Tim 4:11, 13, 16; 5:17; 6:2**). Ili kufanya hilo vizuri, ni LAZIMA uwe na muda wa kutosha katika juma kuutumia kusoma na kujifunza Biblia, kuomba, na kuhubiri ujumbe wako. Kwa hiyo, unahitaji kipindi, au vipindi virefu vya muda kila juma vilivyopangwa kwa ajili ya maombi na kujisomea Biblia. Watu wako wanatakiwa wajue hilo. Wanatakiwa wajue kwamba hawapaswi kukuvuruga wewe, isipokuwa kwa dharura ijitokezapo. Unatakiwa ufanye kila liwezekanalo kupanga zamu za kuongea na watu. Ikiwa mtu fulani anakuja kwako na haja ambayo siyo ya dharura wakati wako wa kusoma, unapaswa uweze—kiungwana tu na kiheshima, lakini si kikuomba msamaha—umpangie muda mwingine wa kuongea naye. Huduma Yak itakuwa bora zaidi kama utafanya hivyo, na watu wako watahudumiwa vizuri zaidi. Nao wakielewa hilo, watalipenda sana hili, nao hawatakwazika pale utakapowajibu kwamba hutaweza kukutana nao nyakati fulani.

c. *Kushughulika na mambo yanayoingilia. Imambo yanayoingilia hayazuiliki.* Watu hupenda kusimama na kuongea nawe. Kudumisha uhusiano mzuri na watu ni muhimu Hata hivyo, Wakati mwingine huwa unaingiliwa kati wakati uko kati-kati kabisa ya kitu muhimu sana. Katika hali kama hiyo, unaweza kusema kitu kama hiki: "Niko kati-kati ya kitu muhimu sana hivi sasa. Je waweza kurudi baada ya saa moja (au mchana huu; ama tunaweza kupanga muda mwingine juma hili tutakapokutanika pasipo kuingiliwa chochote)?" Au, fikiria kusema kitu kama: "Niko kati-kati ya kitu muhimu sana hivi sasa. Lakini naweza kukupa dakika 5." Zikiisha hizo dakika 5, waweza kumwambia huyo mtu, "kama nilivyosema, nilikuwa na dakika 5 tu sasa, kwa hiyo tunaweza kuendeleza hili baadaye tutakapokuwa hatuna mwingiliano." Kisha mnaweza mkapanga kipindi kingine, na kumwelekeza mtu huyo mlangoni. Kwa upande mwingine, kwa kusemaunazo dakika 5 tu kunakupatia fursa ya kuongeza muda kama unataka. Ikiwa unaingiliwa kati kati-kati ya kitu muhimu, hata hivyo, itakuwa juu Yak—si juu ya huyo mtu aliyeingilia kati—kama utaongea na huyo mtu, na, kama ndivyo, kwa muda gani.

5. <u>Orodha ya "kufanya" na ucheleweshaji.</u>

a. *Orodha ifanywe kwa kupangilia vipaumbele.* Kuviweka vitu katika mafungu madogo madogo, kwenye hatua zinazotekelezeka. Jaribu kufanya sehemu ya kazi ambayo haipendezi zaidi na ile ambayo inapingana kwanza. Ukishughulikia sehemu iliyo mbaya kwanza kutakuweka huru kutoka msongamano mwingi ambao vinginevyo ungekuwa unakubana

kichwani kwako, na kufanya kazi nzima kuonekana kwenda vizuri.

b. *Ucheleweshaji.* Kila moja huzembea kwenye mambo fulani. Hata hivyo, imesemekana kiukweli kwamba "uzembe au ucheleweshaji ni wizi wa muda." Uzembe huongeza viwango vyetu vya mikandamizo tunapoacha kufanya mambo ya muhimu mpaka dakika za mwisho. Kwa hiyo, tunatakiwa kuelewa kwa nini hatuna bidii kuhusiana na kufanya kazi fulani. Inawezekana kwamba tukishaitambua sababu ya uzembe wetu, kizuizi cha kuzuia kazi isifanyike kitaondoka. Kwa upande mwingine, kutambua chanzo cha tatizo letu kunaweza kutuonyesha uhitaji wa kutafuta msaada wa mtu mwingine, au kunaweza hata kutuongoza kuikabidhi kazi hiyo kwa mtu mwingine (lakini kama tutafanya hivyo, ni lazima tuwe na hakika kufuata kanuni za uwakili mzuri wa kukabidhi madataka).

6. Nyongeza ndogo-ndogo za muda mara kwa mara kwa ajili ya kazi husika mara nyingi huwa zinazalisha zaidi kuliko vipindi vikubwa vya shughuli ambavyo hutokea mara chache. Kujenga na kudumisha mahusiano mazuri kati ya watu, mazoezi ya mwili, kujifunza lugha ya kigeni, kujifunza kupiga chombo cha muziki, ama kujifunza kitu chochote kipya, hayo yote huhitaji kutenga muda fulani mara kwa mara (kimsingi, ni kila siku) kwenye hiyo shughuli. Kufanya hivyo, kutakuwa na matunda zaidi kuliko kufanya zig-zag au kugusa kwa mara moja- moja kwa kipindi kirefu hilo jambo. Kipindi hicho kikubwa cha muda hakiwezi kuwa mbadala wa shughuli ya mara kwa mara. Kanuni ya kurudia kitu kwa mara hufanya kazi sehemu nyingi za maisha. Hiyo ndiyo sababu kwa nini ni lazima tudhibiti muda wetu, kuliko kuacha muda wetu uangukie kwenye mwanya wa "kuonewa na dharura" na kwenye agenda za watu wengine.

7. Kumbuka muda wetu wote ni wa muhimu. Mara nyingi hatutambui *kwa wakati huo* umuhimu wa kile tufanyacho (au tunapaswa tuwe tunafanya nini). Mara nyingi huwa hatutambui mpaka baadaye (baada ya kuona kumbe haiwezekani tena kubadilisha mambo, au kutenda kile ambacho tulitakiwa kukifanya), umuhimu wa wakati tuliokuwa nao, au fursa ambayo tulishindwa kuitumia vizuri. Kumbuka hata kikombe cha maji kitolewacho kwa mtu fulani kinaweza kuwa muhimu, na hakisahauliki na baba yetu wa mbinguni (**Math 10:42**). Kwa hiyo, wakati au muda ni wa "thamani." Huwezi kuurudisha tena nyuma ukishapotea. Ni uwakili wa umuhimu mkubwa sana.

## IV. Uwakili wa Mwili

### A. *Miili yetu ni ya muhimu na ni zawadi ya ajabu kutoka kwa Mungu.*

1. Tumeumbwa na Mungu.

a. Kitu cha kwanza ambacho Maandiko yanatuambia kutuhusu ni kwamba sisi tu *viumbe, tulioumbwa na Mungu* (**Mwa 1:26-27; 2:7, 18-22**).

b. Maandiko pia yanatueleza Mungu siyo alijifanyizia wale watu wa kwanza (Adamu na Hawa), na kisha kutuacha peke yetu. Badala yake, Mungu anamfanya *mtu moja moja kivyake* (**Kut 4:11; Ayu 10:8; 31:15; Zab 100:3; 119:73; 139:13-16; Isa 44:24; Yer 1:4-5; 27:5**).

2. Mungu ameiunda miili yetu Kiustadi.

a. ***Zab 139:13-16*** *inatuambia kwamba Mungu anahusika kikamilifu kuiumba miili yetu:*

> *"13 Kwani wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu;Uliniunga tumboni mwa mama yangu. 14 Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha; Mdo Yak ni ya ajabu,Na nafsi yangu yajua sana.15 Mifupa yangu haikusitirika kwako, nilipoumbwa kwa siri, Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi;16 Macho Yak yaliniona kabla sijakamilika; Chuoni mwako ziliandikwa zote pia Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado."*

b. *Mkono mkuu wa Mungu uko katika kila kipengele cha maisha yetu na miili yetu:*

(1) Husababisha au huzuia kupatikana mimba na kuzaliwa (**Mwa 20:17-18; 30:2; Kut 23:26; Rut 4:13; 1 Sam 5-6, 19-20; Isa 66:9**).

(2) Yeye ndiye anayesimamia matatizo ya uzazi, kwamba kazi zake mwenyewe zitangazwe (**Kut 4:11; Mith 20:12; Mika 4:6; Yoh 9:1-3**).

(3) Yeye ndiye msimamizi wa mwanzo na mwisho wa maisha ya kimwili (**Kum 32:39; 1 Sam 2:6; Ayu 12:9-10; 14:5; Zab 139:16-18; Mhu 8:8; Dan 5:23; Luka 12:16-20; Mdo 17:24-26**).

3. Kwa vile Mungu alituumba sisi, pia hutumiliki.

a. Mungu humiliki ulimwengu (dunia) na vyote vilivyomo (**Ayu 12:7-10;** Zab **24:1; 50:10-12; 104:1-30; Isa 66:1-2a; Math 5:34-35; Mdo 7:49-50**).

b. Kwa vile Mungu alituumba wanadamu, sisi ni mali yake tangu kuzaliwa hadi kufa (**Kum 10:14; Zab 24:1; 50:10-12; 95:6-7; 100:3; Isa 17:7; 29:19; 44:24; 45:9; 64:8; Yer 18:1-10; Eze 24:15-18; Rum 9:20**).
c. Mungu hasa kabisa anawamiliki Wakristo **(Rum 14:7-8; 1 Wakor 6:19-20; 7:23; 1 Pet 1:17-19; 2 Pet 2:1).**

**B. *Miili yetu ni ya kipekee kwa vile tuliumbwa kwa mfano wa Mungu, na miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu.***

1. Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu.

a. *Katika* **Mwa 1:26-27** *Mungu alisema "'Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba."*
b. *Sura iliyo kamili ya Ki-Mungu ambayo ni mng'ao na mwakilishi wa Mungu ni Yesu Kristo.* Maandiko haswa humwita Kristo kama "Sura yake Mungu" (**2 Wakor 4:4; Wakol 1:15**) na "mng'ao wa utukufu wake na "chapa ya nafsi yake" (**Waeb 1:3;** ona pia **Yoh 14:8-9; 2 Wakor 4:6**). Katika Kristo, tunaona "sura ya Mungu" katika ukamilifu wake wote. Na matokeo yake, "Hakuna njia iliyo bora ya kuiona sura ya Mungu kuliko kumtazama Yesu Kristo. Kile tukionacho na kukisikia katika Yesu Kristo, ndicho Mungu alichokikusudia katika mwanadamu." (Hoekema 1986: 22)
c. *Umuhimu wa mwili unaonyeshwa kwa tendo la Uungu kuutwaa mwili na Kufufuka.*

(1) Ule ukweli kwamba Mungu mwenyewe alitwaa mwili katika mwanadamu aitwaye Yesu Kristo, unaonyesha umuhimu wa mwili. Kusema ukweli, katika mpango wa Mungu wa wokovu, hakuweza kuzivumilia dhambi zetu, isipokuwa kwa kuzibeba kwake mwenyewe kimwili msalabani.
(2) Ule ukweli wa kufufuka na kupaa kwake unazidi kuonyesha umuhimu wa mwili katika mpango wa milele wa Mungu. Kristo alisisitiza kwamba, baada ya kufufuka kwake, hakuwa tu roho, lakini alikuwa na mwili halisi (**Luka 24:36-43; Yoh 20:26-29**).
(3) Vivyo hivyo, nasi tutakuwa na miili halisi wakati wa ufufuo (**Rum 8:11; 1 Wakor 15:20-54**). Hatutaishi milele bila miili kule mbinguni, bali tutakuwa na miili mipya, iliyotukuzwa, na kuishi kwenye mbingu mpya, na dunia mpya (**Ufu 21:1-22:5**).

2. Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu.

a. Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu (**1 Wakor 6:19-20;** ona pia **Yoh 14:16-17; 1 Wakor 3:16-17; 2 Wakor 6:16**).
b. Yesu pia aliuzungumzia mwili wake kama hekalu la Mungu (**Yoh 2:19-21**).
c. *Umuhimu wa ukweli kwamba miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu unaonekana, kwa mrandano, kwa matunzo na gharama iliyochukuliwa katika kulitengeneza hekalu katika Agano la Kale* (ona **1 Nya 29:1-9**). Waisraeli wa Agano la Kale walielewa umuhimu wa kulitunza na kulifanya hekalu la kidunia liwe jema na kuu, kwa sababu Mungu alikuwa anakaa humo. Nasi tunapaswa, pia kufanya hivyo.

**C. *Kuna uhusiano wa dhahiri kati ya hali yetu ya kimwili na hali yetu ya kiakili, kihisia, na kiroho.***

1. Sisi *siyo* akili fulani zisizo na mwili au nafsi ambazo zimehifadhiwa katika miili ya kuonekana "kwa kubahatisha." Kiuhakika, kila mtu anazo sehemu hizi; Ile ya kuonekana (mwili) na isiyo ya kuonekana, isiyo na mada (nafsi) ambazo zimeunganishwa pamoja na kufanya, "nafsi kamili." Kama vile Francis Schaeffer alivyosema: "[Mungu] ameufanya mwili wangu na pia nafsi yangu. Amenifanya kama nilivyo, pamoja na njaa za roho yangu na mwili wangu. Na amefanya mambo yote, kama alivyonifanya mimi. Amalifanya jiwe, nyota, na pande za mbali za ulimwengu. Ameyafanya yote haya!

Kuyafikiria yote haya kama katika hali ya upeo wa chini, kiuhalisi ni kumdhalilisha Mungu aliyevifanya. Kwa nini Wakristo wanapoteza njia yao wakati inaonyesha dhairi kabisa? Kwa nini niseme mwili wangu ni duni kuliko nafsi yangu wakati Mungu ndiye aliyefanya vyote, mwili na nafsi?" (Schaeffer 1982, vol. 5: 35)

2. Watu ni yote mawili *wa vipengele vingi na wa kutegemeana kiukamilifu*

a. *Ili kuwa "wa vipengele vingi " maana yake kila mtu ameumbwa na vipengele au sura kadhaa.* Vipengele hivyo vya kila mtu ni pamoja na mwili ulivyo, akili au uelewa wake, hisia,

kijamii, tabia, na kiroho.
b. *Kuwa "wa kutegemeana kiukamilifu" kunamaanisha kwamba mtu hawezi kujigawanyisha kuwa visehemu vya vipengele vyake (yeye si "10% kipengele kimoja, na "20%, kipengele kingine"); badala yake, vipengele vyote vya mtu vimeunganishwa pamoja kumuumba mtu moja kamili.*
c. *Kwa vile sote tuna miili na kufanya kazi chini ya sheria za uumbaji wa asili, hali yetu ya miili huathiri kila kitu kinachotuhusu.* Kule kuwa "wa kutegemeana kiukamilifu" pia kunamaanisha kwamba hali ya miili yetu huathiri vipengele vingine vyote vya miili yetu. Ikiwa miili yetu itaumwa, au kudhoofika, hatuweze kufanya vizuri kiroho, kijamii, kiakili, kitabia, au kiuchumi.

(1) Kwa mfano, shinikizo siku zote hufikiriwa kirahisi kwamba ni hali ya kushuka kihisia. Kusema ukweli, inaweza kusababishwa na kutokuwiana kwa kemikali za mwili katika ubongo, inaweza kuwa ni matokeo pacha ya matumizi ya madawa. Vivyo hivyo, kiharusi au marue rue ya akili huweza kusababishwa na matokeo ya madawa au uvimbe katika ubongo.
(2) *Lishe* ya mtu na kiasi anachokula, *usingizi wake* na *mazoezi ya mwili* anayoyapata; vyote ni vitu muhimu ambavyo vinaweza kuchangia matatizo kwenye maswala mengine ya maisha yake au vinaweza, vikirekebishwa vizuri, kuleta akili njema zaidi au hisia njema zaidi. Uchovu wa kimwili unaweza kutudhoofisha kiakili, na kutufanya tuwe katika hatari zaidi ya kuingia katika majaribu ya kiroho na tamaa nyinginezo.

d. *Vifungu vingi vya Ki-Biblia vinaonyesha uhusiano wa karibu kati ya hali ya miili yetu, na hali zetu za kiroho (ona* ***Math 5:29-30; 6:22-23; Rum 6:12-13; 8:1-14; 1 Wakor 9:27; 2 Wakor 5:10; Waef 5:28-30; Waeb 10:22****).*

(1) Tunapaswa kuikabidhi miili yetu kama dhabihu iliyo hai na takatifu kwa Mungu (**Rum 12:1;** ona **Wafil 1:19-20**). Na matokeo yake, tunapaswa kuikabidhi kwake miili iliyo kamili, misafi, na yenye afya, kama vile dhabihu zile za Agano la Kale zilivyokuwa safi, njema, na zilizokamilika (ona **Law 1:2-3, 10; 3:1, 6; 4:2-4, 22-23, 27-28, 32; 5:17-18; 6:6-7; 22:18-25; Kum 17:1; Mal 1:12-14**).
(2) Miili yetu huweza kubeba chapa za Kristo (ona **2 Wakor 4:7-10; Wagal 6:17**).
(3) Miili yetu huweza pia kuharibiwa, kudharauliwa, na kushushwa thamani na dhambi (ona **Rum 1:21-27; 1 Wakor 6:12-18**).
(4) Kwa sababu ya mahusiano kati ya hali zetu za kiroho na kimwili, ni lazima tuitunze miili yetu ili kuboresha huduma zetu. Wahubiri lazima wailinde miili yao na sauti zao, ili kwamba waweze kuhubiri vizuri. Kama hatuitunzi miili yetu vizuri, tunajipunguzia mategemeo ya maisha, ambayo pia hupunguza urefu wa huduma zetu. Ikiwa miili yetu ni midhaifu, au haiko katika hali nzuri, imechoka, imetiwa sumu kwa chakula kibaya au kinywaji fulani, inaumwa kwa vile hatujaitunza vyema, basi akili zetu hazitakuwa makini tunavyojifunza Neno la Mungu, na hatuwezi kumtumikia Bwana Mungu kwa bidii.

**D.** ***Tunawajibika kwa Mungu kwa uwakili wetu wa miili aliyotupatia.***

1. Yesu alijali hali za kimwili za watu. Aliwapatia chakula kizuri watu wenye njaa. Aliwaponya wagonjwa na kuurudisha uzima wao tena wale waliokuwa wanateseka kutokana na mapungufu au madhara fulani. Alipochoka, alilala usingizi, na utaratibu wa maisha yake ulimfanya awe na mazoezi ya kutosha.
2. Kwa vile Mungu alituumba sisi, na anatumiliki, akatupatia miili, kwa sababu miili yetu ni muhimu na inahusiana moja kwa moja na viumbe vingine, ikiwa ni pamoja na hali za kiroho, tuna uwakili kwa Mungu kulingana na miili yetu. Kama ilivyo uwakili mwingine, tutawajibika kutoa uwakili kwa Mungu kuhusu jinsi tunavyosimamia miili yetu.
3. Uwakili wa miili ni pamoja na kuwasaidia wengine.

a. ***1 Wakor 12:12-27*** *hulifananisha kanisa (mwili wa Kristo) na mwili wa mwanadamu.* Kama vile miili yetu hutenda kazi kwa kushirikiana, na kama tunavyovitunza viungo vyote vya miili yetu pale vinapoumwa au kuumia au kuchoka, ndivyo tuwasaidie watu wengine hasa wanapokuwa wamepatwa na udhaifu kimwili au udhaifu.
b. *Waume haswa wanapaswa kuwasaidia wake zao kwa kazi za mikono, kwa sababu* ***Waef 5:28*** *inasema kwamba "vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe."* Katika mila nyingi, wake hutegemewa kufanya kazi nyingi za mikono kwa ajili ya

familia (k.m., kuokota kuni, kuchota maji, usafi, kupika, pamoja na kuzaa na kuwalea watoto wengi). Hili ni linachosha sana kwenye miili ya wanawake. Ikiwa waume kiukweli *“wakawapenda wake zao kama miili yao wenyewe”* wasingeweza kuwaachia wake zao kufanya kazi zote ngumu. Badala yake, wangepaswa wazifanye baadhi ya kazi hizo wenyewe. Hilo litasaidia kuitunza miili ya wanawake, na kuwezesha kazi kufanyika mapema zaidi, na itatoa fursa ya waume na wake zao kutumia saa ambazo si za kazi pamoja, na kuwa karibu zaidi kimahusiano.

4. Uwakili wa Mwili yanahusisha Mdo ya msingi ya kiafya yafuatayo:

a. Tunapaswa kula chakula cha kufaa na chenye lishe yenye uwiano mzuri. (ona **Waef 5:29**), si cha sukari nyingi, chumvi nyingi, soda, au “chakula cha ovyo ovyo” na dumisha afya ya mwili uwe wa kawaida tu.

b. Tunapaswa tuwe na usingizi wa kutosha, na kufanya mazoezi mara kwa mara (ona **1 Tim 4:8**).

c. Tunapaswa tupime afya zetu mara kwa mara kwa daktari.

d. Tunapaswa tuachane na tabia zisizofaa (k.m, kuvuta sigara, matumizi yanayozidi ya Alkoholi na sukari, kuendesha gari bila kujali usalama wako au bila kuvaa mkanda) ili kijikinga na hatari za dhahiri.

e. Tunapaswa kukoholea au kupigia chafya eneo la chini ya kwapa au kwenye kitambaa kuliko kwenye viganja vyetu au hewani. (Kukoholea au kupigia chafya kwenye viganja kusema ukweli ni njia mojawapo kuu ya kueneza vijidudu kwa sababu vijidudu hivyo husafirishwa kwa mikono yetu kwenda kwa kila mtu na kila kitu tutakachokigusa).

f. Tunapaswa kujikinga wenyewe kutokana na kunguni, chawa, mende, viroboto, na mbu (tumia chandarua).

g. *Kutumia chandarua, nyavu za kuzuia wadudu madirishani ikiwezekana.* Serikali nyingi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, na huduma nyingine hutoa chandarua bure au kwa bei ambayo ni ya chini sana. Mamilioni ya watu hupata Malaria Afrika kila mwaka, na mamia ya maelfu ya watu hufa. Tkutumia chandarua ni nia isiyo na gharama ya kujilinda na ugonjwa huu wa hatari. Kwa kusaidia kuzuia Malaria, kutumia chandarua pia kutaokoa fedha nyingi ambazo vinginevyo zingetumika kwa madaktari na kununulia madawa.

h. *Kuchimba vyoo vya mashimo (na kufunika matundu yake wakati havitumiwi), na hatua kama hizo za usafi na afya.* Kutokuchimba vyoo husababisha kuenea kwa ugonjwa wa Kipindupindu na magonjwa mengine, hasa nyakati za mvua ambapo vyanzo vya maji huchafuliwa. (*Daily Monitor*, June 26, 2008: 12). Kufunika matundu ya vyoo vya mashimo kunazuia mayai ya nzi na wadudu wengine kuanguliwa (kwa vile yanahitaji mwanga ili kuanguliwa, na kufunika matunadu hayo kunazuia mwanga usiingie kwenye mashimo hayo).

i. *Epuka kuvaa nguo zenye unyevunyevu, hasa soksi mbichi.* Kwa kufanya hivi utajiepusha na magonjwa ya fangasi.

j. *Funika chakula.* Wakati unahifadhi chakula au unapoandaa meza, kwa kukifunika, utazuia nzi au wadudu wengine kuleta maambukizi kwenye chakula hicho.

k. *Tunza nidhamu ya ratiba ya chakula.* Ni vema kula kiasi kidogo cha chakula kwa wakati maalum wa chakula, kuliko kula chakula kingi pasipo kuwa na ratiba inayoeleweka (hasa punde kabla ya kwenda kulala). Pai kufunga kula mara kwa mara husaidia kuondoa sumu mwilini.

5. Uwakili wa Mwili pia unahusu Mdoo yafuatayo ya usafi:

a. Tuzitunze nyumba zetu na kaya zetu katika usafi na kupendeza.

b. Tunapaswa kuzitupa taka taka zetu vizuri kama vile kinyesi, mkojo, kutema mate ovyo, nk.

c. Tutunze vitanda viwe visafi.

d. *Tunapaswa kujiweka katika hali ya usafi mara kwa mara (k.m, kuoga, kupiga mswaki, kutunza nywele, mikono na kucha [hasa Afrika na India ambapo watu walio wengi hutumia mikono badala ya vijiko kulia chakula]).* Kusema ukweli, wale wadhamini wa “Global Handwashing Day (yaani Siku ya Dunia ya Kunawa Mikono)” wanasema kwamba: “Kuosha mikono ni njia inayofaa na isiyo na gharama kabisa ya kuzuia magonjwa ya kuharisha na magonjwa ya njia ya hewa na upumuaji, ambayo huchukua maisha ya mamilioni ya watoto katika nchi zinazoendelea kila mwaka. Kwa pamoja, yanahusika na vifo vya watoto walio wengi. . . . Changamoto iliyopo ni kuibadilisha kutoka tukio tu la kunawa kwa sabuni; kulifanya kuwa tabia na mwenendo wa kawaida majumbani, shuleni, na jumuiya mbali mbali duniani. Kugeuza kutoka kunawa mikono kwa sabuni tu kabla ya kula na baada yake; na tabia ya

kujisaidia chooni kukiwa ni tabia iliyozoeleka; kunaweza kuokoa maisha mengi zaidi kuliko sindano za kinga yoyote au huduma ya kiafya itolewayo, na kuzuia vifo vya magonjwa ya kuharisha kwa karibu nusu na vifo vitokanavyo na magonjwa ya hewa na mapafu kwa karibu robo nzima." (Global 2008: n.p.)

6. Uwakili wa Mwili pia unahusisha usafi wa maswala ya tendo la ndoa.

a. *Kulingana na Biblia, mahusiano ya kindoa (ngono) yanapaswa kufanyika tu katika mtazamo wa mahusiano ya kudumu (m.y. maisha yote), ambayo ni ndoa ya mke moja* (ona **Mwa 2:24; Math 19:4-6; 1 Wakor 7:1-2, 8-14, 36; 1 Tim 3:2; 5:9, 11, 14; Tito 1:6 Waeb 13:4).** Maadili ya Kibiblia kuhusu tendo la ndoa ni kwamba "uhuru wa tendo la ndoa ndani ya ndoa, kutokufanyika kwa tendo la ndoa nje ya ndoa." Biblia inakataza aina zote za matumizi yasiyofaa ya tendo la ndoa **(1 Wakor 6:18; 2 Wakor 12:21; Wagal 5:19; Waef 5:3; Wakol 3:5; 1 The 4:3-5; Waeb 13:4).** Hilo linahusisha kufanya tendo la ndoa kati ya wasiooana (uasherati) **(Kum 22:13-21; 1 Wakor 7:2; 8-9; 1 Wathes 4:3);** tendo la ndoa la watu walio katika ndoa kwa watu walio nje ya wale walio wanandoa wao (uzinzi) **(Kut 20:14; Law 18:20, 20:10; 1 Wakor 6:9-10; Yak 2:11)**; ukahaba **(Kum 19:29; Kum 23:17-18);** tendo la ndoa kati ya watu wa jinsia moja **(Law 18:22; 20:13; Rum 1:26-27; 1 Wakor 6:9-10)**; ufiraji (**Law 18:6-17; Kum 27:20, 22-23; 1 Wakor 5:1**); ubakaji (**Kum 22: 23-27**); na kulala na wanyama **(Kut 22:19; Law 18:23; 20:15-16; Kum 27:21).**

b. *Katika* ***1 Wakor 6:15-18*** *Paulo anaonya:* [15]*Je! hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha!* [16]*Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, "WALE WAWILI WATAKUWA MWILI MMOJA."* [17]*Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye.* [18]*Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.*

*c. Katika kifungu hicho, Paulo anaonyesha kwamba sisi tu watu tulioundwa katika hali ya kuunganika.* Hatuwezi kufanya kitu chochote kwa miili yetu ambacho hakitazidhuru roho zetu. Hiyo ni kweli kwa watu wote, lakini zaidi sana kwa Wakristo. Sababu ni kwamba sisi tumeunganika na Kristo, kwa vyote viwili kiroho na kimwili. Sisi ni mwili wake—**1 Wakor 12:12-27**, na miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu—**1 Wakor 6:19-20** (ona pia **Yoh 14:16-17; 1 Wakor 3:16-17; 2 Wakor 6:16).** Matokeo yake, tunapojihusisha na Mdo machafu ya uzinzi na uasherati, tunakuwa kama tunamfanya Kristo atende mambo hayo machafu kiuhalisi. Biblia inafananisha zinaa kama kumwacha Mungu na kwenda kuitafuta miungu mingine na kufanya Mdo yaliyo machukizo kwa Mungu (ona **Yer 3:6-10; Eze 16: 15-22; Hos 2:2; 4:12; Yak 4:4; Ufu 2:18-22; 14:8; 17; 1-5; 18:1-3; 19:1-2).** Kwa hiyo, dhambi ya zinaa ina maafa ya kiroho. Kwa upande mwingine, usafi wa tendo la ndoa huacha mlango ulio wazi kwa ushirika na Mungu ambao haujafungwa wala kuchafuliwa na dhambi (ona **Isa 59:2; Mal 2:13-16; 1 Wathes 5:19).**

d. *Kuutunza usafi wa tendo la ndoa ni kitu pekee cha muhimu kuliko vyote wawezavyo kufanya watu ili kuzuia kuambukizwa na kueneza magonjwa ya zinaa (Magonjwa Ya Zinaa), yakiwamo UKIMWI/AIDS (*ona **Mith 3:1-8; 5:1-11; 7:1-27; 1 Wakor 7:34**). Magonjwa Ya Zinaa na UKIMWI/AIDS yamenea sana duniani. Yanavyoenea zaidi, aina mpya ya virusi hujitokeza ambavyo ni sugu kwa tiba zilizopo. Magonjwa Ya Zinaa na UKIMWI/AIDS huweza kuleta maumivu makali, gharama kubwa za matibabu, kutokuzaa, ulemavu, na vifo. Kwa hiyo, kufuata mausia ya Ki-Biblia ya usafi wa tendo la ndoa kwamba, kusiweko na tendo la ndoa nje ya ndoa wala kwa mtu asiyeoa au kuolewa – pia kuna manufaa mazito kwa mwili. Kudumu katika hali ya uaminifu katika ndoa, na kuacha kufanya zinaa nje ya ndoa zetu *ni njia ya msingi* ambayo sisi tunatekeleza uwakili mzuri wa miili yetu.

7. Katika kufanya mambo haya, siyo tu tutasaidia miili yetu kuwa na afya nzuri; lakini tutazuia kuambukizwa au, na kuwaambukiza wanaotuzunguka. Kwa hiyo, kufanya mambo haya ni hatua ya msingi sana ya "kumpenda jirani Yak kama wewe mwenyewe" (**Math 22:39-40**).

## V. Uwakili wa Mahusiano

### A. *Mahusiano ya nipe nikupe dhidi ya mahusiano ya neema*

1. Kwa sababu Kristo ametubadilisha, tabia, mwenendo na Mdo yetu yanapaswa yazidi kuelekea kumfanania Yesu. Wakristo ni "*viumbe vipya"* ndani ya Kristo **(2 Wakor 5:17)** Kamwe tusifuatishe

"*kufanania namna ya dunia hii, bali tugeuzwe kwa kuhuishwa nia zetu*" **(Rum 12:2)** . Sasa hatuongozwi na mwili bali na Roho, hivyo basi tusiishi kwa kuufuata mwili **(Rum 8:12-14)**. Matokeo yake tuuache utu wa kale na kuuvaa utu mpya **(Waef 4:17-24; Wakol 3:10).** Maisha haya huathiri hata tunavyopaswa kufikiri **(Rum 12:16; 1 Wakor 2:16; Wafil 4:8; Wakol 3:12**), sema **(Waef 4:15; Wafil 2:14; Wakol 4:6; Yak 3:1-12; Yuda 16),** na tenda **(Rum 12:9; 13:12-13; 1 Wakor 6:9-20; 2 Wakor 4:2; Wagal 5:16-23: 6:9-10; Waef 1:4; 2:10; 4:1, 25-31; 5:3-5; 18-21; Wafil 1:27; Wakol 10:3:5-9; 4:5; 1 Wathes 2:12; 4:3-7; 4:12; 5:22; 2 Wathes 3:13; 1 Tim 3:1-13; 6:11; 2 Tim 2:20-25; Tito 3:1-11; Yak 1:22; 2;14-26; 4:1-17; 5:9; 3 Yoh 11).**

2. <u>Mpango wa mahusiano wa kiulimwengu ni wa "msingi wa utendaji."</u> Kibali hutokana na *utendaji wako* ("iwapo wewe utafanya wajibu wako, *ndipo* nami nitafanya wajibu wangu")*;* kutoa hutegemea na *kustahili* kunakotokana na *juhudi*; kutenda hufanyika tu pale mtu anapojisikia kuwa *kunapaswa,* au ili kupata kitu kutoka kwa mtu mwingine; msukumo huwa katika msingi wa namna gani mtu *anajisikia.* Mpango wa kiulimwengu uko katika hatima ya kujiathiri mwenyewe, kwa sababu ya:

a. kutokuweza kwangu kukidhi matarajio yasiyo halisi;
b. kutokuwezekana kujua kama mtu mwingine ametekeleza wajibu wake;
c. uelekeo wangu kukazia kwenye madhaifu ya mtu mwingine;
d. kuvunjika moyo kwangu kwa mtu mwingine kunakosababisha kukwama kwa utendaji wangu.

Matokeo, kama ilivyoonyeshwa katika **1 Pet 3:9a**, ni mahusiano ya "ovu-kwa-ovu" na "laumu-kwa - laumu", ambayo hukazia kwenye "*haki zangu*" na "hisia *zangu*." Mahusiano kama hayo hatima yake huishia kushindwa kwa sababu mizizi yake ni kutokusamehe na mioyo migumu, ambamo kukubalika na upendo hutokana na utendaji na pia ni wa kufanyiwa kazi, na ambao mkazo ni kujijali mwenyewe. Wahusika katika mahusiano ya aina hiyo mara zote hujisikia ni lazima "kujiweka sawa" pale panapotokea kuhitilafiana kidogo.

3. <u>Mpango wa Kristo kwa mahusiano ni wa "msingi wa neema."</u> Una msingi katika tabia ya Mungu mwenyewe, mizizi yake ni uumbaji, na huakisi uhusiano wa Kristo na kanisa lake., Mahusiano kwa hiyo msingi wake ni kujitoa mwenyewe kwa ajili ya mahitaji na matakwa mema ya mtu mwingine, na kwa mahusiano yote kiujumla. Msukumo wa kutenda kwa jinsi hii kimsingi hutokana na upendo na shukurani kwa Kristo. Katika mahusianao ya aina hiyo, upendo, kukubalika, na mguso wa kiupendo *hutolewa bure,* siyo kufanyiwa kazi, kwa sababu Kristo alitupenda sisi kwanza na mtu mwingine naye anastahili upendo wa aina hiyo, kukubalika, na mguso wa kiupendo, tu kwa vile yeye ni mtoto wa Mungu na analo sura ya Mungu. Itokeapo mtu mwingine hakidhi matarajio yetu, twaweza, twaweza *kusamehe bure* kwa sababu tulisamehewa na Kristo na kupatanishwa na Mungu wakati tukiwa adui zake (**Rum 5:8-10**). Matokeo, kama palivyoonyeshwa katika **1 Pet 3:9b; Rum 12:17, 19, 21; 1 Wathes 5:15**, ni mahusiano ya "Baraka- kwa- laumu" ambayo hukazia kwa Mungu na neno Lake, na hupata nguvu kutoka Kwake, na huonyesha mwitikio wa neema na msamaha unapokosewa. Mahusiano ya namna hiyo m huwa na sifa ya mshikamano, huruma, hisia ya umoja (udugu), moyo wa wema, na unyenyekevu katika roho (**1 Pet 3:8**). Wahusika katika uhusiano wa aina hiyo hujitoa kwa kila moja, na kuweka masilahi ya mwingine kwanza (**Math 5:40-46; Yoh 13:13-15; Rum 12:10; 14:13, 15; 15:21; 1 Wakor 8:13; 10:24; Wafil 2:3-9; 1 Wathes 5:12-13; Yak 2:1-4; 1 Pet 2:17; 1 Yoh 3:16**). Hutafuta amani na umoja (**Math 5:9, 23-25; Rum 12:18; 1 Wakor 1:10; 4:12-13; 10:32-33; 12:14-26; Waef 4:3; Wafil 2:1-3**). Matokeo yake, watu kama hao huonyesha unyenyekevu, uungwana, na uvumilivu (**Math 5:5; Waef 4:1-2; Wafil 4:5; 1 Wathes 2:7**). Hawaoneani husuda (**Wagal 5:26**), bali hufarijiana na wana wema na husameheana kila mtu na mwenzake (**Math 5:7; Rum 12:20; 2 Wakor 1:3-5; Waef 4:32; Wakol 3:10, 13.** Zaidi ya hapo, tofauti na mahusiano yaliyo na msingi wa kanuni za kidunia, watu wanaomweka Kristo kwanza hawajitengi wenyewe kutoka kwa watu wa jamii nyingine au makabila mengine (**Wagal 2:11-14; 3:28; Wakol 3:11**), na hutoa kwa ukarimu kuwasaidia masikini (**Math 5:42; 2 Wakor 8:1-15; 9:6-11; Wagal 2:10; Yak 1:27; 2:5-6**). Njia hizi mpya za kuhusiana kwa watu hutokea kiasili pale watu tunapotambua kwamba, katika Kristo, sisi hatuwi tena watu tuliotengana, bali sote tu sehemu ya familia mpya (**Rum 8:14-17; Wagal 3:26; 4:6-7; Waef 1:5; 1 Tim 3:15; 5:1-2**), tuliounganika kiundani tu*"viungo kimoja kwa mwingine"* (**Rum 12:5; Waef 4:25**). Mahusiano kama hayo hatima yake ni kuwa na mafanikio, kwa sababu yanatiririka kutokana na tabia na maagizo ya Mungu mwenyewe.

**B.** ***Tumeitiwa kuonyesha upendo katika maeneo yetu yote ya mahusiano.***

Moyo wa mahusiano yote yenye msingi wa Kikristo ni UPENDO. Sababu ya hilo kuwa kweli ni kwa

vile upendo watoka kwa Mungu, na kwa sababu Mungu ni upendo (**1 Yoh 4:7-8, 16**), nasi tunatakiwa tuwe kama Yeye (**Rum 8:29; 1 Wakor 15:49; 2 Wakor 3:18**). Kusema kweli, *"Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza"* (**1 Yoh 4:19**; ona pia **Waef 5:2**). "Na akiwauliza mtu awaye yote, 'Inakuwaje hoja kwamba Mungu anawapenda husababisha nyie kuwapenda wengine?' Jawabu ni: Kule kuzaliwa upya huzalisha muunganiko huo. Kuzaliwa upya ni tendo la Roho Mtakatifu linalounganisha mioyo yetu iliyokufa, yenye ubinafsi, na moyo ulio hai, wenye upendo, wa Mungu ili kwamba uzima wake unakuwa wetu, na upendo wake unakuwa wetu." (Piper 2009: 157) Kwa hiyo, upendo ndiyo kipimo au ishara ya msingi ya mtu kuwa kweli amezaliwa mara ya pili au la. Jinsi upendo ulivyo kiini kwa mahusiano ya Kikristo (na kwa Ukristo wenyewe) huonekana kwa njia zifuatazo:

1. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba Yesu alisema amri zile mbili, *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote."* na *"Mpende jirani yako kama nafsi yako,"* ndiyo msingi wa Biblia nzima (**Math 22:36-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28**).
2. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba *"Yeye asiyependa, hakumjua Mungu"* (**1 Yoh 4:8**), na *"Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona" (***1 Yoh 4:20**).
3. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba unahusishwa na msamaha wa dhambi zetu (**Luka 7:36-50; 1 Pet 4:8**).
4. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba "lengo" la mafundisho ya Ukristo ni *"upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema na imani isiyo na unafiki"* (**1 Tim 1:5**).
5. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba sheria yote imetimizwa kwa maneno, *"mpende jirani yako kama unavyojipebda mwenyewe"* (**Rum 13:8-10; Wagal 5:14**).
6. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba usiku ule kabla Hajafa, "amri mpya" Yesu aliyowapa wanafunzi wake ilikuwa *"Mpendane. Kama vile nivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo"* (**Yoh 13:34; 15:17**).
7. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba *"kupendana moja kwa mwingine"* ni ishara aliyoitoa Yesu ambayo kwa hiyo *"watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu"* (**Yoh 13:35**).
8. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba ndiyo *"njia iliyo bora"* (**1 Wakor 12:31**). Ndiyo uliyo mkuu kuliko imani na tumaini (**1 Wakor 13:13**). Ikiwa mtu hana upendo, yeye "si kitu" hata kama anena kwa lugha za wanadamu na za malaika, ana karama za unabii, ana maarifa yote, na anayo imani inayoweza kung'oa milima yote (**1 Wakor 13:1-2**). Ikiwa mtu hana upendo, hapati kitu "chochote" hata kama atatoa kila kitu alicho nacho kuwasaidia masikini na hata akautoa mwili wake wote uunguzwe kwa moto (**1 Wakor 13:3**).
9. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba *"upendano wa udugu"* unapaswa uonyeshwe *"juu ya yote"* (**1 Pet 4:8**).
10. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba ni namba moja kati ya "tunda la Roho" lililoorodheshwa katika **Wagal 5:22-23**, na hujumuisha "tunda lote la Roho" (kimuhimu zaidi, ni "tunda la Roho" ni limoja, siyo uwingi).
11. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba ni *"kifungo kamili cha umoja"* ambao unapaswa udhihirishwe juu ya mambo mengine yote (**Wakol 3:14**).
12. Ni wa kiini sana huo upendo kiasi kwamba Maandiko huita *"Sheria ya kifalme"* (**Yak 2:8**).
13. Kilele cha upendo ni kujitoa dhabihu mwenyewe: *"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake"* (**Yoh 15:13**).
14. Sheria ya upendo ni ya kimatendo sana: *"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii"* (**Math 7:12; Luka 6:31**).
15. Mitume daima hutoa wito kwa waamini kwa misingi ya upendo, na kuwahimiza waamini kuonyesha upendo kati yao zaidi na zaidi (**1 Wakor 8:1; 16:14; 2 Wakor 2:8; 8:24; Wagal 5:6, 13; Waef 3:17-19; 4:2, 15; 5:2, 25, 28; Wafil 2:1-2; Wakol 2:2; 3:14; 1 Wathes 3:12; 4:9; Filemoni 9; Waeb 10:24; 1 Pet 2:17; 4:8; 2 Pet 1:7; 1 Yoh 4:7-11; 2 Yoh 5**).

**C. *Jinsi tunavyowatendea watu huonyesha kikamilifu jinsi tunavyomfikiria Mungu.***

Wakristo walio wengi hutenganisha yaliyo "wakfu" mbali na "ya kidunia." Wanafikiri kwamba yanayotokea kanisani Jumapili ndiyo ya "kiroho," bali jinsi wanavyowafanyia watu na kuwatendea katikati ya juma ni "ya jumla," au "ya kawaida," au kinamna fulani yako mbali na maisha ya kiroho. Mawazo kama hayo si ya Ki-Biblia kabisa. Jinsi tunavyotenda katikati ya juma—na hasa tunavyowatendea watu—huhusishwa moja kwa moja na jinsi tunavyofanya ibada kwa Mungu wetu. Muunganiko huo ni wa karibu kiasi kwamba **Yak 1:27**

huueleza kuwa "*Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu na Baba ni hii*" ni hii: *"Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa."* Neno la Kiyunani analolitumia Yakobo kwa "dini" ni *thrēskeia* ambalo kimsingi huzungumzia shughuli au sherehe za ibada za kidini (Danker 2000: *"thrēskeia,"* 459; Zodhiates 1992: *"thrēskeia,"* 742). Anachokisema Yakobo ni hiki: "kama mtu yeyote anatoa *thrēskeia* iliyo safi kwa Mungu, na aelewe kwamba hilo halishughulikii usafi wa ki-nje au utekelezaji wa kanuni za sherehe; kuna *thrēskeia* iliyo bora zaidi ya madume maelfu ya kondoo na mito ya mafuta, kimajina, kutenda kwa haki na kupenda rehema na kuenenda kwa unyenyekevu na Mungu wake (Mic. 6:7-8). Au, kulingana na maneno yake mwenyewe 'Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa' (k.m. Math. 23:23). . . . Yakobo alidai kwamba mwelekeo huo mpya ulikuwa wa hali ya juu zaidi kuliko ule wa kale kwa sababu *thrēskeia* hiyo mpya hujumuisha matendo ya rehema, upendo, na utakatifu." (Trench 1989: 188) Kusema ukweli, Yesu alisema kwamba ikiwa hatutatenda mambo ya kimatendo kuwajali watu, basi tunamwabudu Yeye Jumapili "bure," na kusifu kwetu si lolote isipokuwa "ibada ya midomo," kwa sababu matendo yetu (au kutokutenda matendo kwetu kumethibitisha kwamba mioyo yetu iko "mbali na [Yeye]" (**Math 15:3-9**).

Yesu alisema kwamba zile amri mbili—Mpende Mungu kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na mpende jirani yako kama nafsi yako (**Math 22:36-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28**)—ndizo msingi wa Biblia yote. Mungu hadhihakiwi kwa maneno yetu. Kwa hiyo, ametupatia kipimo ambacho kwa hicho, kila mtu, akiwamo Mungu mwenyewe, huweza kuona waziwazi ikiwa kweli tunatimiza, kusema kweli, kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote, kwa roho zetu zote, na akili zetu zote. Kipimo ni hiki: jinsi tunavyoitekeleza "ile amri ya pili" (m.y., jinsi tunavyowatendea watu) ni kihakikisho cha kama kweli tunatekeleza ile "amri ya kwanza" (m.y., kumpenda Mungu). Hata wakati Yesu alipomkabili Petro na kumuuliza mara tatu, *"Je unanipenda?"* Yesu hakulikubalia tu lile jibu la Petro, *"Naam, Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda."*Badala yake, Yesu kisha alimwambia Petro, *"Lisha wana kondoo zangu"* (**Yoh 21:15-17**). Kile Yesu alichokuwa anasema kwa Petro ni hiki: "Kama kweli unanipenda Mimi, basi utauthibitisha upendo wako kwa kuwahudumia kondoo Zangu." Sababu kwa nini kipimo hiki ni cha kweli ni kwa sababu kila mwanadamu amefanywa kwa "mfano wa Mungu" (**Mwa 1:26-27; 5:1-3; 9:6; Waef 4:24; Wakol 3:10; Yak 3:9**), na jinsi tunavyoufanyia mfano wa Mungu kwaonyesha kiuhakika jinsi tunavyomuwazia Yeye. Kuliweka kwa namna nyingine: "Matendo huthibitisha ilivyo." Kwa hiyo, Mtume Yohana anakataa kwa dhahiri kabisa kwamba "*kuwa* kiroho kwaweza kutenganishwa na *matendo* ya kimwili. Yohana, kusema ukweli, anasisitiza kwamba kuwa kiroho lazima kutathminiwe kwa matendo kimwili, vinginevyo kuwa kiroho kunakuwa hakuna uhalisia. Ndicho tulichokiona katika 1 Yohana 3:7: 'Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye. *atendaye* haki *yuna* haki, kama yeye alivyo na haki.' Wajidanganyao walikuwa wanasema: Unaweza *kuwa* mwenye haki na *usitende* ki-haki. Yohana anasema: Watu pekee *walio* wenye haki ni wale ambao *wanatenda* haki. Matendo huthibitisha ilivyo." (Piper 2009: 146-47) Hili huonekana mara nyingi na kwa jinsi nyingi kila mahali katika Biblia yote:

1. Jinsi tutendavyo kile asemacho Mungu ni muhimu zaidi kuliko matendo yetu ya utaratibu wa kidini wa kuabudu (**1 Sam 15:22-23; Zab 51:14-17; Isa 29:13-16; Yer 6:16-20; 7:21-23; Hos 6:6; Rum 12:1; Wakol 3:23-24; Tito 1:16; 1 Yoh 5:3; 2 Yoh 6; Ufu 19:7-8**).
2. Kutenda kwetu kile Yesu asemacho ni ishara kwamba kweli tunampenda Yeye (**Yoh 14:15, 21, 23; 15:9-10; 21:15-17**).
3. Ishara ya msingi ya uaminifu na utii kwa Mungu ni jinsi tunavyowahudumia watu (**Mith 14:31; 19:17; 21:3; Mika 6:6-8; Marko 12:28-34; Yoh 13:34-35; Yak 1:27; 2:18-26; 1 Pet 3:7; 1 Yoh 2:10; 14, 18-19, 23; 4:7, 11-12, 21**).
4. Vivyo hivyo, ishara ya msingi ya kupungukiwa imani kwetu na kutomtii Mungu ni jinsi tunavyowahudumia watu wengine (**Mith 14:31; Isa 1:10-17; Eze 16:48-50; Math 12:1-8; 15:3-9; 23:23; Yak 2:14-17; 1 Yoh 2:9; 3:10, 15, 17; 4:8, 20**).

**D.** ***Tuyafanyayo katika maisha haya—hasa jinsi tunavyowafanyia watu wengine—kutakuwa ndicho kipimo tutakachohukumiwa nacho katika hukumu ya mwisho.***

Hatuwezi kujifanyia njia kwenda mbinguni, isipokuwa tunaokolewa tu kwa neema ya Mungu kupitia imani katika Kristo (**Yoh 3:16-18; 6:28-29; Rum 2:16-17; 10:8-13; Waef 2:8-9; Wagal 3:1-14**). Hata hivyo, "Matendo ni kielelezo cha hali ya kiroho ya moyo wa mtu. Hatuambiwi kama vitabu hivi [katika **Ufu 20:11-15**] vimeandikwa matendo mema na mabaya au ni mabaya tu. Hata hivyo, hukumu si kuweka uwiano kati ya matendo mema na matendo mabaya. Badala yake, matendo yanaonekana kama ushahidi usiokosewa wa sura ya utii wa moyo; huonyesha kuamini au kutoamini, uaminifu au kutokuwa mwaminifu. Hukumu itafunua kama utii wa watu uko au hauko kwa Mungu na Kondoo au na maadui wa Mungu." (Ngundu 2006: 1576) Kama asemavyo Mtume Yakobo, *"Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani*

*yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo. . . . Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa."* (**Yak 2:16, 26**)

Kwa hiyo, wakati yule matawala tajiri kijana alipouliza afanye nini ili aurithi ufalme wa mbinguni, Yesu alimwelekeza kwenye ile "sehemu ya pili ya Ile Amri" (m.y., jinsi tunavyoenenda, hasa jinsi tunavyowatendea watu) kama kipimo (**Math 19:16-26; Marko 10:17-27; Luka 18:18-27**). Sehemu ile ya Sala ya Bwana isemayo kwamba, *"Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu"* (**Math 6:12; Luka 11:4**) ni sehemu pekee ya Sala ya Bwana ambapo Yesu alisisitiza rasmi na kuelezea: *"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa."* (**Math 6:14-15;** ona pia **Marko 11:23-26**) Vivyo hivyo, mifano mingi ya Yesu kuhusiana na ufalme wa mbinguni ilionyesha kwamba hukumu ya mwisho itasimamia matendo tuyafanyayo, hasa jinsi tunavyowatendea watu wengine katika maisha haya (**Math 18:23-35; 21:28-32; 21:33-44; 24:45-51; 25:1-13; 25:14-30; Marko 12:1-12; Luka 12:42-48; 16:1-9; 19:12-27; 20:9-18**). Mafundisho ya Yesu yaliyo wazi zaidi ya Yesu kuhusiana na hukumu ya mwisho yalionyesha kwamba, kuangamia milele au kupata baraka za milele kutategemea tunawafanyia nini watu wengine katika maisha haya, kwa sababu: "*kadiri mlivyomtendea* [m.y., mlionyesha kujihusisha au kuhurumia] *mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"* (**Math 25:40**), na *"Kadiri msivyomtendea mmoja wapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi"* (**Math 25:45**). "Kitu kimoja kinachojichomoza katika kifungu hiki kilichofuata, ni jinsi, ama 'kondoo' ama 'mbuzi' wametambua kwa uwazi kwamba, katika kuwahudumia au kutowahudumia masikini, wamekuwa wakionyesha mwitikio kwa Kristo. . . . Hakuna kitu ambacho kingeliweza kuonyesha wazi zaidi jinsi matendo ambayo Mungu anapendezwa nayo, hutiririka kiasilia zaidi kutokana na mahusiano mazuri na Mungu. Ni kile mtu afanyacho pale asipotafuta kusifiwa, ndicho kinachoonyesha tabia yake." (Travis 1982: 191) Matokeo yake kama vile kile tukifanyacho—hasa jinsi tunavyowatendea watu—ndicho kipimo katika maisha haya, ndicho kinachothibitisha nini hasa tunafikiria kuhusu Mungu, ndipo kipimo hicho hicho kinapatikana katika muktadha wa hukumu ya mwisho. Hili huonekana mara nyingi kwa jinsi nyingi katika Biblia yote.

1. Kwa yote mawili; kimafundisho na mfano, Mungu huhukumu watu na mataifa na huwalipiza "kulingana na matendo yao [au "njia" au "kazi"]" (**Waamuzi 1:6-7; 9:22-24, 56-57; 2 Sam 12:9-12; 1 Wafalme 2:32-33; 1 Wafalme 20:35-42; 1 Wafalme 21:17-19; 2 Nyak 6:23, 30; Ayu 34:11; Zab 18:24; 31:23; 62:12; Mith 24:12; Mhu 12:13-14; Isa 59:18; Jer 17:10; 25:14; 32:19; Eze 7:3, 8-9, 20, 23-24, 27; 9:10; 11:21; 16:43, 59; 18:30; 22:31; 24:14; 33:20; 35:6, 11, 15; 39:24; Hos 12:2; Yoeli 3:5-7; Obad 15; Zek 1:6; Math 16:27; 25:14-30; Luka 12:47-48; Yoh 5:28-29; Rum 2:1-6; 12:19; 1 Wakor 3:8, 11-15; 2 Wakor 5:10; 11:15; Wagal 6:7-8; Waef 6:8; Wakol 3:25; 2 Tim 4:14; Waeb 10:26-27; 1 Pet 1:17; 2 Pet 2:20-22; Yuda 14-15; Ufu 2:23; 14:13; 20:11-13; 22:12**).
2. Hukumu ya mwisho ya "matendo" yetu huhusisha maneno yetu (**Math 5:21-22; 12:36-37; Luka 12:2-3; Yuda 14-16**), pamoja na siri na "mambo yaliyofichika" ya mawazo, akili, moyo, makusudio, na misukumo yetu (**1 Sam 16:7; 1 Nyak 28:10; 29:17; 2 Nyak 6:30; Mith 21:2; Isa 29:13-14; Yer 17:10; Math 5:21-22; 6:4, 6, 18; 10:26; Marko 4:21; Luka 2:34-35; 12:2; Rum 2:16; 1 Nyak 4:5; Waeb 4:12; Ufu 2:23**).
3. Jinsi tunavyowatendea watu katika maisha haya, kutakuwa ni msingi wa hukumu yetu ya mwisho, kwa yote mawili – thawabu na adhabu, kwa sababu hilo linafunua hali ya kweli ya mioyo yetu na mahusiano yetu ya uhalisi na Yesu (**Math 6:1-4, 12, 14; 10:42; 24:45-51; 25:31-46; Marko 9:41-42; Luka 6:35; 12:33, 41-48; 14:13-14; 16:1-9; Rum 2:1-6; 1 Tim 6:18-19; 2 Tim 4:14; Waeb 6:10; 1 Pet 5:1-4**).

**E.** ***Orodha ya vipaumbele vya msingi katika maeneo muhimu ya maisha***

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, ni lazima tuwekee vipaumbele muda wetu, na kukazia kwenye mambo yaliyo muhimu zaidi. Wengi wetu hutambua kanuni hiyo kuhusiana na vitu mbali mbali tunavyotakiwa kuvifanya kuhusu kazi zetu au huduma zetu. Hata hivyo, mara nyingi huwa tunapuuza ukweli kwamba kanuni hii ya kuweka vipaumbele na kukazia kwenye mambo muhimu huhusu maisha yote. Na matokeo yake, hata kama tunazalisha sana katika kazi zetu, maisha yetu yote yanakuwa hayana uwiano kwa sababu tumepuuza kutumia muda wa kutosha kwenye maeneo hayo pia na watu ambao walitakiwa kufikiriwa zaidi na sisi. Kwa hiyo,yafuatayo ni mapendekezo ya "orodha ya vipaumbele vya maisha" ambayo yanapaswa kuzingatiwa kichwani wakati tukipanga vipaumbele vyetu vya muda.

1. Umtafute kwanza Bwana, ufalme wake na haki yake (**Math 6:33; 22:37; 1 Wakor 10:31**). Tumia muda wa kawaida kwa maombi, kutafakari, na kujifunza Neno la Mungu ili kupata mtazamo, kweli, na uelekeo wa maisha Yak.

2. Jionyeshe mwenyewe kama mfano wa utauwa (**Math 5:13-15; 1 Tim 4:7-8, 12, 16**). Ili kulitimiza hili itakubidi:

a. Pangilia muda wako—hata kwa kutumia mpango wa kimaandishi ili kuhakikisha vipaumbele vinafuatwa.

b. Utambue mipaka au uwezo wako na uandae matarajio ya kiukweli.

c. Jifunze kusema "hapana" kwa mambo yale ambayo yanakulazimisha kukubana muda wako.

d. Pumzika, cheza, fanya mazoezi, na jiingize kwenye maswala ya kijamii.

e. *Mara kwa mara ukague vipaumbele vyako, umuhimu wa vipaumbele hivyo, na uelekeo wake, unakoenda, na uaminifu wa maisha Yak.* Maendeleo yetu katika kufanyika mfano wa kumfanania Yesu unapaswa uwe dhahiri kwa kila moja kuchanganya na sisi wenyewe (**1 Tim 4:15**). Paulo alitathmini maisha yake mwenyewe (**2 Tim 4:6-7**). Waamini ambao kitabu cha Waebrania kiliwalenga ni dhahiri walikuwa hawajitathmini wenyewe, au kuendelea katika imani yao kama walivyopaswa wawe, na wakahimizwa kwa sababu ya hilo (**Waeb 5:11-14**).

3. Familia Yak mwenyewe ni kipaumbele cha juu zaidi kuliko wale walio nje ya familia Yak; au hata kuliko kanisa lako, kwani hata hustahili kuwa kiongozi katika kanisa ikiwa huwezi kuisimamia nyumba Yak vizuri (**1 Tim 3:4-5**).

a. *Mke wako ndiyo kipaumbele cha kwanza, kwani ndiye aliye "mwili moja" nawe* (**Mwa 2:24**). Mahusiano Yak naye yanapaswa yawe kielelezo kati ya Kristo na kanisa (**Waef 5:25-32**). Yeye pia ni wa kipaumbele cha juu zaidi ya wazazi wako kwa sababu wewe na yeye mmewaacha wazazi wenu ili kuianzisha familia yenu wenyewe. Yeye pia ni kipaumbele cha juu zaidi kuliko watoto kwa sababu wataondoka kwenda kwenye familia zao wenyewe.

b. *Watoto wako ndio kipaumbele cha pili.* Wanapaswa walelewe katika njia za Bwana (**Kum 6:6-7; Waef 6:4**), lakini wataondoka nyumbani na kwenda kuanzisha familia zao wenyewe. Uaminifu wa watoto na heshima kwa wazazi wao ni ishara au dalili ya sifa Yak kuwa kiongozi wa kanisa (**1 Tim 3:4; Tito 1:6**). Kwa hiyo, wana kipaumbele cha juu zaidi kuliko kazi Yak katika kanisa.

c. *Wazazi wako na wazazi wa mkeo ni wa umuhimu wa tatu katika familia.* Watoto siku zote wana wajibu wa kuwaheshimu wazazi wao, na kuwatunza nyakati za uhitaji (**Kut 20:12; Waef 6:21-3; 1 Tim 6:4, 8**).

4. Majirani zako na wale walio nje ya familia Yak (m.y, wale walio katika jumuiya) ndio kipaumbele kinachofuatia. Jinsi tunavyowatendea watu wengine moja kwa moja huonyesha kama sisi tunampenda Mungu (**Math 22:39-40; 1 Yoh 4:20-21**). Udhihirisho wetu wa upendo kwa wengine unahusisha wote, waamini na wasioamini, wale watupendao na wale wasiotupenda (**Math 43-43; Wagal 6:10).** Kusema ukweli, heshima yetu kwa wale walio nje ya kanisa ni moja ya dalili kwamba tunastahili kuwa viongozi wa kanisa au hapana (**1 Tim 3:7**). Kwa hiyo, watu wengine ni wa vipaumbele zaidi kuliko kazi zetu katika kanisa.

5. Kanisa ni muhimu, lakini tunapata sifa ya kutustahilisha kulitumikia ikiwa vipaumbele vyetu vingine vimekaa vizuri. Kazi yetu katika kanisa lazima iwe kulingana na vipawa
vyetu na wito (**Rum 12:3-13; 1 Tim 4:14**). Kazi yetu katika kanisa isiwe ni kwa gharama ya mahusiano yetu. Viongozi wengi mno huweka kazi zao za kikanisa nafasi ya juu zaidi ya miito yao ya kumpenda Mungu, kuwa mume kama Kristo, baba, mwana, na kuwapenda jirani zao kama wenyewe. Hata hivyo, kushindwa kwa maeneo haya mengine hupiga makelele makubwa zaidi kwa washirika wako kuliko mahubiri unayoyahubiri. Tunapaswa kupanga mpango na kupangilia muda wa kanisa na wa huduma vizuri ili kwamba tuweze kuwa utendaji mzuri iwezekanavyo. Hata hivyo, sababu moja ya kufanya hivyo ni ili tuweze kuwa na muda mwingi zaidi wa kuutumia na watu tuwapendao na walio karibu zaidi na sisi. Huko ndiko kunaitwa kudumisha "uwiano wa kazi-maisha."

**F.** ***Njia ya kimatendo ya kudhihirisha upendo: lugha tano za upendo.***[2]

"Kimsingi zipo lugha tano za mapenzi—njia tano ambazo watu husema na kuelewa mapenzi. . . . Lililo muhimu hapa ni kusema lugha ya upendo ya mwenzi wako. . . . Si kawaida kwa mke na mume kuwa na lugha ya upendo inayofanana. Tunapozungumza lugha yetu ya msingi ya upendo, na tunachanganyikiwa mwenzi wetu asipoelewa tunachokiwasilisha. Tunauonyesha upendo wetu, lakini ujumbe haufiki kwa sababu tunazungumza, kile ambacho kwao, ni lugha ngeni. . . . Utakapowezi kutambua na kuzungumza lugha ya msingi ya upendo ya mwenzi wako, naamini utakuwa umegundua ufnguo wa ndoa ya kudumu yenye upendo." (15-17)

1. <u>Maneno ya ukiri chanya.</u> Maneno yaliyo chanya, ya kusifu, ya kujenga, na kutia moyo ni njia mojawapo ya kuuonyesha hisia zetu za upendo. "Hali ya hisia" katika ndoa inatiwa nguvu wakati mume na mke wanapotumia maneno ya kutia moyo mara kwa mara (inamaanisha, jambo la kuinua kila siku).

a. *Weka lengo kumsifu mwenzi wako kila siku kwa muda wa mwezi.* Tunapoambiwa maneno ya kutia moyo tutahamasika zaidi kusema au kufanya kile apendacho mwenzi wetu. Tunapoangalia maeneo ya uwezo wa mwenzi wetu na kumwambia jinsi tunavyobarikiwa na uwezo huo, kwa hakika mwenzi wetu atatendea kazi maneno hayo ili aishi kwa viwango sawa sawa na hayo uliyosema.

b. *Maneno ya kutia moyo yanahitaji kusisitiza, na mwenzi wetu, kujifunza yaliyo muhimu kwake, na kuiona dunia kwa mtazamo wake yeye.* Kwa maneno ya kutia moyo twajaribu kuwasiliana, "Ninajua. Ninajali. Niko na wewe. Nikusaidieje." Hata hivyo, ili uweze "kutia moyo," mwenzi wako lazima *kwanza atamani* kufanya kile unachomtia nacho moyo. Kwa mfano, "Waume wengine hushinikiza wake zao wapunguze unene. Mume anasema, "Ninamtia moyo," lakini kwa mke inaonekana kama hukumu. Waweza kumtia mtu moyo kupunguza unene ikiwa ndivyo anavyotaka yeye. Ni mpaka atamani, vinginevyo maneno Yak yatakuwa kama ya mtu anayehubiri. Maneno ya jinsi hii si rahisi kutia moyo. Mara yanaposikika huchukuliwa kama maneno ya kuhukumu, yaliyokusudiwa kuchochea hatia. Hayadhihirishi upendo bali kukataliwa." (44)

c. *Ili maneno chanya yawe kweli, kile usemacho lazima kisemwe kwa huruma na upole.* Zaidi ya hapo, upendo huleta maombi, na siyo madai. "Unapopeleka ombi kwa mwenzi wako, unaonyesha kuwa unakubali uthamani wake na uwezo wake. . . . Lakini, unapopeleka madai, wewe si mpenzi tena bali dikteta. Mwenzi wako hatatiwa moyo bali atajisikia kudharauliwa." (49)

d. *Waweza kusema maneno mazuri yamhusuyo mwenzi wako wakati yeye mwenyewe hayupo (hatimaye, mtu fulani atamwambia, na wewe utapata sifa njema kwa kuonyesha upendo).* Vile vile, mnenee mwenzi wako mazuri mbele ya wengine wakati yeye mwenyewe akiwepo pia.

2. <u>Wakati wa thamani.</u> "Wakati wa thamani" yamaanisha kumpa mtu usikivu wako wote. Wakati wa thamani ni pamoja na kutazamana mkiwa mmekaa pamoja, kutembea pamoja, kula pamoja, au hali ya kuwa pamoja tu, kufanya kitu anacho kipenda mwenzako.

a. *Kiini cha wakati wa thamani ni kuwa pamoja.* Kuwa pamoja si ukaribu katika hali ya mwili tu, lakini ni *Usikivu wenye fokasi.* "Ninapokaa katika kochi na mke wangu na kumpa dakika ishirini za usikivu usiogawanyika na yeye anapofanya vivyo hivyo kwa ajili yangu, tutakuwa tunapeana dakika ishirini za uhai. Hatutozipata hizo dakika ishirini tena; tunatoa uhai wetu na kupeana. Ni tendo lenye nguvu kimawasiliano na la kuchochea upendo." (60)

b. *Wakati wa thamani mara kwa mara huhusisha mazungumzo yenye mantiki—ikimaanisha., "mazungumzo ya upole ambapo wawili wanashirikishana uzoefu wao, fikra, hisia, na shauku katika hali ya kirafiki, isiyoingiliwa"* (65). Mazungumzo yenye mantiki ni tofauti na maneno ya ukiri chanya: maneno ya ukiri chanya yanafokasi katika kile *tunachosema;* mazungumzo yenye mantiki yana fokasi katikas kile *tunachosikia.*

c. *Wakati wa thamani waweza kuhusisha shughuli zenye kufaidisha—inamaanisha, chochote kile ambacho nyote ama mmoja wenu anapendezwa nacho.* Umuhimu hauko katika kile

[2]Sehemu hii ni kulingana na jarida la Mwanasaikolojia wa Kikristo na mshauri wa ndoa Gary *Lugha Tano za Upendo* (Chicago: Northfield, 1992). Namba katika parandesi ni ukurasa ambao nukuu kutoka katika kitabu hicho
Ingawaje muktadha wa kitabu ni mahusiano ya kindoa, *kanuni* za "lugha tano za upendo" hutenda kazi kikawaida katika kila mahusiano. Chapman mwenyewe ameandika kuhusu kutumia hizo lugha za upendo katika muktadha wa watoto: Gary Chapman na Ross Campbell, *Lugha Tano za Upendo za Watoto* (Chicago: Northfield, 1997); wavulana: Gary Chapman, *Lugha Tano za Upendo za Wavulana* (Chicago: Northfield, 2010); watu wazima wasio katika ndoa: Gary Chapman, *Lugha Tano za Upendo Toleo kwa Wasiooa au Kuolewa* (Chicago: Northfield, 2009); na mahali pa kazi: Cary Chapman and Paul White, *Lugha Tano za Upendo za Shukurani Mahali pa Kazi* (Chicago: Northfield, 2011)

mnachokifanya bali katika sababu ya kukifanya. "Kusudi ni kuwa na uzoefu wa kufanya kitu pamoja, hata mtakapo kuwa mmemaliza ujisikie, 'Ananijali. Alikuwa tayari kufanya kitu kile ninachependezewa pamoja na mimi, na alikifanya kwa mtazamo mzuri.' Huo ni upendo, na kwa watu wengine ni upendo wa hali ya juu." (73-74)

3. Kutoa na kupokea zawadi. Zawadi ni kitu fulani halisi kinachoonyesha kuwa umekuwa ukimfikiria umpaye zawadi. Haijalishi kama inagharimu pesa ngapi; unaweza kutengeneza zawadi. Kilicho muhimu ni kwamba umekuwa ukimuwaza huyo mtu, ukamtafutia zawadi, na ukaitoa zawadi hiyo kama kielelezo cha upendo wako kwake.

a. *Ikiwa kupokea zawadi ni lugha ya msingi ya mwenzi wako, lugha rahisi ya upendo yaw ewe kujifunza ni kuwa mtoa zawadi.* Orodhesha zawadi zile ambazo zimemvutia na kumfurahisha sana mwenzi wako alipozipokea kwa kipindi cha miaka (iwe zawadi hizo zimetolewa na wewe, au marafiki). Hiyo orodha itakupa kuelewa aina ya zawadi mwenzi wako atapendelea kupokea. Inapobidi, pata msaada wa ndugu anayemjua mwenzi wako vema katika kuchagua zawadi nzuri.

b. *Usisubiri mpaka kuwe na tukio maalum ndipo umpe mwenzi wako zawadi.* Endapo kupokea zawadi ndiyo lugha yake ya msingi ya upendo, yeye aweza kupokea karibu kila kitu kama udhihirisho wa upendo. (Kama amezikosoa zawadi zako siku za nyuma, na karibu kila ulichotoa kilikosa ridhaa yake, basi kwa hakika kupokea zawadi si lugha ya msingi ya upendo ya mwenzi wako.)

c. *Uwepo wako kimwili kwa mwenzi wako awapo na wakati mgumu au awapo katika wakati mwingine muhimu yaweza kuwa zawadi yenye nguvu sana kwake.* Mwenzi wako anapokwambia kuwa angependa uwe naye katika tukio falani, chukulia ombi hilo kuwa ni muhimu.

4. Mdo ya huduma. Mdo ya huduma ni yale tutendayo tukijua kuwa mwenzi wetu anapenda tuyatende. Haya ni pamoja na kupika, kuandaa meza, kuosha vyombo, kutoa takataka nje, kumbadilisha mtoto nepi, au kusafisha nyumba. Hata hivyo yanahitaji, kupanga, muda, juhudi, na nguvu. Unatafuta kumpendeza mwenzi wako kwa kumtumikia. Yanapotendeka kwa nia njema, Mdo ya jinsi hii ni Mdo ya upendo. Hivyo ndivyo ilivyo hasa wakati Mdo ya huduma utendayo ni yale ambayo mwenzi wako angeyafanya kwa kawaida (mfano, mume kuosha vyombo baada ya chakula kuonyesha kufurahishwa na chakula na upendo wake kwa mkewe).

a. *Tunayotendeana kabla ya kuoana hayaashirii yale tutakayotendeana baada ya kuoana.* Kabla ya kuona tunabebwa na nguvu ya "upendo wa mwilini". Baada ya ndoa tunarudi katika hali yetu ya kawaida tuliyokuwa nayo kabla ya "kupenda." Kwa hiyo endapo lugha ya msingi ya upendo kwa mwenzi wako ni Mdo ya huduma, yeye atakutarajia uendelee kufanya Mdo ya huduma katika ndoa. Mwenzi wako atajisikia kuwa hapendwi unapoacha kutenda Mdo ya huduma.

b. *Kupenda ni uchaguzi ambao hauwezi kulazimishwa.* Kukosoa na kudai kutendewa husababisha ufa kati ya watu; havihamasishi Mdo ya huduma ya upendo. Mwenzi wako anaweza kufanya kile unachodai afanye, lakini halitakuwa tendo linalodhihirisha upendo. Maombi ni bora kuliko madai. Hatimaye, basi, kupenda ni chaguo. "Kila mmoja wetu lazima achague kila siku kumpenda au kutompenda mwenzi wake. Tukichagua kupenda , basi kuudhihirisha upendo wetu kwa mwenzi wetu kwa namna ile anayootuomba kutafanya upendo wetu ufanikiwe zaidi." (107)

c. *Shutuma za mwenzi wako kuhusiana na tabia Yak hukupa picha iliyowazi kuhusiana na lugha yake ya upendo.* "Kwa kawaida watu hukosoa wenzi wao kwa sauti ya juu katika maeneo ambayo wao wenyewe wana uhitaji mkuu kihisia. Shutuma zao si njia nzuri ya kutaka kupendwa. Tunapoelewa hayo, tutasaidia kuweka hizo shutuma katika mchakato wenye mwelekeo wenye matunda." (107)

d. *Unaweza kutengeneza orodha ya maombi ambayo mwenzi wako amekuomba katika kipindi cha wiki chache zilizopita.* Yatazame maombi hayo kama ishara ya vile vilivyo muhimu kwake. Amua kutekeleza moja kila wiki kama njia ya kuonyesha upendo. Au, waweza kumwomba mwenzi wako aandike orodha ya vitu 10 ambavyo angependa wewe uvifanye katika kipindi cha mwezi unaokuja, na vipange kutegemeana na umuhimu wake. Tumia orodha hiyo kupanga mkakati kwa ajili ya "mwezi wa upendo." Au, kila baada ya kipindi fulani muulize mwenzi wako, "Kama ningeweza kufanya jambo moja maalum la kukuhudumia wiki hii, ombi lako lingekuwa ni nini?" Mwenzi wako atatambua mambo haya. Kwa kufanya hili utakuwa unalijaza "tangi lake la hisia." Mwenzi wako atakuwa na furaha zaidi, na yeye pia, ataanza kutenda kwa namna ya kukufurahisha wewe.

5. Mguso wa Mwili. Mguso wa mwili, ni pamoja na kushikana mikono, kupigana busu, kukumbatiana, kupapasana kimahaba, na kufanya tendo la ndoa, zote hizi ni njia muhimu za kuwasilisha hisia za upendo kwa mwenzi wako. Kwa watu wengine, mgoso wa mwili ndiyo lugha yao ya msingi ya upendo. Bila ya hiyo, hawajisikii kupendwa. Ikiwepo hiyo, hujisikia salama ndani ya pendo na mwenzi wao.

a. *Vipokea mguso viko kila mahali katika mwili, kwa hiyo kumgusa mwenzi wako eneo lolote la mwili kwa namna ya kimahaba kwaweza kuashiria upendo.* Hata hivyo, miguso fulani yaweza kumsisimua zaidi kuliko mingine. Mwenzi wako atakuongoza. Usilazimishe kumgusa kwa namna Yak wewe au kwa wakati wako. Ikiwa mwenzi wako hafurahishwi na miguso ya namna fulani, kuendelea kufanya hivyo kunawasilisha kinyume cha upendo, na kuonyesha kuwa hujali hisia zake. Usifanye kosa la kufikiri kuwa mguso unaokuletea wewe burudiko utamletea na yeye burudiko pia.

b. *Mguso wa mwili unaweza kuwa muhimu sana hasa nyakati za mapito magumu. Inaonyesha ukaribu na mshikamano na mtu anayeteseka.*

c. *Wanaume na wanawake waonyesha kuwa na mahitaji tofauti ya miguso ya kingono.* Kwa wake wengi, hamu ya kujamiiana na waume zao huletwa na ile hali ya kujua kuwa wanapendwa na waume zao. Endapo wanahisi kutokupendwa, kwa kawaida watajihisi "wametumiwa" katika hali ya ngono. Hamu ya mwanamume ya ngono ina kiini katika hali ya mwili zaidi—kujengeka kwa chembechembe za shahawa na manii katika ogani itoayo manii: ogani hiyo inapojaa, kunatokea msukumo wa mwili kuachia. Wana ndoa wengi wanahitaji kutambua tofauti hizi. Hata hivyo, kama asemavyo Chapman: "Kwa kweli, wakati mke wake anaposema lugha yake ya msingi ya upendo na tangi lake la hisia za upendo linapojaa, na yeye akasema lugha yake ya msingi ya upendo, na tangi la hisia za upendo la mke wake likijaa, swala la ngono katika uhusiano wao litajishughulikia lenyewe. Matatizo mengi ya tendo la ndoa katika ndoa nyingi hayasababishwi na ule ujuzi wa namna ya kufanya tendo hilo bali zaidi sana katika eneo la kukidhi haja za hisia." (136)

## UWAKILI WA FEDHA NA MALI

### I. Mtazamo wa Ki-Biblia wa Fedha na Mali[3]

**A.** ***Mungu ndiye Mkuu juu ya vyote, zikiwako fedha na mali.***

1. Mungu aliumba—na anamiliki—dunia na kila kitu kilichomo ndani yake **(Mwa 1:1; Law 25:23; 1 Nya 29:16; Zab 24:1; 50:10-12; Hag 2:8).**

2. Mungu ndiye anawasimamia wanadamu wote, kutoka kuzaliwa hadi kufa **(Kut 4:11; Ayu 12:9-10; Zab 139:13-16; Mith 22:2; Isa 44:24; Eze 24:15-18).**

3. Mungu anawamiliki hasa Wakristo wote **(Rum 14:7-8; 1 Wakor 6:19-20; 7:23; 1 Pet 1:17-19; 2 Pet 2:1).**

4. Mungu huwainua watu, na ndiye anayewashusha watu chini — ikiwa ni pamoja na kuwafanya wengine matajiri na wengine masikini **(1 Sam 2:7; 1 Nya 29:12-16; Ayu 42:10; Zab 75:6-7; Mhu 5:19; Dan 2:20-21; 1 Tim 6:17).**

**B.** ***Chochote tulicho nacho si "mali yetu" hasa—yote tumekabidhiwa tu na Mungu; sisi tu mawakili wake (m.y, waangalizi wa mali zake) na tutatakiwa tutoe hesabu ya uwakili wetu.***

1. Kuwa na fedha na mali kiasi fulani ni lazima. Mambo hayo ni mazuri, na yametolewa kwetu na Mungu kama baraka kwetu kuyafurahia na kuyatumia kwa busara (**Mith 22:4; Mdo 14:17; 1 Tim 4:4-5; 6:17**).

2. Sisi tu mawakili wa Mungu wa kila kitu alichokiweka kwetu kuchanganya fedha zetu na mali zetu **(Mwa 1:27-28; 1 Nya 29:14-16; 1Kor 4:1-2; 1 Pet 4:10).**

3. Tunatakiwa kutumia fedha na mali ambazo Mungu ameweka kwetu kama wasimamizi kwa busara, kumheshimu yeye kwa kufanya mambo mema kwa rasilimali zetu na kutumia rasilimali zetu kuujenga ufalme wake, kwa sababu tutatoa hesabu kwa jinsi tulivyofanyia uwakili wake kwake **(Mith 3:9; Math 25:14-30; Luka 12:35-48; 16:1-13; 19:11-27; 1 Tim 6:17-19).**

[3] Mtazamo huu wa Ki-Biblia unapaswa usomwe pamoja na sehemu zifuatazo kuhusu Utoaji na Makosa ya Injili ya Mafanikio. Sehemu hizo zina vipengele vingi muhimu vya undani, maelezo, na vigezo ambavyo ni vya lazima kwa ajili ya kuelewa vizuri zaidi mtazamo wa Biblia kuhusa fedha na mali. Kitabu bora zaidi kuhusu theolojia ya fedha na mali ni: Craig Blomberg, *Neither Poverty nor Riches* (NSBT 7), Nottingham, England: Apollos, 1999.

**C.** ***Mungu anaweza kutubariki kwa fedha na mali, lakini jinsi atakavyotubariki ni ikiwa tutafanya kazi vizuri, tukimweka Yeye na maswala yake nafasi ya kwanza maishani mwetu.***

1. Ingawaje kupenda fedha—kuwa mbinafsi na kuitumainia, na kujiamini au na kuweka matumaini katika hiyo—ni dhambi, kupata mali na kuishi maisha mazuri zaidi ni mambo yafaayo (**Kum 6:10-11; 1 Wakor 7:21; 1 Tim 6:17).**
2. Mungu alituumba ili tufanye kazi—kazi ni njema na ina heshima yake, na inapaswa ifanywe kwa kumheshimu Mungu (**Mwa 2:15; Mith 6:6-11; Waef 4:28; 6:5-8; Wakol 3:22-25; 1 Wathes 4:11; 1 Tim 6:1-2; Tito 2:9-10).**
3. Kwa kupitia kufanya kazi na kujihusisha na biashara, Mungu huwapa watu uwezo wa kupata fedha **(Kum 8:16-18; Mith 13:11; 22:29; 28:19-20; Waef 4:28; Yak 4:13-15).**
4. Biblia inaagiza watu kutokuwa wavivu au wazembe, lakini kuwa na bidii katika kazi—ndiyo njia ya kupatia mafanikio ya vitu (**Mith 6:6-11; 10:4-5, 26; 12:11, 24, 27; 13:4, 11; 14:23; 15:19; 16:26; 19:15; 20:4, 13; 21:5; 24:30-34; 27:23-27; 28:19; Mhu 10:18; Waef 4:28; 2 Wathes 3:6-13**).

**D.** ***Kitu muhimu kuliko vyote kwetu ni kuwa na mtazamo na vipaumbele sahihi kwa Mungu, fedha, na mali.***

Biblia haisemi kwamba kuwa tajiri ni lazima iwe ndiyo ishara ya kibali cha Mungu (ona **Marko 10:23-25**). Wala hakuleti sifa njema kwa kuwa masikini. Ingawaje tunapaswa tufanye kazi kupata fedha (ona hapo juu, hatupaswi "kuhangaikia" hizo (**Mith 28:20-22**) au kukimbizana ili kupata utajiri (**Mith 23:4-5**). Hali zote mbili; umasikini mkuu na utajiri mkuu husababisha hatari zake (**Mith 30:8-9**). Kwa hiyo, Biblia "huulinganisha" utajiri wa mali waonekana duni kutokana na uthamani wake wa kitambo, ukilinganishwa na zile ambazo ni kuu zaidi, na zidumuzo za hekima, haki, unyofu, upendo, wema, mahusiano yetu na Bwana, nk. (**Mith 3:13-16; 8:10-11; 15:16; 16:8, 16; 19:1; 22:1; 28:6; Math 16:26; Marko 8:36; 1 Cor 13:3; Wafil 4:10-13; Waeb 10:34; 1 Yoh 2:15-17; Ufu 2:9; 3:17-18**). Vivyo hivyo, Biblia siku zote huweka"mtazamo wa kimilele" katika kuangalia, kwa kusisitiza hukumu ijayo ambapo makosa yote yatahukumiwa na ambapo mali zote za kidunia za mtu zitakuwa hazina thamani (**Mith 10:2; 11:4, 28; Isa 2:12-21; Eze 7:19; Zef 1:18; Luka 12:15-21; 16:10-12; Yak 5:1-5**). Kwa hiyo, kote katika Agano la Kale na Agano Jipya, jambo lililo muhimu sana ni mtazamo wetu na vipaumbele vyetu kuhusiana na yote, Mungu na mali zetu. Kusema ukweli, mtazamo wetu kuhusiana na mali zetu huenda ndicho kielelezo muhimu zaidi cha nini mtazamo wetu na vipaumbele vyetu vilivyo kwa Mungu (ona **1 Yoh 3:17**).

1. <u>Kile tunachokifanya kama "hazina" huthibitisha hasa moyo wetu uliko</u> **<u>(Math 6:19-21; Luka 12:33-34).</u>**
2. <u>*Hatuwezi* kumtumikia Mungu na Mali (m.y, fedha na mali)</u> **<u>(Ayu 31:24-28; Math 6:24; Luka 16:13).</u>**
3. <u>Mtazamo wetu kwa Mungu unahusisha yafuatayo:</u>
    a. Mungu na ufalme wake lazima uwe kipaumbele cha kwanza (**Kut 20:1-6; Kum 6:4-15; Math 6:33; 22:34-38; Wafil 2:9-11)**
    b. Ili kumfuata Kristo, ni lazima tuachane na kudai kwamba kila kitu tulicho nacho ni "chetu," lakini ni lazima tutambue kwamba vyote ni mali yake **(Marko 10:17-23; Luka 9:23-25; 14:26-33).**
4. <u>Mtazamo wetu kuhusu fedha na mali unahusisha yafuatayo:</u>
    a. Hatutakiwi kutamani au kuwa wachoyo wa fedha na utajiri wa vitu; wala hatupaswi kuweka tumaini letu katika hizo wala kujivuna juu yake ikiwa tuna zaidi ya tunavyohitaji **(Kut 20:17; Mith 28:20-22; Luka 12:15-21; Waef 5:3; Wakol 3:3-6; 1 Tim 6:17; 1 Yoh 2:15-16).**
    b. Kupenda pesa ndiyo mwanzo wa maovu yote—kunaweza kukwamisha au kulizinga Neno la Mungu maishani mwetu na kusababisha hukumu ya Mungu **(Mith 11:4, 28; Marko 4:18-19; Wakol 3:5-6; 1 Tim 6:10-11; Yak 5:1-6; Ufu 3:17-19).**
    c. Ni lazima tutambue kwamba fedha na mali ni vya kitambo tu **(Mith 23:4-5; 1 Tim 6:7; Yak 1:9-11).**
    d. Badala ya kutotosheka, au kutamani fedha nyingi zaidi na mali zaidi, tunatakiwa kuridhika **(Mith 30:7-9; Wafil 4:10-13; Waeb 13:5; 1 Tim 6:8).**
5. <u>Nyakati zote tunatakiwa tujali na kutenda kwa ajili ya haki za masikini.</u> Lazima tupate mali kwa njia ya uaminifu,na kuonyesha upendeleo au kutumia mali zetu kuwaonea ao kuwadhulumu masikini na wasiojiweza (**Ayu 29:12-17; Zab 41:1; 72:1-4, 12-15; 82:3-4; Mith 17:5; 21:13; 22:16, 22-23; 29:7; 31:8-9; Isa 1:17; 3:14-15; 58:6-7; Yer 9:23-24; 22:3, 16-17; Eze 22:29-31; Amo 2:6-8; 4:1-3; 5:11-12; Mika 2:1-3; Zeka 7:10; Mal 3:5; 1 Wakor 5:9-11; Wagal 2:10; Yak 2:1-7; 5:1-6**).

**E.** ***Uwakili mzuri wa fedha na mali unahusika na yafuatayo:***

1. Kutoa mahitaji kwa ajili Yak na familia Yak **(Mith 21:20; Mhu 5:18-19; 1 Tim 5:4, 8; 2 Tim 2:6).**
2. Kutokupoteza fedha zetu, lakini kuwa mtu azitunzaye kwa ajili ya matumizi ya baadaye **(Mith 13:22; 21:17, 20; Yoh 6:12-13).**
3. Kutoa kwa ajili ya Serikali **(Marko 12:13-17).**
4. Kulipa wanaodai **(Zab 37:21).**
5. Kutoa kwa ajili ya masikini na wahitaji **(Kut 23:10-11; Wal 19: 9-10; Kum 15:10-11; 24: 19-21; Zab 41:1; 112:5-6; Mith 3:27-28; 14:21; 19:17; 22: 9, 22; 31:20; Isa 58:6-7; Eze 16:49; Math 25:31-46; Marko 10:21; Luka 3:10-11; 11:41; 12:33; Rum 12:20; Wagal 2:10; Waef 4:28; Yak:27).**
6. Kuwapatia waamini wenzetu **(Rum 12:13; 15:25-27; 1 Wakor 16:1-4; 2 Wakor 8-9; Yak 2:14-18; 1 Yoh 3:17-18).**
7. Kutoa kwa ajili ya huduma **(Wagal 6:6; 1 Wakor 9:3-14; 1 Tim 5:17-18).**

**F.** ***Kwenye kitovu kabisa cha uwakili wetu wa fedha na mali, ni utoaji.***

1. Kanuni ya Yesu ya msingi ni, "bora kutoa kuliko kupokea" **(Mdo 20:35).**
2. Kutoa kwetu ili kuwasaidia wale wenye mahitaji na kujenga ufalme kunapaswa kuhusishe yafuatayo:
   a. Kutoa mara kwa mara **(1 Wakor 16:1-2).**
   b. Kutoa kwa makini (m.y, kupanga jinsi ya kutoa) **(2 Wakor 9:7).**
   c. Kutoa kwa hiari **(Kut 22:29; 2 Wakor 8:3, 8; 9:7).**
   d. kutoa kwa moyo mkunjufu **(2 Wakor 9:7).**
   e. Kutoa kwa ukarimu **(Kut 36:3-7; 2 Wakor 9:6; 1 Tim 6:18).**
   f. Kutoa kulingana na alivyo navyo mtu **(Hes 35:8; 1 Wakor 16:2; 2 Wakor 8:12).**
   g. Kutoa dhabihu **(Marko 12:41-44; 14:3-9; 2 Wakor 8:1-3).**
   h. Kutoa ili kumpendeza Mungu, siyo ili kutazamwa na watu **(Math 6:1-4).**

**G.** ***Mungu hubariki na hutoa thawabu kwa matumizi na uaminifu wa fedha na mali.***

1. Mungu atatupatia mahitaji yetu ya kimwili ikiwa tutamweka yeye nafasi ya kwanza na kuwa waaminifu **(Math 6:25-33; 2 Wakor 9:6 -11).** Hiyo haimaanishi kwamba Yeye "kiuchawi" au kimuujiza tu atakidhi haja zetu, kutosema lolote kuhusiana na haja zetu, au mahitaji yetu. Kimsingi, Mungu amelipangia kanisa—waamini wengine—kuwa ndiyo njia ambayo ataitumia kukutana na haja zetu (**Marko 10:28-30; Luka 18:28-30; Mdo 2:43-47; 4:32-37; 11:27-30; 15:25-27; 1 Wakor 16:1-4; 2 Wakor 8:1-15**).
2. Mungu atashughulika nasi kwa jinsi hiyo hiyo tunavyozitumia rasilimali zetu kuwasaidia wengine na kuujenga ufalme, ama kwa uhaba au kwa ukarimu. Hilo si lazima limaanishe kwamba Mungu atatupa utajiri wa mali hapa duniani ikiwa tutakuwa wakarimu na waaminifu kwa fedha zetu na mali zetu. Hata hivyo, Mungu atatubariki, ama kwa vitu au kwa njia nyingine, ikiwa tutakuwa mawakili wazuri wa fedha na mali zetu **(Mith 3:9-10; 11:24-25; 28:27; Mal 3:8-12; Marko 10:28-31; Luka 6:38; Wagal 6:6-7; 2 Wakor 9:6-11).**

**H.** ***Kwa sababu ni uwakili utokao kwa Mungu, matumizi yetu ya fedha na mali kusema kweli ni swala la kiroho la umuhimu mkubwa rohoni.***

1.Mtazamo wetu na vipaumbele vyetu kwa mali huenda ndicho kielelezo muhimu cha kuonyesha mtazamo wetu wa kweli na vipaumbele kuhusu Mungu (ona **Yak 2:14-18; 1 Yoh 3:17**). Utoaji kwa maskini na wenye uhitaji huonyesha kwamba tunaelewa maandiko na injili **(Neh 8:8, 10, 12; Mdo 2:42-47; 4:32-35**

2. Biblia hutumia maneno ya "kiroho" kuelezea utoaji wa fedha kuwasaidia masikinina wahitaji:
   a. *Charis*—neno lililotafsriwa kuwa "neema" au "kazi ya neema" katika **2 Wakor 8:1, 6, 7, 9, 19, 9:8,** na **14**; lililotafsiriwa "neema" in **2 Wakor 8:4**; na kutafsiriwa kama "shukurani" katika **2 Wakor 8:16** na **9:15.**
   b. *Koinonia*, ambalo kikawaida humaanisha "kushiriki pamoja" or "ushirika"—lililotafsiriwa kama "kushiriki" katika **2 Wakor 8:4**; na kutafsiriwa kama "michango" katika **2 Wakor 9:13.**
   c. *Leiturgia*, ambalo tunapata neno "liturujia"—linalotafsiriwa kuwa ni "ibada" katika **2 Wakor 9:12.**
   d. *Diakonia*—linalotafsiriwa kuwa "huduma" katika **2 Wakor 9:1, 12-13.**
3. Kutoa ni aina ya kuabudu **(Math 2:11; Marko 14:3-9).**
4. Kutoa ni udhihirisho wa imani **(Yak 2:14-18; 1 Yoh 3:17-18).**

5. Kutoa ni sehemu ya dini ya kweli, aina ya huduma ilinganayo na dhabihu ya Agano la Kale kwa Mungu (**2 Wakor 9:1, 12-13; Wafil 4:18; Waeb 13:16; Yak 1:27).**
6. Kile tunachokifanyia fedha zetu na mali hutuletea matokeo yahusikayo na mambo ya kiroho sasa, na baadaye katika milele ijayo (**Zab 41:1-3; 112:5-6; Mith 19:17; 22:9; Math 6:3-4; 19-21; 19:21; 25:19-30; Luka 12:33-48; 16:9, 19-31; 19:15-26; Mdo 10:4; Wafil 4:17; 1 Tim 6:18-19).**

**I.** ***Uwakili wa kiMdoo unaohusu fedha na mali***

1. Mpango. Mtu anayeshindwa kupanga mipango, anapanga kushindwa (ona **Mith 21: 5**). Watu matajiri hupanga mipango kuwa matajiri; watu masikini hawana mipango yoyote. Unahitaji kufikiria na kupanga mipango ya muda mfupi na kwa mipango mirefu. Kwanza, unapanga malengo; kisha unaandaa mpango ili kufanikisha malengo Yak; kisha unatendea kazi mpango wako na kuuendeleza na kuutathmini mara kwa mara. Unapaswa kuuweka mpango wako katika maandishi. Lazima uanzie hapo ulipo, hata kama utakuwa kama huna fedha. Mpango mzuri ni "mpango wa 70-10-10-10 " (Bruenning, n.d.:15-17):

a. *Ishi kwa kutumia 70% ya kipato chako.* Ikiwa unaingiza $100 kwa mwezi, jifunze kuishi kwa kutumia $70 kwa mwezi. Itakubidi utafute njia za kupunguza gharama ya kuishi. Ni lazima uonyeshe kwamba umeamua kufanya hivyo. Ikiwa umepania vya kutosha, njia itapatikana. Panga mpango na uuandike kwenye karatasi. Ni lazima ujipe nidhamu mwenyewe na fedha zako.

b. *Weka akiba 10% ya kipato chako.* Watu matajiri huweka akiba fedha zao na hutumia kile kilichobaki; wakati watu masikini hutumia kile walicho nacho na kuhifadhi kilichobaki. Matokeo ni kwamba masikini huwa hawabakiwi na kitu chochote. Hutumia chote kabisa. Anza kuweka akiba kwenye akaunti ya Benki yoyote iliyo karibu. Kila siku ya kupokea mshahara, weka 10% katika Benki. Jifunze kuweka akiba kwanza na kutumia baadaye. Kama ungejifunza kufanya hivyo tangu ukiwa kijana, ungekuwa na fedha nyingi sana leo hii.

c. *Toa 10% ya kipato chako.* Watu wengi walio masikini huutumia umasikini wao kama kisingizio cha kutoa. Mpango wa Mungu ni kwamba tutoe kwa imani, upendo, na utiifu kwake. Tunavuna kile tukipandacho. Tukipanda mtama, tunapata mtama; tukipanda mahindi, tunavuna mahindi. Vivyo hivyo na fedha. Jifunze kuwa mpandaji mzuri. Tukitoa kwa kazi ya Mungu — ambako itatenda vizuri kwa kuokoa roho za watu na kujenga ufalme — Mungu ataona na kukurudishia. Kumbuka, hata hivyo, kuna wakati wa kuvuna: usitegemee kupanda leo na kuvuna kesho.

d. *Wekeza 10% ya kipato chako.* Tafuta kitu ambacho utakinunua na kukirekebisha, na kisha ukiuze kwa bei ya juu zaidi. Unaweza kuchukua miezi kadhaa kukusanya fedha za kuwekeza ili uitumie kwa kazi hii. Hata mtu masikini katika nchi iliyo masikini kabisa anaweza kununua bidhaa za chakula, au pipi, na kuuza kupata faida. Huko ndiko kuwekeza kibiashara. Hata hivyo jambo muhimu hapo usitumie faida ile, lakini uiwekeze ili kuzaa fedha zaidi. Unaweza kuuza peremende; lakini kwa kuweka akiba na kuwekeza akiba baadaye utaweza kumiliki nyumba na kukodisha jengo au kuwa na miradi kadhaa ikiendelea itakayozaa faida nyingi zaidi. Kuna mambo mengi unaweza kuyafanya, ama kibinafsi au pamoja na wengine, kuwekeza ili kupata fedha: kuwekeza katika mashine ya ushonaji na kutengeneza na kuuza nguo; kuwekeza katika pikipiki na kisha kumkodishia mtu ambaye atakuwa anabeba abiria, ambapo atakulipa kiasi fulani cha fedha kwa siku kwa kutumia piki piki hiyo, naye atajipatia kipato kwa fedha zilizobakia kwa kazi yake hiyo ya ubebaji abiria; kupanda miri kwenye kiwanja chako na kuiuza kwa makampuni yanayohitaji kuni, au makampuni ya ujenzi, nk. La msingi ni kuwa na mpango na kuufanyia kazi mpango huo. Kama kuna watu wawili wanaofanana, na moja anafanyia kazi mpango huu wa 70-10-10-10 na mwingine hana mpango, lakini anazitumia tu fedha zake. Mwisho wa miaka 15, yule mtu mwenye mpango atakuwa tajiri, na yule mtu asiye na mpango atakuwa masikini.

e. *Unaweza usiweze kuanzia kwenye 70-10-10-10 mara moja, lakini ukaanzia kwenye 80-10-10.* 80-10-10 ni hai kwa 80% ya kipato chako, hifadhi 10%, na utoe 10%. Ufunguo ni kwamba anzzia mahali fulani, na uanze sasa.

2. Bajeti. Bajeti ni msaada kamili wa kukusaidia kufuatilia kipato chako na matumizi Yak, na kupangia na kudhibiti kile unachokifanya na fedha zako (m.y., inakwenda wapi). Weka bajeti Yak kimaandishi. Ili kuandaa bajeti, unachohitaji tu ni kipande cha karatasi, peni au penseli. Unapaswa uorodheshe kipato chako na matumizi Yak *kwa kila mwezi.*

a. *Andika kipato chako.* Ikiwa kipato chako hakieleweki, basi tumia wastani tu, kwa kutegemea

makadirio ya matumizi.
b. *Orodhesha gharama za maisha.* Orodhesha gharama za maisha zisizobadilika na kadiria gharama zinazobadilika. "Gharama zisizobadilika" ni vitu vile ambavyo viko pale pale kila mwezi. Ni pamoja na ile sehemu ya "10-10-10" ya ule mpango wa 70-10-10-10; k.m. Gharama za maji na umeme au kodi nyingine za nyumba, nk. "Gharama zinazobadilika" ni zile gharama ambazo wewe unaweza kuzidhibiti. Ni pamoja na chakula, matumizi mdogo dogo, mavazi, dawa, burudani, nk.
c. *Linganisha gharama zako na kipato chako.* Tafuta njia za kuishi kwa 70% ya kipato chako. Punguza gharama zinazobadilika. Hata gharama za nyumba zinaweza kupunguzwa kwa kuhamia sehemu nyingine au mahali pengine. Simamia bajeti Yak na uitathmini mara kwa mara. Bajeti yenyewe kimsingi ni plani au mpangilio wa baadaye. Unahitaji kufuatilia kipato halisi na matumizi ili kuona yanavyolingana na bajeti. Kisha utahitaji kufanya marekebisho yoyote ambayo yanaweza kuwa yanahitajika.
d. *Ili kuanza kupanga bajeti,unatakiwa kuwa na wazo zuri la nini unafanya na fedha zako kwa sasa.* Watu wengi hawana mawazo mazuri juu ya kiasi gani halisi cha fedha wanakipokea, na wapi hasa zinakwenda. Matokeo yake, hawawezi kupanga bajeti ya maana, na pia hawawezi kuamua ni wapi wapunguze matumizi. Hapa kuna mapendekezo ya kukusaidia kujua hali Yak ya kifedha (wewe na mwenzi wako mnahitaji kulifanya hili pamoja): Kwa miezi ifuatayo 3 au 4 andika kwenye kikaratasi kila shilingi/ faranga/ au dola au fedha inayokujia (m.y kipato chako) na kila shilingi/ faranga/ au dola au fedha yoyote inayotoka nje (m.y, matumizi Yak). Hakikisha unaorodhesha vyanzo vya kila kipato na kila matumizi yalikuwa ya nini. Uwe unaweka vikaratasi hivyo vyote katika bahasha kubwa. Kumbuka, *kila* shilingi/ faranga/ rupia au dola au fedha yoyote — bila kujali ni ndogo kiasi gani — lazima ihesabiwe. Mwisho wa miezi hiyo 3-4 kaa pamoja na mwenzi wako, fungueni bahasha hiyo, kisha jumlisheni kupata jumla zake. Orodhesha vyanzo vya kipato na kisha vile vya matumizi kundi lake pia (akiba, utoaji, kodi, mafuta, vocha za simu, chakula, soda, usafiri, nk.). Ndipo utakuwa na picha nzuri ya nini hasa *kipato chako halisi na matumizi Yak halisi yalivyo*. Huenda ukashangazwa kuona ni kiasi gani, au ni kidogo kiasi gani, unatumia katika maswala fulani. Hata hivyo, ikiwa hujijui kabisa ulipo, hutaweza kufanya mabadiliko yatakiwayo kukufikisha pale unapotaka kuwa.
e. *Ifuatayo ni mfano wa bajeti ya kaya moja, ambayo unaweza kuirekebisha kulingana na mazingira Yak:*

| KIPATO CHA MWEZI | MATUMIZI KWA MWEZI |
|---|---|
| Mshahara | Utoaji |
| Kukodisha | Akiba |
| Faida/Gawio la hisa | Kuwekeza |
| Uwekezaji | Kodi |
| Mengineyo | Chakula (waweza kufafanua) |
| JUMLA | Bili ya maji, umeme n.k, |
| | Petroli, mafuta ya taa, kuni, mkaa n.k. |
| | Kuongea kwa simu |
| | Usafiri |
| | Burudani/mapumziko (elezea) |
| | Mavazi |
| | Matibabu |
| | Mikopo |
| | Bima |
| | Kodi ya mapato |
| | Mengineyo (elezea) |
| | JUMLA |

3. Jielimishe na ujifunze. Usiwe mfuasi; uwe mwanafunzi. Ukitaka mali, ni lazima ujifunze maswala ya mali. Soma. Ongea na wale waliofanikiwa. Tenda kwa busara na kile ulicho nacho. Jizoeze uvumilivu na kiasi katika kila maamuzi ya kifedha. Uwe macho na miradi ya "kukutajirisha haraka" na maamuzi ya kifedha ambayo yanahitaji utekelezaji wa mara moja. Zuia kuendekeza hilo. Usitumie fedha nyingi kwa mambo yasiyo muhimu.

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

## II. Kutoa[4]

**A. *Mungu ni mtoaji.***

1. Utoaji ni sehemu ya tabia ya Mungu.

a. *Mungu alitoa kuanzia mwanzo wa uumbaji.*

(1) Mungu alitoa uhai au uzima kwa Adamu na kumwita kuwa katika uhusiano na Yeye mwenyewe (**Mwa 1:26-27; 2:15-17**)

(2) Mungu aliumba dunia hii ya ajabu na kumpa Adamu kuitawala kama mwakilishi wake (**Mwa 1:28**).

(3) Mungu alimpa Adamu mke (**Mwa 2:18**).

(4) Baada ya Adamu kutenda dhambi, Mungu alimpatia ahadi ya mkombozi atakayekuja (**Mwa 3:15**).

b. *Mungu anaendelea kutoa vipawa hivi kwa mwanadamu hata kama wengi wako katika uasi kinyume naye.* Hutoa na kusamehe bila kujali hali ya kustahili kwetu, lakini hasa ni kutokana na neema na rehema zake.

(1) Huitamalaki dunia pamoja na yuko kazini akivitunza viumbe vyake licha ya dhambi zao. (**Ayu 38-39; Zab 104:1-32; Mate 17:28; Wakol 1:16-17; Waeb 1:2-3; 2 Pet 3:5-7**).

(2) Mungu hutoa baraka kwa wanadamu wote.

(A) *"Maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki"* (**Math 5:45**).

(B) Mungu hutoa vipawa na uwezo wa aina mbali mbali kwa watu wote ili kuwawezesha kubuni vitu vya kupendeza, kupiga hatua za kiafya, na kiteknolojia, na zaidi kuboresha maisha duniani.

(3) Mungu kwa kujitoa huizuia dhambi ya dunia.

(A) Mamlaka ya kiraia "yamewekwa na Mungu" ili kusimamia uratatibu na kuadhibu watendao makosa (**Rum 13:1-6**).

(B) Ukuu wa Mungu huweza kutenda katika mazingira ya kawaida hata kupunguza tabia ya dhambi ya mtu (ona **Mwa 20:6, 1 Sam 25:26**).

(C) Licha ya anguko la mwanadamu katika dhambi, na uasi kinyume na Mungu, Mungu hutenda katika dhamiri zetu, ili watu wote wajue kwamba Mungu yupo, na kujua tofauti kati ya wema na ubaya (**Rum 1:18; 20; 2:14-15**).

(D) Wema wa Mungu, uvumilivu, na saburi yake, uliwafanya watu watubie njia zao za dhambi (**Rum 2:4**).

c. *Mfano mkubwa kabisa wa neema na upendo wa Mungu ni "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"* (**Yoh 3:16;** ona pia **1 Yoh 4:10**).

(1) Mungu aliuonyesha upendo wake kwetu sisi *"wakati tukiwa tungali wadhambi" Kristo alikuja kutuokoa* (**Rum 5:8;** ona pia **1 Tim 1:16**).

(A) Kristo alichukua nafasi yetu na kutii kikamilifu maagizo yote ya Mungu (**Rum 8:3-4**).

(B) Alisimama mahali petu, akafa kwa niaba yetu, na kupokea hukumu yote ya Mungu kuhusu dhambi zetu (**Rum 8:31-32**).

(2) Tunapomwamini Kristo, Mungu hutuingiza katika familia yake, nasi tunapokea *"baraka zote za rohoni katika ulimwengu wa roho,"* na kupewa urithi wa uzima wa milele katika Yeye (**Waef 1:3-14**).

(3) Mungu hujitoa mwenyewe kwa watoto wake kwanza, kisha huwapatia baraka za mwilini ambazo wanazihitaji. (**Rum 8:32**).

d. *Kwa hiyo, historia nzima ya mwanadamu na tukio zima la ukombozi imefungamanishwa pamoja katika ukweli kwamba Mungu ni Mtoaji.*

(1) Wema wa Mungu, neema, na rehema, vyote ni vipengele vya "utoaji".

(2) Kanuni hii ya Mungu kama mtoaji inahusika katika kila tendo la Mungu kwa mwanadamu, na hasa kwa wadhambi onaowakomboa.

[4] Kanuni za utoaji hasa hasa ndani ya kanisa la Afrika zimejadiliwa katika mafunzo ya Kibiblia kwa uongozi wa Mch. Daniel Oguso Obiero, *Christian Giving* (Nairobi: O.A.I.C./T.E.E., 1995). Maswali ya kusaidia mchanganuo wa mjadala yamejumuishwa pia.

(3) Tabia ya Mungu kama mtoaji ndiyo msingi hasa wa maisha yetu ya kiroho.

2. Kama watoto wa Mungu, tumeitwa tufanane naye kwa sura yake.

a. Katika **Mwa 1:26-27** Mungu alisema: *"Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya ya nchi." Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.*

b. *Sura iliyo kamilifu kuliko zote ya mfano na uwakilishi wa Mungu ni Yesu Kristo.* Maandiko yanamwita rasmi Yesu kwamba ni "sura ya Mungu" (**2 Wakor 4:4; Wakol 1:15**) na "mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake " (**Waeb 1:3;** ona pia **Yoh 14:8-9; 1:1:18; 2 Wakor 4:6**). Katika Kristo tunaona sura wa Mungu katika utimilifu wote. Matokeo yake, "Hakuna njia iliyo bora zaidi ya kuuona uso wa Mungu kuliko kumwangalia Yesu Kristo. Kile tukionacho na kukisikia katika Kristo Yesu ndicho alichokikusudia Mungu kwa mwanadamu" (Hoekema 1986: 22).

c. *Watu wote bado wanabeba sura ya Mungu hata ingawa mwanadamu aliangukia katika dhambi* (**Mwa 5:1-3; 9:6; Yak 3:9-10**). Kwa sehemu fulani, ile sura ya Mungu inakaa ndani ya watu wote kama sehemu ya uanadamu wetu. (Ona pia **Zab 8** ambayo, ingawa haitumii maneno "sura ya Mungu," inamzungumzia mwanadamu kulingana na mpango uliowekwa pale katika **Mwa 1**.)

d. *Hiyo sura ya Mungu inahusiana na "nafsi mpya" katika Kristo, ambayo tunaionyesha katika maisha yetu (ona **Rum 8:29, 2 Wakor 3:18, Waef 4:22-24,** na **Wakol 3:9-10** ambayo wote wanaizungumzia, sura katika utendaji na kitabia).* Hii inaonyesha kwamba, kinamna fulani, sura ya Mungu iliharibika kutokana na dhambi, na hatuna tena kikamilifu. Sura ya Mungu inafanyishwa upya katika maisha ya watu wanapokuja kwenye mahusiano ya kiwokovu na Baba kupitia Kristo, na kutakaswa hatua kwa hatua kiutii kwa Mungu na kujitoa kwa ajili ya kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha yao. Kusema kweli, njia moja ya kuutazama utakaso ni kuirejesha tena sura ya Mungu katika utimilifu wake wote kwa watu waliokombolewa.

e. *Kama watu wenye sura na mng'ao wa utukufu wa Mungu, tunapaswa kuwa watoaji.*

(1) Moja ya maeneo ambayo sura ya Mungu huonekana wazi ni katika swala la utoaji.

(2) Utoaji wa fedha na mali ni njia mojawapo tu kati ya picha kubwa zaidi ambayo tumeitiwa kuwa wakarimu kwa wengine (ingawaje ni ya muhimu).

(3) Moyo wa utoaji unafanya msingi kwa huduma ya Ukristo, kama Yesu alivyosema: *"mmepewa bure, toeni bure"* (**Math 10:8**).

(4) Kama Kristo, tunapaswa kujitoa wenyewe kwanza na kisha kutoa mali zetu kwa Mungu na kwa wengine (**2 Wakor 8:5, 9).**

(5) Kujitoa kwetu kwa ukarimu na mali zetu kwa wengine kunaonyesha yafuatayo:

(A) Upendo wetu, na utii wetu kwa Kristo.

(B) Neema na Roho wa Mungu katika mioyo yetu na maisha yetu.

(C)Uhalisi wa imani yetu (**Yak 2:14-26**).

(D) Upendo wetu kwa ndugu zetu wa kiume na wa kike (**1 Yoh 3:16-18**).

(E) Wajibu wetu kama mawakili.

**B.** ***Utoaji chini ya Agano la Kale: sheria ya zaka.***

1. Hakuna yeyote aliyewajibika kutoa zaka kabla haijaja Sheria ya Musa, na hakuna mfano wa yeyote kabla ya sheria ya Musa aliyetoa zaka. Hata hivyo, kuna matukio mawili kabla ya sheria ya Musa, ambapo 10% ya vitu fulani vilitolewa:

a. *Katika **Mwa 14:1-24** Abram alitoa kwa hiari yake dhabihu kwa Melkizedeki kiasi cha 10% ya mali alizoziteka kutoka kwa Fal wanne aliowashinda katika vita (ona pia **Waeb 7:4**).* Hili lilikuwa ni tukio la mara moja. Ilikuwa ni zawadi, siyo lazima. Vitu alivyovitoa havikutokana na mali ambazo Abram alikuwa anazimiliki.

b. *Katika **Mwa 28:10-22,** wakati Yakobo alipotoka nyumbani kwake kwenda kutafuta mke, Mungu alimbariki na kumwahidi ya kuwa atarudi nchi ya nyumbani kwake.* Kama ilivyokuwa kwa zile zawadi za Abramu, nadhiri ya Yakobo ilitolewa kwa hiari tu kuhusiana na hali maalum. Kisha Yaobo akaweka nadhiri, kama atarudi salama, atampatia Mungu sehemu ya Kumi ya yote ambayo Mungu amembariki kwayo. Miaka Ishirini baadaye, Mungu alimtokea Yakobo na kumkumbusha kuhusu nadhiri yake (**Mwa 31:13, 41**). Biblia haisemi kikamilifu kama Yakobo alitimiza kiapo chake. Kama alitekeleza, hata hivyo, basi huenda itakuwa ni

wakati alipompatia Esau ile idadi kubwa ya wanyama aliokuwa amejikusanyia (ona **Mwa 32:9-15; 33:1-11**).

2. Israeli ya Agano la Kale ilikuwa chini ya sheria ya kutoa zaka (fungu la kumi) kwa kulitegemeza Hekalu na ukuhani wa Law.

a. "Zaka" maana yake 1/10 (m.y, 10%).

b. *Waisraeli wa agano la kale waliagizwa kutoa zaka mara mbili kwa mwaka; na kila mwaka wa tatu walitakiwa kutoa zaka ya 10% kwa masikini.* Zaka ile ilikuwa ni aina ya kodi ambayo Waisraeli wote "wawe waumini au la" walipaswa kulipa, ili kwamba taifa liweze kudumu katika nchi. Kama wastani wa kipindi hiki cha miaka mitatu, kilaMwisraeli alikuwa anatakiwa kwa sheria kutoa karibu 23% ya kipato chake cha mwaka kwa kazi ya Mungu (Blomberg 1999:46). Alitoa nafaka, mafuta, divai, mifugo, na fedha.

(1) Zaka ya kwanza, ilitolewa kuwasaidia Waisraeli na makuhani, kwa vile Law hawakuwa wamepewa urithi wa ardhi kama walivyopewa kabila nyingine (**Law 27:30-33; Kum 12:18; Hes 18:21-24**).

(2) Zaka ya pili, iliyojulikana kama "zaka ya sikukuu" ilikuwa ni 9/10' ya mabaki yote ya shamba; ambayo hayakutumika kwa sikukuu za mwaka zilitolewa kwa Law (Kum **12:5-7; 14:22-27**).

(3) Zaka ya tatu ilijulikana kama "Zaka ya hiari" na ilitolewa kila mwaka wa tatu kuwasaidia Law, masikini, wageni, yatima, na wajane (**Kum 14:28-29; 26:12**).

(4) Baada ya kupokea zaka, Law walitakiwa kutoa "zaka ya Fungu la kumi" kwa Bwana katika ghala yake (**Hes 18:25-32; Neh 10:38-39**).

c. *Mazao yote, pamoja na nafaka, matunda, divai mpya, na mafuta yalitolewa zaka, pamoja na mifugo, na kondoo (**Law 27:30-33; Kum 12:17; 14:22-23**).*

d. *Hakukuwa na kutoa zaka au fungu la kumi la fedha.*

(1) Mahali pekee ambapo fedha zimetajwa katika utoaji katika Torati ya Musa, kuhusiana na zaka au fungu la kumi, ni wakati mtu anapokuwa mbali mno kutoka "mahali ambapo Bwana Mungu wenu atakapopachagua". (m.y, hema ya kukutania katikati yao) kuileta zaka (m.y., mazao au wanyama), ndipo huyo mtu alitakiwa abadilishe zaka yake kwa fedha, na ailete fedha hadi mahali Bwana alipopachagua, na kisha kuitumia fedha hiyo kwa chakula na kunywa mahali hapo (**Kum 14:24-26**).

(2) Biblia ya *Africa Bible Commentary* inaelezea: "Hatujui ni lini hasa zaka hizo zilikuwa zinatolewa. Huenda zilipelekwa katika hekalu hilo wakati wa mavuno, ujulikanao kama Sikukuu ya vibanda au Sikukuu ya Majuma (Pentekoste) ([Kum] 16:9-17). Lakini kwa kuzingatia ugumu wa kusafirisha vitu kwa umbali mrefu, Kumbukumbu la Torati liliruhusu njia mbadala ya kubadilisha bidhaa hizo kuwa fedha ambazo zingeweza kutumika kununulia bidhaa nyingine za kutolea dhabihu na kwa vyakula vitakatifu vilivyoliwa na nyumba nzima katika hema ya kukutania." (Adeyemo 2006: 230)

e. *Zaka zilizotakiwa zililipwa kuanzia mzaliwa wa kwanza na mnyama aliye bora kabisa, na mavuno ya kwanza (malimbuko) na mazao yaliyo bora kabisa.* Hayo yaliitwa "malimbuko ya mazao" (ona **Kut 22:29-30; 23:14-19; 34:26; Law 2:14; 23:10, 17; 27:26-33; Hes 18:12, 29-32; Kum 12:17; 14:23; Neh 10:34-37; 12:44**).

3. Sheria ya Agano la Kale pia ilirekebisha utoaji mwingine ambao Waisraeli walitakiwa kuufanya:

a. Waisraeli wote walitakiwa kulipa kodi ya nusu shekeli kwa mwaka kuhudmia madhabahu na hekalu (**Kut 30:11-16; 2 Law 24:4-9; Neh 10:32** [ambapo inaelezwa kuwa ni sehemu ya tatu ya shekeli]; **Math 17:24-27**).

b. Dhabihu iliyotolewa kwa makuhani ilikuwa ni mali ya hao makuhani (**Hes 5:9-10**).

c. Watu walikatazwa wasivune mpaka kwenye mipaka ya mashamba yao, au kuvuna matunda yaliyoanguka, au kupiga mara mbili miti ya mizeituni au kuokota mara mbili mizabibu. Mabaki hayo yalikuwa kwa ajili ya wahitaji na wasio Waisraeli (**Law 19:9-10; Kum 24:19-20**).

d. Sikukuu ya Majuma ilitakiwa itegemezwe na dhabihu ya "hiari" (**Kum 16:10**).

e. Dhabihu yoyote ya hiari ya wanyama iliyotolewa kwa kazi ya Bwana ilitakiwa itokane na vilivyo bora kabisa, au wanyama wasio na kilema chochote (**Wal 22:18-25**).

f. *Kama sehemu ya sheria ya Musa waebrania wa Agano la Kale walikuwa wanatakiwa kuwapatia mahitaji ya kifedha na mali masikini na wahitaji:*

(1) Kwa kutoa **(Kut 23:10-11; Law 19: 9-10; Kum 15:10-11; 24: 19-21; Zab 41:1;**

**112:5-6; Mith 14:21; 19:17; 22: 9, 22; 31:20; Isa 58:6-7; Eze 16:49**).
(2) Kwa kukopesha bila kudai faida kwa Waebrania wenzao (**Kut 22:25-27; Kum 15:7-9; Zab 37:26; Eze 18:3**).
(3) Israeli lilikuwa liwe taifa la kuwakopesha wengine (**Kum 15:6**).

4. Waebrania wa Agano la Kale pia walitoa kwa moyo wa kupenda kwao (zaidi na kuzidi kabisa zaka iliyokuwa imewekwa kisheria) kuitegemeza kazi ya Bwana.

a. Wakati hema ya kukutania ilikuwa inajengwa, Waisraeli walitoa *"zaidi kabisa ya kiasi kilichotakiwa kwa ajili ya gharama za ujenzi wake" kiasi kwamba Musa* alitoa agizo kwa watu wawazuie wasiendelee kutoa tena michango yao (**Kut 36:2-7;** ona pia **Kut 38:21-31**).

b. Wakati hekalu la Sulemani lilikuwa linajengwa, *"Na wale walioonekana kuwa na vitu vya thamani wakavitoa vitiwe katika hazina ya BWANA, chini ya mkono wa Yehieli, Mgershoni. Ndipo hao watu wakafurahi, kwa sababu wametoa kwa hiari yao wenyewe, kwa sababu kwa ukamilifu wa moyo, kwa hiari yao wenyewe, wamemtolea BWANA; Mfalme Daudi naye akafurahi kwa furaha kuu."* (**1 Nya 29:8-9;** ona **1 Nya 29:1-9, 17**).

c. Wakati matengenezo mapya ya Hekalu chini ya mfalme Zerubabeli yalipokuwa yanafanywa, watu pia walitoa kwa moyo mkunjufu kuiunga mkono kazi. (ona **Ezr 8:24-34; Neh 10:32-33**).

5. Agano la Kale na Torati kuliwafunganisha utii kwa sheria (ikiwamo kulipa fungu la kumi linalotakiwa na kodi) na mafanikio katika ardhi.

a. *Agano la Kale [la Musa] lilikuwa ni Agano la "Mdo ya sheria", na siyo ya "msingi wa neema " kama lilivyo Agano jipya ambalo linawatawala waamini leo.* Agano la "Mdo ya sheria" ni Agano halali ambalo lina tabia ya "ikiwa uta. . ., ndipo" —yaani, "ikiwa" utatimiza au kutii masharti yote ya Agano, "ndipo" utabarikiwa, lakini ikiwa hutii masharti yote ya Agano, ndipo utakapolaaniwa; na zaidi ya hapo, Agano la Kale lilikuwa kihalali limeunganishwa na baraka na laana za kimwili, na vitu vya kuonekana (ona **Kut 15:26; 19:3-6; Wal 26:1-43; Kum 28:1-4, 15-19; Josh 23:14-16; Yer 11:1-11; Dan 9:11-14; Yak 2:10**). Ndiyo maana sheria ya Musa (Torati) ilikuwa msingi wa hali ya taifa (Israeli), na siyo ya jamii ya kiroho, ambalo ni kanisa. Ushiriki wa Agano la Kale kwa Israeli ulitokana na unganiko la kimwili kwa uwana toka Ibrahimu na Isaaka, siyo kuzaliwa upya, au kubadilishwa kiroho kama ilivyo kwa kanisa. Agano la Musa na sheria (pamoja na sheria ya zaka) ilikusudiwa kulinidhamisha taifa la Izraeli katika nchi.

b. *Kwa sababu agano la Musa na sheria vilikusudiwah kulinidhamisha taifa la Izraeli katika nchi, katika **Kum 26:12-15** kuna uhusiano kati ya zaka na kutoa mazao kwa ardhi ya Israeli.* Katika **Kum 26:16** Musa aliwahimiza rasmi Waisraeli kutii maagizo yote ya Mungu na sheria zake. Katika **Kum 28:12** Mungu aliahidi kwamba *"Atakufunulia BWANA hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi Yak kwa wakati wake na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe "* ikiwa Israeli ingekuwa na uangalifu na kuyatenda maagizo yote ya sheria. Kama Israeli ingeshindwa kutunza maagizo yote, basi Mungu aliahidi kuizuia mvua, na kuyasababisha mazao kuanguka au kupukutisha; na kuliwa na nzige, harare na, madumadu (**Kum 28:23-24, 38-42;** ona pia **Wal 26:3-6; 14-16, 19-26**).

c. *Blomberg anajumuisha:* "Katika fungato la agano hilo la kipekee alililoliandaa kwa Israeli, anagiza utii kwa Tora, na ni ndani ya fungato hili la agano ndipo sehemu kubwa ya Agano la Kale lazima litazamwe. Mara zote huwa zimefungamana na Nchi ya Ahadi na kwa tabia iliyojitokeza ya hekaluni na tabia zake za kuabudu. . . . Lakini mipangilio ya kipekee ya ki-agano kati ya Mungu na Israeli hutuzuia tusiliweke kiujumla kwamba Mungu ni lazima awape thawabu za vitu watu wake katika mataifa mengine au katika vizazi vingine." (Blomberg 1999: 82-83, 51)

6. Katika **Mal 3:7-12** Mungu aliwakemea na kuwapa changamoto Waisraeli wa Agano la Kale kwa kushindwa kwao kutoa kiasi kilichoamriwa cha zaka na dhabihu. *"7 Tokea siku za baba zenu mmegeuka upande, mkayaacha maagizo yangu, wala hamkuyashika. Nirudieni mimi, nami nitawarudia ninyi, asema BWANA wa majeshi. Lakini ninyi mwasema, Turudi kwa namna gani? 8 Je! Mwanadamu atamwimbia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. 9 Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote. 10 Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. 11 Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala*

*hataharibu mazao ya ardhi yenu, wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema BWANA wa majeshi.* [12]*Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema BWANA wa Majeshi."*

a. *Kitabu cha **Malaki** kilitolewa kwa taifa la Israeli baada ya kurudi kutoka utumwa wa Babeli. Kilikuwa mwito wa toba kwa watu kiujumla na hasa kwa makuhani.*

(1) Katika **Hag 1:1-11** Waisraeli walikuwa wamerudi Yerusalemu na walitakiwa kulijenga upya Hekalu. Badala yake, hawakufanya hivyo. Kwa hiyo, Mungu hakuwaletea mvua, akaifanya mimea yao isizae vizuri, na kuwapatia watu ukame na matatizo mengine.

(2) Sasa, katika **Malaki**, hekalu lilikuwa limejengwa, mafanikio ya kimaisha hayakuwa yamewajia. Taifa likawa bado linateseka na matatizo yale yale ambayo walikuwa nayo wakati wa **Hagai** alipowaandikia ujumbe ule. Licha ya hayo, walikuwa wamemsahau Mungu na kumfanya kuwa asiyestahili heshima yake. Makuhani walikuwa wakimtolea *"chakula kilichotiwa unajisi"ama "wanyama walemavu au wagonjwa"* juu ya madhabahu (**Mal 1:7-14**) na kuwasababisha watu wengi kujikwaa (**Mal 2:1-9**). Walikuwa wanawapa talaka wake zao na kuwaoa wanawake wa kipagani (**Mal 2:10-17**). Zaidi ya yote, kadiri taifa la Israeli lilivyoyaasi maagizo yote ya Agano la Kale, lilikuwa pia linakwenda kinyume na sheria zihusuzo zaka na dhabihu. Na kama matokeo ya kutokutii huku, Mungu Aliwaletea laana ya Agano la Kale ambayo alikuwa ameinena katika **Kum 28:15-24, 38-42.**

b. *Ujumbe wa kitabu unaeleweka wazi kuwa unasimamia Agano la Musa na Torati, na baraka na laana za kimwili, zilizoahidiwa katika Torati.*

(1) Taifa zima lililaaniwa, na makuhani ndio hasa waliokuwa wamekosea (ona **Mal 1:6; 2:1-2, 7-9, 13-14; 3:3-4**).

(2) Kifungu hiki ni tukio maalum la Mungu kutumia baraka na laana za Torati ya Musa kwa Israeli. Zote mbili; baraka zilizoahidiwa katika **Mal 3:10**, na laana za **Mal 3:9, 11** zinahusisha ardhi na mazao. Zote zina msingi wake, na hutegemea Agano la Musa la torati, na mapatano maalum ya kimahusiano kati ya Mungu na Waisraeli wa Agano la kale. Zote hizo ni Baraka na laana kwa taifa zima kama taifa; na si Baraka au laana zilizoahidiwa kwa mtu mmoja mmoja atoaye zaka na asiyetoa zaka. **Mal 3:7-12** ni mfano maalum wa Mungu kutimiza ahadi yake ya kuilaani ardhi kwa sababu ya kutokutii kwa watu wake, lakini pia kuwakumbusha watu wake juu ya baraka zake alizoziahidi ikiwa watatii, na kuwapa changamoto watu ili wamjaribu na waone uaminifu wake kwa kutii.

(A) Katika **Mal 3:10** yale *"madirisha ya mbinguni"* au *"malango ya mafuriko ya mbinguni"* ni maneno hayo hayo yaliyotumika katika **Mwa 7:11** na **8:2,** na huzungumzia mvua kubwa.

(B) *Katika **Mal 3:11** lile neno "kuharibu" ni neno lililotafsiriwa kutoka lugha ya Kiebrania, lakini ni dhahiri kutokana na mtiririko wa maelezo hapo kwamba, aina fulani ya mmea unaohusiana na kilimo ndio unaozungumziwa.* Kwa hiyo, Biblia ya NIV inautafsiri mstari huo kama, *"Nami nitayazuia magugu yasiyaharibu mazao Yak."* Biblia ya ESV ina maelezo yaliyofafanua na kusema neno hilo "huenda ni jina la mdudu mharibifu wa mazao, au ni mdudu tu." Ushahidi wa nyongeza wa Biblia kutoka katika lugha ambazo zinakaribiana, unaonyesha kwamba hicho kinenwacho hapo, ni uvamizi wa viwavi (Hurowitz 2002: 327-36).

(C) *Blomberg anajumuisha:* "Malaki anafafanua vizuri sana ile mipango rasmi kwa ajili ya taifa la Israeli. Na mstari wa 12 unaendelea kusema, 'na mataifa yote watawaiteni heri', ufafanuzi wa dhahiri kuonyesha ahadi zile pekee za Ibrahimu katika Mwanzo 12:1-3. Ni muhimu pia kukumbuka mahusiano ya kipee katika Agano la kale kati ya Zaka na dhabihu na desturi za kihekalu. Pasipo kituo kinachofanana cha dhabihu za damu leo, mtu hawezi kuhamisha kiurahisi tu kanuni zote za utoaji kwa madhabahu ya Mungu ya Agano la Kale kwa bajeti za kanisa la kizazi kipya cha Agano Jipya." (Blomberg 1999: 80)

7. Wakristo leo hawako tena chini ya sheria ya zaka.

a. *Sheria ya Agano la Kale la Musa lilikuwa na kazi rasmi na iliyokuwa na mipaka.* Katika

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

**Wagal 3:22-4:11** Paulo anajadili kwamba ile sheria ilikuwa ni "kiongozi" (**3:24-25**), *"mawakili na watunzaji"* (**Wagal 4:2**), ambayo ilikuwa na ulinzi juu ya which had custody over *"watoto wa kambo"* (**Wagal 4:1-3**). "Kifungo kilichojibana sana katika mjadala huu na upana mkubwa wa himizo katika mistari hii inaelekeza kwenye kazi moja ya sheria. Kazi hii ni ya mlinzi ambaye kazi yake ni kuwaongoza kwa umakini na kuwaelekeza watu wa Mungu katika kipindi cha unyonge wa kiroho. Kama zilivyo kanuni za kawaida za kidunia [**Wagal 4:3, 9**], Sheria inaagiza shughuli za kila siku za hao watumikao, mpaka uana unapopatikana. Ilianzishwa kama kitu cha muda, lakini yale manufaa yaliyotegemewa yakitolewa kwa kanuni itendayo kazi kwa dhambi, na kufanya kazi kama 'hatamu' kwa watu ambao wanauwezekano kuanguka dhambini, na kuleta mwangaza mapenzi ya Mungu kama msingi kwa wajibu waa ki-agano. Kwa kule kuja, hata hivyo, kwa imani katika Kristo, tile kazi ya mlinzi na kiongozi inakoma, na Roho anakuwa kanuni iongozayo kwa ndani." (Belleville 1986: 70)

b. *Yesu alisema kuwa nimekuja ili kutimiliza torati. Kwa maana, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, Yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka,"hata yote yatimie." (**Math 5:17-18**). "Yote yalimalizika" pale msalabani (ona **Yoh 19:30; Rum 10:4; Waef 2:14-15; Wakol 2:13-15**).* Pale msalabani, Kristoalianzisha Agano Jipya na, pamoja na hilo, enzi mpya "sheria ya Kristo" (**Luka 22:20; 1 Wakor 9:19-21; 11:25; 2 Wakor 3:5-6; Wagal 6:2**). Hekalu, mfumu wa kidhabihu, ukuhani, na tabia muhimu za sheria za Agano la Kale, zililetwa kwenye kutimilizwa na kumalizika. Utofauti kati ya Myahudi na Mmataifa, imekwisha, naye ametufanya *"mtu moja mpya"* katika Kristo (**Waef 2:11-22**). Kristo alileta "badiliko la sheria" (**Waeb 7:11-12**; **Waeb 8:13**). hiyo "Sheria ya Kristo" siyo tu ni mafundisho ya Yesu, lakini pia ni ya waandishi wa Agano Jipya (ona, k.m, **Yoh 14:24-26; 16:12-15; 17:8, 18-20; 1 Wakor 14:37; Wagal 1:11-12; Waef 2:20; 1 Wathes 2:13; 2 Wathes 2:15; 3:6, 14; Waeb 2:3; Ufu 1:11**). Kwa hiyo, hatuendelei kuwa chini ya kifungo cha Agano la Kale na sheria zake, maagizo yake na amri zake, lakini sasa tuko chini ya sheria ya Kristo (ona **Rum 6:14; 7:6; 1 Wakor 9:20-21; Wagal 3:1-4:7; 5:18;** ona pia **Wakol 2:8-17**).

c. *Kutajwa kwa mara moja na Yesu kuhusu zaka, kulifanyika wakati lile Agano la Kale lilikuwa bado linafanya kazi, kabla Yesu hajaenda msalabani na kuanzisha Agano Jipya.* Yesu alizaliwa "chini ya Sheria" (**Wagal 4:4**). Huo ndio ujumbe ambao Yesu alikuwa anawaambia waandishi na Mafarisayo (ambao pia walikuwa chini ya Sheria), *"Ole wenu, waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache."* (**Math 23:23;** ona pia **Luka 11:42**). "Hiki ndicho kifungu pekee katika Agano Jipya lote ambacho kinaweza kuchukuliwa kuwa kinahimiza utoaji wa zaka. Lakini kile ambacho ni muhimu kukiona ni kuwa, Yesu anakitaka 'mambo yale ambayo ni ya muhimu zaidi ya sheria' (Math. 23:23), ambayo bado yana nguvu mpaka kukamilishwa kwa Agano Jipya la Mungu wakati wa Pentekoste, hasa kwa viongozi wa Kiyahudi ambao walilisoma kiuangalifu sana." (Blomberg 1999: 136)

d. ***Waeb 7:4-10** ndio sehemu pekee ambapo utoaji wa 10% (yaani zaka) umetajwa.* Kifungu hicho hurejea Mwa 14:18-20, ambapo Ibrahim alitoa kwa Melkizedeki 10% ya nyara alizo teka vitani. Hata hivyo, hoja ya kifungu hicho, sio kubainisha kuwa Wakristo wapo chini ya "sheria ya zaka," kwa kuwa Ibrahim hakuwa "chini ya wajibu wa kisheria wa kulipa zaka kwa Melkizedeki kama wana wa Izraeli ambavyo wangepaswa baadaye kwa sheria ya Mungu, kulipa zaka kwa ukuhani wa Kilawi" (Rayburn 1989:1138). Badala yake wazo la kifungu ni kwamba Melkizedeki alikuwa ni mkuu kwa Ibrahim. Kwa sababu Kristo ni kuhani kwa "*mfano wa Melkizedeki"* (**Waeb 7:15-17**), Kristo ni mkuu ukilinganisha a ukuhani wa Kilawi. Kwa kweli, "kama ambavyo sheria ni kielelezo kati ya kuachiliwa kwa ahadi ya neema ya Ibrahim, na utimilifu wake unaodumu katika kuja kwa Kristo . . . hivyo ukuhani wa kilawi ulikuwa ni kielelezo na wa kitambo tuu, baina ya ukuhani wa mfano udumuo wa Melkizedek, na ule halisi udumuo wa kuhani mkuu Kristo" (Jamieson, Fausset, na Brown 1961: 1415). Hivyo, basi utoaji zaka sio hoja ya kipengele hiki, ukiwapo msisitizo wa kipengele hiki kwa ajili yetu leo kuhusu zaka, utakuwa ni hatuko chini ya sheria ya zaka, kwa kuwa sheria ilikuwa ni sehemu ya agano la kale ambalo lilikuwa ni la kitambo nalo nafasi yake imechukuiwa na sheri ya Kristo.

e. *Kwa vile sheria ya Agano la Kale kuhusu zaka ilikuwa ni sehemu ya Agano lile la zamani, la Kale la Musa, na lilikuwa rasmi kwa Waisraeli wa Agano la Kale, Wakristio leo hawafungwi nalo.* Ili kuirudisha ahadi ya **Mal 3:10** kutoka katika baraka ya kimwili kwa taifa, kuileta kuwa

baraka ya mtu binafsi, ni kuuchukua mstari huo nje kabisa ya ujumbe mzima unaohusu baraka na laana za **Kum 28** ambapo ulisimamia. Ken Sarles anasema kwamba baraka na laana za **Kum 28** "zilikuwa zimewekwa kwa muundo wa kihistoria, na kutimizwa katika historia ya taifa la Israeli kama ilivyoandikwa katika Agano la Kale. Baraka na laana kwa taifa la Israeli lililokuwa chini ya sheria, haziwezi kupanuliwa na kusogezwa hadi kwa Watakatifu wa Agano Jipya" (Sarles 1986: 347). Blomberg anahitimisha, "Ardhi na kuabudu katika Agano Jipya, yote mawili kwa uwazi kabisa 'ni ya kiroho', angalau katika kipindi cha kanisa. . . . Hilo ni kusema yametimizwa katika Kristo kwa jinsi ambayo, waamini hawawezi kudai ahadi hizi kwa jinsi yoyote, kimali au vitu katika kipindi kile cha Ukristo." (Blomberg 1999: 83)

8. <u>Ingawaje hatuko chini ya sheria ya Zaka, au sheria nyingine za Agano la Kale, sheria za Agano la Kale na mifano yake hutoa kanuni za msingi za utoaji kwa Wakristo leo.</u>

a. *Sheria za Agano la Kale, amri, na masharti yake, yatazamwe kama mifano ya kanuni ziongozazo zote, au za ujumla wote, ambazo zinaweza kutuongoza kufikia mahali ambapo panaendana na hali zetu za sasa.* Yesu na Waandishi wa Agano Jipya waliziangalia sheria za Agano la Kale (Torati) kama *mifano* ya kanuni zilizo kuu zaidi. Sheria za Agano la Kale ziliweza kuvunjwa wakati unazitimiza kanuni zake. Kwa mfano, Yesu anaitaja "Sheria ya Sabato akiiiekekeza kwake mwenyewe, na kanuni ya rehema (**Math 12:1-8; Marko 2:23-28; Luka 6:1-11**). Yesu na Paulo, wote wanazitaja Sheria za Agano la Kale kama mifano tu, ya sheria kubwa zaidi iitwayo Upendo (**Math 22:37-39; Rum 13:9**).

b. *Kanuni hizi zitumikazo toka Agano la Kale ni pamoja na zifuatazo:*

(1) <u>Wakati watu wa Mungu wanakuwa waaminifu na kuona hitaji muhimu, hutoa kwa ukunjufu na kwa moyo wa hiari.</u> Kabla ya Sheria ya Musa kutolewa, Bibliahusisitiza kwamba wale mababa zetu walitoa kwa ukarimu mali zao. Baada ya Sheria ya Musa kutolewa Waisraeli walikuwa chini ya maelekezo yaliyochambuliwa sana ya utoaji. Mara zote walishindwa kuitii "Sheria" za utoaji. Hata hivyo, walipomweka Bwana kuwa nafasi ya kwanza katika maisha yao, na kukabiliwa na uhitaji fulani muhimu, walitoa kwa moyo wa ukunjufu na wa hiari kupitiliza kabisa ile 23% walitakiwa kutoa kwa sheria. Ujenzi wa hema ya kukutania, Hekalu la Sulemani, na la Zerubabeli, ni mifano mitatu ya hilo. Kusema ukweli, walitoa zaidi ya kutosha—vingi kiasi kwamba Musa ilibidi awaagize wasimamishe kutoa! Huo ndio mtazamo tunaotakiwa kuwa nao leo.

(2) <u>Mungu huwabariki wale wanaowasaidia masikini na wahitaji, lakini yuko kinyume na wale wasiowapa masikini na wahitaji.</u> Masikini na wahitaji wako karibu na moyo wa Mungu. Kwa hiyo, Mungu aliweka "zile sheria za mavuno" ili kuwasaidia masikini na wahitaji (**Law 19:9-10; Kum 24:19-20**). Zaidi ya hayo, aliahidi rasmi kuwabariki wale watakaowasaidia masikini na wahitaji (ona **Zab 41:1-3; 112:5-6; Mith 11:24-25; 19:17; 22:9; 28:27**). Kwa upande mwingine, ghadhabu yake ilikuwa kinyume na wale ambao walikuwa na uwezo wa kuwasaidia masikini na wahitaji, lakini hawakufanya hivyo (**Eze 16:49**).

9. <u>Tabia ya kutoa Zaka katika zama za Agano Jipya inatakiwa iwakilishe nidhamu ya kiroho na "msingi" wa utoaji, ambao kwa huo tunauonyesha umiliki wa Mungu wa fedha zetu zote na mali pia.</u> Kama ambavyo agano la kale ni msingi wa agano jipya, hivyo utoaji wa zaka unapaswa uwe ni "msingi" (na sio "kikomo") cha utoaji wa Agano Jipya.

a. Paulo alitaja utaratibu wa Agano la Kale, kuwa makuhani walitegemezwa kwa mafungu ya Zaka na dhabihu za watu, kama kielelezo cha utegemezaji wa fedha kwa huduma katika Agano Jipya (**1 Wakor 9:13-14**).

b. *Utoaji wa Fungu la Kumi (Zaka) leo ni kama nidhamu ya kujitoa katika kufunga.* Tunapofunga, tunatangaza kwamba Mungu anatupatia chakula, na ya kwamba hatutawaliwi na hamu za vyakula; tunatambua umiliki wake juu ya miili yetu na kujiweka wenyewe, pamoja na matumbo yetu kwake. Zaka (m.y., kutoa 10%) kunawakilisha sheria nzuri "ya kidole" (ingawaje siyo "sheria" kwa Wakristo; hiyo itukumbushe sisi kuwa, ile 90% iliyobakia siyo "yetu," bali yote100% kimsingi ni mali ya Mungu.

c. *Nukuu za Africa Bible Commentary zinaeleza vizuri juu ya kanuni nzuri nyuma ya utoaji wa Fungu la Kumi (Zaka) ambazo tungezitamani:* "Makanisa mengi yanachukulia utoaji wa zaka kama ni njia ya kutufanya tutoe zaka kwa kila kitu tulicho nacho kwa Mungu. Hakuna tatizo na hili, kama litachukuliwa kama kanuni ya kuongozea. Lakini litakuwa ni tatizo kama

litachukuliwa na kuonekana kuwa ni sheria inayomfunga kila mwamini, kana kwamba ndilo agizo la lazima kumfanya mtu ampendeze Mungu. Kanuni ya Agano Jipya inatutaka tutoe kulingana na jinsi Mungu alivyotubariki (1 Wakor 16:1-2; 2 Wakor 8:13-15). Hii itakuwa na maana kwamba wale ambao wamebarikiwa kwa wingi watakuwa na uwezo wa kutoa zaidi ya lile Fungu la Kumi. Kristo alijitoa mwenyewe kikamilifu kwetu. Kwa nini tujilimbikizie wenyewe na kumpa kidogo sana? Lakini bahati mbaya viongozi wa kanisa hawawezi kuikuza kanuni hii na badala yake wanainua utoaji wa zaka kama ndiyo sheria. Waamini wataridhika tu kutoa lile Fungu la kumi, wakati wangeweza kutoa zaidi ili kusaidia kutosheleza mahitaji ya kanisa katika Afrika. Kile ambacho tunatakiwa kuwa tunakifanya na roho ya Fungu la kumi, ingekuwa ni kuwatia moyo waamini kutoa zaidi, na siyo kuwawekea dhamira ya hukumu wale ambao kwa sababu moja ama nyingine hushindwa kutoa." (Adeyemo 2006: 230)

10. <u>Kiwango cha utoaji katika Agano Jipya siyo Zaka au Fungu la kumi, bali ni Msalaba.</u> Tunapaswa kukaza macho yetu kwa Kristo. Kristo hakujitoa tu 10% yake mwenyewe, bali alijitoa mwenyewe kabisa kwa ajili yetu. Na matokeo yake, tunazo baraka kubwa zaidi kutoka kwa Mungu kuliko Waebrania wa Agano la Kale walizowahi kuwa nazo:

| <u>**Agano la Kale**</u> | <u>**Agano Jipya**</u> |
|---|---|
| 1. Katika Agano la Kale (AK), watu walilazimika kuendelea kutoa sadaka za kuteketeza kwa ajili ya dhambi zao **(Law 4:1-5:13; 5:14-6:7; 6:24-30; 7:1-8; 8:14-17; 16:3-22; Hes 5:-10; Ebr7:27)** | 1. Katika Agano Jipya (AJ), Kristo amefanyika sadaka mara moja tuu, itoshayo kwa msamaha wa dhambi zote za watu wake daima (**Yoh 1:29; Waeb 7:26-28; 9:11-12, 28;10:1-8**) |
| Katika AK, ni baadhi tuu ya dhambi za wana wa Izraeli zilifunikwa, tena kwa kipindi cha mwaka mmoja **(Hes 15:30-31; Waeb 9:7; 10:1-3)** | 2. Katika AJ, dhambi zetu zote, za kale, za sasa na za baadae, zimesamehewa milele **(Yer 31:34; Mdo 10:43; 13:38-39: Waeb 10:1-18)** |
| 3. katika AK halikutolewa uzima wa milele (**Rum 3:21; Wagal 311, 2**) | 3. Kwenye AJ, tunapewa uzima wa milele **(Yoh 3:14-16, 36; 17:2-3; Waeb 5:9)** |
| 4. Katika AK, uwepo wa Mungu ulikaa hekaluni tuu, na watu walilazimika kuenda hekaluni, ili kuukaribia uwepo wa Mungu (**1 Fal 8:10-11; 2 Nya 5:11-14, 7:1-2**) | 4. Katika AJ, sisi ndio hekalu, na Mungu amekuja kwetu (**1 Wakor 3:9, 16-17; 2 Wakor 6:16-7:1; Waef 2:21; 1 Pet 2:5; Ufu 3:12**) |
| 5. Katika AK, makuhani pekee ndio wangeweza kuingia hekaluni (**Hes 18:22-23; Waeb 9:6**) | 5. Katika AJ, Wakristo wote waliooloka ni makuhani **(1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6; 5:10)** |
| 6. Katika AK, ni kuhani mkuu pekee ndio angeweza kuingia patakatifu pa patakatifu katika uwepo wa Mungu **(Law 16:2-34)** | 6. Katika AJ, Kristo ndiye kuhani mkuu wetu **(Waeb 4:14-5:10; 7:1-10:25)** |
| 7. Katika AK, kuhani mkuu aliingia patakatifu pa patakaifu siku moja tu katika kipindi cha kila mwaka **(Law 16:34; Waeb 9:7)** | 7. Katika AJ, Kristo yupo katika uwepo wa Mungu daima akituombea **(Waeb 7:25; 9:24)** |
| 8. Katika AK, Roho Mtakatifu aliliacha hekalu na kamwe hakurudi **tena (Eze 9:3; 10:1-19; 11:22-23)** | 8. Katika AJ, Yesu ameahidi "kamwe hatatuacha wala kutupungukia" **(Waeb 13:5)** |
| 9. Katika AK, Roho Mtakatifu kamwe hajaweka makao ndani ya watu, bali aliwajilia juu yao baadhi ya watu na baadae angeondoka **(Kut 31:3; Hes 11:16-29; Amu 3:10; 6:24; 14:6,19; 1 Sam 10:1-11; 16:13-14; 19:20-24)** | 9. Katika AJ, Roho Mtakatifu amekuja na kuweka makao ndani ya waaminio wote, na kamwe hatatuacha wala kutupungiukia **(Eze 36:27; Yoh 14:16-17; 16:7; Mdo 2:14-18; 38-39; Rum 8:9; 1 Wakor 3:16; 6:19)** |
| 10. Katika AK, watu walikuwa kwenye utumwa wa sheria ambayo kawe hawakuweza kuitimiza (**Mdo 15:10; Rum 7:6, 23; 8:2-3; Wagal 3:23; 5:1**) | 10. Katika AJ, Kristo ameitimiza sheria kwa ajili yetu, naye ameandika sheria yake (sheria ya Kristo) ndani ya mioyo yetu (**Yer 31:33; Math 5:17; Rum 10:4; Wakol 2:13-15; Waeb 8:10; 10:16**) |
| 11. Katika AK, watu walikuwa na mioyo ya jiwe (**Zek 7:12**) | 11. Katika AJ, Mungu amebadilisha mioyo yetu ya jiwe na kuweka mioyo ya nyama **(Eze 11:19; 36:26; 2 Wakor 3:3)** |

Katika AJ tuna mahsiano ya moja kwa moja, ya kibinafsi na Mungu ambao waamini wa AK hawakuwa nao kamwe (**Yer 31:34; Waeb 4:16; 7:19**). Tuna mlango wazi usio na mipaka kwa Mungu, Baba yetu, kupitia Yesu Kristo, ambao waamini wa AK waliweza kuuotea ndoto tu (**Math 27:51; Waeb 10:19-22**). Mungu hata ametufanya sisi kuwa wana katika familia yake mwenyewe (**Rum 8:14-17; Wgal 3:26; 4:6-7; Waef 1:5**). Kwa vile tumepewa mengi zaidi kuliko walivyopewa wao, wanawezaje Wakristo kuitazama zaka (10%) kama kitu kingi, au kama ndicho cha juu zaidi? Badala yake, tunapaswa tuitazame kama kiwango cha chini zaidi. Utoaji wetu hufunua siri ya hali ya mioyo yetu. Swala la msingi si *kama* tunatoa, au hata *kiasi gani* cha kutoa, bali ile *sababu kwa nini* tunatoa: Je tunatoa kwa vile Sheria inatuamuru ki- nje tutoe (AK), au kwa sababu Injili inatubadilisha kwa ndani ili tutake kutoa (AJ)? Mtazamo wetu kuhusu kutoa hufunua, pengine, kiubora zaidi kuliko eneo jingine lolote la maisha yetu, kama kweli tumezaliwa mara ya pili, au hapana. "Ikiwa Kristo aliweza kujitoa dhabihu kiasi kikubwa mno kwa ajili yetu tunawezaje kuthubutu kukataa kutoa kwa ukarimu kwa wahitaji!"

(Blomberg 1999:193)

**C.** ***Utoaji katika Agano Jipya: kwa hiari, kwa ukarimu, na utoaji wa mlingano kukidhi haja halisi.***

Waamini wa mwanzoni walielewa utofauti mkubwa ambao Kristo na Injili ilimaanisha kwa ajili ya maisha yetu. Walielewa manufaa ya Injili katika kila kipengele cha maisha, ikiwa ni pamoja na matumizi ya fedha zao na mali. Walizitumia kanuni za Agano Jipya za utoaji ambazo zilizotangazwa na Yesu na mitume—kwamba utoaji unapaswa uwe we wa uhuru, kwa ukarimu, na kulingana na rasilimali alizo nazo mtu, ili kuujenga ufalme na kukidhi haja halisi. Matokeo yake, kanisa la kwanza lilikuwa na sifa ya ukarimu kupita kiasi na kujitoa kidhabihu uliodumu kwa miaka mamia kadhaa. Utoaji wa namna hiyo unaweza kutokea tena tunapoondoa macho yetu kwenye sheria ya Agano la Kale, na kukaza macho yetu kwa Kristo na Injili, na kuwafundisha watu wetu kanuni za utoaji wa ki- Agano Jipya.

1. <u>Mfano wa Zakayo (**Luka 19:1-10**).</u> Ingawaje Zakayo alikuwa mwanafunzi wakati lile Agano la Kale lilikuwa bado lina nguvu, yeye ni mfano ulio bora kabisa wa mtu ambaye alielewa mattokeo ya Injili kuhusiana na utoaji.

a. *Zakayo kwa hiari yake aliamua kutoa nusu ya mali zake kwa masikini.* Ile "sheria" haikuelekeza hilo. Yesu hakumwagiza kuanza kutoa zaka ili kutimiza maagizo ya Torati.Badala yake, utoaji wa ukunjufu wa Zakayo ni mfano wa kanuni ya Injili: "kwa yeye aliyesamehewa zaidi, hupenda zaidi" (ona **Luka 7:36-50**).

b. *Zakayo kwa moyo wa ukunjufu aliamua kuwarudishia mara nne ya kila kiasi alichomtoza nacho mtu.* Sheria za Agano la Kale ziliagiza tu mtu alipe 20%, siyo 400%, itokeapo mtu ameiba au amemdhulumu mtu (ona **Law 6:2-5; Hes 5:7**). Kule kurudisha kiasi kikubwa kiasi hicho kulikuwa ni ishara ya nje ya ule moyo wake uliobadilika.

c. *Msukumo wa Zakayo kwa ule utoaji wake wa ukunjufu ulikuwa ni kumpendeza Bwana.* Maneno ya Zakayo, *"Tazama, Bwana!"* (au, *"Ona Bwana!"*) ni kama mtoto mdogo asemapo "Tazama, Mama!" ama "Tazama, Baba! Ona ninachokifanya!" Zakayo alikuwa aanakifanya kile ambacho alijua kitampendeza Bwana wake mpya. Hilo linapaswa liwe msimamo wetu pia.

2. <u>Kanisa kule Yerusalemu **Mdo 2:44-47** na **Mdo 4:32-37**.</u>

a. *Waamini walikuwa "pamoja" (**Mdo 2:44**) na "walinia mamoja na kuwa na moyo moja" (**Mdo 4:32**).* Mtazamo wa nanma ile unafuatia baada ya kujiona wenyewe na ndugu wapendwa katika imani kuwa wote ni sehemu ya familia moja. Hata sehemu tunazoishi zilizo mbalimbali, tunapaswa kuwa na hali ya umoja na kunia mamoja kwa moyo na roho. Huu ndio mtazamo wa msingi unaotokea baada ya kumweka kikamilifu Kristo nafasi ya kwanza maishani mwetu. Kama Willard alivyosema, tunapomweka Kristo nafasi ya kwanza na kumfanya Yeye kuwa ndiye hazina ya juu kabisa, "basi tutawaweka kama hazina vivyo hivyo majirani zetu kisahihi, kama jinsi *yeye* anavyowahifadhi." (Willard 1997: 203).

b. *Waamini "walikuwa na vitu vyote shirika" (**Mdo 2:44**) na hawakudai "kwamba kitu chochote kilikuwa ni mali yake mwenyewe, bali vitu vyote vilikuwa mali yao wote" (**Mdo 4:32**).* Waamini walikuwa pamoja na vitu vyote shirika (**Mdo 2:45-46; 4:34-37; 5:4**). Hata hivyo, jambo muhimu lilikuwa ni ule *mtazamo* wao kwenye vitu walivyokuwa wanavimiliki na kwa watu wengine. Tena, mtazamo sahihi wa fedha, mali, na watu wengine, hupatikana kutokana na mtazamo mzuri kwa Kristo na ufalme wake.

c. *Waamini wakawa "wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja" (**Mdo 2:45**; ona pia **Mdo 4:34-35**).*

(1) <u>Walichokifanya kilikuwa ni kwa hiari, si kwa kulazimishwa.</u> Hawakuwa "wameshinikizwa" kuuza au kushirikisha vitu vyao na wengine, wala hawakuhadaiwa au kufanyiwa ujanja fulani au kuhukumiwa au ubinafsi wa kujinufaisha kibinafsi. Kuuza *"viwanja au nyumba"* (**Mdo 4:34**) kulikuwa ni kujitoa sadaka kiukweli. Zaidi ya hapo, hicho kitenzi cha tendo kinaonyesha kwamba hilo halikuwa tendo la mara moja tu kwa mtu kutoa mali yake yote aliyokuwa nayo, bali ni kitendo cha kuendelea cha kutoa kwa moyo kila mahitaji yalipojitokeza (Blomberg 1999:162, 165).

(2) <u>Cha kufurahisha, Barnaba alikuwa Mlawi (**Mdo 4:36-37**).</u> Kulingana na Sheria ya Musa, Law hawakuwa na haki ya kumiliki ardhi (ona **Hes 18:20-26; Kum 10:9; 12:12; 14:27-29; 18:1-2; Yos 13:14, 33; 14:3; 18:7; Eze 44:28**). Ukweli kwamba alifanya hivyo unaonyesha kwamba sheria ya Musa haikuwa tena na nguvu kwao, au haiwahusu waamini.

(3) <u>Utoaji ule ulifanyika ili kukutana na *hitaji halisi* (**Mdo 2:45; 4:35**). Mungu anaahidi</u>

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

kukutana na "haja" zetu, na siyo lazima "matakwa" au "tamaa" zetu (**Wafil 4:19**). Mungu hutupatia haja zetu *kupitia watu wake, kanisa.* Kusema kweli, wakati tunapompatia ndugu yetu wa kiume au wa kike mahitaji yake, hilo huthibitisha upendo halisi wa Mungu ndani yetu (**1 Yoh 3:17**) na uhalisi wa imani yetu (**Yak 2:15-16**).

d. *Mungu aliwabariki waamini kwa sababu walikuwa wakiishi maisha na kutoa sawasawa na njia zihusuzo kuishi ki-Ufalme wake.* Kama matokeo ya kumthamini Kristo juu ya fedha na mali, na kutumia fedha na mali yao kumheshimu Kristo, na kuujenga ufalme, Mungu akawabariki waamini katika yote mawili; kimwili na kiroho.

(1) *"Wala hakukuwa na yeyote aliyekuwa na uhitaji kati yao"* (**Mdo 4:34**). Mungu aliyashughulikia mahitaji yao ya waamini masikini kupitia kule kushirikiana kiukarimu na waamini wengine.

(2) *"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe"* (**Mdo 2:46**). Mungu aliwaunganisha waamini pamoja. Aliwapa furaha. Hayo siku zote huja ikiwa tunaenenda kama tunavyotakiwa.

(3) *"Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote"* (**Mdo 2:47**). Kanisa siku zote hutazamwa na wasioamini. Kanisa linapotenda kama linavyostahili, watu wengine hutambua, na hawawezi kujizuia ila kuutazama upendo huo kiuzuri.

(4) *"Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote"* (**Mdo 4:33**); *"Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa"* (**Mdo 2:47**). Mungu hutupatia nguvu za kiroho pale tunapomtii. Wakristo wanaoishi na kutoa kama wanavyotakiwa, hilo lenyewe ni ushuhuda wenye nguvu kwa ufufuo. Jinsi tunavyishi, kunaweza kuwa ushuhuda wenye nguvu zaidi kuliko yale tuwezayo kuyasema. Kusema ukweli, kile tusemacho kinapaswa kidhihirishwe na jinsi tunavyoishi ikiwa watu hao watapaswa watuamini. Wakati kuishi kwetu kunaendana na maneno yetu, Mungu hubariki hilo na kuongezea katika ufalme wake.

(5) *"Na neema nyingi ikawa juu yao wote"* (**Mdo 4:33**). Mungu huupa thawabu uaminifu. Hutuvuta karibu naye Mwenyewe, na katikati yetu, na kwa watu wengine tunapoishi na kutoa kama tunavyotakiwa. Kwa hiyo, Mungu alimimina baraka zake za kiroho juu ya waaminio na pia alihudumia mahitaji yao ya kimwili.

3. Kanisa kule Antiokia katika **Mdo 11:27-30**.

a. *Waamini katika **Mdo 2** na **4** walikuwa kwa kiwango kikubwa Wayahudi, na walikaa Yerusalemu.* Katika **Mdo 11** waamini kwa kiwango kikubwa walikuwa ni wa Mataifa, na walikaa Antiokia (Syria ya leo).

b. *Roho Mtakatifu alionyesha kwamba kutakuwa na ukame.* Ukame ulitokea miaka ya 45-47 BK, kama miaka baada ya tukio la **Mdo 2** na **4** (Blomberg 1999: 171). Kama matokeo ya kulielewa hilo, *"wale wanafunzi, kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi. 30 Wakafanya hivyo, wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli."* (**Mdo 11:28-29**).

(1) Waamini wa kule Antiokia hawakusita kujitoa walipolijua tatizo halisi. *"Kila moja wao"* aliyekuwa na uwezo alifanya hivyo.

(2) Hawakutoa tu kutokana na hisia zao au kwa sababu walifanyiwa mbinu za ushauri, lakini *"waliazimia"* kusaidia na walipania kuwa tayari kusaidia—m.y, waliitikia kwa makini na kupanga wasaidieje.

(3) Waamini wa Antiokia hawakuwa wanawahudumia wahitaji walioko kati yao, kama waamini wa Yerusalemu walivyofanya; lakini walikuwa wanaonyesha mwitikio ambao ulikuwa tofauti kabisa na wao. Zaidi ya hayo, walikuwa wanaonyesha mwitikio kwa watu ambao walikuwa ni wa asili tofauti na wao. Hilo linaonyesha kwamba waamini katika Antiokia kweli waliamini kwamba kanisa zima ni *"mwili moja"* (**1 Wakor 12:13**) na kwamba, bila kujali utofauti wa rangi za ngozi zetu, lugha, kabila, na asili nyinginezo za watu, sisi sote tu *"mtu moja mpya"* katika Kristo (**Waef 2:15-16**).

4. Kanisa la Makedonia katika **2 Wakor 8:1-5.**

a. *Uhitaji mwingine mkubwa ulitokea kati ya waamini huko Yerusalemu (**1 Wakor 16:1-4**).* Hilo lilitokea kunako miaka ya 54-57 BK, karibu miaka 10 baada ya tukio la **Mdo 11:27-30**. Paulo alikwenda kwenye makanisa ya Uyunani ili kuchangisha fedha kwa ajili ya makanisa yaliyoko

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

Yerusalemu.

b. *Makanisa ya Makedonia (Ugiriki ya Kaskazini) waliitikia kwa ukunjufu na kwa shauku kubwa kwa mwito wa Paulo.*(1) Walikuwa Wamataifa, lakini kwa moyo wa ukunjufu ili kuwasaidia ndugu zao walio masikini, wa Kiyahudi.

(2) Walitoa kwa kwa moyo wa ukunjufu hata kama wao wenyewe walikuwa wako katika hali ya *"umasikini mkubwa"* na *"kiwango kikubwa cha dhiki"* (**2 Wakor 8:2**). Licha ya mazingira yao wenyewe, hao Wamakedonia hata *"Wakituomba sana pamoja na kutusihi kwa habari ya neema hii, shirika hili la kuwahudumia watakatifu"* (**2 Wakor 8:4**).

(3) Walitoa kwa moyo mweupe, *"kwa hiari yao wenyewe,"* na walitoa *"kulingana na uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao"* (**2 Wakor 8:3**).

(4) Sababu ya Wamakedonia kutoa kwa ukarimu kiasi hicho, ni kuwa walielewa matokeo ya Injili: *"Bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu"* (**2 Wakor 8:5**).

(5) Ukarimu wa Wamakedonia ulisababisha hata kanisa la Korintho kutoa pia (**Rum 15:25-27**).

5. Utoaji wa hiari, wa ukunjufu, na wa kuendana na kiwango wa kanisa la mwanzo haukuishia vipindi vya Ki-Biblia tu bali uliendelea angalau kwa miaka mingine 300 ya historia ya kanisa. Nukuu zifuatazo kutoka kwa pande zote mbili Wakristo na Wapagani zinaonyesha kwamba kwa zaidi ya miaka 300 ya historia ya kanisa, waamini walitoa kwa hiari (m.y., siyo chini ya "sheria ya kutoa zaka"), bali kwa ukarimu, na kwa kulingana na uwezo wao, ili kukidhi mahitaji halisi. Nukuu kutoka kwa Wapagani pia zinaonyesha kwamba mtindo wa maisha, na utoaji wa kanisa la mwanzoni ulikuwa tofauti sana na ule wa kidunia, kiasi kwamba hata Wapagani wakagundua hiyo tofauti *nao wakavutwa kanisani kwa sababu ya mtindo wa maisha wa waamini wake na ukarimu wao.* Kusema ukweli, ilikuwa ni kwa sababu ya maisha hayo ya mtindo mtakatifu, na ukarimu usio wa kawaida kabisa; uliowezesha kanisa kuenea kwa kasi, na kubadili himaya katili, na kubwa ya Warumi. Kanuni hizo hizo zinatenda kazi leo na zitafanya kazi leo, katika desturi zetu, sawa tu kama zilivyofanya kazi nyakati hizo.

a. *Didache (c. BK 90).* "Mpe kila akuombaye, nawe usitake kurudishiwa. Kwani Baba anataka vipawa vyake mwenyewe vishirikishwe ulimwengu mzima. Heri mtu yule atoaye kama agizo limtakavyo kufanya, kwani hana hatia! . . . Usiwe ni mtu anayenyosha mkono ili kupokea, na kuufunga itokeapo kwenye kutoa. Ikiwa ijara Yak imekuletea malipo, toa sadaka kwa ajili ya dhambi zako. Usisite kutoa, wala usitoe kwa nia mbaya; kwani utaelewa ni yupi huyo Akulipaye thawabu zenye neema nzuri. Usigeuze kisogo chako kwa mhitaji, bali mgawie kila ulicho nacho ndugu Yak, nawe usiseme kitu chochote kuwa ni chako peke Yak. Kwani ikiwa kilicho cha milele mwashiriki ki-umoja, ni jinsi gani zaidi mnapaswa kuwa na hivi vilivyo duni!" (Didache: 1:5; 4:5-8)

b. *Aristides, Apology (c. BK 124).* "[Wakristo] watendeeni mema adui zenu, na wake zenu;Ee Mfalme, ni wasafi kama bikira, na mabinti zao ni wa heshima; na waume zao hujitunza mbali na Mdo yasiyofaa ya zinaa, na uchafu wa kila namna ,kwa matumaini kuwa na malipo mema katika ulimwengu mwingine. . . . Wanapendana, na kwa wajane, hawajitengi na heshima zao; nao wanawatoa yatima zao kutoka kwa yeye awatendeaye mabaya. Na yeye, aliye nacho, humpa yeye asiye nacho, pasipo kujivuna. Na wamwonapo mgeni, wanamchukua nyumbani mwao na kufurahi pamoja naye kama kwamba ni ndugu halisi; kwani hawawaiti hao ndugu kimwilini, bali ndugu kwa roho na katika Mungu. Na itokeapo mojawapo wa masikini wao anakufa, kila moja wao anahakikisha kulingana na uwezo wake, anatoa msaada kwa mazishi yake. Na wakisikia kuwa moja wao amefungwa au amekutwa na mabaya kulingana na jina la Masihi wao, wote hao huhudumu kulingana na uhitaji uhitaji huo, na ikiwa ni lazima, wanamkomboa kuwa huru.. Na ikiwa yuko yeyote kati yao aliye masikini na mhitaji, na ikiwa hawana akiba ya chakula kilichobaki, wanafunga siku mbili au tatu ili watoe chakula kwa yule mhitaji wa chakula." (Aristides, Apology: 15)

c. *Justin Martyr, First Apology (c. BK 150-155).* "Wale ambao waliwahi kufurahia uzinzi, sasa wanatamani kujizuia peke yake; wale waliokuwa wakitumia mbinu za kichawi, wamejitoa wenyewe sasa kwa Mungu aliye mzuri na wa pekee; sisi ambao zamani tulifurahia sana kujiongezea mali zetu na utajiri, sasa tunaleta kile tulicho nacho kwenye mfuko wa pamoja na kushiriki na kila moja mwenye hitaji; sisi ambao tulikuwa tunachukiana na kuuana na tuliokuwa hatuwezi kuchangamana na watu wa kabila jingine kwa sababu ya [utofauti wao] desturi au

mila, sasabaada ya udhihirisho wa Kristo, tunaishi pamoja na kuwaombea adui zetu na kujaribu kuwashauri wao ambao wanatuchukia pasipo haki, ili kwamba, wao kwa kufuata maagizo ya haki ya Kristo, waweze kushiriki pamoja nasi tumaini jema la kupoke mambo hayo hayo [ambayo tutapata] kutoka kwa Mungu, Bwana wa wote." (Justin Martyr, First Apology: 14)
d. *Lucian of Samosata, Death of Peregrinus (c. BK 165)—Lucian alikuwa Mpagani.* "[Mkristo anapofungwa gerezani] watu walikuja hata kutoka miji ya Asia, waliotumwa na wakristo kwa changizo za pamoja, kuja kumjulia hali na kumtetea, na kumtia moyo huyo shujaa wao. Wanaonyesha spidi ya kushan gaza sana itokeapo kuna jambo la haraka linatakiwa kufanyika; fkwani baada ya kitambo kidogo tu, wanakirimu vyao vyote. Ndivyo ilivyokuwa kwa Peregrinus; fedha nyingi zilimjia kutoka kwa sababu ya kufungwa kwake, naye hakujipatia manufaa katika hizo. Misokoto ya kimasikini, nao wamejidhatiti wenyewe, kwanza kabisa na mbele ya yote, kuwa, watakwenda kuwa na maisha ya milele na kuishi muda wote, na matokeo yake, wanadharau kifo na hata kwa kujitoa wanajitoa wenyewe kifungoni, wengi wao. Zaidi ya yote, mtoa sheria wao wa kwanzar aliwashawishi kwamba wote ni ndugu wa kila moja baada ya kuvuka mara moja, kwani wote; kwa kuikana miungu ya Kugriki (Kiyunani) na kwa kumwabudu mpotoshaji huyo aliyesulubiwa na kuishi kwa kufuata sheria zake. Kwa hiyo wanadharau mambo yote pasipo kubagua na kuyahesabia mali ya umoja." (Lucian of Samosata, Death of Peregrinus: 13)
e. *Irenaeus, Against Heresies (c. BK 175-180).* "Badala ya sheria inayosisitiza kutoa zaka, [Alituambia] kushirikiana mali zetu zote na masikini; na kutowapenda majirani peke yao, lakini hata adui zetu; na siyo kuwa watoaji wakarimu na wafadhili, bali hata tuonyeshe utoaji usio na masharti kwa wale ambao wananyang'anya vitu vyetu. Kwani "yeye akunyang'anyaye koti lako," Anasema, "mpe na kanzu Yak pia; anaye akunyang'anyaye vitu vyako, usitake akurudishie; na kama mpendavyo kutendewa ninyi na watu, vivyo hivyo yatendeni hayo kwao:" hivyo tusihuzunike kama wale wasiopenda kudhulumiwa, bali mweze kufurahi kama wale waliotoa kwa ukunjufu, na kama wawatakiao mema majirani zetu, kuliko kuonyesha kuwa ndio tu wahitaji wakubwa." (Irenaeus, Against Heresies: 5:13:3)
f. *Mathetes, Epistle to Diognetus (c. BK 130-200).* "Kwani Wakristo wanatofautishwa na watu wengine siyo kwa nchi, wala kwa lugha, wala kwa desturi au mila wanazozifuata. . . . Bali, kwa kukaa katika miji ya Ugiriki na Ubarini, sawa sawa tu kama vile wengi wao walivyoamua, kuwa na desturi zinazosomeka dhahiri na wenyeji kwa habari ya mavazi, chakula, na kwa mwenenndo wa tabia zilizobakia, wanaonyesha kwetu njia na aina ya ajabu ya maisha waliyo nayo. Wanaishi katika nchi zao, lakini tu kama wasafiri. Kama raia, wanashiriki mabo yote pamoja na wengine, lakini, wanavumilia mambo yote kama wageni. Kila nchi ya kigeni kwao ni kama nchi yao ya nyumbani, na kila nchi yao waliyozaliwa nayo kama nchi yao ya kigeni. Wanaoa, kama wafanyavyo wote [wengineo]; wanapata watoto; bali hawaharibu watoto wao. Wana meza ya pamoja, lakini si kitanda kimoja. Wako mwilini, lakini hawaishi kwa kuufuata mwili. Wanaishi siku zao duniani, lakini wao ni raia wa mbinguni. Wanatii sheria zilizopo, na kwa wakati huo huo wananazivuka sheria sheria hizo kwa maisha yao waishiyo. Wanawapenda watu wote, na wnadhikishwa na watu wote. Hawatambulikani na kudharauliwa; wanauawa, na kurudishiwa uzima tena. Wao ni masikini, lakini wanatajirisha wengi; wanapungukiwa na vitu vyote, bali wana vitu vyote; hawaheshimiwilakini huko kutokuheshimiwa kwao kunatukuzwa. Wananenewa mabaya, bali wanahesabiwa haki; wanatukanwa, nao wanabariki; wanakashifiwa, nao wanarudisha kashifa hizo kwa kutoa heshima; wanatenda mema, bali wanaadhibiwa kama watendao maovu. Wanapoadhibiwa, wanafurahia kana kwamba wamehuishwa uzimani; wanasumbuliwa na Wayahudi kama wageni, na wanateswa na Wayunani; lakini bado hata hao wanaowachukia hawana uwezo wa kueleza sababu ya kuwachukia kwao." (Mathetes, Epistle to Diognetus: 5)
g. *Tertullian, Apology (c. BK 197-200).* "Watu waliojaribiwa wa hao wazee wanaongoza , wakiipokea heshima hiyo si kwa kuichukua , bali kwa tabia waliliyojijengea. Hakuna kununua wala kuuza chochote kati ya vitu vya Mungu. Ingawaje tuna hazuna yetu,haiundwi kwa fedha ya kununulia, kama kwamba ni dini yenye bei fulani. Katika siku ya mezi, kama akitaka, kila mtu huweka humo chochote kidogo; lakini tu kama anapenda, na tu kama anaweza: kwani hakuna kulazimishwa; ni kwa hiari tu. Vipawa hivi, kama vilivyokuwa zamani, mfuko wa uchaji. Kwani hazitolewi humo na kutumiwa kwa sherehe, na viburudisho vya vinywaji, na majumba ya ulaji, bali kuwasaidia na kuwazikia walio masikini, kuwapatia wavulana na

wasichana na wazazi walio katika upungufu mkubwa, na walio wazee sasa ambao wamekaa nyumbani; hata nao, waliovunjikiwa na meli; na kama itatoke kuwako yeyote kwenye machimbo ya madini, au aliyenaswa kisiwani, au amefungwa kifungoni, si kwa kingine ila kwa sababu ya uaminifu kwa kanisa la Mungu,wanakuwa ni wahanga wa ukiri wao. Lakini zaidi ni Mdo yao ya upendo, yenye uadilifu mkubwa yanayowaongoza wengi kuweka alama juu yetu. Ona wanasema, jinsi wanavyopendana, kwao wenyewe wanachangamshwa na chuki ya kuwanufaisha pamoja; jinsi walivyo tayari hata kufa kwa ajili ya mwingine, kwani wao wenyewe si kitambo kirefu wataondolewa kutoka mauti. . . . Yeye aliye katika mwili na nafsi, hatusiti kushirikiana mali zetu za kidunia na wenzetu. Vitu vyote ni vya umoja kati yetu, isipokuwa wake zetu." (Tertullian, Apology: 39)

h. *Julian the Apostate, Letter to Arsacius (c. BK 360-363)—Julian (Mtawala wa Rumi) alikuwa Mpagani.* "Dini ya Wagiriki bado haisitawi kama ambavyo ningetaka iwe, kwa kuwaangalia wale wanaoishi katika hiyo. Lakini zile zawadi za miungu ni kuu na yenye ubora, inayofaa kuliko maombi sala yoyote au tumaini lolote . . . Kwa nini basi tubafikiri kwamba hii inatosha na hatuangalii jinsi wema wa wakristo kwa wageni, jinsi wanavyojishughulisha kwa mazishi ya waliokufa, na unyofu wa mwenendo wa mai sha yao? Kila moja ya mambo hayo, nafikiri, linatakiwa kuigwa nasi. Haitoshi kwako wewe peke Yak kuyatenda hayo, lakini lazima pia makuhani wote katika Galatia [Uturuki ya sasa] pasipo kubagua. Ama uwafanye watu hao wazuri kwa kuwaaibisha, kuwashawishi kuwa hivyo au uwaondoe . . . La pili, uwahimize makuhani kutosogelea kumbi za maonyesho, wala kunywa kwenye vilabu vya pombe, wala kutojiingiza au kuhusika na biashara yoyote mashuhuri. Waheshimu wale wanaotii na uwaondoshe wasiotii. Anzisha makao mengi, moja kila mji, ili kwamba wageni wapate kufurahia wema wangu, siyo tu wa imani yetu wenyewe, lakini pia na wengineo wote walio na haja ya fedha. Hivi nimekuwa nikiibua mpango ambao utawawezesha kupata haja zenu. Kwani nimeagiza kwamba kila mwaka kila mahali Galatia vipimo 30,000 vya nafaka na painti 60,000 za mvinyo vitatolewa. Asilimia tano ya kiasi hicho kitolewe kwa walio masikini wanaowatumikia makuhani, na kilichobakia lazima kigawiwe kutoka kwangu kwenda kwa wageni na wanaoomba-omba. Kwani ni aibu kuwa hakuna Myahudi aliye omba-omba, na hao Wagalatia wasio na heshima [jina lililotolewa na Julian kwa Wakristo] wanawasaidia masikini wetu zaidi ya wa kwao; kila moja anao uwezo wa kuona kwamba wale wa kwetu wenyewe wanahitaji msaada kutoka kwetu." (Julian the Apostate, Letter to Arsacius)

**D.** ***Utoaji kulingana na Yesu***

1. <u>Yesu alikuwa na mwelekeo wa mtazamo kuhusu fedha zetu na mali tulizo nazo wenye msingi wa mtazamo unaozungukia "Mungu-na-Ufalme - na vipaumbele vyako. Alilidhihirisha hili katika **Math 6:19-34:**</u> *[19] Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; [20] bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; [21] kwa kuwa hazina Yak ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.[22] Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi mwili wako wote utakuwa na nuru. [23] Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani Yak ikiwa giza; si giza hilo! [24] Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali. [25] Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha Je! si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? [26] Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi Je! si bora kupita hao? [27] Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? [28] Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti; [29] nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. [30] Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? [31] Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? au Tunywe nini? au Tuvae nini? [32] Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. [33] Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. [34] Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake.*

2. <u>Dallas Willard anaelezea mtazamo wa Yesu kuhusu mali kwa jinsi hii:</u> "Hazina ni vitu tunavyojiwekea kwa sababu ya thamani tunayoiweka juu yake . . . . Amri iliyo muhimu kuliko zote kwa

Wakristo wa desturi ya Kiyahudi ni kumweka hazina Mungu na ufalme wake kuliko chochote kingine. Hiyo ndiyo maana ya kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, nafsi Yak, akili, na nguvu. Kunamaanisha *kumweka hazina* Yeye, kumshika yeye na mpendwa wake, na kumlinda na kumsaidia katika makusudio yake. Hekima yetu pekee, usalama, na utimilifu unakaa katika kumweka hazina Mungu. Kisha tuwaweke hazina pia majirani zetu kisahihi, kama *yeye* anavyowaweka hazina. . . . Kitu cha kwanza anachotuambia Yesu kuhusiana na hazina ni kwamba, kuweka hazina ya vitu 'vilivyoko duniani' si mbinu nzuri ya kuweka hazina. Hazina za dunia hii, kwa asili yao, kiufupi haziwezi kubakia bila kuharibika. . . . Bila shaka hili linamaanisha kwamba tutawekeza kwa Yesu mwenyewe, na kwa kupitia yeye, kwa Mungu. Lakini zaidi ya hiyo, na katika ukaribu wake, tutajitoa wenyewe kwa ajili ya watu—wale wanaotuzunguka uzingo wa uwezo wetu. Hawa ni miongoni mwa hazina ya Mungu. 'Sehemu ya Bwana,' tunaambiwa, 'ni watu wake' (Kum. 32:9). . . . Kwa hiyo, kule 'kuweka hazina mbinguni' ni kuweka hazina ya vipenzi na nyanja zigusazo maisha ya mbinguni, yote ayafanyayo Mungu duniani. . . . 'Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema;na hasa jamaa ya waaminio' (Wagal. 6:8-10). Hivi ndivyo, kiusahihi kabisa, *jinsi* tunavyoweka hazina mbinguni kwa msingi wa kila siku, na kila saa. . . . Hatuna jinsi, isipokuwa kuzitumikia hazina zetu . . . . Kwa kifupi hatuwezi kuwa na malengo mawili *kwa dhati* au sehemu mbili za kulenga Mdo yetu. . . . Huwezi kuwa mtumwa wa Mungu na mali 'hapa duniani,' kwa sababu mahitaji ya kila upande yanapingana. Mpaka kwanza uwe umemweka Mungu nafasi ya kwanza, kwa mfano, kile utakachohitajika kufanya ili kuwa na uhakika wa kifedha, kuwavutia watu wengine, au kutimiza shauku Yak, vinaweza kukuongoza kinyume na matakwa ya Mungu. Hii ndiyo maana amri ya kwanza kabisa ya zile amri Kumi za mungu, 'Usiwe na miungu mingine yeyote, ambayo utaipa kipaumbele juu yangu mimi,' ndiyo ya kwanza kabisa ya amri zake kumi." (Willard 1997: 203-07)

3. <u>Yesu alielezea gharama inayohitajika ili kuwa na ufahamu huu wa - kiufalme:</u>

a. Ni lazima tumthamini Kristo na ufalme wake kuliko familia zetu za kidunia (**Luka 14:26**).

b. Ni lazima tumthamini Kristo na ufalme wake kuliko sisi wenyewe na juu ya mali zetu (**Math 4:1-4, 8-10; 13:44-46; Luka 4:1-8; 12:13-21; 14:26**).

c. *Tunawajali masikini na wahitaji—hata wale wanaotupinga—na tunalidhihirisha hilo kwa kutoa kwa ukarimu ili kuwasaidia.* Yesu alisisitiza hili katika sehemu zote mbili; kwenye mifano yake na kwa mafundisho yake moja kwa moja:

(1) Mfano wa Msamaria mwema (**Luka 10:29-37**), na yule Tajiri na masikini Lazaro (**Luka 16:19-31**).

(2) Mafundisho yake kuhusiana na kutenganisha kondoo na mbuzi siku ya mwisho hapo atakapokuja tena (**Math 25:31-46**).

(3) <u>Maneno yake katika **Marko 14:7** kwamba *"maana siku zote mnao masikini pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwatendea mema."*</u> Blomberg anasema, "Haya maneno 'mnaweza kuwatendea mema kila mpendapo' hakika yanamaanisha wanafunzi wanapaswa kuwa na huduma inayoendelea kwa masikini" (Blomberg 1999: 142).

(4) <u>Mafundisho yake ya mlimani (**Math 5:38-6:4; Luke 6:24-45**).</u> Blomberg anaelezea kuwa katika **Math 5:42** (*"Akuombaye, mp; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo"*): "Yesu alikuwa akisema kwamba kumpa mhitaji kusitegemee kiasi cha wao kuweza kulipa wewe (k.m. mfano katika Luka 6:30: 'Mpe kila akuombaye, na akunyang'anyaye vitu vyako usitake akurudishie'). . . . Yesu hakuwa anaagiza, ama nyakati za siku zile wala hizi zetu, kwamba wafuasi wake wawape watu waombao kila kitu wanachokiomba. Kilicho bora zaidi kwao si lazima kiwe ndicho wakiombacho. Lakini kwa kiwango ambacho tunaweza kujua mahitaji ya kweli ya watu ya mwilini au ya kivitu, tunapaswa kujali kuwaelekezee msaada ambao uko katika hali ambayo angalau itawaokoa katika tatizo lao linalowakabili. Angalau kwa kiwango kidogo mno, kuondokana na kanuni za kizamani za kutaka kutendewa kwanza, Yesu anawahimiza wanafunzi wake kuepukana na " 'hana' ya Nitakukuna mgongo wako pale utakaponikuwa wa kwangu kwanza' (Blomberg 1999: 129-30)

(5) <u>Ile "Sheria ya Dhahabu" (*"yoyote mtakayotaka mtendewe na watu,nanyi watendeeni vivyo hivyo"*—**Math 7:12; Luka 6:31**).</u> Sehemu zote mbili; Matthew (ona **Math 7:9-11**) na katika Luka (ona **Luka 6:29-30**), hiyo Sheria ya Dhahabu inasemwa kuhusu utoaji.

d. *Yule "mfalme kijana tajiri" ni mfano wa mtu fulani ambaye hakuwa tayari kumthamini Kristo na ufalme wake kuliko hazina zake za kidunia (**Math 19:16-30; Marko 10:17-23; Luka***

***18:18-30****).*

4. Tukizingatia utoaji, mtazamo wa kumweka Yesu nafasi ya kwanza una vipengele au maswala muhimu manne:

a. *Sababu ya Msukumo: utoaji wetu unapaswa uwe na sababu iliyo sahihi—kumtukuza Mungu na kuujenga ufalme wake, siyo kwa sababu ya kupata pongezi, kujulikana, au thawabu za watu.*

(1) Yesu alieleza kanuni hii katika **Math 6:1-4:** *[1] Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni. [2] Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele Yak, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu.* ***3*** *Amin, nawaambieni, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka, hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wa kuume;* ***4*** *Sadaka Yak iwe kwa siri; na Baba Yak aonaye sirini atakujazi.*

(2) Blomberg analijadili hili: "Mgongano wa kimsingi kati ya 6:1-2 na 5:16 [*"Vivyo hivyo, nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona Mdo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni"*] hutatulika haraka pale tunapoelewa kiini kuhusu ni nani apewe utukufu katika kila kifungu; hao wanatofautiana kabisa  (Watu kulingana na Mungu). Yesu anasisitiza kwamba wanafuzi wake wasifanye maonyesho ya Mdo yao ya huruma hadharani. Matthayo 6:3 ('hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wa kuume') halitii nguvu uwakili wa kizembe, kuacha kufuatilia utoaji unavyokwenda au kukataa kueleza una fedha kiasi gani. Kwa umuhimu wa hilo, Paulo alipoagiza changizo kwa ajili ya wahitaji wa Yudea (ona hasa 2 Wakor. 8-9) kutaonyesha umuhimu wa uangalifu katika uwajibikaji. Badala yake, hoja ya Yesu ni kwamba utoaji uwe wa "siri" sana kiasi kwamba mtu asije kujaribiwa kwa sababu zote za kushukuriwa kianadamu au ili kupanta upendeleo." (Blomberg 1999: 130)

b. *Pasiwepo unafiki: utoaji siyo mbadala wa kumpenda Mungu na watu wengine, ila ni mojawapo ya kuonyesha upendo—unapaswa uwe ni ishara ya nje, inayoonekana, ya kile kilichoko ndani, neema ya kiroho katika maisha ya mtu.* Wazo la kumweka Mungu nafasi ya kwanza na kupuuza watu wengine, au familia zetu, ni la makosa kabisa. Utoaji wa namna hiyo si hasa wa kiufalme, bali ni wa kinafiki, na kibinafsi. Kusema ukweli, kutoa kwa kanisa— kama hivyo kunamaanisha tunapuuza matakwa mema ya watu — kunaonyesha hatuna upendo wa Mungu kiukweli. Kama Yoh anavyouliza katika **1 Yoh 3:17**, *"Lakini mtu akiwa na riziki ya kidunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?"* Hivyo hivyo, katika **1 Yoh 4:20** alisema, *"Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambye amemwona hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."* Yesu anatoa mifano miwili:

(1) Katika **Luka 11:39-41** Yesu alisema kwa Mafarisayo: *"Ninyi Mafarisayo mwasafisha kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani yenu mmejaa unyang'anyi na uovu.  Enyi wapumbavu; aliyevifanya vya nje, siye yeye aliyevifanya vya ndani pia? Lakini, toeni sadaka vile vya ndani, na tazama, vyote huwa safi kwenu."*

(2) Blomberg anaelezea: "Dhana iliyopo ni kulinganisha uoshaji wa kidesturi wa kikombe kwa nje na sahani, kulikokuwa kunapendwa sana kwa malengo ya Mafarisayo, wakiwa na uchoyo na uovu  ndani yao (Luka 11:39). Mlinganisho wa vya ndani -na vya nje yao kunaonyesha kwamba, kutoa kile kilichopo ndani ya sahani kimsingi ni sitiari ya ukiroho, pakizungumzia wema unaotokana na moyo wa mtu. Lakini, kama tulivyoona mapema kwenye mifano ile, njia moja kuu ya kuonyesha kujali kiroho ni kwa msaada wa vitu: katika dhana hii, utoaji wowote. Changizo kwa masikini huwa 'picha ya kile kilichoko ndani'." (Blomberg 1999: 135-36)

(3) Katika **Math 15:3-9** (ona pia **Marko 7:9-13**) Yesu alitoa mfano mwingine wa utoaji kinafiki: *[3] Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu? [4] Kwa kuwa Mungu alisema, MHESHIMU BABA YAK NA MAMA YAK, NA AMTUKANAYE BABA YAKE AU MAMA YAKE KUFA NA AFE. [5] Bali ninyi husema, Atakayemwambia babaye au mamaye, Cho chote kikupasacho kusaidiwa na mimi ni wakfu, [6] basi asimheshimu baba yake au mama yake. Mkalitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu. [7] Enyi wanafiki, ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema, [8] WATU HAWA HUNIHESHIMU KWA MIDOMO; ILA MIOYO YAO IKO MBALI NAMI. [9] NAO WANIABUDU BURE, WAKIFUNDISHA MAAGIZO YA*

*WANADAMU.*

(4) Kutoa dhabihu au kuweka wakfu fedha au mali au kitu kwa Mungu, au kuweka nadhiri ya kutoa fedha au kiwanja kwa huduma ya ki-Mungu, kuliitwa na Wayahudi wa siku za Yesu *"korban."* Kuhusu hiyo *korban,* Blomberg anasema, "Fedha zinaweza kutolewa hekaluni kugharimia kifo cha mtu fulani. Fedha hizo haziwezi kutolewa kwa mtu mwingine yeyote, hata kwa familia ya wahitaji, bali bado zingeweza kutumiwa kwa faida yake mhusika aliyeweka" (Blomberg 1999: 135)

(5) Yesu anasema kwamba kutoa fedha kwa "Mungu" (m.y. kutoa kwa kanisa au kwa mtu fulani "Mkuu wa Mungu") ni dhambi ikiwa kwa kufanya hivyo unashindwa kutekeleza mahitaji muhimu ya kianadamu na fedha hizo au mali hiyo. Kusema ukweli,Yesu anaelekeza hoja ya nguvu kwamba watu wanaotoa fedha kwa sababu za kidini—na ikiwa kwa kufanya hivyo hawawezi kukidhi mahitaji ya kianadamu kwa fedha hizo au mali hiyo—ni "wanafiki" ambao kwa hili wanakuwa "wamelifanya Neno la Mungu lisifae," na kuwa wanamwabudu Bwana "bure." Kwa hiyo, kiuhalisi kabisa, Yesu anatufundisha kile tufanyacho na fedha zetu ni kitu cha kiroho, na ni mojawapo ya njia muhimu ambazo kwazo "tunawapenda majirani zetu kama tunavyojipenda wenyewe." Inaam, kulingana na mafundisho haya ya Yesu, ile "amri ya pili" ("Mpende jirani Yak kama nafsi Yak mwenyewe"—**Math 22:39**) ni ndicho kipimo ambacho tunadhihirisha kama kweli tunanaishika ile "amri ya kwanza." ("Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho Yak yote, na kwa akili zako zote "—**Math 22:37**), ama sivyo.

c. *Kutokuwa na ubinafsi: utoaji siyo "kukopesha"—kutoa kwenye mtazamo wa Ki-ufalme hakudai malipo baada ya hapo.* Utoaji usio na ubinafsi, siyo ule wa kutegemea kupokea kitu fulani badala yake, kunaonyesha tumaini kwamba Mungu atakutana na haja zote za vitu, kama Yesu alivyosema katika **Math 6:33**. Yesu anatoa mifano ya jinsi hili linavyofanana:

(1) **Math 5:40-41** Unahusu utoaji kwa wale walio kwenye nafasi za juu zaid yetu: **40***Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu Yak, mwachie na joho pia.* **41***Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili."*

(2) Hata wale watu walio na madaraka juu yetu, au wanaotusimamia, au walio katika nafasi za juu zaidi yetu, hatupaswi kutenda kama dunia ifanyavyo. Badala yake, tunatakiwa kuonyesha "maisha ya kiufalme" na kuwapa wao. Hata hivyo, hatupaswi kutoa kwao walio juu yetu kimadaraka ili tujikombe au kujipendekeza kwao "tupate upendeleo" kwao. Ndivyo inavyofanya dunia kwa wale wenye utajiri na wale wenye nguvu. Badala yake, sisi tusionyeshe upendeleo kwa matajiri na wenye nguvu, bali tuwahudumie watu wa aina zote kwa upendo ulio sawa kwa sababu zilizo safi. Kutoonyesha upendeleo kwa watu wa aina mbali mbali ni njia nyingine ambayo tunaonyesha kwamba"tunampenda jirani kama nafsi yetu wenyewe (ona **Yak 2:1-9**).

(3) **Luka 14:12-14** inahusu: kutoa kwa wale walio chini zetu giving to those who are in positions inferior to us: "[12]*Akamwambia na yule aliyemwalika, Ufanyapo chakula cha mchana au cha jioni, usiwaite rafiki zako, wala ndugu zako, wala jamaa zako, wala jirani zako wenye mali; wao wasije wakakualika wewe ukapata malipo.* **13***Bali ufanyapo karamu waite maskini, vilema, viwete, vipofu,* **14***nawe utakuwa heri, kwa kuwa hao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki."*

(4) Masikini hawana cha kutulipa au kutunufaisha, lakini pamoja na hilo tunawapa. Hii inaonesha tunatembea kwa imani na sii kwa kuona (ona **2 Cor 5:7**).

d. *Sadaka: utoaji wa sadaka (mfano; utoaji ambao hutugharimu sana) huonyesha kile tunachothamini kuliko vyote—Kristo na ufalme wake au hazina zetu za kidunia, kwa sababu "mahali ziliko hazina [zetu], ndiko uliko na moyo [wetu] pia" (**Math 6:21**).* Yesu mwenyewe ni mfano kamili wa utoaji dhabihu. Aliacha utukufu wa mbingu zenyewe na kuja kufanyika mwanadamu kwa ajili yetu (**Wafil 2:5-7; 2 Wakor 8:9**). Ingawaje alikuwa Mungu katika mwili, alizaliwa katika hori (**Luka 2:6-7**), hakuwa na nyumba yake mwenyewe (**Luka 9:58**), na aliishi ili kuwatumikia wengine (**Math 20:28; Marko 10:45; Yoh 13:5-15; Wafil l 2:7**). Aliyatoa maisha yake kwa ajili ya wengine, hata kwa adui zake (**Math 20:28; Marko 10:45; Rum 5:6-8; Wafil 2:8**). Yesu aliongelea mifano miwili ya dhabihu ya kujitoa:

(1) Katika **Marko 14:3-9** mwanamke alimimina mafuta ya manukato kichwani pa Yesu, yenye thamani ya dinari 300. **3** *Naye alipokuwapo Bethania, nyumbani mwa*

*Simoni mkoma, ameketi chakulani, alikuja mwanamke mwenye kibweta cha marhamu ya nardo safi ya thamani nyingi; akakivunja kibweta akaimimina kichwani pake. [4] Palikuwa na watu waliochukizwa katika nafsi zao wakisema, "Kwani kupoteza marhamu namna hii? [5] maana marhamu hii ingaliweza kuuzwa kwa dinari mia tatu na kuzidi, wakapewa maskini." Wakamnung unikia sana yule mwanamke. [6] Yesu akasema, "Mwacheni; mbona mnamtaabisha? Amenitendea kazi njema; [7] maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwaatendea mema; lakini mimi hamnami siku zote. [8] Ametenda alivyoweza; ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko. [9] Amin, nawaambia, Kila ihubiriwapo Injili katika ulimwengu wote, na hili alilotenda huyu litatajwa kwa kumbukumbu lake."*

(2) Dinari moja ilikuwa ni sawa na wastani wa mshahara wa siku moja. Kwa hiyo, alitoa sadaka iliyogharimu mshahara wa mwaka mzima kumheshim Yesu. Yesu akasema kwamba *"Ametenda alivyoweza,"* na kama matokeo ya kutoa sadaka kwake "*Kila ihubiriwapo Injili katika ulimwengu wote, na hili alilotenda huyu litatajwa kwa kumbukumbu lake."*

(3) Katika **Luka 21:1-4** Yesu alimwona mwanamke akiweka senti mbili za shaba kwenye hazina ya hekalu: *"[1]Akainua macho yake akawaona matajiri wakitia sadaka zao katika sanduku la hazina. [2] Akamwona mjane mmoja maskini akitia mle senti mbili. [3] Akasema, Hakika nawaanbia, huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote; [4] maana, hao wote walitia sadakani katika mali iliyowazidi, bali huyu katika umaskini wake ametia vyote alivyokuwa navyo."*

(4) Yesu aligundua hata kutoa senti mbili za shaba zinaweza kuwa na umuhimu mkubwa kiroho kuliko kutoa shekeli au talanta maelfu. Sababu ni kwamba, kulingana na kanuni za Sadaka au dhabihu, kitu kilicho muhimu kuliko vyote siyo kiasi gani mtu anatoa, lakini ni kiasi gani mtu anabakiwa nacho baada ya kutoa.

(5) Wakati ule ule, kwa hatua nyingine, kifungu hicho "chaweza kuonyesha huzuni kubwa kuhusiana na utaratibu ambao ulimlazimisha mwanamke yule kutokuwa na namna nyingine ya kupata rasilimali nyingine" (Blomberg 1999: 144-45). Katika makanisa yetu, ni lazima tuwe waangalifu kutowalangua au kutowafanyia mbinu za kijanja watu utoaji na kuwafanya watu ambao tayari ni masikini kuwaingiza kwenye umasikini zaidi. Badala yake, wakati tukifundisha kuhusu kanuni za Ki-Biblia za utoaji, tunapaswa pia kufundisha watu hao jinsi ya kujimudu kiuchumi.

**E. *Kutoa kulingana na Mitume***

Katika Agano Jipya, Mitume, hasa Yakobo na Yoh, wanajadili kanuni za utoaji na umuhimu wa utoaji. Hata hivyo ni Mtume Paulo tu ndiye mwenye maelekezo ya dhati kuhusiana na utoaji. Maelekezo yake yaliyochambua na yaliyopanuka sana yahusuyo utoaji yanapatikana katika **1 Wakor 16:1-4** na **2 Wakor 8-9** (ona pia **1 Tim 6:17-19**).

1. Mtume Yakobo—kitabu cha Yakobo. Matumizi yetu ya fedha na mali kuwasaidia masikini na wahitaji kujenga ufalme wa Mungu ndicho kiini cha ujumbe katika kitabu cha Yakobo.

a. ***Yak 1:27*** *hueleza "Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba" ni hii, "Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo m*awaa." Neno analolitumia kwa ajili ya "Dini" (Kiyunani = *threskeia*) "huzungumzia mwonekano wa ki-nje wa mfumo wa dini ya mtu" (Blomberg 1999: 151), au usafi wa kweli, ibada ya kweli, na utaratibu wa ibada ya kuabudu (Zodhiates 1992: 742). Kwa hiyo, kuwajali yatima na wajane (m.y., wahitaji wa kweli) NI sehemu muhimu ya kile kinachomaanishwa kwa kumwabudu Mungu kwa kweli.

b. ***Yak 2:1-9*** *panaeleza kwamba kuwapendelea matajiri kuliko masikini "kunavunjia heshima masikini" (**2:6**) na ni dhambi (**2:9**).* Kwa upande mwingine, kuwatendea masikini heshima ile ile unayowafanyia matajiri, ni njia moja unayoonyesha kwamba "lunampenda jirani Yak kama unavyojipenda mwenyewe" (**Yak 2:8**).

c. ***Yak 2:14-17*** *panaonyesha kwa nguvu kabisa kwamba "maneno matupu" ya kumtakia mtu mema, yaliyo matamu, ya yaliyojaa uzuri, yasiyokuwa na Mdo, wala msaada wa kuwalisha chakula, kuwavika mavazi, na kuwasaidia masikini na wahitaji, kunaonyesha kwamba imani hiyo ni ya uongo—na imani kama hiyo "imekufa."* Blomberg anaeleza kuhusiana na hili: "Wakristo thabiti leo ambao wana kipato cha kuwazidi . . . wanaoelewa kuwako kwa watu

wenye mahitaji makubwa maeneo waliyopo au sehemu nyingine duniani, bila kusahau ndani ya jamii ya Kikristo . . .wasiotoa chochote kati ya kipato chao, ama kupitia kanisa au mashirika mengine ya Kikristo, kusaidia wale ambao wametindikiwa vitu duniani, wanapaswa kujiuliza wenyewe ikiwa madai yoyote ya kiimani wanayoyataja, yataweza kusimama mbele za kipimo cha Mungu cha hukumu" (Blomberg 1999: 155).

d. ***Yak 5:1-6** panatoa tamko kali la hukumu kwa wale ambao wanaokumbatia utajiri wao badala ya kuutumia kuwasaidia masikini na wahitaji.* Kiukweli wanakuwa wamejinenepesha wenyewe kwa kipindi kitakachoishia kwa kuchinjwa kwao, kama nguruwe walionenepa (**Yak 5:5**). Zaidi ya hayo, utajiri wao wenyewe, ambao hawakuutumia vizuri "utakuwa shahidi kinyume nawe" kwenye hukumu (**Yak 5:3**).

2. <u>Mtume Yoh—**1 Yoh** na **3 Yoh**.</u>

a. ***1 Yoh 2:15-17** panaonya kuhusu kuipenda dunia au "mambo yaliyo katika dunia."* Yeyote aipendaye dunia au mambo yaliyo katika dunia, "kumpenda Baba hakumo ndani yake" (**1 Yoh 2:15**).

b. ***1 Yoh 3:17-18** kunaunganisha kumpenda Mungu na kuwasaidia masikini na masikini vitu.* Kama ilivyokuwa kweli kwa Yakobo, Yoh anauliza, "mtu akimwona riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, Je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?" (**1 Yoh 3:17**) Tena, kama alivyosisitiza Yakobo, Yoh naye anaagiza "tusipende kwa neno wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli" (**1 Yoh 3:18**). Jinsi tunavyowafanyia masikini ki-vitu ni mwonekano wa nje, unaoonekana wa kama kweli tunayo imani inayookoa.

c. ***1 Yoh 4:20-21** panaongeza umuhimu kwamba "asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."* Kule "kumpenda ndugu" kunahitaji kwambatupende *"kwa tendo na kweli"*—m.y, kwa masaada wa vituwith— siyo tu *"kwa maneno au kwa ulimi."*

d. ***3 Yoh 3-8** Panampongeza Gayo kwa kuonyesha ukarimu kwa wengine.* Yoh analinganisha msaada wa vitu wa Gayo kwa wageni na *"kuenenda katika kweli"* (**3 Yoh 3-4**), *"akitenda kiuaminifu"* (**3 Yoh 5**), na kuonyesha upendo (**3 Yoh 6**). Kwa hiyo, msaada wetu wa vitu kwa masikini na wahitaji kimsingi ni la rohoni, na huonyesha ukweli wa imani yetu.

3. <u>Mtume Paulo—mazingira yake na hoja ijadiliwayo **1 Wakor 16:1- 4** na **2 Wakor 8-9**.</u>

a. *Tukio lililopo katika **1 Wakor 16:1-4** ni maagizo ya changizo ambayo Paulo aliliagiza kanisa la Korintho kufanya, ili kuwasaidia waamini masikini na wahitaji wa Yerusalemu (**Rum 15:26; 1 Wakor 16:1-4**).* **1 Wakor** nayo yaliandikwa labda kukaribia mwaka wa 54-55 Baada ya Kristo.

b. *Kufikia sehemu ya baada ya 55 B.K. Au mwanzoni mwa 56 B.K, hata hivyo, changizo hiyo ilikuwa haijatekelezwa.* Kwa hiyo, Paulo akaandika **2 Wakor**, kwa sehemu kidogo, ili kumalizia upatikanaji wa hiyo changizo (**2 Wakor 8:6-7, 10-11; 9:1-5**).

c. **Mdo 20:2-3** na **Rum 15:25-27** panaonyesha kwamba baada ya kuandika **2 Wakor**, Paulo alirudi tena Korintho, na kukaa karibu miezi mitatu, kisha akapokea ile changizo kwa ajili ya wale masikini na wahitaji aliyoitegemea.

4. <u>Sura halisi ya kiroho ya utoaji wa kweli wa Kikristo.</u> Utoaji wa Kikristo siyo tukio la kuonekana nje tu, kwamba ni kuzitoa tu fedha. Badala yake, katika maana yake halisi, utoaji ni tendo la kiroho. Utoaji ni karama ya neema ya Mungu katika utendaji. Paulo analifanya hili liwe wazi kwa njia kadhaa:

a. Ingawaje **2 Wakor 8-9** ndiyo maelekezo ya Paulo yaliyo ya wazi zaidi kuhusu fedha na utoaji, kamwe hatumii neno "fedha" au kitu chochote cha kuonyesha "kitu mbadala" wa fedha.

b. *Lugha au maneno anayoyatumia Paulo zaidi kuelezea utoaji ni "neema" (*Kiyunani=*charis).*

(1) Paulo anatumia *charis*, inayotafsirika katika Biblia ya NASB kama "neema" au "kazi ya neema," kuzungumzia utoaji katika **2 Wakor 8:1, 6, 7, 9, 19, 9:8,** na **14**.

(2) *Charis*, itumikayo kuzungumzia utoaji, imetumiwa pia **2 Wakor 8:4** (iliyotafsiriwa kama "kibali"), na katika **2 Wakor 8:16** na **9:15** (ilipotafsiriwa kama "shukurani").

(3) Ule uhalisi wa kiroho wa utoaji kama ni *charis* au neema unaonekana katika **2 Wakor 8:7** ambapo utoaji unafananishwa na neema nyingine za kiroho za "imani," "unenaji," "maarifa," "uaminifu,"na "upendo."

c. *Maneno mengine yanayotumiwa hasa kuhusiana na sura halisi ya utoaji wa kiroho.*

(1) Paulo anahusisha utoaji na *koinonia*, ambao hutajwa kama "meza ya Bwana" au "ushirika,"katika **2 Wakor 8:4** (iliyotafsiriwa kuwa "shirika") na katika **2 Wakor 9:13**

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

(iliyotafsiriwa kuwa "changizo").
(2) Paulo anazungumzia utoaji kwa neno *leiturgia*, ambalo linatupa neno jingine "liturgy," katika **2 Wakor 9:12** (lililotafsiriwa kuwa "utumishi").
(3) Paulo pia anaita utoaji *diakonia* katika **2 Wakor 9:1, 12-13** (lililotafsiriwa kuwa "huduma").
(4) Katika **Wafil 4:18** Paulo anatumia lugha ya Agano la kale la dhabihu za kuteketezwa kuelezea utoaji"harufu ya manukato" na"sadaka yenye kibali, yenye immpendezayo Mungu" (ona pia **Waeb 13:16** ambapo panaita kule kushirikiana "dhabihu").

5. <u>Utoaji unaonyesha picha ya kujitoa kwa Kristo mwenyewe.</u>
a. *Katika **2 Wakor 8:7-8** Paulo anatoa hoja kwa Wakorintho kutoa kwa changizo ili kuthibitisha " uthabiti wa pendo lenu."* Kisha anaendeleza wazo na hoja yake **2 Wakor 8:9** kwa kusema *"kwa"* (au, *"kwa sababu"*) *"Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake."* Kwa hiyo, kwa kutoa tunawasaidia wahitaji, tukimfuatisha Kristo aliyejitoa mwenyewe kutusaidia tulipokuwa wahitaji tusioweza kujisaidia wenyewe.
b. *Katika hoja yake kwa Wakorintho, Paulo anawataja Wamakedonia waliojitoa kwa hiari kwa changizo ile.* Walitambua ule utoaji wa rohoni, unaomfanania Kristo, kama Paulo asemavyo katika **2 Wakor 8:5**, *"Tena walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu."*

6. <u>Nani anatakiwa kuttoa.</u>
a. *Neema ya kiroho ya utoaji imetolewa kwa kila mwamini katika kanisa.*
(1) Maelekezo ya Paulo kupokea changizo hayakuishia kwa watu fulani wenye mali au matajiri katika kanisa, lakini yalitolewa kwa kanisa kiujumla (**1 Wakor 16:1-2; 2 Wakor 8-9** [hebu ona hasa **2 Wakor 9:7**]).
(2) Kusema ukweli, kila moja alitoa, au aliitiwa kutoa, kuanzia wale ambao walikuwa katika *"umasikini mkuu"* na wale *"waliokuwa katika dhiki nyingi"* (**2 Wakor 8:2**) na kwa wale ambao *"wana vitu vingi"* (**2 Wakor 8:7**).
(3) Katika **Waef 4:28** Paulo anasema kwamba, "Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji."
(4) In **1 Tim 6:17-18** Paulo anasema kwamba "matajiri . . . [uwaagize] watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo." Ikatika fungu lile "matajiri"kimsingi ni wale ambao wana zaidi ya wanavyovihitaji kwa haja zao. Hilo linakuwa dhahiri tunapoangalia **1 Tim 6:8** panaposema, "Ila tukiwa na chakula na nguo, tutaridhika na vitu hivyo." Matokeo yake, hao "matajiri", ni wale walio na vyakula na mavazi yaliyowazidi.
b. *Pamoja na hiyo neema ya ujumla (charis) utoaji, hali ambayo kila mwamini anayo, kuna kipawa maalum (charisma) cha utoaji ambacho siyo wote wanaweza kuwa nacho (**Rum 12:6-8**).*
(1) Wale wenye kipawa maalum cha rohoni (*charisma*) cha utoaji wanapaswa kukitumia *"kwa moyo mkunjufu"* (**Rum 12:8**).
(2) Ukweli kwamba kuna kipawa cha kiroho cha utoaji pia unaonyesha, katika sura yake halisi, utoaji wa fedha na vitu kuwasaidia wahitaji na kuujenga ufalme ni wa rohoni, siyo wa kimwilini tu.

7. <u>Jinsi utoaji wa kweli wa Kikristo unavyotakiwa kufanywa.</u>
a. *Utoaji unatakiwa ufanywe kwa uhuru na kwa hiari (**2 Wakor 8:3, 8; 9:7**).*
(1) <u>Wakristo hawako chini ya sheria ya Zaka au Fungu la kumi kama walivyokuwa Waisraeli.</u> ingawaje Paulo *"aliyaagizaza"* makanisa ya Galatia and Korintho kutoa kwa ajili ya changizo (**1 Wakor 16:1**), alisisitiza kwamba *"Sineni ili kuwaamuru"* (**2 Wakor 8:8**), kwamba kutoa kunafanywa *"si kwa huzuni, wala si kwa lazima;"* (**2 Wakor 9:7**), na kwamba si ili*"mpate dhiki."* (**2 Wakor 8:13**).
(2) <u>Paulo alitaja mfano wa Wamakedonia ambao *"kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao"* (**2 Wakor 8:3**).</u> Anasema kwamba *"Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima."* (**2 Wakor 9:7**).
(3) <u>Ikiwa mtu ataamua kwa hiari kutoa, kwa vile anajua kutoa ni neema inayomtukuza</u>

Mungu, basi bila shaka mtu anaweza, na atapaswa, kutoa kwa moyo wa ukunjufu na furaha, *"maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu"* (**2 Wakor 9:7**). Matokeo ya utoaji wa moyo wa ukunjufu utakuwa *"furaha tele"* (**2 Wakor 8:2**).

b. *Utoaji unapaswa ufanyike kwa utaratibu (**1 Wakor 16:2; 2 Wakor 9:6-7**).* Utoaji wa utaratibu unahusisha yafuatayo:

(1) Utoaji unapaswa uwe umepangwa na kukusudiwa mapema. **2 Wakor 9:7** kila mtu na atoe *"Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake ."* "Kukusudia" kunamaanisha "kupanga uamuzi tangu mapema, kuchagua." Kwa hiyo, kutoa hakupaswi kuwa ni mwitikio wa kihisia wa hitaji fulani, bali uwe wa kuwazia.

(2) Utoaji unapaswa ufanyike mara kwa mara. **1 Wakor 16:2** panasema fedha ziwe zinatengwa kando *"Siku ya kwanza ya juma."* **2 Wakor 9:6** panatumia mlinganisho wa mfano wa mkulima anayepanda na anayevuna. Mkulima, bila shaka, hawezi kupanda mbegu mara moja na kisha kutegemea kuvuna maisha yake yote yaliyobakia. Badala yake, ni lazima apande mara kwa mara, kila msimu wa kupanda. Hivyo tunatakiwa tufanye upandaji kuwa tabia ya mara kwa mara maishani.

c. *Utoaji unapaswa ufanyike kulingana na rasilimali ya mtu na uwezo wake (**1 Wakor 16:2; 2 Wakor 8:3, 11-12**).*

(1) Kadiri mtu alivyo na uwezo wa kutoa, na atoe zaidi. Paulo analisisitiza hili mara nne nzima. **1 Wakor 16:2** (kila moja na atoe *"kwa kadiri ya kufanikiwa kwake"*); **2 Wakor 8:4** (Wamakedonia walitoa *"kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao"*); **2 Wakor 8:3** (kila moja na atoe *"kwa uwezo wake"*); **2 Wakor 8:12** (kila moja na atoe*"kwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadiri ya asivyo navyo"*).

(2) Swala muhumi kuhusiana na hili ni kwamba, siyo tu kwamba mtu aliye na uwezo zaidi atoe zaidi kwa ukunjufu zaidi, lakini anapaswa *kutoa kiasi kikubwa zaidi ki- asili mia ya kipato chake na rasilimali zake* kuliko mtu aliye na kidogo.

d. *Utoaji unapaswa ufanyike kwa hiari na kwa ukarimu (**2 Wakor 8:2, 9; 9:5-6, 13**).*

(1) Wamakedonia, licha ya *"wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao"* (**2 Wakor 8:2**). Wamakedonia hata walitoa *"zaidi ya uwezo wao"* (**2 Wakor 8:3**). Hilo ni kweli, ni utoaji wa Sadaka. Kama vile Yesu alivyomsifu yule mwanamke aliyetoa senti mbili zake na yule wa marhamu iliyokuwa ghali sana, Paulo anawataja Wamakedonia kama mfano wa utoaji ambao utoaji wa Wakorintho unapaswa kufuata (ona **2 Wakor 8:7-8; 9:1-4**).

(2) Paulo pia alitaja mfano wa Yesu Kristo aliyejitoa kila kitu kwa ajili yetu, *"ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake"* (**2 Wakor 8:9**).

(3) Mwishowe, Paulo alisisitiza kuwa utoaji lazima uwe wa *"Ukarimu"* (**2 Wakor 9:5-6**). Kutoa kwa hiari bila shaka hufuatia wakati waamini wanajua kuwa kutoa ni neema ya Mungu inayomtukuza Yeye.

8. Kusudi la utoaji wa kweli wa Kikristo ni kukutana na haja halisi (**2 Wakor 8:4, 13-15; 9:12**).

a. *Mahitaji yanaweza kuwa ya kimwili* (k.m; matatizo ya umasikini; kukosa chakula, mavazi, hata makao; kiafya). Hiyo ndiyo iliyokuwa sababu rasmi ya changizo katika **1 Wakor 16:1-4** na **2 Wakor 8-9**.

b. *Mahitaji yanaweza pia kuwa ya kiroho* (k.m; umisheni; kumtegemeza mchungaji na viongozi wa kanisa; kutunza majengo na mali za kanisa; kuhudumia jamii ya nje kwa njia yoyote ile; kutoa nafasi ya mafunzo na vitu vingine vya Kikristo kwa mchungaji, washiriki wa kanisa, na watu wengine).

c. *Paulo alisisitiza kwamba "si jambo la urahisi kwa wengine"* (**2 Wakor 8:13**). Kwa hiyo, makanisa na watu binafsi wanahitaji kupima *nini* walichoitiwa kufanya na *kwa nini* wameitiwa kufanya hicho. Kupima na kujua kama kuna hitaji la kweli kunaendana na utoaji wa makini. Ikishajulikana kwamba kuna hitaji la kweli, basi kanisa au mtu binafsi akiguswa ili alihudumie, basi hapo utoaji wake unapaswa uwe wa moyo mkunjufu na wa hiari.

9. Matokeo ya utoaji wa kweli wa Kikristo.

a. *Mungu anatukuzwa (**2 Wakor 9:11-15**).* Shukurani kwa Mungu, na kukuzwa kwa utukufu wake hutokea wakati watu wake wanatoa inavyotakiwa. Sababu, bila shaka, ni kwamba wanapotoa inavyotakiwa, Watu wa Mungu huurudisha mng'aro wa utukufu kwake.

b. *Walengwa husaidika (**2 Wakor 8:13-15; 9:12**).*

(1) Kutoa kunawategemeza watakatifu kimwili na kiroho. Itokeapo wale wanaopewa ni waaminio, mwili wa Kristo hujengwa na kuenezwa duniani (**2 Wakor 9:12**).

(2) Kutoa kunawawezesha watakatifu kusaidiana kila moja kwa mwenzie. Kutoa usawa kati ya waamini ambao mwanzoni walikuwa masikini, lakini sasa wana rasilimali za kuwasaidia waamini wengine ambao baadaye wataangukia katika janga la umasikini na uhitaji (**2 Wakor 8:13-15**).

c. *Watoaji wanabarikiwa (**2 Wakor** 8:2; 9:1-4; 6-11; 13-14).*

(1) Utoaji unatulinda sisi kutokana na aibu inayotokana na *kushindwa* kutekeleza wajibu wetu (**2 Wakor 9:1-4**).

(2) Mungu aliwapa aliwasababisha Wamakedonia kuwa na *"wingi wa furaha"* kwa sababu walitoa sana kiajabu, licha ya dhiki yao na umasikini wao mkubwa (**2 Wakor 8:1-3**).

(3) Mungu humimina neema kubwa kwa watoaji wenye moyo wa ukunjufu (**2 Wakor 9:8;** ona pia **2 Wakor 8:1; 9:13-14).**

(4) Mungu anaahidi kutushughulikia haja zetu za kimwili na kiroho tunapokutana na haja za wengine kwa kutoa (**2 Wakor 9:6-11**).

(A) *Paulo anasema kwamba "Yeye apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu" (**2 Wakor** 9:6).* Hoja ni kwamba, Mungu atakutana na haja zetu za mwilini kwa njia hiyo hiyo kama tunavyokutana na haja za wengine (ona **2 Wakor 9:8-11**). Kanuni hii siyo "sheria" fulani au wajibu unaomfunga Mungu kutoa kiasi fulani cha vitu kama tukitoa. Kwa mfano, hakuna dalili kwamba, baada ya kutoa kwa ukarimu sana, wale wa Makedonia mara moja wakawa matajiri (ona **2 Wakor 8:1-3**). Badala yake, ni katika kutekeleza kanuni ya msingi kwamba Mungu anajua na atayashughulikia mahitaji yetu kadiri tunavyomtumaini na kuwa watii kwake, na kutupatia thawabu na kushughulika nasi kama tunavyoshughulika na wengine, kiroho na kimwili. Tunaweza kumwamini kabisa kuwa atafanya hivyo (ona **Mith 3:9-10; 11:24-25; 28:27; Mal 3:8-12; Math 6:12, 33; 10:42; Marko 10:28-31; Luka 6:38; Wagal 6:6-7**).

(B) *Mungu siku zote atatubariki kiroho na kutuongezea "wingi wa haki yetu" na "shukurani kwa Mungu" (**2 Wakor 9:10-11**) tunapotoa kama inavyotakiwa.* Baraka za Mungu za vitu juu yetu sisi huweza kuja katika njia fulani moja kwa moja kutoka kwake, lakini kulingana na **2 Wakor 8:13-15** is kimsingi kabisa huwa zinatufikia kupitia mwili wake duniani, ambao ni kanisa.

(C) ***1 Tim 6:19** panasema kwamba wao watoao "wanajiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli."* Hilo linazungumzia hali yetu ya umilele zamani zijazo. Kwa kutoa fedha zetu na mali zetu kuwasaidia masikini na wahitaji na kuujenga ufalme sasa, Mungu atatupa thawabu za milele ambazo zitadumu milele. Kwa hiyo, tunajiandaa kwa ajili ya siku zet za mbeleni kidunia kwa kuweka akiba na kuwekeza fedha na kujifanya katika hali ya kujitosheleza, lakini tunajiandaa kwa milele ijayo kwa kutoa.

d. *Utoaji unalifungamanisha kanisa pamoja.*

(1) Utoaji unawavuvia watakatifu kutoa kila moja kwa ajili ya mwingine. Unachochea wivu kwa waamini wengine nao watende vivyo hivyo, kwa sababu kutoa ni mfano wa kumfanania Kristo (**2 Wakor 9:2, 13**).

(2) Utoaji unawawezesha wale wanaopokea vilivyotolewa na waamini wengine kuomba kwa ajili ya hao waliotoa na *"wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu"* (**2 Wakor 9:14**).

## III. Upotofu wa Injili ya Mafanikio[5]

### A. *"Injili ya Mafanikio" ni nini*

1. Baadhi ya watu huhubiri kile kiitwacho "injili ya mafanikio" (pia inajulikana kama "Injili ya afya njema na utajiri").

a. *Aina hii ya mafundisho kimsingi hufundisha kwamba ni mapenzi ya Mungu kwa waamini kuwa na mafanikio ya kimwili, kifedha na mali.* Madai hayo daima huendana mkono kwa mkono na madai kwamba waamini wote wanapaswa wawe na afya njema kimwili. Hoja za mara kwa mara kati ya wahubiri wa mafanikio, huwa za mawazo kama vile: imani ni "nguvu" ambayo huchochewa tunapoinena; tunahitaji tu "kitaja au kukiri hicho kitu na kukidai" (m.y, kutaja kile tunachokihitaji kisha kukidai kwa imani); tunahitaji tu "kupanda mbegu kwa imani" (m.y, toa fedha kwenye huduma fulani maalum ili kuonyesha imani Yak); kuna sheria ya "kurudishiwa" ambayo Mungu amefungwa nayo (m.y, ile kanuni ya "kupanda na kuvuna" na ile ya "kurudishiwa mara mia") ambapo, ikiwa tuta "panda mbegu" katika huduma fulani kwa kutoa kiasi fulani cha fedha, ikiwa tutakuwa na imani ya kutosha kwa Mungu, atarudisha mara mia kiasi cha fedha tulizo "panda."

b. *Wahubiri wa mafanikio wana ladha iliyo dhahiri, rahisi, na ya "mbinu ya utendaji" ya mahusiano kati ya baraka za vitu na baraka za rohoni*. Kwa hiyo, umasikini au magonjwa hunenwa kuwa ni matokeo ya dhambi, au ukosefu wa imani, bali ukiwa na imani ya kutosha, na kunena au kudai baraka zetu, au kutoa fedha kwenye huduma humlazimisha Mungu atoe hata zaidi kabisa kwetu na kwa hiyo kutusababisha tupokee baraka za mwilini.[6]

c. *Kile injili ya mafanikio inachofanya, ni kuchukua ujumbe ambao kimsingi ni mzuri na wa kweli—m.y:, "Umasikini ni kitu kibaya; ni heri kuwa tajiri kuliko kuwa masikini; ni bora kuwa na afya kuliko kuwa mgonjwa; hujakusudiwa kuwa mgonjwa au kuwa masikini, lakini unaweza kufanya kitu kurekebisha hali Yak katika maisha"—na wanaupotosha ujumbe huo kwa kuitumia vibaya Biblia.* Kimsingi hasa, injili ya mafanikio inajaribu "kubatiza" ujumbe ule ambao kihalisia ni wa kidunia na wa kawaida, na kuugeuza uwe wa kiroho —m.y., kugeuza ujumbe wa kujiboresha mwenyewe, uwe wa injili ya Yesu Kristo. Si dhambi kuwa tajiri na kuwa na afya badala ya kuwa masikini na mgonjwa. Si dhambi kufanya kazi kuboresha hali Yak ya kiuchumi na kimaisha. Bali pamoja na hayo, ni makosa kupotosha Biblia. Ni huo upotofu, ndio sababu ya kuleta somo hili.

2. Kauli za kuwasilisha za "walimu wa mafanikio" ni pamoja na zifuatazo:

a. *Creflo Dollar:* "Umasikini si mapenzi ya Mungu kwa mwamini yeyote. . . . Wewe uli "*fanyishwa"* uwe na mali na tajiri hata kabla hujaja duniani. Umeandaliwa kufanikiwa kifedha. . . . Ukiwa mwenye haki wa Mungu, urithi wako wa mali na utajiri umejumuishwa katika "baraka zako za kiroho" (au kitu cha kiroho) Mtume Paulo alichokizungumzia katika Waefeso 1:5. Kulingana na Zaburi 112:3, haki, mali, na utajiri huendana pamoja mkono kwa mkono. Unayo haki kabisa kumiliki mali za kidunia—nguo, vito vya thamani, nyumba, magari na fedha — kwa uwingi kabisa. Ni mali hizo ambazo siyo, tu zinakukidhi mahitaji Yak, lakini pia hueneza ujumbe wa Injili, na kukidhi haja za wengine. Biblia inasema mali *zimehifadhiwa kwa ajili ya wenye haki* (Mith 13:22, Biblia ya *New American Standard)*. Hata hivyo, itabakia imehifadhika mpaka wewe utakapoitamka na kuiita au kuidai. Kwa hiyo, uidai sasa! Unao uwezo wa kuimiliki na kuamuru mali na utajiri kuja kwako (Kum 8:18). Dhihirisha nguvu hiyo kwa kusema maneno yaliyojaa imani kila siku, na kuchukua hatua za kiMdoo kuondokana na madeni. Kama Mungu, unaweza kutamka baraka za rohoni zikatokea (Warumi 4:17). Kumbuka, mashaka hukufanya uwe kimya, imani hunena!" (Dollar 2008: n.p.)

b. *Kenneth Copeland:* "Katika dunia nzima Mungu anaonyesha wazi kwamba mapenzi Yake kwa watu wake wa Agano kuwa na ziada ya mahitaji yao. Aliahidi kumfanya Ibrahimu tajiri, na ahadi ya Ibrahimu ni yetu leo (Wagalatia 3:13-14; Mwanzo 17:6). Mapenzi ya Mungu ni

---

[5] Injili ya mafanikio hasa katika Afrika, imekosolewa kwa mapana sana na Femi Adeleye kwenye kitabu chake kiitwacho *Preachers of a Different Gospel* (Kampala, Uganda: International Fellowship of Evangelical Students, 1999).

[6] Waalimu wa Injili ya mafanikio wanafanana sana na wale rafiki watatu wa Ayubu, ambao walifikiri kuna muunganiko wa moja kwa moja 1:1 kati ya kufanya mema na kupewa thawabu au kufanya mabaya na kuhukumiwa.
Kwa sababu hiyo wakafikia hitimisho kwamba Ayubu alikuwa ametenda dhambi na alikuwa akiteswa kwa sababu ya dhambi hiyo (**Ayu 4:7; 8:1-22; 11:1-20**). Tabia hiyo iyo ilioneshwa na wanafunzi wa Yesu waliofikiri kwamba upofu wa yule kipofu ulitokana na labda dhambi zake au za wazazi wake (**Yoh 9:1-2**).

mafanikio kwako—kiroho, nafsi, na mwili. . . . Mafanikio ya kuonekana kimwili Yak katika sehemu mbili—kiafya na mali. Yesu alitukomboa kutokana na laana ya sheria—magonjwa, umasikini na mauti (Kum 28: 15-61). Afya na mali ni mali ya mwamini. Kulitafakari Neno na kulitendea kazi Neno kutaleta matokeo (Yoshua 1:8). Wakati unalitendea kazi Neno, changanya imani Yak nalo, na usione shaka moyoni mwako, Neno litatenda kazi kwa ajili Yak." (Copeland 2008: n.p.)

c. *Charles Capps:* "Ili uweze kuhamasika kikamilifu kupata mafanikio, kwanza ni lazima tujue ni mapenzi ya Mungu kwetu kufanikiwa! . . . Mungu ni mwaminifu; atalitenda Neno lake. Alisema, Neno langu halitanirudia bure. (Isaya 55:11) Lakini Mungu anakutaka wewe urudishe Neno lake kwake. Hivyo ulichukue Neno la Mungu kuwa ni ahadi kuhusiana na kitu fulani rasmi. Ikiwa hitaji lako ni katika eneo la maswala ya fedha, liweke Neno lile katika moyo wako kwa kulinena. Weke hazina nzuri ya Neno la Mungu katika kinywa chako, kisha linene. Hivyo utalitokezea jambo hilo nje nalo litadhihirika. . . . Utoaji ni mojawapo ya njia muhimu za kanuni za mafanikio. Si kiasi kilichotolewa ambacho ni muhimu kwa Mungu lakini ni ile asilimia. . . . Thawabu kulingana na ile asilimia iliyotolewa. Kurudishiwa kwake kunatokana na kiasi unachotoa. Kanuni hii inatenda kazi kwako, sawasawa kama inavyotenda kazi kwa mamilionea. Tofauti tu ni kwamba, yeye anatendea kazi kiasi kikubwa zaidi. Kama utaendelea kuitumia kanuni hii, senti zako zitakuja kugeuka kuwa dola Milioni!" (Capps 2008: n.p.)

3. <u>"Mistari ya ushahidi" ya Maandiko inayotumiwa mara kwa mara na "waalimu wa mafanikio" ni pamoja na ifuatayo:</u>

a. **Yos 1:8—***Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapofanikisha njia Yak, kisha ndipo utakapositawi sana.*

b. **Mith 3:9-10—***Mheshimu BWANA kwa mali Yak, na kwa malimbuko ya mazao Yak yote. Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, na mashinikizo Yak yatafurika divai mpya..*

c. **Mal 3:10—***Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha au la."*

d. **Marko 10:28-30—***Petro akaanza kumwambia, Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata wewe. 29 Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili, 30 ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mshamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele."*

e. **Yoh 10:10—***Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*

f. **2 Wakor 8:9—***Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake.*

g. **2 Wakor 9:6—***Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.*

h. **3 Yoh 2—***Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya Yak, kama vile roho Yak ifanikiwavyo.*

**B.** ***"Injili ya mafanikio" ina mtazamo wa makosa wa Mungu, mpango wa Mungu, na Injili.***

Hilo wazo kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba kila mtu awe tajiri kifedha na afya kamili, au kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja na wa mara moja kati ya imani ya mtu na uwingi wa vitu, au kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya uwingi wa vitu kwa mtu na baraka zake za rohoni kutoka kwa Mungu, si kweli wala si wa Ki-Biblia.

1. <u>Mungu ni mkuu amilikiye juu ya dunia yote, vikiwamo kila kitu na kila mtu ndani yake.</u>

a. *Matukio yote Yak katika mpango kamili wa Mungu nayo hujitokeza ili makusudi Mungu atukuzwe.* Kama sehemu ya ukuu wa umiliki wake, Mungu huwajibika kikamilifu kwa yote yatokeayo, kwa yaliyo mazuri au mabaya (**Mwa 1:1; Ayu 12:9-10; Zab 24:1; 50:10-12; 139:13-16; Isa 44:24; 45:5-7**).

b. *Hii "injili ya mafanikio" inapinga ukuu wa Mungu, na matokeo yake, inamfanya mwanadamu ndiye mkuu na mwenye enzi*. Injili ya mafanikio inageuza ukuu wa Mungu na

mwanadamu kwa sababu:

(1) Inashikilia kwamba Mungu amefungwa na, au anawajibishwa kwa sheria fulani (kama vile "sheria ya marejesho");

(2) Inadai kwamba mwanadamu anyo tabia ya uungu ya "kukamata na kuamuru mali na utajiri kuja kwako . . . Kama Mungu, waweza kutamka baraka za rohoni zikatokea" (Dollar 2008: n.p.); na

(3) Inamgeuza Mungu kuwa mtumishi wa mwanadamu, akiongozwa na mapenzi ya mwanadamu na mipango ya mwanadamu, wakisema "neno litafanya kazi kwa ajili Yak" (Copeland 2008: n.p.).

2. <u>Si kweli kwamba Mungu hasa hutaka kila mtu awe na afya nzuri kabisa.</u>

a. Mungu huwainua wengine, na huwashusha wengine chini—ikiwa ni pamoja na kuwafanya wengine matajiri na wengine masikini **(1 Sam 2:7; 1 Nya 29:12-16; Ayu 42:10; Zab 75:6-7; Mhu 5:19; Dan 2:20-21; 1 Tim 6:17).**

b. Mungu huamuru magonjwa yaje kama vile aamuruvyo kuhusu afya (**Kut 4:10-11; Ayu 1:1, 6-2:7; Mith 20:12; Mika 4:6; 2 Wakor 12:7-10).**

c. Mungu huua na kufanya hai; hutenda yote mawili pia; yaani kufunga tumbo na kulifungua (**Mwa 20:17-18; Rut 4:13; 1 Sam 2:6; Eze 24:16-18; Mdo 2:23; 4:27-28**).

3. <u>Si kweli kwamba magonjwa, umasikini, kifo, au mambo mengine ni matokeo ya dhambi au ukosefu wa imani.</u> Kati ya mifano mingi ya hili, sehemu mbali mbali za Biblia ni hii:

a. Mtu moja alikuwa kipofu tangu kuzaliwa, si kwa sababu ya dhambi zake wala za wazazi wake (**Yoh 9:1-3**).

b. Dhambi haikuwa sababu ya kifo cha Wagalilaya ambao damu yao ilichanganywa na Pilato katika sadaka zao, wala za watu kumi na nane waliouawa wakati mnara ulianguka juu yao (**Luka 13:1-5**).

c. Mungu aliruhusu Ayubu kupoteza mali yake yote, watoto, na afya, ingawaje Ayubu alikuwa mtu mwenye haki ambaye hakutenda dhambi (kusema ukweli, hakukosa kabisa, *kwa sababu* Ayubu alikuwa ni mwenye haki wa Mungu ambaye hakuwa ametenda dhambi) (**Ayu 1:1, 22**).

d. Mungu alisababisha Yusufu apoteze vyote alivyokuwa navyo, si kwa sababu ya dhambi yoyote, au kwa kupungukiwa na imani, lakini ili kuwa sehemu ya mpango ulio mkuu zaidi, na ulio mzuri (**Mwa 50:20**).

e. *Paulo aliteswa na mwiba "mwiba wa mwilini":* Mungu akakataa kumjibu maombi ya Paulo aliyotaka amwondolee mwiba huo; na Paulo akateseka maisha yake yote kwa umasikini, na dhiki, siyo kwa sababu ya dhambi yoyote, au ukosefu wa imani, lakini hasa ni kwa sababu ya uaminifu wake na kudhihirisha nguvu ya Kristo ndani yake (**2 Wakor 12:7-10;** ona **2 Wakor 11:23-33; Wafil 4:10-13**).

f. *Yesu Kristo mwenyewe alikuwa mtu masikini:* alizaliwa katika familia ya kimasikini (Ile dhabihu au sadaka waliyoitoa Mariamu na Yusufu walipomtoa mtoto Yesu na kumweka wakfu kwa Bwana ilikuwa imeandikwa kwa ajili ya watu waliokuwa masikini; ona **Luka 2:22-24; Law 5:11; 12:8**); na katika maisha yake yote "hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake" (**Math 8:20**); Baba alikataa kutenda kama Yesu alivyotaka katika maombi ya bustani ya Gethsemane (**Luka 22:41-42**); na Yesu akateseka na kufa kama asiye na haki, akiwa na mali moja tu ya kidunia, lile vazi lake alilolivaa, ambalo nalo lilitwaliwa kutoka kwake hata kabla hajafa (**Luka 23:34**). Umasikini huu wote na ugumu haukuwa kwa sababu Yesu alikuwa ametenda dhambi, au "alikosa imani," lakini ulikuwa hasa ni kwa vile hakuwa na dhambi na alikuwa amemwakilisha Baba kikamilifu hapa duniani.

4. <u>Siyo kweli kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja, au sababu kati ya kuwa na imani; au kutenda mema na kubarikiwa kwa utajiri wa kidunia, na kukosa imani au kutenda mabaya na kujikuta unakabiliwa na umasikini.</u>

a. *Kwa vile Mungu aliumba dunia na kuunda sheria na taratibu ambazo kwazo inaenenda, ikizifuata taratibu hizo (k.m., kuishi maisha ya uaminifu, kufanya bidii katika kazi Yak, kuweka akiba na kuwekeza kipato chako, nk.) kwa ujumla hukuwezesha kupata utajiri wa mali; hata hivyo, si lazima kwamba hilo lazima litokee.* Kuna uhusiano wa kawaida kati ya kupanga, kufanya kazi, uangalifu, maisha ya kujitunza kiafya; na uwezo wa kuwa na mafanikio kimaisha; na upande wa uvivu, uhusianavyo na maisha mabaya, na umasikini. Hata hivyo, uhusiano huo haudhibitiwi na Mungu wala na Biblia. Uwezo wa mtu kupata kiasi cha fedha za kuridhisha unahusiana na mambo mengi, ikiwa ni pamoja na elimu ya mtu, uwezo wake vipaji, wapi na lini

mtu anaishi, watu anaojuana nao, nafasi za kimaisha, na mambo mengine. Kupata kanuni za Ki-Biblia za jinsi ya kijiboresha mwenyewe katika kuwa kweli hata katika maswala ya kawaida, ni lazima mtu aitawale kazi yake mwenyewe, maisha, na familia, na lazima pasiwepo na matatizo mazito ya kimfumo ya kijamii. Kwa hiyo, ingawaje kuna uhusiano wa ujumla kati ya jinsi mtu anavyoishi,na jinsi anavyoweza kuwa na mafanikio kimaisha, hatuwezi kupangilia kuhusu baraka za Bwana za kidunia.

b. *Yote mawili "neema ya kawaida" ya Bwana kwa wote na neema yake iokoayo kwa wenye dhambi yanapingana na muktadha wa "moja kwa moja wa baraka/laana za mali."* Mungu amejifunua mwenyewe kama mwingi wa rehema, hata (hasa, kabisa) kwa wenye dhambi (**Kut 34:6-7**). *"Maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki"* (**Math 5:45**). Ingawaje inawezekana isionekane sawa kwetu, waovu mara nyingi hufanikiwa (**Zab 73:1-14**). Zaidi ya yote, *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi"* (**Rum 5:8**). Mfano ulio bora kabisa wa Mungu kuwapenda wadhambi walio wabaya kabisa ni kwa Mtume Paulo. Mungu alimimina neema na rehema zake kwa Paulo wakati Paulo alikuwa katikati kabisa ya kufanya uovu mkuu—alikuwa njiani kwenda Dameski kuwatesa na kuwaua Wakristo, ambako ni sawa na kumtesa Kristo Mwenyewe (**Mdo 9:1-5**). Hata hivyo, Paulo alisema kwamba *"Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele"*(**1 Tim 1:16**).

c. *Mungu hulipiza kisasi kwa watu wake, lakini hajaahidi kufanya hivyo mara moja au si lazima sana iwe wakati wa maisha haya duniani.* Maagano yote mawili, yaani Agano la Kale na Agano Jipya huonyesha kwamba Mungu huwalinda masikini na tendo la kuwalipiza kisasi waovu *hayajitokezi* "hapo hapo" *au lazima iwe wakati huu wa maisha haya* (ona **Zab 9:17-20; Ufu 6:9-11**). Mamilioni ya Wakristo, (wakiwamo wasio na idadi leo hii) wameishi katika umasikini, wameteseka, wamepata dhiki, na kufa kwa ajili ya imani yao vizazi na vizazi. Katika maisha haya, waamini hao hawakuwa na afya nzuri wala kuwa na uwingi wa mali. Umasikini wao, mateso yao, na kudhikika kwao, hakukuwa kwa sababu walitenda dhambi, au kukosa imani; lakini ni kwa sababu walikuwa ni wenye haki na waliishi maisha ya imani. Hata hivyo, Mungu amewarudi hao—na watu waaminifu kama hawa wanatawala pamoja na Kristo sasa (**Ufu 20:4**), na milele yote wataishi katika mbingu mpya na nchi mpya ambamo *"wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena"* (**Ufu 21:4**). Gordon Fee anatukumbusha sisi kwamba: "Ingawaje Mungu ameahidi kulipa kisasi walio wake, ni mara chache ameahidi kutenda hivyo papo kwa papo. Kwa mfano katika Waeb 11:32-39 wengine kwa imani walipata ushindi mkubwa; lakini wengine *kwa imani walikuwa wahitaji.* Lakini *wote* wamesifiwa kwa imani yao.

Na maneno haya yalinenwa ili kuwatia moyo waamini ambao wenyewe walikuwa "kwa furaha walikubali kunyang'anywa mali zao" (10:34, N.I.V.), lakini kwa sasa walikuwa karibu kukata tamaa. Kisasi cha papo kwa papo, hata hivyo, hakikuahidiwa kwao (10:35, 36)." (Fee 1984: 41)

5. <u>Mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu—injili—haihusiani na watu kuwa na mali katika dunia hii, ila kwamba wanakuwa kama Kristo.</u> Mpango wa Mungu si kuwaita watu kwake, ambao wanajisikia kujitosheleza na kujisikia kushibishwa katika yeye, siyo na vitu vya dunia hii.

a. *Injili inahusika hasa na kutuokoa sisi na dhambi na kutuleta katika uhusiano ulio hai na Yesu Kristo, anayetubadilisha kuwa katika mfano wake (ona* ***Yoh 1:12; 3:16; Rum 8:13-16, 29-30; 10:9-10****).* "Tusisahau kabisa kwamba kusudi la msingi la Injili ni kutuokoa na kutuleta katika uhusiano ulio hai na Mungu, na kila moja wetu. Inazaa watu waliobadilishwa, na ambao wana ushuhuda wa haki ya Mungu . . . Kila mtu anayejitambua kwamba ni mdhambi, na yuko tayari kugeuka kutoka katika dhambi zake, na kuamini kwamba Yesu Kristo alikufa na kufufuka kutoka kwa wafu kwa ajili ya kumuokoa yeye, anaweza, kwa kupitia sala fupi kufanyika mtoto wa Mungu." (Adeleye 1999: 137)

b. *Tabia ya mapenzi ya Mungu kwa waaamini ni ya utashi au kitabia zaidi kuliko mali.* "Vifungu viwili vya Agano jipya ambavyo rasmi vunazungumzia mapenzi ya Mungu kwa mwamini hueleza kuwa katika lugha ya utashi, kuliko lugha ya kiuchumi. Mapenzi ya Mungu kwa waamini ni utakaso wao na kujitenga na ubaya au uovu (1 The. 4:3), pamoja na kutoa shukurani kwa kila jambo (1 The. 5:18). Mtazamo wa Mungu kama ulivofunuliwa katika

Maandiko hujihusisha na swala kwamba waamini ni nani, kuliko nini walivyo navyo. Matokeo yake mkazo mdogo zaidi unapaswa uelekee katika mazingara ya nje na kuzidisha zaidi kwenye mitazamo ya ndani na tabia za mtu." (Sarles 1986: 341).

c. *Matarajio yatokanayo na Injili kwa watu wa Mungu ni kama ifuatayo:*

(1) Tunapaswa kuwa katika dunia, lakini si "wa" dunia (**Yoh 17:14-19**)—m.y, tunapaswa kusema *"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu"* (**Rum 12:2**).

(2) Tunapaswa kuwa *"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake"* (**1 Yoh 2:15**).

(3) Tunapaswa kugeuzwa na kumfuatisha Kristo (**Rum 8:29**) na kuishi maisha *"ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo"* (**Waef 1:4**).

(4) Mtume Paulo alieleza wazi juu ya uhusiano kati ya kuwa na mali na vitu na kutimiza mapenzi ya Mungu katika **Wafil 3:7-8:** [7] *Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo.* [8] *Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo.*

(5) Matokeo ya Mungu ya kweli kwa watoto wake mara nyingi ni kinyume cha kile ambacho walimu wa "mafanikio" hufundisha.

(A) Mbali na mapenzi ya Mungu kwamba waamini wawe na uwingi wa vitu, Kristo alisema*"Basi, kadhalika kila moja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"* (**Luka 14:33**).

(B) Yesu aliwaambia rasmi wanafunzi wake kwamba maisha yao yataandamana na dhiki, badala ya anasa, raha na urahisi kwa sababu *"mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake"* (**Math 10:16-39; Yoh 13:16; 15:18-20**).

(C) Kule kupenda fedha kunamwondoa mtu kutoka kuwa na sifa ya uongozi katika kanisa (**1 Tim 3:3, 8; Tito 1:7**).

6. Hiyo"injili ya mafanikiol" inaharibu mpango wa Mungu wa kupatia mahitaji ya watoto wake.

a. *"Injili ya Mafanikio" si injili lolote kwa sababu inamwondoa Kristo kwenye kiti chake cha enzi.* "Yesu ndiye Injili. Injili ni rahisi na imenyoka sana kwetu kiasi kwamba tunaweza kuwakwepa wale wanaoongeza ya kwao ili kuiharibu. Injili yoyote ambayo inaharibu nafsi, au utume wa Yesu Kristo siyo Injili kabisa. Injili yoyote inayosisitiza miujiza au mafanikio zaidi kuliko kifo cha Yesu na kufufuka kwake ni ya kutilia mashaka. Na kila mhubiri au mwalimu anayejiinua mwenyewe juu ya Kristo na utume wake si mjumbe wa Mungu kamwe." (Adeleye 1999: 137)

b. *"Injili ya Mafanikio" inayainua maswala ya mwilini kuliko kukuza ya kiroho.* "Hebu tuwe wakweli. Kama tungekuwa na uchaguzi, wengi wetu tungetamani kuwa na afya nzuri, maisha marefu, kuwa na vitu vingi na nafasi nzuri zenye ushawishi katika kanisa ana taifa. Shauku za namna hiyo ni za kikawaida na kiasilia, kwa sababu ile asili yetu ya dhambi hutafuta faida zake yenyewe, kujiinua na mafanikio. Lakini mpango wa Mungu kwa watu wake ni kuwaona wanakua katika neema. Ile asili ya kiburi, na yenye kujiona yenyewe ni lazima isulubishwe katika mpango wa Mungu wa kupatia haja, ambayo hupitia majaribu ya kila namna. "Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno' (Ja 1:2-4)." (Editorial 2001: 2)

c. *"Injili ya mafanikio" ina makosa ki-hoja na ki-historia.* "Ni kujidanganya mwenyewe kufikiri mtu ataishi Afrika na kuishi maisha bila kupitia dhoruba za maisha. Tangu siku za baba zetu hadi siku za karibuni, maisha ya siku kwa siku ni kwa njia ngumu na ya jasho. Hata hivyo, tunazingirwa na maumivu, magonjwa, na katika nchi nyingi, njaa. . . . Ni jinsi gani basi tutawazia kujitoa mara moja kutoka uhalisi huu ati tu kwa kumfuata Yesu . . . . Injili hii ya mafanikio imekuwa kimya mno kuhusiana na maumivu na mateso kwa sababu haina theolojia yeyote kuhusiana nayo. Mambo yote yahusuyo kukosa raha, maumivu, mateso, umasikini, na na kifo, huonekana kuwa ni ya yule mwovu na hivyo hupaswa kukataliwa. Mawazo yaliyo nyuma yake huwa ni kutokusoma vema Warumi 8:28 na kufanya pasomeke , "ni mambo mazuri tu

huwakuta wale walio katika Kristo Yesu" au kuamini kuwa Wakristo hawapaswi kuteseka. . . . tunajua kutokana na Maandiko na historia ya kawaida kwamba Watakatifu wengi waliteseka sana. Ni kweli, kifo cha kimwili ni tukio la kawaida ambalo haliwatenganishi wenye haki na wasio na haki. Mungu katika hekima yake amekiteua hicho kiwe hivyo. . . . Ile injili ya "afya na mali" kwa hiyo inakuwa si lolote isipokuwa ni mvuto wa ulaghai kuingiza katika mkanganyiko." (Adeleye 1999: 99-103)

**C. *"Injili ya mafanikio" ina mtazamo wa makosa kuhusu imani na maombi.***

1. Uhusiano wa "Injili ya mafanikio' na "imani" au "kuamini" ni kinyume na kile kinachomaanishwa na Biblia kuwa Imani na Kuamini.

a. *Hoja ya injili ya mafanikio kuhusu imani ni kimsingi ni aina ya uchawi.* "Huenda hoja iliyo ngumu kuliko zote kueleweka katika injili ya mafanikio, ni imani ya mwanadamu. Imeondolewa kutoka katika maana iliyomo katika Biblia, na kupewa maana nyingine kabisa. Imani imetafsiriwa kuwa ni nguvu njema. "Imani ni nguvu ya kiroho, ni nguvu ya msukumo ya kiroho, ni nguvu ya utendaji. Ni nguvu hii ya imani ambayo inaufanya ulimwengu wa rohoni utende kazi yake. . . . Kuna kanuni fulani zilizofunuliwa katika Neno zinazotawala mafanikio. Imani inazifanya zifanye kazi. Zitatenda kazi pale zinapowekwa kazini, na zitaanza kufanya kazi pale nguvu ya imani itaapoacha kufanya kazi" [nukuu kutoka kwa Kenneth Copeland].

Kulingana na tafsiri hii, imani ya mwanadamu ina thamani yake halisi licha ya uasili wake. Imani inakuwa nguvu inayotolewa na wahusika. . . . Imani pia imekuwa na tafsiri mpya ya mahusiano yasiyo ya kawaida yanayohusu uwezo wake katika kunenwa neno. Kuamini kwa moyo kumeunganishwa na ukiri wa kinywa ili kuumba uhalisi mwingine. "Unapokea katika maisha haya kile unenacho kwa kinywa chako. Neno katika kinywa chako ni imani Yak inenayo. *Maneno uyanenayo katika kinywa chako, ndicho uaminicho.* Maneno Yak yanaweza kuwa kwa faida Yak, au yakawa kinyume chako. Hukupatia afya au magonjwa. Maneno Yak yanaamua kama uishi katika uwingi wa vitu, au ufukara" [nukuu ya Gloria Copeland].

Katika mtazamo huu, imani ni aina ya uchawi, ambapo neno lile linalonenwa ndiyo ulogaji wake. Mbinu iliyojificha ya wazo la mafanikio inadai kwamba kwa vile mwanadamu ni kiumbe wa mfano wa Mungu, maneno yake, yanenwapo kwa imani, yana uwezo ule ule wa kiutendaji ndani yake kama ya Mungu. Lakini hoja hii ya imani ya mwanadamu ni ya kiuchawi, siyo ya kiroho." (Sarles 1986: 347-48)

b. *Kitovu cha "imani" ya injili ya mafanikio—mwanadamu na mafanikio yake kivitu katika dunia hii, badala ya Mungu—ni kinyume moja kwa moja na imani ya Biblia.* "Katika msingi wake kabisa, imani potofu [ya] mafanikio hutoa theolojia ya kumweka mwanadamu katikati, badala ya kumweka Mungu katikati. Ingawaje mtu huambiwa mara kwa mara kwamba ni utukufu wa Mungu - kwamba tunapaswa tufanikiwe, tunda hilo kusema kweli huwa ni kwa ajili ya ubinafsi wetu na hali ya kutaka kujinufaisha.

Kusema ukweli, mtu pekee ambaye angeweza kuyaamini mafundisho haya yasiyo ya Ki -Biblia ni mtu ambaye *anataka* kuwa hivyo; na sababu *pekee* ya kutaka hivyo ni ile hali ya kuinua hali ya ubinafsi wake. Mungu hayuko kwa ajili yetu; sisi ndiyo tupo kwa ajili yake. Na imani katika Mungu haipimwi kutokana na hoja ya furaha ya mwanadamu. Mungu, licha ya yote, si mtu ambaye yeyote aweza kumwajiri katika imani yake kwa ajili ya manufaa yake binafsi. Kuweka furaha ya vitu kuwa ndiyo lengo la imani ya Kikristo, ni kuigeuza iwe kichwa chini." (Fee 1984: 42-43)

c. *Kwa vile injili ya mafanikio inapotosha kiini cha imani, ni dhahiri kabisa inapotosha kuhusu Mungu na mahusiano yake na watu wake.* "Huyu 'Mungu' mpya ni yule ambaye, na hasa wahubiri fulani, humtumia kiujanja kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Huyo 'Mungu' anapendwa sana na kukubaliwa na watu sana—kwa sababu nzuri tu.

Kwanza, yeye huweza kuamriwa, kuelekezwa, au 'kuagizwa' kufanya lolote mwanadamu apendalo. . . . Pili, huyo 'Mungu' ni yule ambaye hana utukufu uliobaki kwake, au yote yakishafanyika, mkazo wa kusudi zima la 'utukufu' huwa siyo wa 'Mungu' lakini wa 'mtu wa Mungu' aliyeweza 'kumfanya' Mungu kufanya lile ambalo hao watu walitaka afanye. . . . Tatu, huyu 'Mungu' ni yule ambaye hajali sana kuhusu jinsi watu wake wanavyoishi. Yeye ananenwa kuwa ni yule ambaye anamkonyeza yeye asiye mcha Mungu au aishiye maisha yenye sura mbili za viongozi na wafuasi wake. Yeye anaridhika tu, ili mradi apate 10% ya mapato, muda, na rasilimali za wafuasi wake na haingilii maswala mengine ya maisha yao. . . . Hii ndiyo

sababu 'Mungu' huyu siye Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni 'Mungu aliyeumbwa kwa mfano wa mwanadamu mwenye dhambi.'" (Adeleye 1999: 106-07)

2. Kinyume chake, hoja ya Ki-Biblia ya imani na kuamini kimsingi ni kumtumaini na kumwamini Mungu na kutoa maisha ya mtu kiutii kwa Mungu kupitia Kristo kulingana na alichokisema.

a. *Imani ya kweli ya Biblia ni karibu kinyume kabisa cha "imani" ya injili ya mafanikio kwa karibu kila hoja.* "Biblia inafundisha kwamba imani ni kutumainia kikamilifu kwenye, na kutumainia kitu kingine. Badala ya kuwa kile kitu kilichowekwa, imani ya Ki-Biblia huzungmzia pumziko au kuamini ahadi zake. Thamani ya imani ni nje, siyo ndani ya kitu. Umuhimu wa imani unaonekana katika kitovu chake, yaani aitwaye, Mungu." (Sarles 1986: 348)

(1) Katika Agano la Kale, imani kimsingi inahusishwa na Yule aliye kitovu cha tumaini la mtu huyo, siyo kama aina ya "nguvu" au "uwezo fulani" ndani na nje yake yenyewe. Mafungu fulani ya maneno ya Kiebrania ya makundi ya imani au kuamini huelezea hoja ya "kuenzi au kuwa na matumaini kwa mtu fulani au kitu"; Fungu jingine la maneno ya Kiebrania ambayo huelezea hoja hiyo hiyo "huonekana mara nyingi zaidi katika Biblia ya Kiebrania, lakini hutafsiriwa mara nyingi kuwa 'kuweka tumaini' badala ya 'kuwa na/kuamini'" Kwa hiyo, "Utayari wa Abramu kumtumaini Mungu. . . humweka yeye kuwa mtu wa msingi kwa hoja ya Ki-Biblia ya imani. Kukubali kwake kumtumaini na kumtii Mungu ni kutimizika kwa agano ambalo Mungu aliliweka Yeye." (Schowalter 1993: 222)

(2) Mtazamo au hoja ya imani ya Agano Jipya ni sawa na wa Agano la Kale, utofauti wa msingi ukiwa ni kile kiini cha imani ya mtu ni Yesu Kristo. Kwa hiyo, lugha ya imani inatumiwa "kwa yote mawili; utambulisho wa kiMdoo wa mamlaka yasiyo ya kawaida ya Yesu, na pia kama mwitikio halali kwa injili ambayo alikuja kuitangaza. . . . [Katika Injili ya Marko, 'kuamini] kunatambulikana dhahiri kwa kuhusishwa kwake na *metanoia* ('toba') kama zaidi ya hali ya kutumainia kiMdoo au kuamini kwa kiakili. Ni hatua ya kujitoa ambako kunabadilisha maisha, mwanzo wa mahusiano mapya na Mungu. . . . [Katika Injili ya Yoh, kuamini] ni Ufuwa mwitikio, na mamtokeo yake katika kuijua kweli. Lakini kwa vile ufahamu huo umekuja kwetu kwa njia ya mtu, ambaye mwenyewe ni kweli, si imani wala uelewa unaoweza ukaeleweka katika uelewa wa kiakili. Kiini cha kuamini huko, kinaweza kuwa ni Yesu mwenyewe peke yake." (France 1992: 223-25)

b. *Mifano mizuri ya imani huonyesha kwamba imani ya Ki-Biblia haikufanya kazi kama "nguvu," na haitumiwi kamwe kama kitendea kazi kutimiza tamaa ya utajiri wa mali au fedha.* Biblia ya *Africa Bible Commentary* inatoa maelezo yafuatayo kuhusiana na mifano mizuri ya imani, **Waeb 11,** kwa kuangalia, "Mwandishi anaanza kwa kueleza imani kama uwezo wa kuwa na *uhakika wa kile tunachokitarajia* na bayana ya mambo yasiyoonekana (**11:1**) na kisha panaorodhesha mifano mingi ya Agano la Kale ya yale ambayo imani inawezesha kuwa (**11:2**)" (Adeyemo 2006: 1504). Katika mifano hiyo, hakuna hata moja ambao angalau unakaribia hata kwa umbali wazo la walimu wa mafanikio la imani ni nini au imani inatakiwa itumiwe kwa ajili ya nini. Badala yake, mifano ya imani katika **Waeb 11** inaonyesha yafuatayo (Ibid.: 1504-05):

(1) Imani huona kile ambacho wegine hawakioni (**11:3-4**).
(2) Imani huwawezesha waamio kutembea karibu na Mungu (**1:5-6**).
(3) Imani huwawezesha waamio kuiona hatari au uharibifu mapema (**11:7**).
(4) Imani huwawezesha waamio kumtii na kumfuata Mungu wakati hawaijui, njia ya kuiendea (**11:8-10**).
(5) Imani huwawezesha waamio kuipokea ahadi ya Mungu katika hali zisizowezekana (**11:11-12**).
(6) Imani huwawezesha waamio kuvumilia hata kama ahadi hiyo haikutekelezwa mara moja (**11:13-16**).
(7) Imani huwawezesha waamio kuitimiza dhabihu ya ahadi (**11:17-19**).
(8) Imani huwawezesha waamio kutambua na kuzijia baraka za Mungu (**11:20-22**).
(9) Imani huwawezesha waamio kufanya vitu vya hatari (**11:23**).
(10) Imani huwawezesha waamio kukataa anasa za maisha ya kidunia (**11:24-28**).
(11) Imani huwawezesha waamio kuishinda hofu na makwazo mengine (**11:29-31**).
(12) Imani huwawezesha waamio kuvumilia magumu mengine mengi (**11:32-39a**).

3. Kama injili ya mafanikio ilivyo na mtazamo usio sahihi wa yote mawili; tabia na kiini cha imani, vivyo hivyo ina mtazamo usio sahihi wa tabia na kiini cha maombi.

a. *Waalimu wa "Mafanikio" mara zote huelekeza kwamba mtu ataomba kwa ajili ya hitaji la kitu fulani, Mungu anapaswa kulijibu* . Wanasimamia hili katika:

(1) **Math 7:7-8—**[7] *Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa;* [8] *kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa*; na

(2) **Marko 11:23-24—**[23] *Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.* [24]*Kwa sababu hiyo nawaambia Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*

b. *Hakuna kifungu chochote hapo kinachoonyesha kwamba, au kinahusiana na mafundisho ya mafanikio.* Kiasi kwamba vinahusiana na maombi, vifungu hivyo vinahusiaana na kuhakikisha kwamba tunakuwa na kiini halisi sahihi na lengo (m.y, Mungu, siyo fedha), na tabia njema na aina sahihi ya maisha (m.y, unyenyekevu na msamaha, na siyo uchoyo).

(1) Katika **Math 7:7-8** hoja inayofuatisha mara hushughulika na: siyo kujiwekea "hazina duniani"; hali ya kutowezekana kwa kuyatumikia yote mawili; "Mungu na mali"; na kwamba tunapaswa kumtegemea Mungu pekee na siyo kutafuta mali na vitu ambavyo watu wa mataifa huvitafuta (**Math 6:24-34**). Zaidi ya hayo, sala au maombi yanapaswa kutokea katika maisha matakatifu ambamo hatuwahukumu wengine, lakini tunaondosha "boriti la jichp letu" kabla hatujashughulika na "kibanzi kilicho katika jicho la ndugu yetu," na ambamo ninyi "mwawatendea watu wengine jinsi mpendavyo wao wawatendee ninyi" (**Math 7:1-5, 12**). Kifungu kinachoendana na hicho cha **Luka 1:9-13** pia kinasema kwamba "vipawa vyema" Baba atakavyotupatia tunapomwomba, kutafuta, na kubisha mlango, ni Roho Mtakatifu, siyo fedha.

(2) Katika **Marko 11:23-24** hoja inayofuatia pale mara moja inashughulikia: Kuingia kwa shangwe kwa Yesu mjini Yerusalemu kama Masiha; kuwafukuza wauzao na wafanya biashara kutoka hekaluni; kuulani mtini (ishara ya taifa lisilo na imani la Israeli); na mwitikio wake kwa viongozi wa Kiyahudi waliohoji juu ya mamlaka yake kwa kuwaeleza mfano wa mwenye shamba la mizabibu, ambao kwao alikuwa akisema ufalme utaondolewa kwa Israeli na kupewa watu wa Agano Jipya la Yesu ambao wanamwamini (ukiwa kwa kiwango kikubwa na watu wa mataifa) (**Marko 11:1-12:12;** ona pia kifungu kinachoendana nacho cha **Math 21:1-46**). Zaidi ya hayo, kiini cha imani yetu kinapaswa kuwa ni Mungu, siyo utajiri wa vitu (**Marko 11:22**), na maombi yetu yanapaswa kutokea kutoka katika maisha matakatifu ya masamaha (**Marko 11:25-26**).

c. *Mjadala mpana zaidi wa ki-Biblia wa maombi unaondoa wazo kwamba hakuna kifungu au hata unaonyesha kwamba Mungu "anafungwa na tuyatakayo" na ni lazima atupatie kila kitu tunachokitaka au kukiomba katika sala. Kusema kweli, hoja kama hiyo ya maombi kiuhalisia ni kinyume na uhitaji wa Ki-Biblia kwa maombi yenye kufaa.* Vifungu kadhaa huthibitisha hili:

(1) **Yoh 15:7—***Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.* "Kukaa ndani ya Yesu" ni sharti la kwanza ili maombi yajibiwe. Hoja hii inajadiliwa na D. A. Carson: "*Ikiwa mtakaa ndani yangu* panafafanuliwa katika mstari wa 9, na mrandano wake kwa jinsi Yesu alivyosema; *Ikiwa . . . maneno yangu yakikaa ndani yenu* ni namna nyingine ya kufikia kweli hiyo hiyo. *Maneno* ya Yesu (*rhēmata*) ni matamshi yote halisi ambayo kwa pamoja hufanya "neno" la Yesu (mstari wa 3; *logos*). Maneno hayo lazima yajikite katika akili na moyo wa mwanafunzi na kumfanania Kristo, utiifu kwa Kristo, ni kitu cha kiasilia zaidi au (nje ya kiasilia?) duniani. . . . Kumfanania katika upande moja na kumfanania katika jingine; mtihani kwa maeneo yanayoonekana kwa macho ya Kristo, ni mtihani wa eneo lisiloonekana kwa macho ya umuhimu wa kiroho. Yote haya ni sawa na kubakia katika mzabibu; na huko ndiko kuunganika ambako matunda yataonekana. Kuliweka hilo katika maombi, mwamini aliye mwaminifu kiasi hicho, huthibitisha kuwa ni ya kufaa, kwa vile yale ayaombayo yote yanaendana na mapenzi ya Mungu." (Carson 1991: 517-18)

(2) **Yak 4:3—***Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili*

*mvitumie kwa tamaa zenu.* Sababu ya kuomba kwetu lazima iwe sahihi—lakini tamaa ya fedha na vitu ili kuvitumia kwa ajili yetu wenyewe ni msukumo wa makosa. Zaidi, lengo la maombi lisiwe kujitazama mwenyewe—hata hivyo, mwito wa injili ya mafanikio, kwa asili yake halisi, ni mwito wa ubinafsi. Kwa hiyo, mstari huu, kama huo wa juu, ni kinyume moja kwa moja na hoja ya walimu wa mafanikio ya maombi.

(3) **Yak 5:16b—***Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.* Ili kufae kuomba kwake aombaye, ni lazima awe ni "mwenye haki." Hiyo inamaanisha kwamba, ni lazima awe na *"nia ya Kristo"* (**1 Wakor 2:16**), na anabadilishwa kumfanania Kristo (**Rum 8:29**). Ili uwe kama Kristo ni kinyume na fikira za injili ya mafanikio. Zaidi ya hayo, hoja ya **Yak 5** inaanza na lawama kali juu ya matajiri (**Yak 5:1-6**), na inaendelea kuwabariki wale ambao wanateseka kama Ayubu (**Yak 5:7-11**), hoja zote mbili ni kinyume na fikira za mafanikio.

(4) **1 Yoh 3:22—***na lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake.* Kupokea kile tunachokihitaji, hutegemea utiifu wetu na maagizo ya Kristo na kutenda mambo yampendezayo. Kule kuyatafuta na kuishi kwa ajili ya utajiri na anasa, kamwe hakuonyeshi utii wala kufuata maagizo ya Kristo, wala hakupendezi mbele yake, lakini ni tofauti ya moja kwa moja na jinsi alivyoishi yeye.

(5) **1 Yoh 5:14-15—**[14]*Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia.* [15]*Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.* Maombi yanayojibiwa yana masharti kwamba yawe *"kulingana na mapenzi yake"* (siyo kulingana na mapenzi yetu). Mungu hatutumikii sisi; sisi ndio tunamtumikia yeye. Kifungu hiki, kwa mara nyingine, kinapingana moja kwa moja na injili ya mafanikio.

**D. *"Injili ya mafanikio" inamtazamo wa kimakosa wa fedha na mafanikio.***

1. Biblia *inatufautisha* mali za kidunia na utajiri wa kiroho. *Mifano mingi inathibitisha hili, pamoja na:*

a. ***Luka 12:13-34.*** Katika kifungu hiki Yesu anaonya kuhusu uchoyo na hasa hupinga theolojia nzima inayosimamia "mafanikio ya Kiinjili," pale asemapo: *"Angalieni, jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake, alivyo navyo"* (**Luka 12:15**). Yesu anaendelea kuelezea mithali ya mtu tajiri aliyejenga ghala kubwa zaidi ili kuhifadhia mali zake zote. Hitimisho la mithali ile ni: *"Lakini Mungu akamwambia, Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu."* (**Luka 12:20-21**) Mwisho wa kifungu, Yesu anaelezea mtu *aliye* "jitajirisha kwa Mungu": *"Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo ndipo itakapokuwa na mioyo."* (**Luka 12:33-34**)

*b.* ***Luka 16:10-12.*** Mistari hiyo "Inaeleza kwa njia tatu uhusiano kati ya utajiri wa kidunia na wa kiroho. Huo wa kwanza ni msingi wa kuuthibitishia ule wa baadaye. Mali za kidunia hutajwa kuwa ni 'kiasi kidogo sana', 'utajiri wa kidunia', na ''mali' ya mtu mwingine. Kwa njia ya kulinganisha, baraka za rohoni hutajwa kama 'zaidi', 'utajiri wa kweli', na 'mali Yak mwenyewe'." (Blomberg 1999: 122)

*c.* ***Marko 8:36***. *"Itamfaidia n ini mtu kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?"* "Kuna ukipaumbele wa wazi wa usalama wa mali za kiroho kuliko za mwilini katika mada hii" (Ibid.: 137).

*d.* ***Waeb 10:34.*** *"Maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo, tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo."* Kwa mara nyingine mali za kiroho zina yote mawili *"bora zaidi"* na *"ni za kudumu"* kulinganisha na mali za kuonekana.

*e.* ***Ufu 2:9; 3:17.*** "Katika ujumbe uliopelekewa yale makanisa Saba, Smirna na Laodikia kunaonyesha utofauti mkubwa. Smirna lina umasikini wa mali za kidunia lakinini tajiri kiroho (2:9), ambapo Laodikia lilijipatia mali nyingi na likadhani haja zake zimekwishatoshelezwa. Kumbe, kwa mtazamo wa kiroho, jumuiya ilikuwa imeharibikiwa, yenye kutia huruma na masikini (3:17)." (Ibid.: 236) Hivyo mtu inabidi kuwa makini sana kuhusiana na walimu wowote wale ambao thamani zao na vipaumbele vyao ni tofauti kabisa na vile vya Biblia.

2. Kupungukiwa au kukosa fedha siyo dhambi, na kuwa nazo siyo dhambi. Kama mtu ajajaliwa kuwa na uwezo kifedha, hilo linaweza kuwa jambo jema; lakini injili ya mafanikio ni kitu potofu.

a. *Ziko sababu nyingi sana kwa nini mtu anaweza kuwa masikini, na si lazima iwe sababu ya uvivu au dhambi.* Siasa mbaya za Serikali, misingi mibaya ya kijamii, kukosa elimu, kuishi maeneo yasiyo na maendeleo, kudhalilishwa, na mambo mengine mengi yanaweza kuleta umasikini.

b. *Kupata elimu nzuri, kufanya kazi kwa bidii, kuweka akiba na kuwa bahili na kutofuja fedha ili kujiongezea fedha na mali katika dunia kwaweza kuwa kwema sana.* Ingawaje kupenda fedha —kuwa mbinafsi na mchoyo wa kuitaka hiyo, na kujitumainia na kuitegemea—ni dhambi, kujipatia mali na kujiboresha kimaisha ni mambo mema (**Kum 6:10-11; 1 Wakor 7:21; 1 Tim 6:17**). Kusema ukweli, kwa kupitia kufanya kazi na kufanya biashara, Mungu huwapa watu uwezo wa kujipatia fedha **(Kum 8:16-18; Mith 13:11; 22:29; 28:19-20; Waef 4:28; Yak 4:13-15).** Fedha zinaweza kuwa baraka kwa wengi ili mradi ziwe katika mtazamo mzuri na kutunzwa vizuri.

c. *Jambo la msingi ni kuhusu mtazamo wetu.* Ni kule kupenda na uchoyo wa fedha na kuwa na mali ndiko kunakuwa dhambi kuu **(Kut 20:17; Luka 12:15-21; Waef 5:3; Wakol 3:3-6; 1 Tim 6:17; 1 Yoh 2:15-16).** Kupenda fedha kunaletesha maswala yote ya uovu—kunaweza kulisonga Neno katika maisha yetu, na kutaleta hukumu ya Mungu **(Mith 11:4, 28; Marko 4:18-19; Wakol 3:5-6; 1 Tim 6:10-11; Yak 5:1-6; Ufu 3:17-19).** Tamaa ya fedha ni hatari kiasi kwamba mjadala wa Paulo ulio mrefu kuliko yote, ukawa ni uhusiano wa Injili na fedha. **1 Tim 6:3-19**, panarudia mara kwa mara kuonya kuhusu hilo: tunapaswa kuridhika kwa kuwa na kitu cha kula na kitu cha kuvaa (**6:6-8**); wale watakao kuwa na utajiri huangukia katika majaribu na tanzi, na kujiingiza katika majaribu (**6:9**); kupenda fedha ni chanzo cha uovu wa kila namna na kuwatoa watu katika imani na kuwachoma katika maumivu mengi (**6:10**); tunapaswa *"kukimbia kutoka katika mambo haya"* (**6:11**). Injili ya mafanikio, zaidi ya kuwa ni theolojia iliyo ya kutisha na isivyo ya Ki-Biblia, ina msingi hasa katika uchoyo na tamaa, ambayo Paulo anaonya kwa nguvu na kwa kurudia mara kwa mara. Kwa hiyo, tunapaswa *"kuyakimbia mambo haya,"* kutoka kwa walimu wa mafanikio, na mafundisho yao.

3. Wakati Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba (yaani, ile "sala ya Bwana"), hakutuambia kuomba utajiri, lakini kuomba kwa ajili ya "mkate wetu wa kila siku" (m.y, cha kutosha kuishi kwacho) (**Math 6:11; Luka 11:3**).

a. *Sababu ya muhimu nyuma ya jambo hili ilitajwa na Aguri katika* ***Mith 30:8-9:*** *[8] Uniondolee ubatili na uongo; usinipe umasikini wala utajiri; unilishe chakula kiliho kadiri yangu. [9] Nisije nikashiba nikakukataa, Nikasema, BWANA ni nani? Wala nisiwe masikini sana nikaiba, na kulitaja bure jina la Mungu wangu.*

b. Hayo yanaendana na mafundisho yaliyopo kila mahali katika Biblia kwamba tusiwe na tamaa ya fedha wala mali **(Kut 20:17; Luka 12:15-21; Waef 5:3; Wakol 3:3-6; 1 Tim 6:17; 1 Yoh 2:15-16).** Badala yake, tunapaswa kutosheka tukiwa na vya kututosha kuishi **(Wafil 4:10-12; Waeb 13:5; 1 Tim 6:8**), kwa sababu Mungu ameahidi kwamba uwepo wake utatosha (**Waeb 13:5-6**). Iwe ndiyo au hapa kwamba sisi tunaridhika na tulicho nacho hufunua hali yetu ya kweli ya kiroho. Hili hasa ni muhimu kwa Wakristo, kwa sababu Yesu Mwenyewe alikuwa mtu masikini. Yesu hakuwa na nyumba (**Math 8:20; Luka 9:58**). Kusema ukweli, Yesu alikuwa na mali moja tu—nguo alizozivaa—na Warumi walizichukua kutoka Kwake kabla hawajamsulubisha (**Math 27:35; Marko 15:24; Luka 23:34; Yoh 19:23-25**). Yesu alisema, "wala mtumwa hampiti bwana wake" (**Math 10:24; Luka 6:40; Yoh 13:16; 15:20**). Paulo asemapo katika **1 Tim 6:8** "ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo," anatulenga sisi—kwa sababu chakula na mavazi ndivyo pekee alivyokuwa navyo Yesu, Bwana wetu.

4. Ingawaje kuna manufaa yasiyopingika ya kitambo yanayohusiana na kuwa na fedha na vitu vingi, katika Agano Jipya hakuna uhusiano kati ya utajiri wa vitu na baraka za kiroho. "Katika mtazamo kamili wa Ki-Biblia, mali na vitu vina thamani ya sifuri mbele ya macho ya watu wa Mungu. Hayo yalitolewa sana hasa nyakati za Agano la Kale—bali *kamwe si* katika Agano Jipya—kuwa na mali siku zote kumehusishwa na maisha ya utii. Lakini hata hapa yanaoneka kuwa na dosari ya hatari ya aina mbili kwa kuondosha jicho kutomtumainia Mungu, na kuja kummiliki mweney mali hizo. Umasikini, hata hivyo, *siyo* kwamba unaonekana kuwa ni bora zaidi. . . . Hali hii ya kutokujali kuhusu mali na vitu, ambazo kwazo wala *siyo* mafanikio wala umasikini una thamani, imeshughulikiwa kirefu katika Agano Jipya. . . . Ukiwa katika utaratibu mwingine ulioletwa na Yesu, utajiri hauna maana. Ikiwa mtu anayo

mali, anaweza kuyatumia katika upendo kuwahudumia wengine; lakini ikiwas mtu hana, asiyatafute. Mungu hushughulikia mahitaji ya kila mtu; yaliyozidi haya siyo ya lazima; mtu tajiri anayetafuta zaidi na zaidi ni mpumbavu; maisha hayawi katika uwingi wa mali. . . . Ni hii hasa hali ya mtazamo wa kutojali chochote kuhusu mali na vitu, ndiyo inayomtofautisha Paulo kabisa. Yeye ni mtu huru katika Kristo, ajuaye kuridhika katika hali yeyote. . . . Hoja ni kwamba, katika kizazi kipya mafanikio kwa kifupi hayana thamani yoyote. Vipi, basi, Mungu anaweza kuwatakia kitu kilicho sifuri kama mapenzi yake kwa watoto wake?

Imani ya uongo ya mafanikio kwa hiyo, inakosa kuungwa mkono mahali popote katika Agano Jipya. Ni ya Ki-Biblia kwa jinsi *yoyote*." (Fee 1984: 42)

5. Injili ya mafanikio inaharibia mtazamo wa Ki-Biblia wa mafanikio ya kweli. "Kwa bahati mbaya, wahubiri wa injili ya mafanikio wameleta katika filosofia ya mali katika kizazi hiki, kuamini kwamba kupata vitu vingi ni kushinda. Ni injili iliyoundwa kwa misingi ya vitu na desturi zetu za kawaida. Mafundisho ya Ki-Biblia Yak wazi. '[6] Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. [7] Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; [8] ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. [9] Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. [10] Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi.' (1 Tim 6:6-10). Kinyume na mafanikio ya vitu, mafanikio ya kweli mbele za Mungu, ni utajiri wa imani. '… Je! Mungu hakuwachagua masikini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme...' (Yakobo 2:5)." (Editorial 2001: 2)

6. Hata hivyo, mali yanabeba umuhimu wa kiroho katika nyanja tatu za kiroho:

a. *Mali hubeba pamoja nayo hatari zaidi za kiroho.* Yesu alionya kwamba utajiri ni "mdanganyifu" na unaweza ukalisonga neno la Mungu katika maisha ya mtu (**Marko 4:18-19**). Tamaa ya kutaka kuwa tajiri ni hatari sana na inaweza kuongoza kwenye uovu wa kila namna (**1 Tim 6:9-10**). Alisema kwamba tamaa huongoza kwenye ibada ya sanamu, na kuonya kwamba ghadhabu ya Mungu itakuja juu ya mtu mchoyo au mwenye tamaa (**Wakol 3:5-6**). Yoh alionya kwamba kumpenda Baba hakuko ndani ya yeyote aipendaye dunia au mambo ya ulimwengu huu (**1 Yoh 2:15-16**). Vivyo hivyo katika Agano la Kale, Mitilionya kwamba yeyote azitegemeaye mali zake ataanguka (**Mith 11:28**), na mtu aliye na mali huwa katika kumkataa Mungu (**Mith 30:8-9**). Ayubu alijua kwamba kutumainia mali ni dhambi, kunaiita hukumu kwani kunaletesha kumkataa Mungu (**Ayu 31:24-28**). Mifano ya Gehazi (**2 Fal 5:15-27**), Anania na Safira (**Mdo 5:1-11**), yule mfalme kijana (**Marko 10:17-25**), na yule tajiri aliyemdharau Lazaro (**Luka 16:19-26**), yote inaonya hatari za kiroho zinazoweza kuletwa kwa kuwa na, au kutafuta mali. Kama Adeleye asemavyo, "Kama mwisho wake yenyewe, fedha zina tabia ya kufanyika sanamu inayomaliza maisha yetu wenyewe. Hiyo ndiyo sababu Yesu anatuonya kujihusisha na fedha tunavyohusiana na Mungu." (Adeleye 1999: 97)

b. *Utajiri unabeba pamoja nao wajibu zaidi.* Biblia iko wazi kuhusu kwa nini Mungu hutubariki kwa fedha, "ili mtu awe na kitu cha kumgawia mwingine aliye na hitaji" (**Waef 4:28;** ona pia **1 Tim 6:17-18**). John Piper anaonyesha kwamba, kinyume na wahubiri wa mafanikio, kwamba **Waef 4:28** "si kisingizio cha *kuwa* matajiri ati ili kutoa zaidi. Ni wito wa kupata zaidi, ili kutunza vichache ili utoe zaidi" (Piper 2007: n.p.). Anaongezea kusema: "Hakuna sababu kwa mtu anayetengeneza fedha [zaidi] kuishi tofauti na mtu anayetengeneza kipato kidogo[chache]. Amua kuishi maisha ya kadiri; uwe na kiasi katika matumizi Yak; kisha toa vilivyobakia. Kwa nini utake kuwahamasisha watu kwamba wamiliki mali ili wawe watoaji wa ukarimu? Kwa nini usiwahamasishe watu kuishi maisha yaliyo ya kawaida na kuwa watoaji wakarimu zaidi? Je hilo lisingeongeza kwenye ukarimu wao ushuhuda mkubwa zaidi kwamba Kristo, na siyo mali, ndiye hazina yao?" (Ibid.)

c. *Mali inabeba pamoja nayo, kuwajibika zaidi.*

(1) <u>Kila moja anakabiliwa na hukumu kwa yale tuliyoyafanya, au tuliyoshindwa kufanya, katika maisha haya (**Waeb 9:27;** ona **Ufu. 20:11-15**).</u> Kanuni ya msingi ya hukumu ya Mungu ni "Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi." (**Luka 12:48b;** ona **1 Wakor 3:10-15**). Wale wenye utajiri katika maisha haya, wanakabiliwa na hukumu kubwa zaidi kuliko wale wasio matajiri, kwa sababu utajiri wao unabeba pamoja nao, wajibu mkubwa zaidi, na hivyo, kuwajibika zaidi. Kwa hiyo **Mith 11:4** inaonya kwamba mali zitawafanya matajiri waanguke siku ya hukumu.

(2) Kulundika kiasi kikubwa cha mali na kutoitumia kwa makusudi ambayo Mungu aliitoa kwayo kwetu kunapingana na sheria ya Kristo, na ni dhambi. Yesu alisema kutu na nondo huharibu hazina zilizoko duniani (**Math 6:19**). Mtume Yakobo anaitumia lugha ya Kristo kuwaonya watu matajiri ambao hawakutumia mali zao kama zinavyopaswa (m.y, wameiruhusu "kupata kutu"), *"Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto. Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho"* (**Yak 5:3**). Anaongeza kwamba kwa sababu ya hukumu wanayokabiliwa nayo walio matajiri, wanaambiwa *"lieni, mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia"* (**Yak 5:1**). Anamalizia kwamba wale ambao *"mmefanya anasa katika dunia, na kujifurahisha kwa tamaa; mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo"* (**Yak 5:5**).

**E. *"Injili ya mafanikio" inamtazamo wenye makosa kuhusu utoaji.***

1. Injili ya mafanikio inaharibu sababu ya kutoa kwetu. Yesu alifundisha kwamba tunapaswa kutoa*"kwa mategemeo ya kutorudishiwa kitu"* (**Luka 6:35**). "Sadaka zinapaswa kutolewa kwa Mungu kama tendo la kuabudu (Isa 43:22-24; Zab 16:12-17) na siyo kwa kujinufaisha mwenyewe. Ni ukweli wa Ki-Biblia ambao Mungu anaahidi kuwapa thawabu wale wampaye kwa ukarimu (2 Wakor 9:6-11). Lakini baraka za kiungu hutoa picha ya kipawa cha neema ya Mungu, na siyo kuwajibika kwa Mungu au kibali chake. Kutamani mafanikio kamwe kusiwe sababu ya utoaji. Kabla mtu hajatoa kitu chake, anapaswa kwanza ajitoe mwenyewe kwa Bwana (2 Wakor 8:5; Rum 12:1). Mungu anamjali zaidi mtoaji kuliko kilichotolewa. Ingawaje utoaji wa ukarimu ni muhimu katika Maandiko (2 Wakor 8:1, 2), mtu anapaswa atoe kama kwa Bwana kama dhabihu ya shukurani (Zab 116:17). Kamwe mtu asiitoe akiwa na kusudio la kibinafsi la kutaka mafanikio yake." (Editorial 2001: 1)

2. Kiini cha utoaji wa injili ya mafanikio kusema ukweli ni dhambi—ambayo Mungu hawezi kubariki. Injili ya mafanikio inasema tunakiwa "kutoa ili tupate. Ni kwa kutoa . . . tunahakikishiwa mafanikio yetu wenyewe!" (Fee 1984: 43) Huo si wito wa kingine, isipokuwa *ubinafsi na uchoyo.* Ubinafsi na uchoyo yote mawili ni dhambi ambazo Mungu *hatazibariki* (ona **Kut 20:17; Mith 11:4, 28; Marko 4:18-19; Luka 12:15-21; Waef 5:3; Wakol 3:3-6; 1 Tim 6:10-11, 17; Yak 5:1-6; 1 Yoh 2:15-16; Ufu 3:17-19**). Bila shaka, tamaa au ubinafsi ni aina ya *ibada ya sanamu* inayoleta ghadhabu ya Mungu (**Wakol 3:5-6**).

3. Zaidi ya hapo, "kutoa ili upate" si hasa "utoaji" kabisa. Hiyo ni shughuli ya kibiashara tu, ni aina ya "kuazimana fedha" kwa faida, au ni kama kuwekeza kwenye tukio la kibiashara, au kununua hisa. Kulingana na kanuni ya "'Tegemea Muujiza', ambayo inasisitiza kwamba kutoa mbegu, matatizo yote yasiyoondoleka yatajibiwa . . . Kimsingi Mungu anafanyika wakala wa bima ambaye mtu anapowekeza kwake hutazamia kurudishiwa" (Adeleye 1999:83).

**F. *"Injili ya mafanikio" ina tafsiri isiyo sahihi.***

1. Injili ya Mafanikio imekosea sana kwa sababu njia za walimu wake za kutafsri maandiko zinachagua sana na ni karibu za swala maalum, hazina msingi maalum, ni nje ya hoja kabisa.

a. *Sarles anaelekeza kwamba,* "Mistari ya Biblia inanukuliwa kuwa utele bila kuangalia maneno yaliyotumika yamekaaje, na maana iliyokusudiwa, au kusudio na maana ya kihistoria kuhusu andiko hilo. Matokeo ni mfululizo wa mambo na kanuni zinazosimamia upotofu wa maana ya kimaandiko" (Sarles 1986: 337).

b. *Zaidi ya hapo, maana ya andiko lolote "lazima kwanza ya yote liwe na kitu cha kumhusu mwandishi wake, kusudio la awali la mwandishi; ni lazima lihusiane na kile ambacho kingekuwa wazi kwa wale ambao maneno hayo yalikuwa yamekusudiwa kwao" (Fee 1984: 40).* Kwa upande mwingine, walimu wa mafanikio, kama matokeo, huanza na kueleza wanachokiita ujuzi wa karne ya 20-21, mara nyingi ujuzi wa Kimagharibi, desturi, na utajiri, na "kuubatiza" uzoefu wao huo kuwa kwa kuuingiza kwenye mistari ya Biblia, wakiacha kujali hoja za Ki-Biblia, ambazo hupotosha na kuharibu maana ya vifungu vya Biblia.

c. *Tabia ya kulenga kitu na ukosefu wa dhana wa walimu wa mafanikio na "tafsiri zake" hujazilizwa na mistari inayochaguliwa ambayo huisimamia mara kwa mara.* Kwa hiyo, injili ya mafanikio "pia siyo ya Ki-Biblia kwa upana wake katika neno hilo, kwamba linaonyesha picha duni ya kilicho katika maandiko kwa ujumla wake. Uchaguzi wa mistari ya Biblia unaofanywa na wahubiri hawa unawaruhusu waone yale ambayo *hayajafundishwa popote katika Agano Jipya,* na pia kwa uangalifu kabisa kukwepa mamia ya maandiko yanayosimama kinyume na

mafundisho yao." (Ibid.: 41).

2. Kutokuelewa Jinsi Maagano ya Ibrahimu, Musa, na Agano Jipya yanavyoendana pamoja kunaharibu "tafsiri" ya hao walimu. Katika Agano la Ibrahimu (ona **Mwa 12:1-3; 13:14-17; 15:1-21; 17:1-21;** na **22:15-18**) kuna mihimili mitatu ya ahadi "zilizoingiliana pamoja": (ahadi ya "mbegu"); umiliki wa ardhi wa taifa (ahadi ya "nchi"); na mafanikio ya duniani (ahadi ya "baraka"). Walimu wa mafanikio kimsingi hufundisha kwamba Wakristo wamerithi ahadi za Ibrahimu, ambazo wanazitafsiri kumaanisha kwamba, ni zote mbili; za kiroho *na mafanikio ya kimwili* kuwa ni zetu tunaposimamia imani. Uelewa huo ni wenye makosa na wa mauaji makubwa.

a. *Agano la Ibrahimu lilikuwa ni agano lisilo na masharti yoyote lililotolewa kwa Ibrahimu, na baraka zake hazikutegemea kusimamia imani.* Agano la Mungu na Ibrahimu halikutokana na Ibrahimu kutumia imani yake au utii. Kwa hiyo, katika **Mwanzo 15** Agano hilo lilikuwa la upande moja; kwa hakika, maana Ibrahimu alikuwa usingizini. Hakukuwa na masharti yoyote yaliyotajwa katika agano lile. Agano hilo lilipofanywa upya katika **Mwa 17:7, 13,** na **19** likaitwa "la milele." Zaidi ya hayo, Agano hilo lilithibitishwa licha ya kutokutii kwa Ibrahimu na kukosa imani kwake. Sarles anaongezea yafuatayo: "Ikiwa baraka zake binafsi za Ibrahimu katika agano lisilo na masharti zinatumika kwa wazao wake wote, basi ingekuja kwamba, kulingana na injili ya mafanikio, wazao wote wa Ibrahimu wangefanikiwa kifedha kama Ibrahimu. Lakini hii dhahiri sivyo ilivyo. Kwa hiyo, ikiwa baraka zake binafsi za Ibrahimu zinawahusu wazao wake wote—hoja ambayo wahubiri wa mafanikio wanaisisitiza—basi hilo agano ni lazima lieleweke kwamba ndiyo sharti, ili kuelezea kwa nini wazao wake wote hawakufanikiwa kimafanikio. Lakini jawabu hili la njia panda hii halitafanya kazi, kwa sababu ukweli usiopingika kwamba Abramu aliitwa na Mungu wakati akiwa mwambudu sanamu. Njia nyingine pekee ni kukataa kwamba baraka zake binafsi Ibrahimu, ni sehemu ya agano linalofanya kazi kwa wazao wake. Ni dhahiri ufumbuzi huu haupokelewi vizuri sana na walimu wa mafanikio na watu kwa sababu unaondosha matumizi ya Agano la Ibrahimu katika kudai haki zao za baraka za kifedha kama vile Ibrahimu. Hata hivyo, ndio ufafanuzi pekee unaotosheleza takwimu za Biblia." (Sarles 1986: 346-47)

b. *Agano la Ibrahimu ni "mchoro wa ramani" wa historia ya ukombozi ambao unashikilia ndani yake maagano yote mawili, Agano la Kale [la Musa] na Agano Jipya.* "Sehemu kubwa ya maandiko imejizatiti kueleza au kuandika jinsi Mungu alivyotekeleza ahadi zake kwa Ibrahimu. Watu huchanganyikiwa kuhusu ni jinsi gani Agano la Ibrahimu linatekelezwa, na jinsi linavyohusiana na maagano mengine. Agano la Ibrahimu lina maagano yote mawili, la Kale na jipya. Yaani, Agano la Kale na Agano Jipya ni utimilifu wa maswala ya kimwili na kiroho wa Agano la Ibrahimu. Agano ambalo Mungu alilifanya na Ibrahimu linafunua mpango wa Mungu wa kuwaokoa watu na kuwaleta katika nchi yake. Chini ya Agano la Kale, Mungu, kimwili anawaokoa watu wake wa Israeli (uzao wa kimwili wa Ibrahimu) kutoka kwa Wamisri na kuwaleta katika nchi ya ahadi, ya Palestina. Katika Agano Jipya, na Mungu, kiroho huwaokoa watu wake (uzao wa kiroho wa Ibrahimu) kutoka dhambi na hukumu na kuwaleta katika nchi ya kiroho (pumziko la wokovu sasa na mbinguni). Kwa hiyo, Agano la Ibrahimu "linayo" yote mawili; Agano la Kale na Jipya." (Lehrer 2006: 29)

c. *Umuhimu wa hili ni kwamba, walimu wa mafanikio kimakosa hulitumia Agano la Ibrahimu kimwili, ambalo lilitegemea utii wa Israeli kwa ile Sheria ya Kale ya Musa, kwa Wakristo wa leo ambao hawahusiki na sheria ya Musa, na ambao hawakupewa masharti yale, yahusuyo baraka za kimwili.*

(1) Agano la Kale [Musa] lilikuwa la "Ki-Matendo," siyo agano la "msingi wa neema" kama lilivyo Agano Jipya linalowatawala waamini leo. Agano ambalo ni "la ki-Matendo" ni agano halali linapokuwa na tabia ya "kama . . . ndipo" —yaani., "ikiwa" utatii maagizo yote ya agano, "ndipo" utabarikiwa, lakini ikiwa hutatii maagizo yote ya agano, basi ndipo utakapolaaniwa. Na zaidi, Agano la Kale lilikuwa kwa kiwango kikubwa kwa baraka na laana za kimwili, na ulimwengu wa vitu (ona **Kut 15:26; 19:3-6; Law 26:1-43; Kum 28:1-4, 15-19; Yos 23:14-16; Yer 11:1-11; Dan 9:11-14; Yak 2:10**). Sababu ni kwamba, Torati ilikuwa ni msingi wa taifa lile (Israeli), na siyo wa jamii ya kiroho (Kanisa).

(2) Ingawaje baraka za kimwili ziliahidiwa kwa Israeli ya Agano la Kale kama ingetii sheria ya Musa, wazo kwamba utajiri ulikuwa ni ishara ya kubarikiwa na Mungu lilikuwa na mipaka.

(A) *Sheria ya AK iliwadhibiti kikamilifu Waisraeli.* "Ufupisho wa kodi zote na zaka zote zilizotajwa wakati moja au mwingine kwa jinsi fulani zinayumba: kazi ya kitumwa chini ya mfalme, kodi kwa mfalme, changizo za dharura kwa ajili ya vita, kodi ya hekalu, yale mabaki ya mavuno shambani miaka ya Sabato na Jubilee, malimbuko na dhabihu nyingine zote za hiari, na zile 'zaka mara tatu' . . . Mtu ni vigumu kusema kwamba watu wa Mungu walikuwa huru kufurahia mafanikio ya mali isiyoingiliwa ya rasilimali zao." (Blomberg 1999: 47) Zaidi ya hapo, ahadi za baraka za kimwili zilikuwa baraka kwa taifa kiujumla, *siyo* ahadi binafsi kwa watu maalum kama thawabu kwa utii kibinafsi.

(B) *Ukweli kwamba mtu alikuwa tajiri haukuwa ni ishara ya uhakika kwamba alikuwa na mali hivyo kwa vile alikuwa na kibali mbele za Mungu.* Katika Agano la Kale, na hata Agano jipya, Mungu anajihusisha na mtazamo wetu juu ya fedha, siyo na kiasi cha fedha tulizo nazo. Utajiri lazima ugawiwe kwa ukarimu, hasa kwa wale ambao ni wahitaji. Mungu anajali jinsi tunavyozipata, tunafanya nini nazo, na tunazitumia wapi; kama usalama wetu badala ya kumtumaini yeye. Kwa mfano, "Katika Zakaria 11:5, wale wanunuao wafungwa wanadai, 'Na ahimidiwe BWANA, kwa maana mimi ni tajiri!' kama kwamba Mungu ndiye aliyewabarikia mali zao. Lakini kwa Zakaria, ilikuwa dhahiri kwamba Bwana hatawahurumia watu tena wenye mtazamo kama huo (11:6)." (Blomberg 1999: 75) Sehemu nyingine nyingi katika AK, zikiwamo **Ayu 21:1-21; Zab 73; Isa 3:14-15; 5:8-9; Amosi 4:1-3; 6:1-7**, huweka bayana kwamba kuwa na mali *si* lazima iwe ni ishara kwamba mtu ni mwaminifu au ana kibali kwa Mungu.

(C) *Mifano mingi ya Kibiblia ya umasikini na kutofanyiwa haki kwa watu waaminifu huonyesha kwamba, hata katika AK, hakuna uhusiano thabiti wa 1:1 kati ya mali na baraka za Mungu, au kati ya laana ya Mungu au adhabu.* Katika **1 Wafal 21** Nabothi anaonekana kuwa mtu mwaminifu, mwenye haki. Hata hivyo, alishitakiwa pasipo haki, akapigwa hadi kufa, na shamba lake la mizabibu likanyang'anywa na mfalme Ahabu. Ingawaje walimu wa mafanikio mara nyingi hunukuu baadhi ya Mithali (m.f., **Mith 3:9-10**) kama "mtindo sahihi wa maisha halisi, ambamo wema hulipwa mara moja na waovu huadhibiwa papo," kusema kweli "Mithali hutawala ulimwengu ambamo wasio na hatia hushambuliwa na waovu hufanikiwa kuipotosha sheria (Mith. 1:11; 6:17; 13:23; 17:23, 26; 18:5). Kwa hiyo, Mithali angalau kwa uchache hutazama kupitiliza mauti kwa ajili ya kuikosoa dhuluma (10:7; 12:7; 11:7; 12:28)." (Johnson 2007: 308, 308n.41) Zaidi ya hapo, "Mhubiri, Ayubu, na Zaburi fulani (37; 73) hukabili uhalisia wenye utata kwamba wenye haki hufanikiwa daima, wala si waasi wanaoteseka mara zote, kwa sasa. Hatimaye, mvutano huu unaweza tu kutatulika kwa namna ya Ki-Ungu: waama Bwana wa agano azuia ghadhabu yake ya haki kinyume na wale wanaodharau mamlaka yake na wanaonajisi uumbaji wake, wale wanaoshika agano lake watateseka, wanaovunja agano wataishi na kusitawi, na ulimwengu wa mpangilio uliofikirika katika Mithali utaonekana ni mawazo ya kutamanika. Hivyo Hekima ya Israeli inalilia kwa ajili ya kuja kwa mwisho kwa Bwana wa agano katika haki, kama ilivyoahidiwa katika Torati (Kumb. 32) na kutabiriwa na manabii." (Ibid.: 371)

(3) <u>Yesu alikuja kutimiliza Torati (**Math 5:17**).</u> Torati isingekamilika pasipo "mpaka yote yatimizwe" (**Math 5:18**). "Yote yalikwisha " pale msalabani (ona **Yoh 19:30; Rum 10:4; Waef 2:14-15; Wakol 2:13-15**). Kristo alianzisha Agano Jipya (**Luka 22:20; 2 Wakor 3:5-6**). Pamoja na hilo, kumekuwa na *"mabadiliko ya shera"* (**Waeb 7:12**) kwa *"sheria ya Kristo"* (**Wagal 6:2**). Kwa hiyo, "baraka na laana kwa taifa la Israeli walioishi chini ya sheria haziwezi kusogezwa kwa Watakatifu wa Agano Jipya. Vinginevyo neema si neema tena. Kuthibitisha kwamba baraka na laana za Kum 28 zinatenda kazi kwa Wakristo, huleta mawazo yaliyo kinyume na ukweli wa utofauti mkuu uliopo kati ya sheria na neema ya nyaraka za Agano Jipya, hasa nyaraka za

Paulo" (Sarles 1986: 347).
(4) Utofauti kati ya Agano la Kale na Jipya unaonekana katika **Wagal 3:14.** Walimu wa mafanikio mara zote hunukuu sehemu ya kwanza ya mstari ule, *"ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo"*; hata hivyo, mara kwa mara wanapuuza sehemu iliyobakia ya mstari huo, *"tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani"*. Hii inaonyesha baraka za kiroho zilizotolewa, siyo baraka za kifedha, zinapatikana kupitia Kristo Yesu. Wagalatia 3 inajadili manufaa ya milele ya, kiroho, siyo manufaa ya kimwili" (Sarles 1986: 347).

**G. *"Injili ya mafanikio" ina tafsiri mbaya za vifungu vya Biblia ambavyo inasimamia.***

1. **Yos 1:8.** Neno lililotafsiriwa kuwa "mafanikio" katika mstari huu ni aina ya tendo tzelah linalomaanisha "kufanikiwa" katika jambo fulani. Mafanikio ya mtu yanaweza kuwa katika maeneo mengi; kama vile kijeshi, kifedha, kiroho, kisiasa, nk. Hoja ya mstari huo inaathiri maana ya mstari. Hoja ya ahadi ya Mungu kwa Yoshua kwamba Yeye angemfanikisha katika njia yake na kumpa ushindi wa kijeshi, na siyo kifedha. Ililenga hasa utekaji wa Waisraeli wa nchi ya ahadi, utendaji wa ki-nje wa nchi ya ahadi uliotolewa bila masharti katika Agano la Ibrahimu. Kitabu cha Yoshua kinaonyesha ushindi wa Yoshua katika utekaji wa nchi ya Kanani. Yoshua alikuwa kiongozi wa jeshi, siyo mweka hazina wa Benki; hivyo mafanikio ya kifedha hayaonekani hapa. (Sarles 1986:338) Ikiwa mtu atachukua mistari hii kama inaonyesha kanuni inayopitiliza Yoshua na kutekwa kwa Kanani, basi mtu huyo awe mwangalifu kuangalia mambo mawili:

a. *Msisitizo katika mistari hii ni utii wa moyo wote.* Yoshua anaambiwa *"uangalie kutenda sawa sawa na sheria yote . . . usiache kwenda mkono wa kuume au wa kushoto . . . Kitabu hiki cha Torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda maneno yote yaliyoandikwa humo."* Aweza mtu yeyote awe wa kiume au wa kike akasema kweli anafanya hayo? "Mafanikio" pekee yaliyoahidiwa yana msingi wa utii kamilifu na wa kudumu kutoka moyoni. Hata hivyo, katika uhalisia sisi sote hutenda kutokana na misukumo mchanganyiko; huwa tunatii wakati fulani tu, tena kwa sehemu tu. Kwa hiyo, hakuna mtu anayeweza kudai kwa misingi halali kwamba Mungu "humlipa" yeye "mafanikio" yake kutokana na mistari hii.

b. *Mtazamo wa Mungu kuhusu "mafanikio" ni tofauti na mtazamo wa mwanadamu wa mafanikio.* Sisi huelekea kutazama mafanikio na ufanisi moja kwa moja kwa namna za kimwili na kimali. Hivyo sivyo Mungu anavyopima ufanisi au mafanikio. Mungu haangalii kwa nje, bali huangalia moyo (**1 Sam 16:7**). Yesu alikuwa na "ufanisi" kwa sababu siku zote Alifanya na kutenda tu mapenzi ya Baba Yake (**Math 26:29; Yoh 4:34; 5:17-20, 30; 6:38; 8:28-29; 10:18; 12:49-50; 14:10. 24, 31; 17:4**), ingawaje hilo lilimsababishia awe mtu masikini aliyekuja kuteswa, kushitakiwa isivyo haki, na kusulubiwa kama mhalifu wa kawaida. Mitume walianzisha kuishi "kiufanisi" na "kimafanikio" ingawaje walipoteza mali zote za kidunia na kufa vifo kama wahanga. Kwa vile Mungu huanngalia "ufanisi"na "mafanikio" halisi tofauti na wanadamu wafanyavyo, tunapaswa kuweka akili zetu kwenye mambo ya Mungu (ona **Math 16:23**).

2. **Mith 3:9-10.**

a. *Katika mistari hii, waalimu wa mafanikio hushindwa kuelewa tabia ya hiyo "mit" ilivyo.* Mitni usemi wa hekima—kauli ya kanuni kuhusu jinsi mambo yanavyokwenda, *siyo* ahadi, uthabiti, au "sheria" ya jinsi mambo yatakavyoenda katika kila hali. Kwa hiyo, **Mith 3:1-8** husema kwamba kushika maagizo ya Mungu kutaletesha maisha marefu, kibali kwa watu wengine, na afya njema. Ahadi hizo za ujumla si za kweli katika hali fulani maalum kuliko ahadi za ghala kujazwa katika **Mith 3:9-10**. Kutafsiri hii au kila Mitkama ahadi ya kusimamia, ambayo lazima itimie kila wakati; kunaigeuza kuwa ni mfumo wa imani, ambao vitabu vingine vya Agano la Kale, hasa **Ayubu** na **Mhubiri**, vinaukataa wazi. Kama Wolvaardt anavyoonyesha, "Mchango mkuu wa Ayubu kwa ujumbe mzima wa Biblia, ni kuonyesha kwamba duniani hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya dhambi na kuteseka, pia kwamba haki ya waamini usipimwe kwa kuangalia kama ana mafanikio kivitu, au anaelewa mazingira yake" (Wolvaardt 2005: 250). Kwa hili, au Mithali nyingine yeyote kuwa kweli, hata kiujumla wake tu, mtu ni lazima atawale kazi yake, maisha yake, pasipo matatizo yoyote mazito ya mfumo wa kijamii. Hakika, "sehemu ndogo zaidi ya theluthi ya Mithali zote hushughulika na utajiri na masikini hufundisha kwamba watu hupata kile wanachostahili, ambapo zilizobakia

hutambua uwepo na matatizo ya kukosa haki kwa uchumi wa kijamii" (Blomberg 1999: 65). Walimu wa mafanikio, badala yake, wanafanya mambo mawili ya kimakosa kwa mithali hii: (1) Hupuuza muktadha Mithali zilizobaki (pia na vitabu vingine vya Ki-Biblia ambavyo hutoa mtazamo unaowiana zaidi wa maisha; (2) Wanaigeuza hiyo kuwa "sheria"; na (3) Wana "*mfunga Mungu"* kwa hiyo "sheria" waliyoiunda (m.y, wanasema kwamba "ikiwa utafanya hili, basi *Mungu anawajibika* kulifanya"). Kwa hiyo, kama Johnson anavyoeleza, hugeuza hilo kuwa "mtindo rahisi wa maisha halisi, ambamo wema hutuzwa papo kwa papo na waovu kuadhibiwa papo kwa papo" (Johnson 2007: 308).

b. *Walimu wa mafanikio pia wanaelewa vibaya "ufuwa hatua kwa hatua" (m.y, Mungu amefunua mpango wake hatua kwa hatua kuanzia mwanzo wa Biblia hadi mwisho).* Mithii ni mfano wa tabia ya "kimwili" ya baraka za Agano la Kale kwa kumtii Mungu [ona mjadala wa hapo juu kuhusiana na agano la Ibrahimu, Musa, na Agano Jipya]. Kwa upande mwingine, Yesu alituahidi kwamba katika dunia hii *tutakuwa na dhiki* (kiuhalisi ni kwa ajili ya utii wetu kwa Mungu) (**Yoh 16:33**).

c. ***Mith 3:9** ina masharti ya kumheshimu Bwana kwa mali Yak."* Injili ya mafanikio kimakosa hudhania hayo kwamba yanamaanisha "kupanda mbegu" kwa kuwapatia wao! Hilo kimsingi ni kosa kabisa. Dhana ya Mithali, na Biblia yote nzima, inaonyesha kuwa "kumheshimu Bwana kwa mali zako" ni kutumia mali zako kuwasaidia masikini na wahitaji, na kuujenga ufalme (ona **Mith 3:27-28; 11:24-26; 21:13; 29:7; 31:20**).

d. *Mwishowe, kwa kufuatisha baraka za msingi wa agano lamaswala ya kilimo ya Agano la Kale, hoja maalum na lugha ya Mitni ya kilimo (m.y, inazungumzia kumheshimu Bwana na Bwana kuzijaza ghala zake na shinikizo la divai).* Hakuna kutajwa kokote dhahiri kwa fedha, au kutoa fedha kama "kupanda fedha kama mbegu ya imani" kwa huduma ya mtu fulani, au kupokea fedha badala yake. Kwa hiyo mtu ni lazima awe makini kuhusu kuifanya mistari hii miwili iseme mambo ambayo haikukusudiwa kiasili.

3. **<u>Mal 3:10.</u>** Matumizi ya lugha za *"madirisha ya mbinguni"* na *"kumimina baraka"* zilivyo katika mistri hii kwa walimu wa mafanikio ni matumizi mabaya kabisa ya ahadi a kimwili, ya mpangilio wa Agano la Kale.

a. *Baraka zote mbili zilizoahidiwa za **Mal 3:10** na laana za **Mal 3:9, 11** zinahusu nchi na mazao.* Zote zinategemea na kusimamia Agano la Musa na mahusiano maalum ya kiagano kati ya Mungu na Waisraeli wa kale. Katika **Kum 26:12-15** kuna uhusiano kati ya kutoa zaka (fungu la kumi) na kutoa mazao kwa nchi ya ahadi ya Israeli. Katika **Kum 26:16** Musa alikuwa amewaagiza Waisraeli kutii maagizo yote ya Mungu na sheria zake. Katika **Kum 28:12** Mungu aliahidi kwamba *"Atakufunulia BWANA hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi Yak kwa wakati wake na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako"* ikiwa Israeli wangekuwa waangalifu kutenda maagizo yote ya sheria ile. Ikiwa Israeli watashindwa kushika sheria yote ile, ndipo Mungu alikuwa amewaahidi kuizuia mvua, na kuyafanya mazao yasizae, na kuliwa na nzigs, madumadu na parare (**Kum 28:23-24, 38-42;** ona pia **Law 26:3-6; 14-16, 19-26**). **Mal 3:7-12** ni mfano maalum wa Mungu kutimiza ahadi yake kulaani nchi kwa sababu ya kutokutii kwa watu wake, lakini pia wa kuwakumbusha watu wake ahadi za baraka zake za kutii, na kuwapa changamoto watu waujaribu uaminifu wake kwa utii wao wenyewe. Katika **Mal 3:10** yale*"madirisha ya mbinguni"* (NASB) au *"malango ya mafuriko ya mbinguni"* (NIV) ni uasemi huo huo uliotumika katika **Mwa 7:11** na **8:2,** na huzungumzia uwingi wa mvua.

b. *Hoja iliyopo hapo ni kutoa zaka chini ya sheria ya Musa, siyo "kupanda mbegu ya imani" kwa huduma ya mtu fulani.* Jambo la kuvutia, na kinyume na mtazamo wa fedha wa walimu wa mafanikio kuhusu fedha, ni kwamba katika sheria ya Musa *hakukuwa na utoaji wa zaka au fungu la kumi la fedha.* Sehemu pekee inayozitaja fedha katika sheria ya Musa, kuhusiana na kutoa zaka, ni pale itokeapo mtu amekuwa mbali mno na "mahali ambapo Bwana Mungu alikuwa amepachagua" (m.y, hema ya kukutania) ya kuletea zaka (m.y, mazao ya nchi au wanyama), ndipo mtu huyo alitakiwa kubadilisha vitu hivyo viwe fedha, alete fedha hizo mahali ambapo Bwana alikuwa amepachagua, na kisha kutumia fedha hizo, na kula na kunywea akiwa mahali hapo (**Kum 14:24-26**).

4. **<u>Marko 10:28-30.</u>** Kifungu hiki ndicho asili ya mafundisho ya "kurudishiwa mara 100" kwa fedha Yak ikiwa utapanda kwa imani kwa kutoa kwa walimu wa mafanikio. Vyote hoja iliyopo na lugha iliyotumiwa katika fungu hilo ni kinyume kabisa na tafsiri ya mafanikio.

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

a. *Hoja iliyopo hapo haina lolote kuhusiana na watu "kupanda mbegu ya imani" kwa kutoa kwenye huduma ya mtu.* Kusema ukweli, fedha hazitajwi kabisa katika kifungu hicho. Badala yake, kinawahusu wale ambao tayari *"wameacha kila kitu na kumfuata* [Kristo]" (**10:28**).
b. *Yesu kamwe hakuagiza mtu yeyote achangie huduma yake, wala kwa kuahidi "kuwarudishia 100" au chochote cha jinsi hiyo.* Hoja iliyopo kabla tu ya kifungu hiki ni maelezo ya " kijana mfalme fulani aliye tajiri" ambaye Yesu alimwambia "aende "akauze yote aliyo nayo na *kuwapa masikini"* (**10:21**). Yesu hakumwahidi yule mtu kwamba kama angeuza mali zake na kuwapatia masikini angelipata fedha nyingi zaidi hapa duniani. Badala yake, yesu alisema kwamba, "utakuwa na hazina mbinguni" (**10:21**). Ni dhahiri kabisa, tofauti kabisa na kuahidi kwamba kutoa kutamwongezea mtu fedha na mali, Yesu anaonya, *"Jinsi itakavyo kuwa shida wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu! . . . Ni rahisi zaidi ngamia kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.* (**10:23, 25**). Kwa hiyo huko "kurudishiwa marab 100" kunakoahidiwa na walimu wa mafanikio kunapuuza hoja iliyopo, na kufundisha somo ambalo ni *kinyume kabisa* la kile kinachoendelea katika kifungu hiki.
c. *Zaidi ya hayo, hoja iliyopo ni lazima ihusu Yesu kuwatayarisha wanafunzi wake kwa ajili ya huduma yao ya kitume wakati wa dhiki au udhia.* Kwa hiyo, sehemu ya kile ambacho Yesu anakiahidi katika "kurudi kwake" ni kujitoa kwake na *"udhia"* (**10:30**). Kiini cha mateso hayo na udhia kinaendelezwa katika **10:32-45**. Pia, hii ni kinyume kabisa na jinsi walimu wa mafanikio wanavyopatumia.
d. *Tafsiri ya injili ya mafanikio ya kifungu hiki kimsingi ni: "ukitoa shilingi 10 kwa huduma, basi Mungu atakurudishia shilingi 1000 ."* Hata hivyo, pamoja na *"udhia huo,"* ambao Yesu ndio alioahidi, moja wapo ya ahadi nyingine aliyoiahidi katika "kurudi kwake" ni *"na katika ulimwengu ujao uzima wa milele"* (**10:30**). Kama walimu wa mafanikio wangekuwa wakweli katika tafsiri yao, kile mbacho ni tafsiri yao, ingekuwa hivi: "Kama ukitoa shilingi 10 kwenye huduma yangu, basi Mungu atakupa *"na katika ulimwengu ujao uzima wa milele"* Kusema kweli, kanuni nyuma ya "kurudishiwa mara 100" ni sawa kabisa na Waromani Katoliki walivyodai kuuza uzima wa milele kwa kuuza au kuendekeza vibali vya kuwaachia watu kutoka majengo ya utauwa wakati wa Miaka ya Kati (Adeleye 1999:83).
e. *Walimu wa mafanikio hulenga fedha (ambazo hazikutajwa) na kuacha "kurudishiwa mara 100" kwa nyumba, ndugu wa kiume, ndugu wa kike, mama, baba, watoto, na mashamba (ambayo Yesu, kusema kweli, anaahidi).* Je Yesu anazungumzia nini hasa? Jawabu ni kwamba anawazungumzia waamini kuhusu *familia mpya na Kristo*. Tunapookoka, Mungu anatuingiza katika familia yake (ona **Rum 8:15-17; Waef 1:5**). Kanisa hasa huitwa *"nyumba* [au, familia] *ya Mungu"* (**1 Tim 3:15;** ona pia **1 Tim 5:1-2**). Kama Sarles anavyoliweka, "Wakati wanafunzi walipopoteza nyumba zao kwa ajili ya injili, walipewa nafasi katika nyumba za ndugu waamini wenzao ambao walishiriki pamoja nao wakati wanahama kutoka mahali pamoja kwenda mahali pengine wakihubiri injili. Vivyo waamini walipoziacha familia zao kwa ajili ya Kristo, waliingia katika mahusiano mapya katika familia ya Mungu, ambayo yalikuwa mara mia zaidi." (Sarles 1986: 338)

5. **<u>Yoh 10:10.</u>** Huo *"uzima tele*" ulioahidiwa na Yesu katika mistari hii, hauna lolote kuhusiana na kuwa na fedha nyingi, au wingi wa vitu. "'Uzima' au 'uzima wa milele' katika injili ya Yoh unalinganishwa na 'ufalme wa Mungu' katika injili nyingine. Kimsingi hasa unamaanisha 'uzima katika zama zijazo'. Ni uhai ambao Mungu anao, na ni wake mwenyewe; na ni zawadi yake kwa waamini katika kizazi kilichopo. Neno la Kiyunani *perrison*, lililotafsiriwa 'uzima tele' katika K.J.V., linamaanisha kimsingi kwamba waamini wanapaswa kukifurahia kipawa hiki cha uzima 'kwa kikamilifu (N.I.V.). Uwingi wa vitu hauhusiki wala katika neno 'uzima' au 'uzima tele'. Zaidi ya yote, Wazo lenyewe ni geni kabisa na andiko la Yoh 10 na pia kwa mafundisho yote ya Yesu." (Fee 1984: 40-41)

6. **<u>2 Wakor 8:9.</u>** Kwa walimu wa mafanikio kudai kwamba Kristo alifanyika masikini [yaani, aliacha mbingu, akafanyika mwanadamu, na kufa msalabani] *"ni ili kwamba kwa umasikini wake, ninyi mfanyike tajiri* [yaani, ili kwamba tuwe na fedha nyingi sana]" ni kama kinyume kabisa. Mstari huu haumaanishi kwamba Yesu alikuwa na fedha nyingi sana na akafanyika masikini ili sisi tupate fedha nyingi mno. Unamaanisha kuwa alikuwa na kila kitu mbinguni, na akaacha huko yote, akafanyika mtu, akatwaa dhambi zetu na kufa, ili kwamba tuwe na uzima mpyya wa milele, na kurithi mambo yote katika yeye (ona pia **Wafil 2: 6-11**). Mada nzima na hoja iliyoko katika kifungu hiki ni kuwa Paulo anawafundisha Wakorintho kwamba, kwa vile Kristo alikamislisha mengi kwa ajili yao kupitia kujitoa kwake, ni kiasi gani zaidi wanapaswa kutoa katika uwingi wa mali zao kuwasaidia wengine wenye

mahitaji. Hivyo, muktadha wa habari hii unaonyesha kwamba Kristo alitoa kila kitu alichokuwa nacho kwa ajili yetu ili kwamba sisi "*tupate kuwa matajiri kwa ukarim*," na sio kwa kuonyesha utajiri wetu kwa ubinafsi. Au, kama Blomberg anavyoliweka, "Ikiwa Kristo aliweza kujitoa dhabihu kiasi hicho kwa ajili yetu, tunawezaje kuthubutu kuacha kutoa kwa ukarimu kwa wahitaji!" (Blomberg 1999:193) Hivi ndivyo hasa Paulo alivyosema **1 Tim 6:17-18** alipomwabia Timoteo *"walio matajiri wa sasa uwaagize . . . wawe matajiri kwa matendo mema, wawe wakarimu na tayari kutoa mali zao kuwashirikisha we."*

Hebu fikiria hicho ambacho ni 'theolojia ya waalimu wa Mafanikio inavyoufanyia mstari huo: Je sababu iliyomfanya Kristo afe ili tuwe na fedha nyingi mno? Je ilikuwa ni lazima Kristo afe kwa ajili yetu ili tuwe na fedha nyingi? Bila shaka, ni hapana! Watu wengi wasio wacha Mungu wana fedha nyingi tu. Hawahitaji imani katika Kristo ili kuipata, na kwa wao kuwa nayo, *siyo ishara kwamba wana kibali maalum cha Mungu kwao*. Ni kurahisisha Injili sana kudai kwamba Kristo alikufa ili ili tupate fedha kwa ajili ya miaka micchache ya hapa duniani. Zaidi yake, mada inenwayo katika kifungu hiki inaonyesha walimu wa Mafanikio hutumia mstari huu kimakosa.

a. *Kifungu hiki kilikuwa kinaelekezwa kwa kanisa la Korintho wakati huo.* "Ninyi" na "yenu" katika **8:9** ni maneno yaliyo katika uwingi, siyo maneno ya umoja. Vivyo hivyo ni kweli kwa neno "ninyi" katika **8:7**. Kwa hiyo, Paulo kimsingi anaagiza huduma ya ushirika kwa kanisa la mahali pamoja.

b. *Wakorintho hawakuhitaji "kupanda mbegu" ili wapate mafanikio ya vitu, kwa sababu tayari walikuwa na mali nyingi sana (8:14).* Kusema kweli, katika **1 Wakor 4:6-16** Paulo *alikemea* mtazamo wa Wakorintho kwamba walikuwa "matajiri". Aliwaambia kwamba yeye mwenyewe alikuwa "na njaa na kiu, aliyevaa nguo duni, na hakuwa na makao," lakini aliwaagiza Wakorintho kumfuatisha yeye!

c. *Mwanzoni mwa kifungu, Paulo aliwasifu Wamakedonia kwa ajili ya utajiri wao—lakini aliweka bayana kwamba "utajiri katika utoaji wa ukarimu" na kutoa licha ya "umasikini mwingi" (8:1-5).* Hakusem kwamba, kwa kutoa, Wamakedonia sasa ni matajiri wa mali, au wangekuwa hivyo. Badala yake, Wamakedonia walifurika katika *baraka za rohoni* ambazo Bwana alizimimina juu yao kwa sababu ya uaminifu wao: ile *"neema ya Mungu"* na *"furaha tele"* (**8:1-2**). Paulo anashauri kwamba wakorintho waufuate mfano wa Wamakedonia wa *kutoa kwa ukarimu kwa masikini* (**8:7**), na kisha kuvuna baraka hizo hizo za kiroho.

d. *Paulo anahimiza Wakoorintho kufuata katika ahadi zao kutoa ili kuwasaidia masikini na waamini wenye uhitaji wa Yerusalemu—siyo kumpa fedha Mhubiri au huduma ambayo tayari ni tajiri (**1 Wakor 16:1-4; 2 Wakor 8:6-15**).* Paulo hasa alisema kwamba utoaji haukuwa *"kwa ajili ya kuwadhikisha wengine"*. (**8:13**). Utoaji kwa hiyo usingeweza kuwa kwa ajili ya "kujinufaisha mwenyewe"! Mbali kabisa na ahadi ya jinsi hiyo, kwa kutoa, Wakorintho wangepokea fedha nyingi zaidi, Paulo alisisitiza kwamba kuwapa wahitaji kunasaidia kuleta usawa kati ya waamini, na hivyo kuwawezesha waamini wengine kuwasaidia Wakorintho *walipokuwa na uhitaji* (**8:14**). Kauli hizo siyo tu zinapangua *msukumo au sababu ya* injili ya mafanikio kwa utoaji, bali pia unapangua *ahadi* ya injili ya mafanikio kwani ukitoa hutakuwa na mahitaji ya vitu kwa ajili Yak.

7. **2 Wakor 9:6.** Kifungu hiki hakika kinafananisha utoaji na *"kupanda mbegu"* na **9:10** unaendeleza mlinganisho kwa kulinganisha rasilimali za vitu na "*mbegu za kupanda."* Zaidi ya hayo, kifungu kinasema kwamba Mungu atatupa thawabu kwa njia hiyo hiyo kama tunavyowapa wengine. Hata hivyo, yote mawili; mpangilio wa maneno, na hoja iliyopo huonyesha umuhimu tofauti kabisa na ule ambao walimu wa mafanikio wanamaanisha wakati wanapozungumzia "kupanda mbegu ya imani" kwemye huduma na "sheria ya kurudishiwa."

a. *Uoaji unaozungumziwa katika kifungu hiki ni wa kuwasaidia masikini na wahitaji, siyo kuwasaidia walimu matajiri wa mafanikio (**1 Wakor 16:1-4; 2 Wakor 8:4, 14; 9:9, 12**).* Kila mahali katika Biblia, Mungu amerudia mara kwa mara kujihusisha kwake na wale ambao ni masikini na wahitaji wa kweli (ona **Kut 23:10-11; Law 19: 9-10; Kum 15:10-11; 24: 19-21; Zab 41:1; 112:5-6; Mith 14:21; 19:17; 22: 9, 22; 31:20; Isa 58:6-7; Eze 16:49; Math 25:31-46; Marko 10:21; Luka 3:10-11; Rum 12:20; Wagal 2:10; Waef 4:28; Yak 1:27**). Hicho ndicho kilichokuwa kinaendelea hapo.

b. *Sababu au msukumo wa kutoa katika kifungu hiki ni tofauti sana na ni kinyume na wa injili ya mafanikio.* Msukumo wa utoaji wa injili ya mafanikio umelaaniwa katika mstari wa **9:5** unaosema kwamba tunatakiwa kutoa kwa ukarimu, lakini *"bila kuonyesha ubinafsi."* Kwa vile makusudi ya utoaji ni ya kinyume kabisa na Maandiko, na unakatazwa kabisa katika fungu hili

hapa, tafsiri ya kifungu hiki haiwezi kuwa sahihi.

c. *Injili ya mafanikio hupotosha kanuni ya "kupanda na kuvuna."*

(1) Kanuni ya "kupanda na kuvuna" (m.y, "sheria ya kurudishiwa") ni kweli kama mwongozo wa ujumla, au kanuni—kile kipandwacho ndicho kitakachovunwa. Hata hivyo, siyo lazima kwa Mungu atoe thawabu ya fedha—au ya vitu (mali) kwa - wote watoao. **Yer 17:9-10** inaelezea vyema kanuni ya "kupanda na kuvuna". Moyo ni mdanganyifu, lakini Mungu huuchunguza moyo na "kumlipa kila mtu sawa sawa na njia zake" Kwa maneno mengine Mungu atatulipa sawa sawa na tunavyostahili. Tunaweza kutoa pesa nyingi lakini kama tunatoa kwa nia mbaya (kwa mfano kama "tunapanda mbegu" kwa sababu ya uroho na tunafikiri kuwa kwa kule kutoa tutapata pesa nyingi zaidi) Mungu anajua hilo na hataachilia baraka zake.

(2) Ukweli kwamba watu wote wametenda dhambi kwa upande moja, na kwamba Mungu ni mwenye rehema kwa upande mwingine, ikimaanisha kwamba kanuni ya "kupanda na kuvuna" siyo siku zote hufuatwa moja kwa moja, mara moja, au hufuatia ki-vitu. "Hekima ya kidunia huona hekima kama *michezo tu au* kitu kimoja kubadilisha na kingine. Kwa kila ovu, kuna sababu fulani ya moja kwa moja, na sababu inayohusika rasmi . . . na kwa kila jema, hasa kila baraka za mali, pia kuna sababu ya moja kwa moja iliyo rasmi . . . lakini hekima ya kidunia *siyo ya Kibiblia. Hata kama kuna nyakati ambapo Mungu huwalinda wa kwake, ni wazi kutokana na Maandiko yote, kwamba yote mawili – mvua na vimbunga vya kudhuru mazao na kuyafanya matunda kuanguka kabla ya kukomaa huwakuta wenye haki na wasio na haki hivyo hivyo.* . . . Hekima ya kidunia kiufupi huwezi kuitegemea. Anguko limeharibu utaratibu wa uumbaji kiasi kwamba watu wote wamedhurika kwa maafa yake; na Mungu mwenyewe amejifunua kama Mungu mwingi wa rehema — hata kwa mdhambi. Wakati mwingine hakuna hata sababu ya msingi kwa nini wenye dhambi wawe "wanabarikiwa" wakati "wenye haki" siyo, na kinyume chake! . . . Hekima ya kidunia, kwa hiyo, haiwezi kuwa sehemu ya mafanikio na umasikini wa Ki-Biblia." (Fee 1984: 41)

d. *Hoja iliyomo katika kifungu hicho inaonyesha kwamba thawabu kimsingi hutolewa kwa kanisa, siyo kwa watu binafsi.* Katika **9:8, 10,** na **11** ile *"ninyi"* na *"yenu"* ni uwingi, na siyo umoja. Hali ya kuhama kutoka umoja katika **9:6-7** kuwa katika uwingi **9:8, 10-11** kunaelea kukana moja kwa moja kati ya ni kiasi gani kila mtu anapanda, na kiasi gani kila mtu atavuna. Kinashauri, ingawaje kila mtu inabidi aamue ni kiasi gani cha "kupanda", huyo mtu binafsi anafanya hivyo kama mwakilishi wa kanisa la mahali. Ndipo Bwana atalipa thawabu kama mwili wakati washiriki wake wanatoa kwa ukarimu.

e. *Hoja ya kifungu inaendelea kuonyesha kwamba Mungu ni kweli, atawahudumia watoaji wa ukarimu, ambao wanatoa kwa sababu sahihi, na thawabu zake ni za kiroho.* Katika kifungu hiki, hata zile mali zitolewazo zimewekwa kwa uangalifu katika maelezo ya hoja ya kiroho: (1) Katika **9:8** hiyo "thawabu" ni kwamba *"Mungu aweza kuwapa neema ya kila namna kwenu,"* na sababu ya kuwa na mali ni ili mwamini *"mpate kuzidi sana katika kila tendo jema;* (2) Katika **9:10** "mavuno" yaliyoahidiwa ni *"mazao ya haki yenu"* ambayo hutokea pale "mwenye kupanda" anapotoa kile anachokipata kuwasaidia masikini na wahitaji. Kwa hiyo, **9:10** husema kwamba *sababu* ya Mungu hutoa na kuzidisha "mbegu" ya mtu ni *"kupanda na kuzidisha, na atayaongeza mazao ya haki yenu."* (3) Katika **9:11** kusudi la "kutajirishwa" ni *"mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu."*

f. *Maana iliyo kuu zaidi katika Agano Jipya vivyo hivyo inaonyesha kwamba "baraka" au "thawabu" za kanuni ya kupanda na kuvuna ni za kiroho, na kama ni za ki-vitu, basi zitatolewa wakati wa kuwa katika nchi mpya, na siyo katika uzima huu.* Katika **Luka 6:38**, Yesu alisema, *"wapeni watu vitu nanyi mtapewa"* Hata hivyo, siyo dhihirisho ya ufanisi wa vitu kama " kupanda mbegu" kwa kutoa pesa (hela) kwa huduma fulani, ijapokuwa huu mstari ni sehemu ya mjadala mrefu jinsi waumini wanapaswa kuishi. Hakika katika huo mjadala Yesu anasema kwamba tutoe na *"tusiitishe kurejeshewa"* **(Luka 6:30)** kwa hivyo yatupasa kutoa pasipo kutarajia kupata chochote kutokana na kutoa kwetu (**Luka 6:35**). Ikiwa tutafanya hivyo, basi *"na thawabu yenu itakuwa nyingi; nanyi mtakuwa wa Aliye juu"* (**Luka 6:35**). Katika **Wagal 6:7-9** Paulo kwa mara nyingine anaelezea kanuni ya "kupanda na kuvuna" lakini anaweka wazi kwamba *"[7] kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. [8] Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa*

*Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele."* na kwamba huko "kuvuna" hakutafanyika mara moja, au ki-vitu, lakini kutatendeka *"kwa majira yake . . . kama hatutachoka."* Katika **1 Tim 6:18-19** Paulo vivyo hivyo anaelezea kwamba wale ambao ni "matajiri" na *"watende mema wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo."* Tena kwa mara nyingine, hizo "thawabu" watakazo"vuna", kimsingi ni za kiroho, na za milele, kwa vile kwa kuwa wakarimu na fedha zao, wanakuwa *"huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli"* (ona pia **Marko 10:21; Waeb 10:34**).

8. **<u>3 Yoh 2.</u>** Katika mstari huu, Paulo alimtakia rafiki yake Gayo *"afanikiwe na kuwa katika afya njema."* Walimu wa mafanikio hawaelewi wala hoja iliyopo, wala lugha ya Kiyunani iliyotafsiriwa "ufanikiwe", na kwa hiyo wanalitafsiri na kuutumia vibaya mstari huu.

a. *Neno lililotafsiriwa "ufanikiwe" ni neno la Kiyunani euodoō. Linamaanisha "mambo na yakuendee vizuri" au kwamba mambo na "yaende vema" kwa mtu (Danker 2000: 410).* Neno hilo hilo linatumiwa katika **Rum 1:10** ambapo Paulo anazungumzia kutembelea Rumi. Hilo halimaanishi kwamba anatamani kutengeneza fedha nyingi aendapo Rumi, bali afanikiwe kufika kule. Tafsiri ya Agano Jipya ya **3 Yoh 2** hunasa vizuri uelewa wa maana ya Yoh, *"Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya Yak, kama vile roho Yak ifanikiwavyo."*

b. *Hoja ya mstari huu ni salamu tu kwa Gayo, na siyo maelekezo, ahadi, uhakika, kanuni, au sheria kwa waamini wote.* Kule kumtakia mema mtu apokeaye waraka "kulikuwa ni kawaida tu ya barua au waraka wa binafsi wa mlengwa. Kuanza kupanua matakwa ya Yoh ya Gayo kuzungumzia mafanikio ya fedha na vitu kwa Wakristo wa nyakati zote ni *jambo la kigeni mno* kwa mstari huo. Yoh kamwe hakukusudia, wala Gayo mwenyewe hakuelewa hivyo." (Fee 1984: 40)

c. *Sehemu iliyobakia ya **3 Yoh** inapingana na wazo kwamba **3 Yoh 2** inaunga mkono injili ya mafanikio.* Hakuna mahali popote katika sehemu iliyobaki ya kitabu hicho ambapo Yoh hata alidokeza kwamba injili ya mafanikio inaendana na salamu zake kwa Gayo. Yoh anasisitiza kuona *tabia* ya Gayo na bila shaka hali yake ya kiroho, siyo ya ki-vitu. Katika mistari ya **3-4** anasisitiza *"kuenenda katika kweli."* Katika mstari wa **5** anamsisitiza Gayo' *"kutenda kwa uaminifu."* Katika mistari ya **6-8** Yoh anamsisitizia Gayo *"upendo,"* na anaelekeza kwamba ndugu Wakristo wapendwa wasaidiwe (yaani, anasisitiza kwamba tuwe tunawapa wengine, siyo kutafuta kujinufaisha wenyewe). Kusema ukweli, katika mstari wa **9** Yoh anamshutumu Diotrefe *"apendaye kuwa wa kwanza kati yao."* Tabia ya Diotrofe inafanana na walimu wa mafanikio wanaoweka matakwa ya mafanikio yao binafsi mbele. Kwa hiyo, kwa kupuuza hoja iliyopo, na mtiririko wa maandishi, walimu wa mafanikio hulipa andiko maana ambayo ni mbali kabisa na ile ambayo imekusudiwa.

**H. *Hoja za nyongeza kuhusiana na injili ya mafanikio***

1. <u>Ingawaje Yesu aliweza kuwa na maneno makali kwa watu, kama Mafarisayo, waliokuwa wakimwakilisha Mungu kwa watu katika hali ya kimakosa (ona **Math 23:13-36**), ni kitu kimoja tu kilichomfanya achukue hatua kali kiMdoo: *watu waliokuwa wanafanya maswala ya biashara ya fedha katika hekalu* (**Math 21:12-16; Marko 11:15-18; Luka 19:45-47; Yoh 2:13-16**).</u> Kiuhakika kabisa, injili zote nne zimeandika kuhusu tukio hilo, ambalo linaonyesha umuhimu wake. Katika kila moja, Yesu anasema nyumba ya Mungu isigeuzwe kuwa*"ya wanyang'anyi, pango"* au *"mahali pa biashara."* Walimu wa mafanikio wanafanana na "wabadilio fedha" katika hekalu, na wsivumiliwe na watu wa Mungu leo, kama ambavyo Yesu hakuwavumilia miaka 2000 iliyopita.

2. <u>Ingawaje injili ya mafanikio inawavutia watu ambao ni masikini na kuishi katika mazingira magumu, inatoa matumaini yasiyo sahihi, kusema ukweli, *inawakandamiza masikini.*</u> Kwa vile injili ya mafanikio ni theolojia isiyo sahihi na inasimamia sababu ambazo ni za makosa, Mungu hawezi, na wala hataibariki. Watu masikini wanapotoa kwa walimu wa mafanikio wakitegemea kwamba yamkini watakuja kuwa tajiri, hawatakuwa tajiri kamwe, bali watakuwa masikini zaidi. Mafundisho ya injili ya mafanikio kwamba mtu aliye masikini anapokuwa mgonjwa, au anaendelea kuwa masikini ni kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe, au kukosa imani; "kunaweka mzigo mzito kwa masikini kwani si haki na si Ki-Biblia" (Editorial 2001: 2). Matokeo yake, injili ya mafanikio inawakandamiza masikini *kwa yote mawili, kimwili na kiroho.* Walimu wa mafanikio kiukweli, ni*"wanyang'anyi"* kama Yesu alivyosema.

3. <u>Walimu wa mafanikio ni wanafiki ambao hawakiamini hata kile wanachokifundisha wenyewe.</u> Ikiwa

kweli walimu wa mafanikio wanaamini kwamba ukimpatia mtu masikini, basi Mungu atakurudishia mara 100 zaidi ya ulichotoa, basi wao (ambao tayari ni matajiri) wangekuwa *wanatoa fedha zao kwa hao masikini, kuliko kupokea kutoka kwao,* kwa sababu wangekuwa wanapokea mamilioni mengi zaidi kutoka kwa Mungu. Sababu ya wao kutokutoa, bali kupokea au kuchukua, kunaonyesha ukweli kwamba hawaamini kile wanachokifundisha.

4. Walimu wa mafanikio mara kwa mara, na kwa ukali kabisa hushutumiwa kila mahali katika maandiko, na hukabili hukumu ya kutisha. Katika AK, Mungu kiukali anawakemea wale wanaotabiri kwa ajili ya kujipatia fedha, na wale ambao wanapendelea kujijengea majumba makubwa na kujilisha wenyewe badala ya kuwajali walio masikini. Wanakemewa kama manabii wa uongo wanaowapotosha watu wa Mungu nao watakabiliwa na hukumu Yake. Ona **Yer 6:13; 8:10; 22:13-17; Ezek 34:7-10; Hos 7:14; Mika 3:5-7, 9-12.** Yesu aliwakemea Mafarisayo kwa kuapa kwa dhahabu ya hekalu (**Math 23:16-20**). Aliwashutumu haswa kwa kuwa *"wanyang'anyi na wenye kujipenda wenyewe"* (**Math 23:25**). Aliwaita*"nyoka"* na *"wana wa majoka"* (**Math 23:33**) na akasema kwamba, kama matokeo, ya dhambi zao hawataweza *"kukwepa hukumu ya jehanamu"* (**Math 23:33**). Petro anasema kwamba mtu anapaswa kulichunga kundi la Mungu *"si kwa kutaka fedha ya aibu"* (**1 Pet 5:2**). Katika **2 Pet 2:3** anasema kwamba, Waalimu wa uongo "katika tama yao" hao "watajipatia faida kwenu" kwa maneno yaliyotungwa; ambao "hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii"(ona pia **2 Pet 2:14**). Paulo anaeleza kwamba mtu yeyoye ambaye *"anapenda fedha"* au *"hutaka kujinufaisha"* hana sifa kuwa kiongozi katika kanisa (**1 Tim 3:3, 8; Tito 1:7**). Yeye anawashambulia wale ambao *"walighoshio Neno la Mungu"* (**2 Wakor 2:17**), na wale wajao kunena *"maneno ya juu juu ya kuficha choyo"* (**1 Wathes 2:5**) ), na hufundisha *"kwa makusudi ya kujinufaisha"* (**Tito 1:11**). Kusema kweli, Paulo aliwakemea kwa ukali wale wanaofundisha na kusema kwamba*"utauwa ni njia ya kupata utajiri"* an kuwaita watu hao *"na majadikiano ya watu walioharibika akili zao, walioikosa kweli, huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia hakupata faida."* (**1 Tim 6:5**). Neno la Kiyunani lililotafsiriwa "haribika" ni *diaphtheiro*. Ni neno la nguvu au kali sana likimaanisha "kuharibika akili, kupotoka, kuwa bovu" (Danker 2001: 239), "lenye uharibifu kila mahali," "limekuwa nje ya maadili, limepotoshwa" (Zodhiates 1993: 445-46). Watu kama hao wanakabiliwa na hukumu mbaya zaidi ya wale ambao Paulo anawajadili katika **Rum 1:18-32**. Katika kifungu kile, watu walitambua kuwa Mungu yupo, lakini waliamua kumpuuza na kuabudu vitu vilivyotengenezwa au vilivyoumbwa. Matokeo yake, Mungu *"akawaacha"* waendelee katika uovu wao (**Rum 1:24, 26, 28**), na wakawa *"wanastahili kifo"* (**Rum 1:32**). Ikiwa hukumu ya Mungu ilikuwa kali kiasi kile kwa wale ambao walijua kwamba Mungu yupo ila walimpuuza, ni jinsi gani itakavyokuwa mbaya zaidi kwa wale ambao hawampuuzi Mungu tu, bali wanajaribu *kumtumia* Yeye na Neno lake katika kutosheleza tamaa zao za fedha?

5. Injili ya mafanikio ni ya udanganyifu na yenye kuua; wachungaji wale ambao wamefundishwa nayo wanapaswa kutubu na kuwaongoza watu wao na makanisa yao katika nuru ya injili. Kifupisho A hapo chini ni toleo la John Piper kuhusu "Mahubiri ya mafanikio: Ya Udanganyifu na Yenye Kuua." Ni wito au ombi muhimu kwa wachungaji kuyarudisha makanisa yao kutoka kwenye kosa la injili ya mafanikio na kurejea kwenye kweli. Mungu na akubariki ufanyapo hivyo.

## HITIMISHO

http://www.desiringgod.org/ResourceLibrary/TasteAndSee/ByDate/2007/1993_Prosperity_Preaching_Deceitful_and_Deadly/

**Mahubiri ya Mafanikio: Ya Udanganyifu na Yenye Kuua, na John Piper, February 14, 2007**

Wakati ninaposoma kuhusu mahubiri ya mafanikio katika makanisa, mwitikio wangu huwa: "Kama nisingekuwa ndani ya Ukristo, nisingetaka kujiunga nao." Kwa maneno mengine, Ikiwa huu ndio ujumbe wa Kristo, hapana, sitaki kabisa.

Kuwavuta watu waje kwa Kristo ili wawe matajiri, ni yote mawili–udanganyifu na uuaji. Ni *udanganyifu* kwa sababu wakati Yesu mwenyewe alipotuita, mambo kama: "Basi, kadhalika kila moja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu." (Luka 14:33). Na ni ya *uuaji* kwa sababu tamaa ya watu kuwa tajiri "huwaingiza katika uharibifu na upotofu" (1 Timotheo 6:9). Kwa hiyo, wito wangu kwa wahubiri wa injili ni huu.

**1. Usianzishe falsafa ya huduma inayowafanya watu waone kwamba ni vigumu mno kufika mbinguni.**

Yesu alisema, "Yesu akatazama kotekote, akawaambia wanafunzi wake, Jinsi itakavyokuwa shida wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu! Wanafunzi wakashangaa kwa maneno yake. Yesu akajibu tena, akawaambia, Watoto, jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu! Ni rahisi ngamia kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Nao wakashangaa mno, wakimwambia, Ni nani, basi, awezaye kuokoka? Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu." (Marko 10:23-27).

Swali langu kwa wahubiri wa mafanikio ni kwamba: Kwa nini utake kuanzisha huduma ambayo inalenga kuwafanya watu waone vigumu kabisa kuingia mbinguni?

**2. Usianzishe falsafa ya huduma inayochochea kujiua ndani mwa watu.**
Paulo alisema, " Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi" (1Timotheo 6:6-10)

Hivyo swali langu kwa wahubiri wa mafanikio ni kwamba: Kwa nini kuanzisha huduma inayowachochea waanguke katika majaribu na tanzi na mengineyo yenye kudhuru na kuwafanya wajichome katika maumivu mengi?

**3. Usianzishe falsafa ya huduma ambayo inawaongezea kunasika na hasara za kupata kutu na nondo.**
Yesu alionya kuhusu kujilundikia mali na hazina za kidunia. Maana yake, anatuambia tuwe watoaji, siyo wakuhifadhi. " Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba;" (Mathayo 6:19).

Ndiyo, sote huwa tunaweka kitu fulani. Lakini kwa kujijengea hali ya kutamani na kujiwekea zaidi kwa ajili yetu wenyewe, kwa nini tuondoe lengo la kumtazama Yesu na kuligeuza kichwa chini?

**4. Usianzishe falsafa ya huduma ambayo inafanya iwe kazi ngumu kufanikiwa vitu au mali.**
Paulo alisema tusiibe. Kinyume chake, ni kwa sisi kufanya kazi kwa mikono yetu. Lakini kusudi kuu halikuwa kukosa au *kuwa nacho*. Lengo lilikuwa "kuwa na *kitu cha kutoa*." " ... bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. " (Waefeso 4:28) Huku siko kuhalalisha *kuwa tajiri* ili kutoa zaidi. Ni wito wa kuzalisha zaidi, na kubakiza kidogo ili utoe zaidi. Hakuna sababu kwa nini mtu anayezalisha $200,000 asiishi tofauti na mtu anayejipatia $80,000 tu. Amua aina ya maisha ya kadiri; uyadhibiti matumizi Yak; kisha toa kilichobakia.

Kwa nini uwatie moyo watu ukiwachochea watake kwamba wawe na mali ili wawe watoaji wakarimu? Kwa nini usiwatie moyo waishi maisha rahisi zaidi, na kuwa watoaji wakarimu zaidi? Je hilo lisingeongeza ukarimu wao na kuwa ushuhuda mkubwa zaidi kwamba Kristo, na siyo mali, ndiyo hazina yao?

**5. Usianzishe falsafa ya huduma inayosababisha imani ndogo zaidi kwa ahadi za Mungu kuwa zetu, ambapo fedha haziwezi kuwa hivyo.**
Sababu ya Waebrania kutuandikia sisi kuridhika na kile tulicho nacho ni kwamba kinyume chake hutumia imani kidogo zaidi kwa ahadi za Mungu. anasema, "Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. 6 Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; Mwanadamu atanitenda nini?'" (Waebrania 13:5-6).

Ikiwa Biblia inatuambia kuridhika na kile tulicho nacho kunatoa heshima kwa ahadi za Mungu asiyetusahau kamwe. Kwa nini tutake kuwafundisha watu kupenda kuwa matajiri?

**6. Usianzishe falsafa ya huduma inayochangia watu wako kusongwa hadi kufa.**
Yesu anaonya kwamba, Neno la Mungu, ambalo limekusudiwa kutupatia uzima, linaweza likasongwa na mali kabisa na kuwa halizai tena. Alisema ni kama mbegu iliyooteshwa na kumea kati ya miiba ambayo iliisonga hadi ikafa: "Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali.... za maisha haya, wasiivishe lolote" (Luka 8:14)

Kwa nini tuwatie moyo watu kutafuta kitu kile kile ambacho Yesu anakionya kitatukaba au kutusonga hadi kufa?

**7. Usianzishe falsafa ya huduma inayoondoa ladha ya chumvi kutoka katika chumvi, na kuiweka nuru chini ya pishi.**
Ni nini hicho kilicho ndani ya Wakristo kinachowafanya wawe chumvi ya dunia na nuru ya dunia? Siyo mali. Tamaa ya mali na kufukuzia kuwa tajiri kuna ladha na kuonyesha mwangaza wa kidunia. Hauipatii dunia lolote jipya ya lile wanaloliamini. Maafa makubwa ya mafundisho ya mafanikio ni kwamba mtu hahitaji kuwa amehuishwa kiroho, ili aweze kupokea; badala yake, anachotakiwa mtu ni kuwa mbinafsi tu. Kupata utajiri kwa Jina la Yesu siyo chumvi ya dunia, wala si nuru ya dunia. Katika hili, dunia huona ni picha yake yenyewe inayojitokeza. Na kama itatenda kazi, watainunua.

Hoja ya kile anachosema Yesu kinatuonyesha chumvi na nuru ni nini. Ni furaha ya kuteseka kwa ajili ya Kristo. Yesu alisema hivi, "akafumbua kinywa chake, akawafundisha, akisema, "Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. *Furahini,* na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu. Ninyi ni chumvi ya dunia. . . Ninyi ni nuru ya dunia" (Mathayo 5:11-14).

Nini kitafanya *tuwe na ladha* (chumvi) na *kuona* (mwanga) wa Kristo ndani yetu, siyo tunapopenda mali kama jinsi wanavyopenda wenyewe. Badala yake, ni ule utayari na uwezo wa Wakristo wa kuwapenda wengine, katika hali ya mateso,

katika furaha kwa sababu thawabu yao iko mbinguni na Yesu. Hili silo la kawaida katika maisha ya wanadamu wa duniani. Hili ni nje ya ulimwengu wa kawaida. Lakini kuwavuta watu kwa ahadi za mafanikio, ni kawaida ya ulimwengu tu. Si ujumbe wa Kristo. Sicho alichokifia ili kukileta.

© Desiring God **Ruhusa:** Unaruhusiwa na unashauriwa kutoa nakala na kurudufu maandishi haya katika hali yoyote upendayo, ili mradi usibadili maneno yake wala mpangilio wake na kutokuuza kwa gharama zaidi ya gharama za kuchapishia. Kwa kunukuu kutoka ukurasa wetu wa "web" katika intaneti, waweza kuunganisha na kulipata somo hili. Utofauti au mabadiliko yoyote katika haya lazima kwanza uwasiliane na "Desiring God". **Tafadhali andika lifuatalo katika kila chapisho utakalolipeleka au kulitoa kwa yeyote:** By John Piper. © Desiring God. Website: desiringGod.org

## UWAKILI WA KANISA

## I. Utume na Kusudi la Kanisa

**A.** ***Kanisa lipo kwa ajili ya neema ya Mungu na utukufu wa Mungu.***

1. Mungu katika Kristo ametuokoa na kulianzisha kanisa kwa njia tu ya neema yake (**Math 16:18; Yoh 1:14-17; Rum 3:21-24; 5:14-21; 8:29-30; 11:5-6, 36; 1 Wakor 15:10; Waef 1:5-6, 18-23; 2:8-10; 3:1-7; Wakol 1:13-23; 2 The 2:16-17; 1 Tim 1:12-15; 2 Tim 1:8-11; Tito 2:11; 3:5-7; Waeb 2:9**).

2. Mwisho kamili wa kanisa ni kumtukuza Mungu (**Math 5:16; Yoh 5:44; 12:27-28; 14:13; 17:22-24; Rum 11:36; 15:7-9; 1 Wakor 6:19-20; 10:31; Waef 1:3-14; Wafil 1:9-11; 1 Pet 2:12; 4:11**).

**B.** ***Neema ya Mungu imedhihirishwa kwetu, naye anatukuzwa nasi, kupitia imani yetu kwake.***

1. Imani ndiyo hasa humtukuza Mungu kwa sababu, kwa tafsiri, imani hutazama nje ya mhusika na kumwangalia Mungu. *"Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu"* (**Waeb 11:6**). *"Lolote lisilo la imani ni dhambi"* (**Rum 14:23**).

2. Imani ni kutumaini kikamilifu katika Mungu katika maswala yote ya maisha yetu (**Waeb 11**). Imani katika Mungu, ni kupata maana, kusudi, na Kama John Piper asemavyo, "Mungu hutukuzwa zaidi ndani yetu wakati twajitosheleza kikamilifu katika Yeye" (Piper 2003: 31).

3. Imani halisi siku zote hujieleza yenyewe mbele za Mungu (**Math 7:13-27; Yoh 14:21-24; 15:1-11; Yak 1:22-2:26**).

4. Imani ya kweli na utii kwa Mungu utajionyesha wenyewe kwa utii kwa Mungu na kwa watu wengine.
   - a. Upendo ndiyo amri kuu kuliko zote ya Kristo (**Math 22:36-40; Yoh 13:34-35; 15:12-17**).
   - b. Upendo ndiyo kitu cha muhimu kuliko vyote (**1 Wakor 12:31-13:13; Wagal 5:6**).
   - c. Upendo ndiyo lengo la maelekezo ya kweli (**1 Tim 1:5**).
   - d. *Kufikiria utume na kusudi la kanisa kwa mtazamo wa upendo kunatuhitaji sisi:*
     - (1) Kufikiri kikanisa katika hali ya *kimahusiano*; na
     - (2) Kuwazia siyo tu *nini* kanisa linatakiwa kufanya, lakini *jinsi* kanisa litakavyolazimika kufanya.

5. Kanisa litadhihirisha neema ya Mungu na upendo katika njia zifuatazo:
   - a. *Kumwabudu Mungu.* Kuabudu *kunarudisha picha ya* neema na upendo wa Mungu kwake.
   - b. *Kujengwa (malezi ya waamini.* Kujengwa au kuimarishwa(malezi) ya waamini *huhitaji* neema na upendo wa Mungu kwa mwili wa Kristo.
   - c. *Huduma (kwenda nje) kwa wasioamini.* Huduma (kutoka nje) *hueneza* neema na upendo wa Mungu kwa wale ambao bado si waamini.
   - d. *Umoja (mshikamano).* Umoja na mshikamano *huonyesha* kanisa kama mahali palipo pema na kufaa, na kama chombo cha Mungu cha neema na upendo.

**C.** ***KUABUDU—utume na kusudi la kanisa linapatikana katika kumwabudu Mungu.***[7]

**Zab 29:2** hutuitia ili tuabudu: *"Mpeni BWANA utukufu wa jina lake; mwabudu BWANA kwa uzuri wa utakatifu"* (ona pia **Zab 96:7-9**).

1. Kuabudu kikawaida ni msimamo wa ndani na kiroho unaohusisha maisha yote, mbali kabisa na mwonekano wa nje, na wa mwilini.
   - a. *Kuabudu ni kumweka Mungu na Kristo kati.* Kuabudu ni *mwitikio wetu* wa Mungu ni nani, amefanya nini, na anafanya nini, na atafanya nini. Msingi wa kuabudu ni kutoshelezwa katika Mungu na Kristo (ona **Zab 32:11; 37:4; 42:1; 100:2; Wafil 1:20-21; 4:4, 10-13; Wakol 3:4**).

---

[7] Mengi kati ya mafundisho yafuatayo yametokana na nakala za David Bruenning, *Semina za Wachungaji Kimataifa na Viongozi wa Kikristo* (Neenah, WI: International Christian Assistance: International Children Fund, n.d).

(1) Kumwabudu Mungu mbinguni kunalenga katika: Mungu ni nani (utukufu wake; tabia yake ya ajabu), na nini Mungu alichokifanya katika Kristo, Anafanya nini, na atafanya nini(uumbaji; wokovu; utawala wake; hukumu yake inayokuja)—ona **Isa 6:1-8; Ufu 4-5; 7:9-17; 11:15-19; 15; 19:1-6**.

(2) Mambo hayo yote—tabia ya Mungu na Mdo yake—ndiyo lengo la kumtukuza, kama zilivyo katika Zaburi kuu za kuabudu (ona **Zab 8; 19; 24; 29; 33; 46-48; 63; 65-68; 76; 84; 87; 92-93; 96-100; 103-04; 111; 113; 115; 117; 135; 145-150**).

(3) Kuabudu kutadumu milele kwa sababu Mungu hudumu milele.

b. *Kuabudu kunamtukuza Mungu na hutusaidia kutubadilisha kuwa katika kumfanania Kristo.*

(1) Mungu ndiye mwenye zile sifa bora kabisa na kiwango pekee cha juu sana—utakatifu, wema, upendo, kweli, hekima, haki, huruma, neema, uaminifu, etc.

(2) Watu huthamini kile wanachokisifu. "Tukimsifu Mungu kwa haki yake, basi tuisifu na kuijali haki. Ikiwa tunamsifu yeye kwa wema wake wa upendo, basi tuinue wema wenye upendo. Kwa kumsifu Mungu kwa sifa kama hizo, tunaziweka kuwa hazina na tunavutwa nazo wenyewe" (Doriani 2001: 92).

2. Kuna uwanja *mpana* wa kuabudu (m.y, kuishi kwa ajili ya Mungu na kutoa huduma kwake katika kila sehemu ya maisha yetu), na uwanda *mdogo* wa kuabudu (m.y, kuja pamoja kama ushirika wa mwili moja kumwabudu Bwana). Hayo mawili yanahusiana—*tunamwabudu Bwana bila mafanikio ikiwa ule uwanda mdogo wa kuabudu hauambatani na ule wa pili* (ona **1 Sam 15:22-23; Zab 51:14-17; Isa 1:11-17; 29:13-16; Yer 6:16-20; 7:21-26; Eze 16:48-50; Hos 6:6; Mika 6:6-8; Math 12:1-8; 15:5-9; 23:23; Marko 12:28-33; Luka 6:6-10; Rum 12:1; Wakol 3:23-24; Yak 1:27**).

3. Kuabudu kunahusisha kila sehemu ya maisha yetu na nafsi yetu yote.

a. *Kuabudu kwa kweli kunafanyika kila muda wa maisha yetu, na siyo Jumapili tu.* Mtazamo wa kuabudu unatakiwa uathiri jinsi tunavyowatazama watu, na nyanja nYohgine zote za maisha yetu (ona **Yoh 4:21-24; Rum 1:9-10; 12:1; Wafil 3:3**). Mtazamo huu unafupishwa katika **Wakol 3:23** ambapo panasema, *"Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu"* (ona pia **Waef 6:7**).

b. *Kuabudu kwa kweli huhusisha sehemu zote za utu wetu (kichwa na moyo; akili, hisia, na nia).* Ibada ya kweli ni *"katika roho na kweli"* (**Yoh 4:21-24**).

(1) "Roho" huonyesha kwamba kuabudu kwetu kunapaswa kuhusishe mioyo yetu, hisia, na roho, kama tuwezeshwavyo na kuvutwa kuabudu na Roho Mtakatifu (ona **Math 15:8-9; 1 Wakor 14:25**).

(2) "Kweli" inaonyesha kwamba kuabudu kwetu kuwe na kiini katika injili na Neno (kusimamie Biblia), kwa vile Mungu hulikuza Neno lake na amejifunua kwetu katika Neno lake, na kumfanya mwili (Yesu) katika, na ndani ya Neno lake lililoandikwa (Biblia), ambalo ndiyo kweli (**Zab 119; 138:2; Yoh 1:1-14; 14:6; 17:17; Waef 1:13; 1 Tim 2:15; 3:16-17; Waeb 1:1-2; Yak 1:18**).

4. Kuabudu kunamwonyesha Mungu kujitoa kwetu kwake katika njia zake zote alizozichagua. Kwa hiyo, tunamwabudu Mungu kupitia:

a. *Kuimba* (**Zab 47:67; 95:1-7; 96:1-10; 98:1-6; Marko 14:26; 1 Wakor 14:26; Waef 5:18-19; Wakol 3:16; Ufu 5:8-10**).

b. *Kumsifu* (**Zab 111:1-10; 112:1; 135:1-4; 144:1-150:6; Luka 24:52-53; Mdo 2: 46-47; Rum 15:7-13; Waeb 2:11-12; 13:15; 1 Pet 4:11; Ufu 4:8-11; 5:11-14; 7:9-14; 19:4-6**).

c. *Kukiri na kufanya toba kwa dhambi.* Kumtukuza Mungu kunapaswa kuendane na hali ya dhamira ya kujitambua dhambi zetu wenyewe. Hii inapaswa iongoze kwenye toba ya kweli, na kisha uhakika wa msamaha (ona **Zab 34:18; Zab 51:16-17; Isa 6:3-7; Luka 5:8; 2 Wakor 7:9-11; Yak 5:16; 1 Yoh 1:5-9; Ufu 5:2-5**).

d. *Meza ya Bwana* (**1 Wakor 10:16-17; 11:23-26**).

e. *Kusoma, mahubiri, na mafundisho ya Neno lake* (**Mdo 2:42; 5:42; 1 Wakor 14:19; 2 Wakor 4:5; 1 Tim 4:6, 11, 13, 16; 6:2b; 2 Tim 2:2; 3:16-17; 4:1-4; Tito 2:1**).

f. *Maombi* (**Mdo 1:14; 2:42; 1 Tim 2**).

g. *Utoaji* (**1 Wakor 16:1-2; 2 Wakor 8-9**).

h. *Mwitikio wa maisha ya dhabihu iliyo hai* (**Yoh 10:27; 15:8; Rum 12:1; Waef 2:8-10; 4:11-5:21; Wakol 1:9-10; 2:6-7; 3:23-24**).

**D. *KUIMARIKA (MALEZI)—utume na makusudi ya kanisa yanapatikana katika kuwakamilisha watakatifu kwa kazi ya huduma.***

1. Kazi ya kanisa, na hasa ya viongozi wa kanisa, ni kuwakamilisha na kuwawezesha watu katika kanisa ili kuitenda huduma yao.

a. *Kifungu cha msingi kunachoelezea utume huu wa muhimu na ambalo ndilo kipaumbele cha kanisa ni* ***Waef 4:11-16:*** *[11]Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu; [12] kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; [13] hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha utimilifu wa Kristo; [14] ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. [15] Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. [16] Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.*

b. *"Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" kunahusika na mambo kadhaa:*

(1) Kuvitambua vipawa, karama, na uwezo wa washirika wa mwili, na kuviwezesha vipawa vingine kutumika, karama zao, na uwezo wao (ona **Rum 12:6-8; 1 Wakor 12:7-31; 14:12; 1 Pet 4:10-11**).

(2) Kufundisha, ni kuelekeza, kuinua, kufariji, na kutahadharisha mwili kutokana na Neno la Mungu, kuhusiana na mafundisho ya msingi ya Ukristo na maisha (ona **Mdo 2:42; 5:42; 1 Wakor 14:19; 2 Wakor 1:34; 4:5; 10:8; 1 Wathes 4:1; 5:12-14; 1 Tim 4:1-6, 11, 13, 16; 6:2b; 2 Tim 2:2; 3:16-17; 4:1-4; Tito 2:1**).

(A) Ili kufundisha vizuri, mchungaji anahitaji kuwa na rasilimali nzuri ya Ki-Biblia, kama vile vidokezo vya maandiko, itifaki, fursa ya kuhudhuria semina, na mafunzo mengine ya kitheolojia yanayoweza kupatikana kwake.

(B) Kwa vile mambo yote haya yanagharimu fedha, kanisa linatakiwa liwe na fungu kwa ajili ya mambo haya katika bajeti yake.

(C) Kwa sababu makanisa mengi, hasa katika maeneo ya vijijini, yanaweza kuwa na fedha kidogo sana, basi uongozi wa Wilaya au Dayosisi zao usaidie kwa hilo na kuanzisha maktaba ya kitheolojia hapo wilayani, kwenye makao makuu yao ambayo wachungaji wote wanaweza kuitumia.

(3) Kuwatambua na kuwainua viongozi wapya katika kanisa (ona **Kut 18:17-26; Kum 34:9; 2 Wafal 2:1-15; Yoh 17:18; Mtend 1:15-25; 6:1-7; 14:23; 2 Wakor 8:16-22; 1 Tim 3:1-13; Tito 1:5**). Hili linahitaji kwamba viongozi wa kanisa waliopo wawajue watu wao vizuri, na kukaa pamoja kwa muda na hawa viongozi wanaoinukia, wakiwafundisha na kuwaandaa katika uongozi wa Kikristo.

(4) Kuwaadibisha wale ambao wanasababisha mgawanyiko, wanaofundisha mapotofu, au wanaohusika na matukio ya mikasa ya aibu (ona **Rum 16:17-20; 1 Wakor 5:1-8, 12-13; 1 Tim 1:3; 2 Tim 2:14-18**). Baraza la kanisa, na kanisa kama mwili, linahitajika kujihusisha na nidhamu ya kanisa (ona **2 Wakor 2:6**). Kuwadibishwa kunawanufaisha wale wakosaji (**1 Wakor 5:5; 1 Tim 1:20**) na ni kwa manufaa ya kanisa lenyewe. Ikiwa kanisa linahusika katika hatua za kuwaadibisha kinidhamu, watu wanajisikia kwamba wanayo sehemu katika uhai wa kanisa hilo, na huchukua wajibu wao kama Wakristo kwa dhati zaidi, na husogezwa karibu zaidi na kanisa.

(5) Kurejeza ushirika kwa wale ambao waliadibishwa na kanisa, waliotubu, na kubadili maisha yao (ona **2 Wakor 2:5-11; 7:8-12; Wagal 6:1**).

2. Huduma huwahusu watu wote wa kanisa hilo, siyo tu wachungaji.

a. *Makanisa mengi yanaongozwa kwa namna kwamba ni mchungaji peke yake ndiye anayehusika kuliongoza—yeye ndiye mwenye mamlaka yote, na huamua nini kifanyike na nini kisifanyike.* Watu wanakuwa ni wa kusikiliza tu—wao kazi yao ni kuja tu na "kuabudu" siku za Jumapili. Mtindo wa kuliongoza kanisa kwa jinsi hiyo si wa Ki-Biblia, kwa sababu:

(1) Ingawaje katika Agano la Kale kulikuwa na ukuhani maalum, katika Agano Jipya, watakatifu wote huitwa "makuhani" (**1 Pet 2:9; Ufu 1:6**).

(2) Waamini wote wamepewa vipawa vya kiroho ambavyo vinatakiwa kutumika kwa

faida ya mwili wote (**Rum 12:6-8; 1 Wakor 7:7; 12:7-11, 28; 14:12; Waef 4:7-8; 1 Pet 4:10-11**).

(3) Ingawaje kuna kiwango kikubwa cha uwezekano wa mpangilio tofauti kuhusiana na serikali ya kanisa, na si kila mtu ameitwa ili kuongoza, mkondo wa uongozi wa kanisa siku zote huangukia juu ya viongozi kadhaa wa kanisa, na siyo mtu moja (**Mdo 11:30; 14:23; 15:2-6, 22-23, 28; 16:4; 20:17-18; 21:18; Wafil 1:1; 1 Tim 5:17; Tito 1:5; Yak 5:14; 1 Pet 5:1**).

b. *Maana ya msingi ya "huduma" ni "utumishi."*

(1) Neno kuu la Kiyunani la "huduma" katika Agano Jipya ni *diakonia* ambalo linamaanisha "utumishi" (ona **Mdo 1:17, 25; 6:4; 12:25; 20:24; 21:19; Rum 11:13; 12:7; 1 Wakor 16:15; 2 Wakor 4:1; 6:3; 8:4; 9:1; Waef 4:12; Wakol 4:17; 1 Tim 1:12; 2 Tim 4:5, 11**).

(2) Maneno makuu ya Kiyunani ya "watumishi" ni *diakonos* likimaanisha "mtumishi" (ona **Math 23:11; Marko 9:35; 10:43; Yoh 12:26; Rum 16:1; 1 Wakor 3:5; 2 Wakor 3:6; 6:4; Waef 3:7; 6:21; Wakol 1:7, 23, 25; 4:7; 1 Wathes 3:2; 1 Tim 4:6**), na *doulos* likimaanisha "mtumwa" (ona **Math 24:45, 46, 48, 50; 25:14, 19, 21, 23, 26, 30; Marko 10:44; Luka 17:10; Yoh 13:16; 15:20; Mdo 2:18; 4:29; Rum 1:1; 2 Wakor 4:5; Wagal 1:10; Waef 6:6; Wafil 1:12 Tim 2:24; Tito 1:1 Yak 1:11 Pet 2:16; 2 Pet 1:1; Yuda 1:1; Ufu 1:1**).

(3) Umuhimu wa maneno haya kwa viongozi wa kanisa uko katika pande mbili:

(A) Agano Jipya linakwepa kwa makusudi kutoa vyeo ambavyo vinaonyesha nguvu, heshima, na utendaji wa "kikuhani".

(B) Kristo alisisitiza kwamba viongozii wa kanisa, wakiwamo mitume wake mwenyewe, walitakiwa kuutumikia mwili (**Math 18:1-4; 20:25-28; 23:8-12; Marko 9:33-35; Luka 9:46-48; 22:24-27**).

(4) Matumizi ya maneno haya pia husisitiza kwamba kwa vile waamini wote ni watumishi au watumwa wa Kristo, waamii wote ni "watumishi" na wana "huduma" ya utumishi katika ufalme.

3. Malezi na kuimarishwa ndani ya kanisa kunahusishwa na ulimwengu wa "kuonekana" na ule wa "kiroho".

a. *Yesu na Mitume, katika yote mawili; yaani waliyofundisha na waliyofanya, walisisitiza umuhimu wa kujali hali za kimwili, na za kiroho, za waamini wenzao.*

(1) "Amri mpya" ya Yesu ya "Pendaneni, kama vile nilivyowapenda ninyi" ilitolewa kwa wanafunzi (**Yoh 13:34**). Upendo wao ukionyeshwa kwa *kati kati yao* ulikuwa ishara moja ambayo *"watu wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu"* (**Yoh 13:35**).

(2) Usemi wa Yakobo kwamba *"imani pasipo Mdo imekufa"* (**Yak 2:26**) ulitolewa kwa hoja kwamba*"Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki"* (**Yak 2:15**).

(3) Paulo aliliitia kanisa kutoa fedha ili kukutana na haja za ndugu waamini (**2 Wakor 8-9**). Kanisa la kwanza lilionyesha hali ya kujali haja za vitu kwa ajili ya waamini wenzao (**Mdo 2:44-45; 4:32-37**). Hakika, kanisa la mwanzo lilianzisha huduma ya ushemasi kwa nia njema kabisa ili kwa utaratibu na kwa ukamilifu waweze kutimiza haja za mahitaji ya vitu ya waamini (**Mdo 6:1-6;** ona **1 Tim 3:8-13**).

b. *"Vipawa vya kiroho" kuchanganya na vipawa vinavyohusiana na maswala ya vitu vya maisha.* "Vipawa" vya kiroho ni pamoja na mambo kama vile: utumishi na kutumika (**Rum 12:7**); kutoa (**Rum 12:8**); kuonyesha rehema (**Rum 12:8**); uponyaji (**1 Wakor 12:9, 28**), masaidiano (**1 Wakor 12:28**), na uongozi (**1 Wakor 12:28**). Hii inaonyesha kwamba Mungu anahusika na maswala yote ya maisha yetu. Kwa hiyo, tunapaswa tuhusike na maswala yote ya maisha ya maisha ya waamini wenzetu.

**E. *HUDUMA (KUWAFIKIA WENGINE)—utume na kusudi la kanisa unapatikana katika kuwahudumia wengine, na kuwafikia wale ambao wako nje ya kanisa.***

1. Kanisa limeitwa ili liwafanye wanafunzi watu pote duniani.

a. *Ule "Utume au wito Mkuu wa kanisa" unapatikana katika* ***Math 28:18-20:*** *[18] Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbiguni na duniani. [19] Basi,*

*enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;* [20] *na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote hata ukamilifu wa dahari."*

b. *Vifungu vya namna hiyo hiyo vya Ki-Biblia vinavyosisitiza umuhimu wa kumshuhudia Kristo ni pamoja na:* ***Math 9:35-38; Marko 16:15; Yoh 17:18-21; Mdo 1:8; 5:27-32; 10:34-43; Rum 10:14-17; 15:18-21; 1 Wakor 1:21-25; 2 Wakor 4:4-13; 2 Tim 4:1-2; 1 Yoh 1:1-3.*** Kitabu cha **Mdo** kinatoa mfano baada ya mfano wa waamini wakiwashuhudia wengine katika hali zote.

c. *Ukristo ni dini ya "nenda na ukawaambie." Waamini wote wameitwa ili wamshuhudie Kristo*.

(1) Wajibu wa kumshuhudia Kristo hauishii kwa wale walio ofisi za kikanisa, au wenye ofisi au kipawa maalum cha uinjilisti. Ndiyo maana, katika **Waef 4:11-16,** wale ambao Mungu amewaita kuwa "wahubiri" wanapaswa kutumia kipawa chao ili *"kuwakamilisha watakatifu"* ili kwamba wao nao, wawe washuhudiaji wazuri.

(2) Kanisa limetumwa "kuwapeleka" watu kuitangaza Injili na kuwafanya wawe wanafunzi (**Rum 10:14-15**). Kwa hiyo, fedha ili kuisaidia huduma ya kutoka nje inahitajika kuwekwa katika bajeti ya kanisa.

d. *Kanisa limeitwa kuwafanya "wanafunzi," na siyo tu kuwafanya "waokoke" (**Math 28:18-20**).*

(1) Mwanafunzi, ni mtu anayefundishwa, anayeelimishwa, mtu aliyeamua kuwa pamoja na mjuzi wa jambo au mwalimu (na katika tukio hili, kuwa na Yesu), ili kusudi awe kama huyo bwana, au mwalimu wake. Mwanafunzi hupokea malezi na tabia ya bwana au mwalimu, na anafanya kile ambacho bwana au mwalimu wake anakifanya (ona Willard 1997: 282-310).

(2) Ukweli kwamba tunatakiwa kuwafanya wanafunzi, na siyo waliookoka tu, wa mataifa yote kwaonyesha kwamba "Huu Utume Mkuu" unahusika na mengi zaidi ya mahubiri. Kubadilika kwa mtu ni mwanzo tu wa aina ya maisha ya uanafunzi. Uanafunzi ni mpana (unajijumuisha). Uanafunzi unahusisha utakaso, siyo tu kuhesabiwa haki kwao. Uanafunzi unahusisha sehemu zote za maisha ya mtu. Kwa hiyo, Utume Mkuu unahusisha maisha ya mtu yote.

e. *Utume wa Kristo wa kuwafanya "wanafunzi" ni pamoja na "kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi."* Kuna matokeo mawili ya hili kwa kanisa la mahali pamoja:

(1) Wale walio katika uongozi wa kanisa wanapaswa kuwa walimu wazuri, na wanapaswa kuwa wanalingana na, injili. Washiriki wa kanisa wanapaswa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Ukristo ni nini, mafundisho ya imani ni nini, na Wakristo wanapaswa kuishije. Hii ndiyo sababu moja ya sifa ya kuwa kiongozi katika kanisa ni pamoja na kuwa *"na uwezo wa kufundisha"* (**1 Tim 3:2; 2 Tim 2:24**). Kati ya njia mbali mbali za kufundisha na kuleta ushawishi, "tabia ya mtu" [*ethos*] ndiyo yenye nguvu kuliko zote" (Cooper 1932: 9). Kwa hiyo, kwa mara nyingine,unajijumuisha; na kuhusisha maisha yote ya mtu.

(2) Kanisa la mahali pamoja ni lazima liweke mkakati kinamna fulani juu ya "kuwafanya wanafunzi" waamini wapya—wa kuwaimarisha katika imani, na kuimarisha uelewa wao. Badala ya kutosheka na kuwa na washirika wapya na kuwabatiza tu, na kuja kanisani Jumapili, linapaswa kuwe na "madarasa ya uanafunzi" kwa kusudi kwamba waamini wapya wanageuzwa kuwa "wanafunzi." Kuwapanga watu wa kanisa katika vifungu vidogo vidogo ambavyo hukutana mara kwa mara kwa ajili ya kuomba, kujifunza Biblia, na kufanya ushirika, ni njia nyingine bora kabisa za kuwafanya waamini wapya kukua katika imani na katika kujitoa kwao kwa wengine na kanisa pia.

f. *Sehemu ya kutimizwa kwa "Utume Mkuu" ni kuanzisha makanisa sehemu mbali mbali.* Kanisa siyo tu ni ushirika wa ulimwengu wa waamini katika Kristo, lakini pia ndani yake kuna ushirika wa mahali mahali. Mkondo ulioandikwa katika kitabu cha **Mdo** ni kwamba waamini walihubiri injili kila mahali; wakawafanya wanafunzi waamini wapya, wakawaimarisha katika imani; na kisha wakaanzisha makanisa mahali hapo (ona **Mdo 14:21-23**).

2. Kanisa limeitwa kuwa shahidi wa Kristo kwa kuwa mfano na kuwatumikia wengine katika dunia.

a. *Yale tuyatendayo hunena wazi zaidi kuliko yale tusemayo, na hudhihirisha kweli ya kile tukiaminicho.* Katika **Math 5:13-16** Yesu alituambia kwamba kwa Mdo yetu, tunakuwa mfano

wa upendo wake Yeye ulimwenguni: [13] *"Ninyi ni chumvi ya dunia , lakini chunvi ikiwa imeharibika itatwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu* [14] *Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.* [15] *Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani.* [16] *Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona Mdo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni."*

b. *Mifano ya Yesu ya "chumvi" na "nuru" inaomyesha kwamba kanisa linapaswa kujihusisha na maeneo yote ya maisha, na siyo kuishia kuhubiri na kusifu siku za Jumapili.*

(1) Chumvi hutumika kama *kitu cha kuhifadhia.* Kanisa linapaswa kutenda kama kitu cha kuhifadhia hali kinyume na uharibifu wa kiroho na kimaadili. Chumvi pia hutoa *ladha;* kanisa linatakiwa litoe ladha ya uzima wa milele na uvumilivu wa mbinguni katika dunia iliyo mbovu na iliyo na ugumu.

(2) Nuru inatakiwa *ionekane.* Kanisa linatakiwa liishi na kutenda katika njia ambazo watu wanaweza kuiona injili na uzima mpya wa upendo, rehema, amani, haki, na kweli ambayo Kristo anaileta. Nuru pia huwapa joto watu; hulitupa nje giza; huleta uwazi; husababisha kukua; huwawezesha watu kuona njia yao; huwasababisha watu wanaotaka kutenda uovu au mambo ya aibu, kujificha; huleta furaha. Kanisa linatakiwa kutenda hayo yote linayotakiwa kuyafanya, ili kwamba watu wote waaone wazi wazi.

c. *Kila mahali katika Maandiko kuna uhusiano mkubwa kati ya yale tuyasemayo, jinsi tunavyotenda, na nini tunaamini.*

(1) Yesu alijali hali za kivitu (kimwili) za watu kama vile hali zao za kiroho. Kwa hiyo, aliwalisha wenye njaa na kuponya wagonjwa. Kusema ukweli, ilikuwa ni huduma ya Yesu katika ulimwengu wa kimwili ambao ilionyesha uwezo wake katika ulimwengu wa kiroho (ona **Math 8:5-13; 9:1-8; 11:2-6; Marko 2:1-12; Luka 5:17-26; 7:1-10, 18-23**).

(2) Kanisa ni *lazima* liuonyeshe kwa kuudhihirisha upendo wa Kristo, huruma kwa masikini, kuwasaidia wahitaji, na wale walio katika matatizo, nk. Ikiwa ni kweli litahitaji kutekeleza wajibu wake na huduma yake kwa wengine (ona **Math 5:38-48; Luka 10:25-37; Rum 12:9-21; 15:1-3; 2 Wakor 8:21; Wagal 6:9-10; Wakol 4:5; Tito 2:7-8; Yak 1:27; 1 Pet 2:12**). Kusema kweli, ikiwa kile tunachodai kuwa tunakiamini *hakiendani* na Mdo mema, basi imani yetu inakuwa "imekufa" (**Yak 2:14-26**).

**F.** ***UMOJA (MSHIKAMANO)—utume na kusudi la kanisa unaonekana katika umoja na mshikamano.***

1. Kristo ameliita rasmi kanisa ili kuudhihirisha umoja katika maombi ya ukuhani wake mkuu **Yoh 17:18-21**: [18] *Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo nalitwatuma hao ulimwenguni.* [19] *Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli.* [20] *Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao.* [21] *Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani Yak; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*

2. Umoja na mshikamano wa kanisa humiminika kutokana na tabia ya kanisa.

a. *Kristo* aliomba kwamba*"Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani Yak; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma." (**Yoh 17:21**; ona pia **Yoh 17:11**).* Paulo alionyesha kwamba, kwa vile Kristo hakugawanyika, nasi tusigawanyike kamwe (**1 Wakor 1:11-13**).

b. *Mifano au vielezo inavyovitumia Biblia kulielezea kanisa huonyesha kwamba kanisa lazima lionyeshe umoja na mshikamano.*

(1) Kanisa ni mwili wa Kristo. Kanisa ni mwili moja na kichwa (Kristo). Kila mtu ni muhimu, kwa kuwa kila mtu ni "kiungo" cha mwili. Mtu akiugua, mwili mzima unaumwa. Viungo vyote vinafanya kazi, na vinatakiwa kufanya kazi vizuri, ili mwili uwe kamili na kutenda kazi vizuri (**1 Wakor 12;** ona **Rum 12:4-5; Waef 1:22-23; 4:1-6, 11-16; Wakol 1:18, 24; 2:19; 3:15**).

(2) Kanisa ni jengo au hekalu la Mungu. Sisi tu "mawe yaliyo hai" ambayo kila moja lina mahali pake katika jengo moja. Sehemu ya jengo ambayo haiko mahali pake, au pana mahali pamevunjika, hali hiyo sivyo jengo lilivyoandaliwa liwe (ona **1 Wakor 3:9-17; 2 Wakor 6:16; Waef 2:19-22; 1 Pet 1:4-6**).

(3) Kanisa ni familia ya Mungu. Familia iliyo nzuri, na iliyo na utendaji mzuri kabisa, haina sifa ya hasira au ugomvi, utengano, au kupigana wenyewe kwa wenyewe. Familia iliyo nzuri, na iliyo na utendaji mzuri kabisa, huonyesha upendo, heshima, furaha, umoja, na mambo mengi pamoja. Kanisa linatakiwa kuonyesha, ndani yake lenyewe na katika dunia, ni familia nzuri kiasi gani, itendayo mambo kiuzuri, nayo hupendeza kuiona (ona **Marko 10:29-30; Rum 8:14-17; 2 Wakor 6:18; Waef 1:5; 2:19; Wagal 3:26-4:7; 1 Tim 3:15; 5:1-2**).

3. Umoja na mshikamano wa kanisa hutokana na kile alichokifanya Yesu.

a. *Kristo ametupatanisha sisi na Baba.* Kwa hiyo, tunayo huduma ya kuwapatanisha wengine (**Rum 5:10; 2 Wakor 5:18-20; Waef 2:16; Wakol 1:21-22; Waeb 2:17**).

b. *Kristo aliuvunja ukuta pekee wa utengano wowote uliokuwepo katika Agano la Kale (ukuta kati ya Mataifa na Wayahudi).* Kwa hiyo, tusiwe tunajenga kuta nyingine kabisa katikati yetu (**Yoh 17:11, 20-21; Rum 3:21-22; 1 Wakor 12:12-13; Wagal 3:26-28; Waef 2:11-3:6; Wakol 3:9-11**).

c. *Kristo alitenda zaidi ya kuvunja kuta za utengano kati ya watu; alimuumba "mtu mpya moja" kutokana na watu ambao mwanzoni walikuwa wamegawanyika.* Kwa hiyo, lazima tuonyeshe yote mawili; umoja na upya katika Kristo (**Waef 2:11-22**).

d. *Kristo amewanunua watu wake kutoka katika kila kabila, ulimi, jamii, na mataifa ya dunia.* Kwa hiyo tunapaswa kumweka Kristo kwanza, na tusitengane wenyewe kwa ajili ya rangi ya ngozi, ukabila, lugha, au tofauti za kumila (**Ufu 5:9; 7:9**).

4. Umoja na mshikamano wa kanisa ni muhimu kwa ushuhuda wa kanisa katika dunia.

a. *Kristo aliomba kwamba tuwe na umoja "ili kwamba ulimwengu ujue kwamba umenituma" (**Yoh 17:21**).* Umoja wetu, au kukosa umoja kwetu na mshikamano kama mwili, vitaathiri jinsi watu watakavyomwona Yesu alivyo. Kusema ukweli, kitu kimoja ambacho Kristo alitupa ambacho *"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."* (**Yoh 13:34-35**). Kama kweli tunao upendo huo kila moja kwa mwingine, na kuuonyesha, ndipo *tutakapokuwa na umoja na mshikamano.*

b. *Mitume walionyesha yote mawili, na wametuitia sisi tuonyeshe umoja huo na mshikamano. (**Zab 133:1; Mdo 1:14; 4:32; Rum 12:16; 15:5-6; 1 Wakor 1:10; 12:24-25; 2 Wakor 13:11; Waef 4:11-13; Wafil 1:27; 2:1-5; Wakol 3:14; 1 Pet 3:8**).*

5. Umoja na mshikamano unapaswa udhihirishwe katika ngazi zote—ndani ya mtu; kimahusiano ndani ya kanisa la mahali; na kati ya makanisa mbali mbali na mdhehebu mbali mbali.

a. *Mshikamano huanzia ndani ya mtu mwenyewe.* Kristo huokoa watu kutokana na dhambi zao na kuleta uponyaji (**Math 1:21**; **8:16-17; 1 Pet 2:24**). Amemtuma Roho Mtakatifu wake kukaa ndani ya waamini (**Yoh 14:16-18**). Hutuongoza katika kweli (**Yoh 14:26; 16:13**). Hutupatia amani na "tunda" la Roho" linalotuongoza kwenye maisha yaliyojipangilia kiutoshelevu (**Yoh 14:27; Wagal 5:22-23**). Nasi tuna nia ya Kristo (**1 Wakor 2:16**). Ametuingiza katika familia yake mwenyewe (**Rum 8:14-17**). Ni wazi kabisa, Yesu alikuja ili watu *"wawe na uzima, na kisha wawe nao tele"* (**Yoh 10:10**). Kristo atendavyo maishani mwetu, na kama tunavyotii na kufuata na kuzidi kumfanania, kila mwamini anapaswa aonyeshe utimilifu mkubwa zaidi na zaidi wa ndani.

b. *Wito wa Mitume kuhusu umoja kwa kiwango kikubwa ulilenga kwa watu walio katika kanisa la mahali pamoja.* Mitume walisisitiza kuwa na nia moja na umoja wa *mahusiano* katika mwili wa Kristo (ona **Rum 12:16; 15:5-6; 1 Wakor 1:10; 12:24-25; 2 Wakor 13:11; Waef 4:11-13; Wafil 1:27; 2:1-5; 1 Pet 3:8**). Umoja wa namna hiyo wa kimahusiano hutiririka kiasilia na kuwa dhahiri kwa wengine ikiwa na pale kanisa litakapoitii "amri mpya" aliyowapa wanafunzi wake usiku kabla hajasulubiwa *"amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo."* (**Yoh 13:34-35**) Kama kweli tunaliona kanisa letu kama familia, na wenyewe kama ndugu wa kiume na wa kike, kimsingi tunapaswa tuwe tunaonyesha upendo na umoja kwa kila moja wetu.

c. S*wala jingine muhimu kuhusu umoja na utimilifu katika kanisa ni umoja kati ya makanisa ya mahali pamoja na kati ya madhehebu mbali mbali.*

(1) Ingawaje madhehebu yalijitokeza baada ya Biblia kuandikwa, sala ya Yesu katika **Yoh 17** na miito ya Yesu na Mitume katika Agano Jipya kwa ajili ya umoja, ni mipana kiasi kwamba inahusisha umoja kati ya makanisa mbalimbali na kati ya dini na madhehebu.

(2) Kauli nyingine za Yesu (**Math 12:25, 30; Marko 3:24-25; 9:38-40; Luka 9:49-50; 11:17, 23**) na Paulo (**1 Wakor 1:10-15; Wafil 1:12-18**) pia hushughulika na hali ya umoja kati ya idara mbali mbali katika kanisa.

(3) Umoja kati ya makanisa mbali mbali au madhehebu haumaanishi kwamba tunatakiwa kupeana itikadi za mafundisho au Mdo ambayo ni muhimu kwetu. Tunatakiwa kutofautisha mambo yale ambayo ni msingi wa mafundisho, na Mdo yanayoendana na imani (m.y, Biblia kama Neno la Mungu; Tabia ya Mungu; mwanadamu kuwa na asili ya dhambi, na ukweli kwamba hana uwezo wa kujiokoa mwenyewe; Nafsi na kazi ya Yesu Kristo; njia pekee ya wokovu, kwa neema katika imani ndani ya Kristo. Umoja unapaswa kuwa na msingi katika mambo hayo ya msingi katika Kristo. Tunapaswa kufanya kazi, kushirikiana, na kujenga mahusiano kati yetu. Tusiziruhusu imani zetu mbali mbali au Mdo ambayo siyo ya msingi wa imani yenyewe yatenganishe ushirika wetu. Ikiwa tutafanya hivi, tutagundua kwamba mengi zaidi yanatuunganisha kuliko kututenganisha.

6. Umoja na mshikamano ndani ya kanisa hudhihirishwa kwa njia mbali mbali.

a. *Kukusanyika pamoja kwa ajili ya kuabudu* (***Waeb 10:23-25***).

b. *Kushiriki katika sakramenti mbali mbali pamoja (ona **Math 28:19; Mdo 2:38; 1 Wakor 10:17**).* Ingawaje ubatizo, tofauti na meza ya Bwana, unatakiwa kufanywa mara moja tu, ni tendo jema linalosaidia kutuunganisha mwili pamoja, pale tunapoukumbuka ubatizo wetu mara kwa mara. Njia moja ya kufanya hivi ni kuunganika kama mwili moja, na kukiri viapo vya ubatizo wakati mtu fulani anapobatizwa, na kuahidi kumwombea mtu huyo anayebatizwa.

c. *Milo ya pamoja na ushirika (**Mdo 2:42, 46-47**).* Ushirika wa Kikristo katika kanisa unatokana na neno la Kiyunani *koinonia* ambalo linamaanisha "uhusiano wa karibu unaohusisha kuwa na malengo mamoja, na kushirikiana; kumega mkate pamoja; mtazamo wa nia njema unaodhihirisha shauku ya kuwa na mahusiano ya karibu." Ushirika wa namna hiyo unapaswa uwe umoja wa kweli, upendo, na furaha unaoonyeshwa na wapendwa katika familia hiyo kwa kila moja. Kule kukusanyika kama kanisa zima, na katika vikundi vidogo vidogo ndani ya kanisa ni njia nzuri kukuza ushirika.

d. *Kushirikiana na kusaidiana kila moja ki-vitu (**Mdo 2:44-45**).* Familia hujitunza kwa kuangaliana. Kuwasaidia wale wenye mahitaji kunaonyesha kwamba kweli sisi ni familia (ona **Wagal 6:10; Yak 2:14-26**).

7. Umoja na mshikamano utatokea ikiwa kanisa litafanya yale ambayo linatakiwa kuwa linafanya.

a. *Sala ya Kristo"ili kwamba wawe na umoja" (**Yoh 17:21**) inakuwa iko katika hali ya matokeo ya tendo.* Hilo linaonyesha kwamba umoja (umoja; mshikamano) ni *matokeo* au *kitu kitokeacho* kutokana na kitu kingine, siyo kitu ambacho tunaweza kukipata "moja kwa moja". Kwamba "kitu kingine" ni pande nyingine tatu za msingi za kusudi na utume wa kanisa: kuabudu; kuimarika (malezi); na huduma (kwenda nje).

b. *Kanisa litadhihirisha upendo na utimilifu ikiwa—na kwa kiwango—kwamba linaonyesha utume wake wa msingi na makusudi.*

(1) Hatuwezi kuwa "wakamilifu" ikiwa tunapuuza sehemu yoyote ambayo ni kusudi kuu la kanisa. Katika hali hiyo tunakuwa hatujawiana.

(2) Kanisa linavyomwabudu Mungu kiukweli "katika roho na katika kweli" linakuwa halina namna bali kuunganika na kuwa timilifu.

(3) Kanisa linapowajali walio ndani kama ndugu wa familia, waamini watakuwa wamoja kadiri wanavyolelewa, kuimarishwa, na kuandaliwa.

(4) Kanisa linavyotumikia na kuwafikia wengine, waamini katika kanisa watakuwa *wakitumia* vipawa vyao na vipaji vyao walivyojaliwa kuwa navyo. Watakuwa wakiijenga "misuli ya kiroho" kama vile ambavyo mazoezi ya mwilini yanavyojenga mwili (ona **1 Tim 4:7-8**).

(5) Kanisa linavyotumikia na kuwafikia wengine, hao wengine watafanyika sehemu ya waamini na kuja kanisani. Kanisa litakua.

(6) Waamini wapya watakuwa waabuduo wapya. Kama wale waamini wapya wanavyofundishwa kuwa wanafunzi, na kulelewa, na kuimarishwa, wanafanyika wakamilifu. Ndipo nao watatumia vipawa na karama zao kuwafikia wengine. Kisha mduara huo utakuwa unajirudia wenyewe.

c. *Makusudi yote ya utume na kusudi la kanisa kimsingi yanahusiana, na ni ya lazima.* Hakuna

Uwakili Wa Kibiblia copyright © 2008-2014 Jonathan Menn All right reserved

lolote kati utume wa msingi na kusudi la kanisa linajitosheleza binafsi. Kuyafanya yale matatu ya makusudi na utume wa msingi kutaleta *matokeo* ya umoja na utimilifu na *kuletesha ongezeko la* kuabudu, kuimarika, na kuwafikia wengine. Sababu ni kwamba kanisa litakuwa linafanya kile ambacho linatakiwa kuwa linafanya. Huo ndio mtazamo wa kuabudu; hiyo ndiyo tabia ya upendo. Wakati kanisa linafanya kile ambacho linatakiwa kufanya, tunaweza kupumzika na kusema kwamba*"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema"* (**Wafil 2:13**), hata mwisho Kristo anatukuzwa, sasa na milele ijayo.

## II. Kanisa na Fedha

**A. *Kanisa linatakiwa kuonyesha uwajibikaji wake wa fedha.***

1. Kanuni, mfano, na uwajibikaji wa fedha umeonyeshwa katika **2 Wakor 8:16-24:** [16] *Lakini ahimidiwe Mungu atiaye bidii ile ile kwa ajili yenu katika moyo wa Tito.* [17] *Maana aliyapokea kweli yale maonyo; tena, huku akizidi kuwa na bidii, alisafiri kwenda kwenu kwa hiari yake mwenyewe.* [18] *Na pamoja naye tukamtuma ndugu yule ambaye sifa zake katika Injili zimeenea makanisani mwote.* [19] *Wala si hivyo tu, bali alichaguliwa na makanisa asafiri pamoja nasi katika jambo la neema hii, tunayoitumikia, ili Bwana atukuzwe, ukadhihirike utayari wetu.* [20] *Tukijiepusha na neno hili, mtu asije akatulaumu kwa habari ya karama hii tunayoitumikia;* [21] *tukitangulia kufikiri yaliyo mema, si mbele za Bwana tu, ila na mbele ya wanadamu.* [22] *Nasi pamoja nao tumemtuma ndugu yetu tuliyemwona mara nyingi katika mambo mengi kuwa ana bidii, na sasa ana bidii zaidi sana kwa sababu ya tumaini kuu alilo nalo kwenu.* [23] *Basi mtu akitaka habari za Tito, yeye ni mshirika wangu, na mtenda kazi pamoja nami kwa ajili yenu; tena akitaka habari za ndugu zetu, wao ni mitume wa makanisa, na utukufu wa Kristo.* [24] *Basi waonyesheni mbele ya makanisa hakika ya upendo wenu, na ya kujisifu kwetu kwa ajili yenu.*

2. Hoja ya kifungu hiki ni changizo za fedha ambazo Paulo alikuwa ameagiza zikusanywe kwa ajili ya kuwasaidia waamini masikini wa Yerusalemu (ona **Rum 15:25-27; 1 Wakor 16:1-4; 2 Wakor 8:1-15**).

3. Paulo alianzisha taratibu za uwajibikaji za kushughulikia fedha zilizokuwa zinakusanywa.
   - a. Paulo hakuzipokea wala kuzikusanya fedha yeye mwenyewe.
   - b. *Alianzisha kamati ya kupokea na kuhusika na fedha.*
     - (1) Kamati ilikuwa na watu watatu—Tito na watu wengine wawili (**2 Wakor 8:16, 18, 22**).
     - (2) Kila moja wa watu hao alijulikana na makanisa hayo, alikuwa amejaribiwa, na kujithibitisha mwenyewe kuwa mwaminifu (**2 Wakor 8:18-19, 22-23**).
     - (3) Angalau moja kati ya hao watatu alikuwa amechaguliwa na kanisa, si kwa kuchaguliwa na Paulo (**2 Wakor 8:19**). Hilo lilihusiana na uchaguzi wa mashemasi *ulifanywa na kanisa* (siyo kwa Mitume kuwachagulia) katika **Mdo 6:3**. Paulo basi anatoa mamlaka yake ya kitume kwa mashemasi wa kanisa.
     - (4) "Ndugu" hao wawili katika kamati walikuwa wawakilishi wa kanisa (**2 Wakor 8:23**).
   - c. *Sababu ya kamati ya fedha ilikuwa kuhakikisha udhibiti wa fedha unafanyika ipasavyo* (**2 Wakor 8:20-21**).
     - (1) Tahadhari lazima zifanywe ili kwamba asiwepo mtu yeyote ambaye atatumia vibaya fedha (**2 Wakor 8:20**).
     - (2) Tunawajibika kwa Mungu, kwa kanisa, na kwa wengine pia kwa uwajibikaji mzuri wa utunzaji wa fedha (**2 Wakor 8:21**). Mpangilio wa maneno katika **2 Wakor 8:21** unasisitiza umuhimu wa unyofu *"mbele za wanadamu"* (kwa kuwa Mungu anajua tayari kama unyofu upo au hapana).
     - (3) Unyofu wa fedha na usimamizi mzuri wa fedha mwisho wake huonyesha picha ya*"utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo"* (**2 Wakor 8:19, 23**).

4. Muundo wa kamati ya Paulo kusimamia fedha unaendana na muundo kwa makanisa yaliyoanzishwa sehemu mbali mbali katika Agano Jipya.
   - a. Kanisa la Agano Jipya lenyewe lilikuwa na muundo wa kushirikiana madaraka (**Mdo 6:1-7; 14:23; 16:4; 20:17, 28; 21:18; 1 Tim 3:1-13; Tito 1:5-9**).
   - b. *Kwa vile wanadamu kiasili ni wadhambi, si busara kwa mtu awaye yote peke yake, hata kama ni wa mcha Mungu kiasi gani, kushikilia madaraka yote katika kanisa.* Kwa hiyo, baraza linalosimamia, ambalo mara nyingi huwamo pia mchungaji ndani yake, linapaswa kwa pamoja

liongoze kanisa na kutoa miongozo ya kanisa.

c. *Risiti za fedha zihesabiwe, zishuhudiwe, na kukaguliwa na zaidi ya mtu moja.* Hilo litasaidia kuzuia ufujaji wa kifedha, wizi, na ubadhilifu.

5. Utaratibu wa kudhibiti maswala ya fedha unapaswa uwe na vitu kadhaa, licha ya kutolewa na zaidi ya mtu moja (Obiero 1995:52; Hussein 1998: 21):

a. *Kuandaliwe sheria za kuhusiana na maombi ya fedha za kanisa.*

(1) Utaratibu wa usimamizi wa fedha za kanisa unapaswa uendane na "taratibu zinazokubalika za uhasibu za kawaida."

(A) Kusema kweli, "barua ya Paulo inaonyesha taratibu za kiutawala na utaratibu wa kawaida kufuatwa . . . [kwa sababu] unyofu na uadilifu wa makanisa kama taasisi za uongozi zilitegemewa kwa kiwango kikubwa katika miaka hiyo ya mwanzo kiasi kwamba zilifikia kiwango cha leo kinachotumiwa katika maswala ya kiofisi katika dunia" (Betz 1985: 134).

(B) Unyofu na uadilifu wa kanisa bado leo unategemewa ufikie hali ya kuendana na taratibu halisi za kihasibu na kuendesha maswala ya fedha za kawaida katika kusimamia fedha na kuendesha biashara.

(2) Kuwa na sheria kunamsaidia yeyote anayeshugulika na fedha na uhasibu ili kuchukua maamuzi ambayo yanakubalika kwa wakati husika, na ya kufaa. Ikiwa tutatoa uamuzi wa kiupendeleo, wengine huendelea kujiuliza maswali, au unaanzisha mkondo wa kufuatwa hata wakati wa matukio yasiyofaa; ambao matokeo yake unaweza kuwa ni wa kukatisha tamaa, na kutumia nguvu ambazo zingetumika kwa maswala mengine.

(3) Sheria zinasaidia kulinda mali ya kanisa na huzuia mianya ya hisia mbaya kwa washirika. Sheria hizo ni pamoja na:

(A) Kupanga malipo ya mchungaji na gharama nyingine anazotakiwa kulipwa.

(B) Kupanga kiwango cha gharama zinazohitaji kibali cha uongozi, au makubaliano ya ushirika mzima wa kanisa. Kwa mfano, Unaweza ukahitaji kuwa na risiti kwa kitu chochote chenye gharama kuanzia zaidi ya dola 5, na labda kuomba kibali kabla ya kununua kitu ambacho gharama yake inazidi Dola 50.

(C) Panga kimaandishi kabisa gharama au utaratibu utakaofuatwa kuazima vitu au mali za kanisa: k.m, Je utaruhusu viti au mabenchi ya kanisa, vyombo vya muziki na sauti, jenereta, nk. Kuazimwa na watu walio nje ya kanisa bila malipo, au bila fedha?

(D) Zisihifadhiwe fedha kiasi kikubwa kwenye maeneo ya kanisa. Badala yake, kanisa liwe na akaunti ya Benki ambako huhifadhi fedha zake.

b. *Weka hesabu za fedha na za matumizi yake vizuri.* Kuweka kumbukumbu kunahusisha kutumia taratibu zinazoeleweka za uhasibu.

(1) Kwa kiwango cha chini kabisa, kumbukumbu za uhasibu lazima ziwe na: (A) Uingizaji na matumizi yake; (B) Fedha zilizoingizwa; (C) Fedha zilizolipwa; (D) Fedha zilizobakia; na (E) Hesabu za Akiba ya benki.

(2) Kumbukumbu za kiuhasibu zinapaswa kuwa katika hali ya kutazamika na yeyote ambaye anataka kujua shughuli za kanisa.

(3) Kumbukumbu nzuri zinasaidia uongozi wa kanisa kunena kwa ujasiri juu ya maswala yahusuyo kanisa kwa ushirika au mtu yeyote anayetaka kujua mambo fulani.

(4) Kumbukumbu nzuri pia huwavutia wafadhili na vikundi vingine vya misaada ambavyo navyo vinatakiwa kutoa ripoti kwa mashirika yaliyowatuma.

(5) Kumbukumbu nzuri zinaonyesha historia ya kifedha ya kanisa. Zitaonyesha ama uwakili mzuri au mbaya, na hilo litakuwa na athari yenye nguvu mno kwa utoaji wa mbeleni na afya ya kanisa.

c. *Risiti za kununulia zinatakiwa ziwepo, na risiti kwa fedha zile zitolewazo nje pia ziwepo.* Risiti na kumbukumbu huondoa mashaka kuhusu jinsi kanisa linavyoongoza na kusimamia mambo yake. Moja ya ahadi za msingi sana ambazo kanisa linaendeshwa ni kweli; kwa hiyo, kuingiza hesabu za fedha zinazoingia na zinazotoka ni muhimu.

d. *Weka kumbukumbu wazi.* Kumbukumbu za fedha zinapaswa ziwe wazi kwa ukaguzi kwa washirika wa kanisa. Zaidi ya hapo, uongozi wa kanisa unapaswa mara kwa mara (k.m, kila

mwezi) *upokee* ripoti ya fedha na pia unapaswa utangaze ripoti hiyo kwa kanisa kueleza fedha zilivyoingia, na zilivyokwenda (k.m; ripoti iliyofupishwa inaweza kuwekwa kwenye ubao wa kanisa ili washirika waweze kuisoma na kutoa mawazo).

(1) Washiriki wa kanisa wanayo haki ya kujua kile kinachoendelea kuhusiana na matumizi ya fedha yao.

(2) Zaidi ya hapo, washirika wana haki ya kujua kitu kinachohusiana na fedha zao—watu hutaka "kujua hali ilivyo."

(3) Taarifa za mara kwa mara za fedha huondosha hofu kwamba fedha zinatumiwa vibaya na pia hulihakikishia kanisa kwamba fedha zao zinasimamiwa vizuri.

(4) Kuweka taarifa za fedha wazi kutaonyesha pia sehemu ambazo kanisa linatumia au linahitaji fedha zaidi.

e. *Hamasisha watu wa kanisa wachangie mawazo yao.* Liwepo sanduku la maoni ambapo washiriki wa kundi hilo wanaweza kutoa mapendekezo. Ruhusu maswala muhimu ya kanisa yajadiliwe katika vikao vya kanisa. Kufanya hivi kutazuia mhali ya kutokuelewana, kutawasaidia watu wajihusishe na kanisa, na kunaweza kuleta mapendekezo mazuri sana ya kuliboresha kanisa.

**B. *Kanisa linatakiwa kuelekeza fedha na rasilimali zake kufuatana na bajeti iliyoandikwa.***

1. Bajeti ni mpango ulioandaliwa wa matumizi wenye makusudi ya:

a. Kuonyesha vipaumbele vya juu vya kanisa;

b Kutumia fedha siyo tu kwa kuonyesha mwitikio kwa mahitaji yanayojitokeza kwa sasa, bali ni kwa kulingana na, mtazamo wa jumla na mpango;

c. Dharura ishughulikiwe kibusara kabisa, na pia litokeapo ongezeko lisimamiwe kwa hekima nzuri; na

d. Husisha sehemu zote muhimu za kusaidia fedha na za kutumia, kwa muda mfupi na kwa mda mrefu.

2. Taaluma ya Bajeti:

a. *Bajeti ni lazima iandaliwe kwa mwaka mzima.*

b. *Bajeti ya mwaka inatakiwa iwe na mgawanyo wa vipato/matumizi ya miezi, ili kwamba watenda kazi wa kanisa wajue kikamilifu nini kinahitajika kuendesha huduma ya kanisa.*

(1) Kila bajeti ya mwezi inaweza kuwa sawa na 1/12 ya bajeti ya mwaka, au asilimia fulani ya nyingine (kipato au matumizi hayategemewi kufanana kila mwezi katika mwaka mzima).

(2) Matumizi ya mwezi lazima yaendane na kipato halisi.

c. *Kutenganisha katika idara na kutathmini matumizi kufanywe.*

(1) Mfano wa idara ungeweza kuwa na: Watenda kazi wa kanisa; Elimu ya Kikristo; Muziki; Vifaa na usafiri; Huduma za jamii; Huduma za Kidunia; na Uongozi wa Kanisa.

(2) Kabla mwaka wa kalenda haujaanza, maombi yanatakiwa kufanywa kutoka katika kila idara kuu. Maombi hayo yanapaswa kuandamana na makadirio ya vitu vya idara hiyo (orodha ya vitu). Wale wanaohusika na kufanya bajeti, lazima wapange asilimia ngapi ya bajeti nzima kila idara itatumia. Kila mwaka, bajeti ya kila idara inatakiwa ianzie na kiasi cha Dola Ziro (sifuri), kulingana na bajeti iliyokubaliwa kila mwezi. Ongezeko la matumizi bila matarajio lisitegemewe katika idara yoyote ile.

(3) Vipengele zaidi na bajeti ya nyongeza inaweza kuongezwa ikilazimu.

d. *Bajeti inaweza kutazamwa upya na kupitiwa upya ikiwa lazima ili kudumisha gaharama ziendane na kipato.*

3. Msingi wa bajeti. Vifuatavyo ni vipengele ambavyo kanisa linatakiwa kufikiria katika kupanga bajeti yake:

a. Je ni vipaumbele gani vya huduma ya kanisa? (Ona "**Utume na Uwakili wa Kanisa**" katika vidokezo vya somo hapo juu.)

b. Je ni nini kauli mbiu ya kanisa letu?

c. Je maono ya kanisa letu ni nini?

d. Je matumizi ya fedha *yaliyopo* yanaonyesha utume na maono yetu rasmi ya kanisa, au yanatakiwa kubadilishwa?

e. *Je ni mpangilio gani upo wa vipaumbele kwa huduma hizo (kutoka muhimu sana kuja*

*muhimu kidogo)?*

(1) Je ni vipaumbele gani rasmi vyetu wenyewe?

(2) Je utoaji wetu kwa huhuma za Duniani unalingana vipi na matumizi yetu hapa kanisani?

f. Je ni malengo gani mafupi ya kanisa tunayo (miezi 12 ), na ni kiasi gani malengo hayo yatagharimu kwa mwaka (na kwa mwezi)?

g. *Ni yapi malengo ya muda mrefu ya kanisa letu (kwa mwaka mzima)?*

(1) Je malengo hayo yatagharimu kiasi gani?

(2) Je malengo hayo yatagharimu kiasi gani kwa kila miaka mitano ijayo, kwa mwaka?

h. Je ni malengo gani yanaweza kuachwa ikiwa kutakuwa na upungufu, au ni malengo gani mapya yataanzishwa ikiwa kuna ongezeko la fedha?

i. Je ni akiba kiasi gani kanisa linahitaji kuwa nayo kwa tahadhari?

4. <u>Mambo ya kuzingatia kuhusiana na vipaumbele vya bajeti.</u>

a. *Kuna makusudi mawili ya msingi ambayo zaka na matoleo ya kanisa yanapaswa kutumia.*

(1) <u>Kwanza ni kulipia matumizi ya ndani ya kanisa:</u> Watumishi, vifaa, majengo na matumizi kwa idara mbali mbali za kanisa (**1 Wakor 9:7-14**).

(2) <u>Ya pili ni kufadhili kazi ya Kikristo iliyo nje na kanisa:</u> Umisheni wa nchi za nje, umisheni wa ndani, huduma ya rehema, nk. (**1 Wakor 16:1- 4; 2 Wakor 8-9**).

b. *Kanisa likishakubaliana kwa vipaumbele hivyo viwili, swali la muhimu linakuwa: ni kiasi gani cha fedha kitumiwe kwa kuendesha kanisa, na kiasi gani kitolewe nje?* Maandiko hayatupi sheria dhahiri kuhusiana na hili, kwa hiyo makanisa hujiwekea misimamo yao yenyewe. Viongozi wa kanisa lazima wajiwekee mwongozo wao wenyewe kulingana na uongozi wa Bwana na kile kinachofundishwa na Biblia.

c. *Siku zote ni vizuri zaidi kuuliza swali: Je sisi kama kusanyiko la watu, tunajiwekea kingi mno kwa ajili yetu wenyewe?* Wakati wa kujibu swali hili, tunatakiwa tuwe na vitu vitatu kichwani:

(1) Maandiko yanaonyesha kwamba, makusanyiko yaliyo na kipato kikubwa zaidi yanapaswa kufikiria jukumu lao rasmi la kuwasaidia wao ambao wana vichache (**2 Wakor 8:13-15**).

(2) Maandiko hayafundishi mahali popote kwamba fungu la kumi, au zaka ni rasmi kwa ajili ya kanisa la nyumbani; au kwa wazee, na matoleo mengine ndiyo kwa ajili ya huduma za nje.

(3) Utoaji wa fedha kwa ajili ya masikini na wahitaji ni kundi pekee lililo kubwa ambalo limenenwa katika Agano jipya.

d. Makanisa yote yanapaswa kujiandaa kujiuliza: "mbele ya Neno la Mungu, je sisi kama kanisa tunapaswa turekebishe utaratibu wetu wa utoaji?"

5. <u>Mfano wa fomu ya Bajeti—Bajeti ya Kanisa, kwa mwaka:</u>

| *RASILIMALI ZA HUDUMA:* | *MAHITAJI YA HUDUMA:* |
|---|---|
| 1. Mabaki yaliyopo | 1. Viongozi wa Kichungaji |
| 2. Uingizaji katika Mradi (sadaka nafungu la kumi) | 2. Gharama za Kiutendaji |
| 3. Sadaka maalum | a. Wafanya kazi |
| 4. Zawadi | b. Kodi ya pango |
| <u>5. Vipato vingine</u> | c. Ukarabati majengo |
| JUMLA: | d. Bili za maji na umeme |
| | e. Vifaa na ugavi |
| | f. Mahitaji ya ofisi |
| | g. Bima |
| | h. Chakula |
| | i. Usafiri |
| | j. Mengineyo |
| | 3. Elimu ya Huduma na Uanafunzi |
| | 4. Umisheni na Uinjilisti |
| | 5. Mfuko wa ukarimu |
| | 6. Muziki na kuabudu |
| | 7. Matukio maalum |
| | 8. Gharama za kidhehebu |
| | <u>9. Akiba (dharura)</u> |
| | JUMLA: |

**C. *Kanisa linatakiwa kumlipa Mchungaji wao.***

1. Agano Jipya linaonyesha kwamba kanisa linatakiwa kumlipa mchungaji wake au kiongozi afundishaye **1 Wakor 9:7-14**: [7] *Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?* [8] *Je! ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo?* [9] *Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, USIMFUNGE KINYWA NG'OMBE APURAPO NAFAKA. Je! hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe?* [10] *Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini; naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.* [11] *Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini?* [12] *Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi? Lakini hatukuutumia uwezo huo; bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo.* [13] *Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudimiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu?* [14] *Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.* (ona pia **Rum 15:27; Wagal 6:6; 1 Tim 5:17-18**)

2. Agano Jipya halitaji kiasi au njia maalum ambayo kanisa linatakiwa litumie kumlipia mchungaji wake.

a. Wengine hupokea malipo kamili; wengine hupokea asilimia fulani ya zaka au matoleo.

b. *Kipato cha mchungaji kinapaswa kwa nanma fulani kiwe sawa na kipato cha wastani cha washirika hao, yamkini kwa mfano kiasi ambacho mwalimu wa wastani wa shule fulani anapokea.* Kutakuwa na utofauti mkubwa kati ya makanisa mbali mbali, na kati ya wachungaji wa kijijini na wale wa mjini, kwa vile vipato wa washirika wao vitatofautiana sana. Hata hivyo, ikiwa zipo familia10 tu katika kanisa la mahali, na kila familia inatoa fungu la kumi, kanisa hilo lazima liwe na uwezo wa kumtegemeza mchungaji wake.

c. *Huko vijijini ambako kuna, maisha ya kilimo, wachungaji wa jinsi hiyo wasiolipwa fedha moja kwa moja, wanaweza basi wakalipwa kimazao na kwa kupewa wanyama.* Katika maeneo kama hayo kipande cha shamba kinaweza kutolewa kwa mchungaji wa mahali hapo. Katika maeneo ya jinsi hiyo, wachungaji wanaweza kulipwa kwa kupewa huduma (k.m, kujenga nyumba kwa ajili ya mchungaji, kuchimba choo, kulima katika shamba la mchungaji, nk).

d. *Mtume Paulo, kama mwinjilisti na mwanzilishi wa makanisa wakati mwingine alifanya kazi ya "kawaida" (kushona mahema) ili kupata fedha wakati akifanya kazi ya injili* (ona **Mdo 20:33-34; 2 Wakor 11:9-12; 1 The 2:7-9; 2 The 3:7-8**). Paulo pia alipokea vipawa kutoka kwa waamini (**2 Wakor 11:8; Wafil 4:14-18**).

e. *Kwa vile Paulo hakuwa mchungaji wa kanisa la mahali, mazingira yake si lazima yafanane na ya wachungaji wa mahali popote.* Hata hivyo, itokeapo wachungaji wanaanzisha makanisa, au pale ambapo makanisa ni machanga na hayawezi kumsaidia mchungaji kikamilifu, mchungaji anaweza akafanya kazi nje ya huduma yake kujitosheleza mwenyewe kama alivyofanya Paulo. Hata hivyo, kanisa linavyokua, linatakiwa liingie katika kumtegemeza mchungaji wake kipato cha kumwezesha kuishi kulingana na maelekezo ya Biblia yaliyotajwa hapo juu.

f. *Kuna sababu kadhaa kwa nini ni vibaya mchungaji kuendelea kujitegemea mwenyewe kwa kazi za nje baada ya kanisa kuwa limeshaanzishwa.*

(1) Kanisa litakuwa linakosa fursa kushiriki wajibu wa Kibiblia kumtegemeza mchungaji wake. Hilo huleta kupoteza maono ya kanisa na baraka zake.

(2) Kanisa linapoteza matunda yapatikanayo na huduma ya kichungaji ya ukamilifu muda wote. Atakuwa na muda mfupi wa kuwatembelea, kukosa muda wa kipindi cha kati kati ya wiki cha kujifunza Biblia, na huduma nyingine za kati kati ya wiki.

(3) Mchungaji na huduma yake itaathirika. Atakuwa na muda mfupi zaidi na nguvu kidogo kwa huduma, kufanya maombi, kutembelea, na mambo mengine ya huduma.

(4) Kazi ya kawaida ya kidunia, inaweza kuwa tanzi au jaribu linalomshawishi mchungaji aache wito wake kabisa.

(5) Kukosekana msaada wa kumtegemeza mchungaji wake kutakuwa na tabia ya kuambukizika baadaye. Kutakuwa vigumu kwa wachungaji wanaofuata katika uchungaji, kwa sababu washirika huenda wakadai kwamba nao, pia, watalazimika kujisaidia wenyewe. (Hodges 1953: 81)

3. Makanisa (na hasa madhehebu ya dini) yanapaswa yaandae fungu la kustaafu kwa ajili ya

wachungaji. Wachungaji wengi wanaostaafu, au wanaotakiwa kustaafu, huacha huduma wakiwa hawana kitu chochote. Madhehebu mengi, na hata makanisa yenyewe, yanatambua kwa sasa kwamba hali hiyo ni kosa kubwa. Kama matokeo,wanaanzisha fungu la kustaafukwa ajili ya wachungaji. Kiasi kidogo kinachowekwa kila mwezi au kwa mwaka kitaongezeka na kuwa kiasi kikubwa sana baada ya miaka mingi. Hili ni kwa yote mawili: swala la uwakili wa fedha, na na pia ni njia ya kuwaheshimu wazee wale waliotumikia makundi yao vizuri (**1 Tim 5:17-18**).

**D. *Usimamizi wa fedha moja kwa moja unahusiana na utume wa kiroho na kufanikiwa vizuri kwa kanisa.***

1. Wakati kanisa linasimamia vizuri fedha zake, linauonyesha utume wa kanisa na kuwaonyesha waaminio na wasioamini kwamba ni nuru ya ulimwengu.

2. Usimamizi mzuri wa fedha utaondoa kwa kiwango kikubwa lawama ambazo zinaweza kutokea katika kanisa. Lawama hazipaswi kutokea kabisa katika kanisa kwa sababu mambo hayo huiambia dunia kwamba kanisa lina ufisadi na ufujaji, na halina utakatifu. Wakati dunia inaona hayo, huwa haioni sababu kwa nini ije kwa Kristo—hivyo lile kusudi na msingi la lengo la kanisa huwa limeharibika.

3. Usimamizi mzuri wa fedha unapaswa ulete matokeo ya kuongeza utoaji wa kusanyiko la washirika. Makanisa mengi yanahangaika kujaribu kupata fedha nyingi za kuendeshea shughuli zake pia na kupata fedha kwa ajili ya umisheni, na makusudi mengine ya kanisa. Yote mawili, Biblia na utafiti kuhusu utoaji, unapendekeza angalau mambo matatu ambayo makanisayanapaswa yawe yanafanya, ambayo yanaelekea kuleta ongezeko la utoaji.

a. *Kanisa linapaswa lifundishwe vizuri kuhusiana na usimamizi mzuri wa fedha na matokeo yake ya kiroho (ona "**Uwakili wa Fedha na Mali**," hapo juu).* Utoaji ni aina ya tabia ya uadilifu. "Yesu Kristo alizielezea fedha kama aina ya kipima joto cha hali ya moyo: mahali ilipo hazina Yak, ndiko uliko na moyo wako (Math. 6:24). . . . Kukuza matumizi ya fedha kuwa ndiyo kiwango cha uadilifu, ambavyo ndivyo imefafanuliwa kila mahali katika Biblia, kutasaidia washirika wa kanisa watathmini vipaumbele vyaokatika sehemu zote mbili: maisha yao ya faragha, na majukumu ya kiushirika wote.Inawezekana kabisa kwamba, watu wanapoweka imani na Mdo katika uthibitisho juu ya fedha, badiliko hili linaweza kuwa na mabadiliko mazuri kwa maeneo mengine ya maadili katika maisha yao wenyewe, na kijamii kiujumla." (Ronsvalle and Ronsvalle 2005: 121-22)

b. *Kanisa lenyewe linahitaji kufanya bajeti ya fedha zake kama liwezavyo kwenye huo umisheni na miradi ambayo ushirika unaitambua kuwa ni ya muhimu na ya thamani kuu.* "Jinsi ushirika unavyotumia fedha pia kunaweza kutazamwa kama tabia ya kimaadili. Kusanyiko la washirika linaloona kuwa ni rahisi kupunguza bajeti ya umisheni kwa sababu matumizi yamezidi, ni bora zaidi kuliko kuzidi kuwabana watu waongeze utoaji kulipia gharama hizo na kuongeza shughuli za umisheni zaidi , ni maamuzi ya kimaadili." (Ibid.: 121)

(1) Watu huelekea kutoa zaidi ikiwa wanaamini kuwa kile wanachokitolea fedha kina thamani. Utafiti uliofanywa Marekani kuhusu utoaji makanisani uligundua kwamba, washirika wengi sana ambao wangeweza kutoa zaidi ya kile wanachokitoa makanisani; walikuwa hawatoi zaidi kwa sababu "kusanyiko halifanyi kitu chochote muhimu cha kutosha, au kikubwa cha kutosha kukidhi kiwango cha msaada ambacho mshirika angeweza kutoa. Wengi wa watu hao wangeweza kutoa kiasi cha kutosha kama wanapokuwa wamepewa changamoto ambayo wanaiita ni ya muhimu. Tati zo ni kwamba, shughuli za kuendesha kanisa hazipewi agenda za kuwasukuma washirika kutoa kulingana na uwezo." (Ronsvealle and Ronsvalle 2002: 100). Viongozi wa kanisa wanahitaji kuwaelimisha watu wao kuhusu umuhimu na thamani–kuhusu umisheni wa kanisa na kwa watu wenyewe—kuhusu miradi ambayo wanataka watu wao waitolee fedha.

(2) Watu hupendelea kutoa kwenye miradi kuliko "mfuko wa jumla." "Kwa mapendekezo ya madhehebu yao' Kuhusiana na utoaji wa kawaida, utoaji wa miradi ya misheni maalumu hubakia kujulikana kwa kiwango cha ushirika wa kanisa." (Ibid: 105). Uamuzi kwamba watu wanatakiwa kutoa kwa miradi maalum, kutofautisha na "utoaji wa jumla tu—ikiwa miradi hiyo inaonekana na watu kuwa ni ya muhimu na ya thamani—ni kweli kwa aina zote za mashirika ya kujitolea, siyo tu makanisa.

c. *Fedha yoyote itolewayo lazima isimamiwe vizurina ripoti kwa watu lazima itolewe kuhusiana na jinsi fedha hiyo ilivyotumika.* "Watu hupenda kujua fedha yao inafanya nini. Katika kaburi tupu, Utafiti wa Kitaifa wa Uwakili uliofanywa, ulionyesha kwamba; 89% ya wachungaji

waliojibu walikubaliana kwa kauli kuwa, 'Washirika walio wengi wa makanisani wanataka kujua "fedha yao inanunua nini" wanapotoka usharikani.' . . . Makanisa mengi hayatoi taarifa za undani kuhusu miradi kwa washirika wanaochangia huduma za umisheni wao. Wakati mwingine, hata usharika unapotaka taarifa ya kitu fulani, huwa hawawezi kuipata kutoka uongozi wa dini hiyo. Kukosekana huku kwa mawasiliano, ni kinyume kabisa na matakwa ya wafadhili wanaotaka kujua hizo dola zao zinafanya nini. . . . Hata madhehebu yanayotoa mwelekeo wa miradi fulani rasmi, pengine zaidi hata ya kiwango cha kawaida cha mategemezi ya ushirika, hakuna utaratibu wa kueleweka wa kupata ripoti au taarifa zinazohitajika. Je zile fedha zilifika? Nini kinaendelea kule kwenye mradi?" (Ronsvalle and Ronsvalle 2002: 101-02, 105) Hisia za ufujaji wa fedha na matumizi mabaya ya fedha husababisha watu kutokutoa tena, na kupunguza washirika katika kundi kwa sababu imani yao kwa uongozi inapungua. Kutangaza ripoti ya fedha kunafanya kazi ya kichocheo kwa watu kutoa zaidi, kwa vile watu watajua kwamba fedha zao zinakwenda kukutana na mahitaji muhimu na zinatumika vizuri.

4. Uwakili wa kweli wa fedha unamaanisha kwamba makanisa ya Afrika yanapaswa kuwa—na kuyatia nguvu makanisa yawe—yanajitegemea (Hussein 1998: 14-15; Hodges 1953: 67-86; ona pia Obiero 1995).

a. *Kujitegemea ni muhimu zaidi kwa sababu:* (1) Ni Ki-Biblia—makanisa yote yaliyoanzishwa na Paulo yalijisaidia yenyewe yakitegemea msaada kutokea Yerusalemu au wamishinari wa nje; (2) Inaonyesha kufaa—kwani hata familia 10 zinazotoa zaka au fungu la kumi zinaweza kumtegemeza mchungaji, na hata waamini masikini walikuwa na uwezo wa kuwategemeza makuhani wao na waganga wa kienyeji, kununua pombe, nk, kabla hawajakuwa waamini; (3) Vita vya kiroho vya ushirika huhitaji—uelewa wa kuwajibika, ubunifu, na baraka za kiroho; (4) Watumishi wa huduma wa muda wote huwa na ubora zaidi wanapokuwa hawategemei msaada wa kutoka nje—kusanyiko na mchungaji huwa wanakaribiana karibu zaidi, na hakuna yeyote anayeweza akalaumiwa kuwa ni kibaraka au mpelelezi kutoka nchi za Magharibi; na (5) Kijitegemea wenyewe hufungua mlango kwa upanuzi usio na mwisho—kutegemea msaada kutoka nje hufungua mara moja uelewa wa kudumaa na wa kusaidiwa, na hudumaza shauku ya kanisa na uwezo wa kupanuka.

b. *Kufanyika hali ya kujisaidia wenyewe kuna matokeo mawili ya mara moja:* (1) Kanisa litakuwa na msukumo wa uinjilisti na kuwafanya wale wanafunzi (kujizalisha); na (2) Kanisa litaweza kujitawala lenyewe (kujisimamia).

c. *Kuwa katika hali ya kujisaidia au kujitegemea kunahitaji kutolewe mafundisho mazuri kuhusu utoaji, na uwajibikaji wa fedha wakati kanisa linaanzishwa, na mara mtu anapookoka.* Ni rahisi zaidi kuingiza tabia njema kuliko kuvunja tabia mbaya. Watu wanaookoka wanatakiwa kujua nini kinategemewa kutoka kwao kabla hawajakubaliwa kama washirika wa kanisa. Hodges anasema "Wachungaji wetu wa Amerika ya Kati wanawafundisha washirika wapya kwamba wanatakiwa kutoa fungu la kumi au zaka, hata kabla hawajabatizwa kwa maji mengi. Hakuna faida kuwapokea watu waliookoka na kuwa washirika wapya wa kanisa ambao hawana lengo la kutimiza wajibu wa Mkristo wa kawaida." (Hodges 1953: 80) Wajibu huu una mapana zaidi ya wajibu wa kawaida wa ushirika wa kanisa. "Inasemekana kwamba kanisa la Korea linamtaka kila mtu amvune mtu mwingine kwa Kristo kabla mwenyewe hajakubaliwa kubatizwa" (Ibid.: 35). Ikiwa viongozi wa kanisa watafundisha na kuwafanya wanafunzi walio waamini wapya kile ambacho Ukristo na uanachama wa kanisa unahitaji, na kuuingiza kiMdoo, na kuhakikisha kwamba linajitawala lenyewe.

d. *Makanisa na madhehebu ya mahali pamoja huchukua hatua nyingi kufikia kujitegemea yenyewe.* Makanisa yanaweza kujihusisha na shughuli za kuzalisha fedha, ili kwamba yasiwe tegemezi katika vipato vyao kwa misaada ya washirika wao. Makanisa mengi yana viwanja, lakini huwa hayatumii ardhi ile kwa uzalishaji. Makanisa yangeliweza kupanda bustani katika mashamba yao na kisha kuuza mazao yake. Makanisa mengine hupanda miti, ambayo ingeweza kuuzwa kwa makampuni ya umeme, makampuni ya ujenzi, au kuchomwa mkaa. Kwa mfano, mchungaji moja wa Kenya alionyesha kwamba kama miti 200-250 ya Mikaliptusi inaweza kupandwa katika ekari moja ya ardhi. Inapokomaa, inaweza kuuzwa kwa karibu Ksh 10,000 kila moja. Mchungaji wa Uganda alikadiria kwamba viazi mviringo vyaweza kuuzwa kwa karibu bei ya Ush120,000 kila gunia. Kwa hiyo, ekari moja ya ardhi iliyopandwa viazi mviringo yaweza kufikisha thamani ya kati ya Ush milioni 5-10. Rasilimali hizo (na kipato) ni za kujirudia. Dayosisi moja ya Kenya ilianzisha ufugaji wa nguruwe, na Askofu anataka kila

parishi zake imiliki ng'ombe wake. Makanisa yanaweza kutoza sherehe za arusi na kwa makundi yanayotaka kufanyia vikao katika majengo ya kanisa kulipia matumizi ya majengo hayo, umeme, nk. Makanisa mengine yana migahawa ya chakula au nyumba za wageni kuzalisha kipato. Uwezekano wa shughuli za kuzalisha fedha ni kama hauna kikomo, kulingana na ubunifu wa mtu, na rasilimali zilizopo. Hata hivyo, lazima daima ikumbukwe kwamba shughuli za uzalishaji kipato ni *njia ya* kusaidia utume na makusudi ya kanisa hilo. Hazipaswi *kuwa,* au kulemea utume na makusudi ya kimsingi ya kanisa.

## III. Wajibu wa Kanisa kwa Masikini na Wahitaji

**A.** ***Kila mahali katika Biblia, kuwahudumia masikini na wahitaji kumesisitizwa.***

1. Kanisa linatakiwa liwahudumie masikini na wenye uhitaji **(Rum 12:13; 15:25-27; 1 Wakor 16:1-4; 2 Wakor 8-9; Yak 2:14-18; 1 Yoh 3:17-18).**

2. Kanisa pia linatakiwa liwahudumie masikini na wenye uhitaji kwa ujumla **(Kut 23:10-11; Law 19: 9-10; Kum 15:11; 24: 19-21; Zab 41:1; 112:5-6; Mith 14:21; 19:17; 22: 9, 22; 31:20; Isa 58:6-7; Eze 16:49; Math 25:31-46; Marko 10:21; Luka 3:10-11; Rum 12:20; Wagal 2:10; Waef 4:28; Yak 1:27).**

**B.** ***Kifungu kikuu kinachoshughulikia kanisa kuwahudumia masikini na wahitaji ni 1 Tim 5:3-16.***
*3 Uwaheshimu wajane walio wajane kweli kweli. 4 Lakini mjane akiwa ana watoto au wajukuu, na wajifunze*
*kwanza kuyatenda yaliyo wajibu wao kwa jamaa zao wenyewe, na kuwalipa wazazi wao. Kwa kuwa hili*
*lakubalika mbele za Mungu. 5 Basi yeye aliye mjane kweli kweli, ameachwa peke yake, huyo amemwekea Mungu*
*tumaini lake, naye hudumu katika maombi na sala mchana na usiku. 6 Bali, yeye asiyejizuia nafsi yake amekufa*
*ingawa yu hai. 7 Mambo hayo pia uyaagize, ili wasiwe na lawama. 8 Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio*
*wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini. 9 Mjane*
*asiandikwe isipokuwa umri wake amepata miaka sitini; naye amekuwa mke wa mume mmoja; 10 naye*
*ameshuhuduwa kwa Mdo mema; ikiwa amelea watoto, ikiwa amekaribisha wageni, ikiwa amewaosha*
*watakatifu miguu, ikiwa amewasaidia wateswao, ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema. 11 Bali wajane walio*
*vijana ukatae kuwaadika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo,wataka kuolewa; 12 nao wana*
*hukumu kwa kuwa wameiacha imani yao ya kwanza. 13 Tena, pamoja na hayo, hujifunza kuwa wavivu,*
*wakizunguka-zunguka nyumba kwa nyumba; wala si wavivu tu, lakini ni wachongezi na wadadisi, wakinena*
*maneno yasiyowapasa. 14 Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, watawale na*
*madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu. 15 Kwa maana wengine wamekwisha kugeuka na*
*kumfuata Shetani. 16 Mwanamke aaminiye, akiwa ana wajane, na awasaidie mwenyewe, Kanisa lisilemewe; ili*
*liwasaidie wale walio wajane kweli kweli.*

**C.** ***Paulo anajadili kanuni kadhaa za kuamnua yupi kanisa limsaidie.***

1. Kulingana na hoja iliyopo katika kifungu hiki "heshima au kuwajali" wajane kwazungumzia *msaada wa vitu* kwa wajane (ona **1 Tim 5:4, 8, 17-18**).

2. Wajane walikuwa katika hali ya hatari zaidi na watu waliohitaji kusaidiwa katika jamii ya kale kwa sababu kwa kawaida walikuwa wanawategemea kabisa waume zao.

3. Kifungu hiki ni *mfano* wa msaada kwa kundi moja maalum la watu wahitaji. Paulo anatoa maelekezo ya undani zaidi ya kanuni ya ujumla iliyotajwa katika **Yak 1:27,** *"Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa."* Ukweli kwamba nukuu ya Paulo katika **5:3-16** kwa "wajane" ni *mfano* wa aina za watu wenye uhitaji ambao kanisa linapaswa kuwasaidia waonekana katika **5:4** ambao huzungumzia "wazazi," na katika **5:8** ambao huzungumzia mtu awahudumiaye "walio wake mwenyewe." Huduma zote mbili huendeleza kanuni ya kuwasaidia wenye uhitaji zaidi ya "wajane." Kanuni ambazo Paulo anazijadili zinaweza kufuatwa na kutumiwa kwa makundi mengine ya watu wenye uhitaji, kama vile wazee wa kiume na wa kike; wasio na kazi; yatima; punguani, nk.

4. Kifungu kina vipengele vitano vya muundo unaosimamia tofauti ambazo kanisa linaweza kuwasaidia; na wale ambao kanisa halipaswi kuwasaidia, ni kama ifuatavyo:

   a. *Waheshimu wajane walio wajane kweli kweli (**5:3**)*—lakini mjane akiwa ana watoto au wajukuu, na wajifunze kwanza kuyatenda yaliyo wajibu wao kwa jamaa zao wenyewe (**5:4**).

   b. *Basi yeye aliye mjane kweli kweli, ameachwa peke yake, huyo amemwekea Mungu tumaini lake, naye hudumu katika maombi na sala mchana na usiku.(**5:5**)*—bali yeye asiyejizuia nafsi

yake amekufa ingawa yu hai (**5:6**).

c. *Mambo hayo pia uyaagize, ili wasiwe na lawama (5:7)*—lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini (**5:8**).

d. *Na wale wajane walio wachaji wa kweli wa Mungu walio na umri uzidio miaka 60 ndio waorodheshwe (**5:9-10**)*—bali wajane walio vijana ukatae kuwaadika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo,wataka kuolewa (**5:11-13**).

e. *Ufupisho:* Wajane walio vijana ukatae kuwaadika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo,wataka kuolewa tena; wajane wanaweza kuolewa (**5:14-15**); wale wenye watoto na wapokee msaada kutoka kwao (**5:16a**)—lakini kanisa liwahudumie wale ambao ni wajane "kweli" (**5:16b**).

5. <u>Kifungu kinashughulikia makundi matatu ya watu, waliowekewa alama ili kuhudumiwa waitwao "wajane wa kweli" kama ifuatavyo.</u>

**5:3**—Wahudumieni "wajane wa kweli"

**5:4, 7-8, 16a**—majukumu ya familia

**5:5, 9-10**—"wajane wa kweli"

**5:6, 11-15**—Wajane vijana na wawezao kuolewa tena

**5:16b**—Kanisa litawategemeza "wajane wa kweli"

6. <u>Kutokana na kifungu hiki, kanuni mbili zinajitokeza:</u>

a. *Fikiria mahitaji ya mtu.* Je mtu anayetaka msaada "kweli ni wa kusaidiwa," au je mtu huyu ana familia na wanandugu au watu wa kumsaidia (Je kuna misaada kiserikali, bima, pensheni, urithi, au vyanzo vingine vya misaada vinaweza kutolewa kwao)?

b. *Fikiria tabia ya mtu, mwenendo, au mkondo wake wa maisha.*

(1) <u>Je mtu huyo ni mnyenyekevu au ana kiburi?</u> Je mtu huyo ana mpango wa kuishi maisha ya dhambi au ana mpango mwingine? Je mtu huyo anamtumaini Mungu au hapana?

(2) <u>Watu wengi wanaokuja kanisani wakitaka msaada si lazima wawe Wakristo, na wanaweza kuwa na maisha ya dhambi tu.</u> Ikiwa watu kama hao wanakuja kanisani na moyo wa unyenyekevu, kanisa linaweza kuwasaidia. Kwa kuwasaidia, mlango unafunguliwa wa kuwaambia kuhusu Yesu Kristo.

**D.** ***Mambo mengine ya kutafakari kuhusu 1 Tim 5:3-16 na kuwasaidia masikini na wahitaji***

1. <u>Huo "umri wa miaka 60" siyo sharti lililo "sheria" ya kufuatwa dunia nzima.</u> Makanisa mengi huifuata hii jinsi ilivyo tu, kama agizo la wazi kwa makanisa yote:

a. *Uelewa wa kihistoria na hoja ya desturi ihusikayo hapo inatupatia picha nzuri zaidi.* Miaka Sitini ndiyo miaka iliyotambuliwa rasmi nyakati za zamani kwamba ndiyo "uzee" (Knight 1992: 223). Sitini "huenda inaonyesha picha ya umri wa juu zaidi wa zamani ya kale ambapo kimsingi alikuwa anategemewa kufanya kazi na kujitegemea" (Blomberg 1999: 209). Katika karne ya kwanza, ni chini ya 4% ya wanawake waliishi kufika miaka 50 (Lysaught 2005: 67n.18). Walikuwa kati ya watu waliokuwa hawatambuliwi kabisa, na walikuwa na rasilimali chache za kuzitegemea.

b. *Kinyume chake leo, kwa mfano katika nchi za Magharibi, umri wa miaka 60 haujulikani hasa kama ni "mzee" na ziko serikali nyingi na rasilimali mbalimbali zinazowashughulikia watu wazee.* Matokeo yake, hiyo sheria ya "umri wa miaka Sitini" ilihusu mambo mengine tofauti yaliyotajwa na Paulo zaidi ya yanavyotazamika katika desturi zetu leo.

c. *Zaidi ya hayo, hoja pana ya kimaandiko ya Biblia haiashirii kuwa hiyo namba ya Sitini, au umri wa miaka Sitini, ina umuhimu wowote* (lakini k.m **Wal 27:1-7** wakati kulikuwa na kigezo cha kutumika wakati wa kuwakomboa watu waliofanya viapo vigumu; gharama ilikwenda chini kwa watu wa umri wa miaka 60). Fikira hizi huashiria kwamba kigezo cha miaka 60 hakipaswi kuchukuliwa na dunia nzima kama "sheria," lakini kinaweza kubadilika kulingana na mazingira yaliyopo.

2. <u>Inawezekana kwamba "orodha hiyo" iliyotajwa katika **1 Tim 5:9** iliwaelekea wajane walioorodheshwa katika huduma rasmi katika mabadilishano nao katika kuhudumiwa na kanisa.</u>

a. *Wengi hutoa maoni kwamba "orodha" ambayo wajane waliorodheshwa (**1 Tim 5:9**) ilitajwa kama "utaratibu, au idara ya wajane" ambamo wajane waliokuwa wamejiandikisha walipewa majukumu ya kikanisa ya maombi na huduma za kujitolea kwa wengine, kama kurudisha*

*fadhila kwa misaada ya vitu wasaidiwavyo na kanisa.* Hii iko hivyo kwa sababu matakwa yaliyotajwa katika **5:9-10** hayafanani na yale ya **5:5**, na sifa zilizotajwa katika **5:9 -10** zinafanana na zizizotajwa katika huduma ya kawaida ya kanisa (ona **1 Tim 3:1-13**). Kusema ukweli, kanisa katika karne zilizofuata, lilianzisha utaratibu wa aina hiyo wa wajane kulingana na ukurasa huu. "Utaratibu wa wajane ulidumu sana katika karne ya nne. Lakini uliozoeleka zaidi kwa Wakristo wa sehemu mbali mbali za Uyunani na Latini ni huduma ya mashemasi, kama sehemu iliyojitokeza ya 5:3-10. Viongozi wa kike walidhaniwa kuwa ni bora zaidi kwa huduma ya maombi na kuhudumia maswala kanisani, hasa kwa yale ambayo yasingeliwafaa wanaume kuhusiana nayo—hasa kutoa ushauri, kutembelea watu, kuhudumia au kubatiza wanawake." (Blomberg 1999: 209)

b. *Ingawaje hili halitajwi hapo kama agizo zito la kutafsiriwa, kwa vile kanisa kihistoria limewatumia wajane katika huduma wapewe msaada wa vitu, kanisa leo linapaswa kufikiria kufanya kitu cha jinsi hiyo hiyo.* Watu wazee zaidi wana hazina ya ujuzi na hekima ambayo inayoweza kufaa kuadibisha na kuujenga mwili wa Kristo uliobakia.

3. Kanisa linatakiwa kujaribu kuwasaidia masikini na wahitaji ili waweze kujitegemea.

a. *Watu wengi walio wahitaji wangependa wajitegemee wenyewe kuliko kuwa wanasaidiwa tu.* Kanisa linaweza kuwafanya wajisaidie na kujitegemea. Baadhi ya mapendekezo ni pamoja na:

(1) Kutoa mikopo midogo midogo kwa wahitaji. Hii itahitaji kwamba hawa walengwa wawe na miradi maalum iliyokubalika. Patahitajika pia ufuatiliaji na hatua za uwajibikaji. Tatizo moja muhimu huwa ni pale mikopo inapokuwa hairudishwi.

(2) Kuwapatia ajira rasmi walio wahitaji. Hii itahitaji kujua nani katika washirika ana biahsra au shughuli fulani, anahitaji msaada, au anaweza kutoa ajira au kazi kwa watu. Kanisa lenyewe linaweza kuwalipa watu kwa usafi wa jengo na usafi wa viwanja, au kufanya kazi nyingine kwa ajili ya kanisa. Zana ya "utaratibu wa wajane" ni wazo jingine.

(3) Kutoa misaada ambayo siyo ya ki-fedha. Kanisa lingeweza kuwa "ghala" kama vile lilivyokuwa hekalu la zamani (ona **Mal 3:10**), kwa ajili ya mavazi, vyakula visivyoharibika, au vitu vingine vinavyohitajika. Pia, kanisa linatakiwa kujua ni watu gani katika kusanyiko wanaweza kutoa chakula,mavazi, au vitu vingine kwa watu wahitaji. Kanisa moja la PAG hukoUganda lilikuwa na wajane 43. Badala ya kuwapa fedha, liliwanunulia mbuzi. Baada ya miaka miwili, wale mbuzi 43 wakaongezeka kufikia mbuzi 281. wajane hao wakawa na uwezo wa kujitegemea wenyewe: wakawa na maziwa; waliweza kuwauza kondoo hao kupata fedha; na baadhi ya wajane hao wakanunua ng'ombe kama matokeo ya kufanya biashara hiyo, au kuuza mbuzi. Na matokeo yake, wajane hao wakawa karibu zaidi na kanisa na wengi wao wamekuwa waaminifu, "mashujaa wa maombi," na wanatoa tena kwa kanisa.

b. *Kanisa linatakiwa kujua vyanzo vingine vya misaada katika eneo lake.* Kanisa la mahali pamoja lina uwezo wa kutoa vitu vyote kwa watu wote. Hata hivyo, linaweza kushirikiana na, au kuwasiliana na, mashirika yale mengine ambayo yanaweza kutoa vitu na huduma ambayo kanisa lenyewe haliwezi kutoa.

(1) Vyanzo vingine vya misaada ya vitu ni pamoja na: Taasisi za serikali; Mashirika ya Kujitolea, Mashirika ya Ki-Kristo na yale mengine ya kujitolea.

(2) Madhehebu mengine yana taasisi za Misaada na Huduma za jamii. Kanisa la Anglikan lina "Umoja wa Wakina mama." Kanisa la PAG Uganda lina "Sekretarieti ya PAG ya Mipango na Maendeleo." Makanisa tofauti, na makanisa ya madhehebu tofauti yanatakiwa kufanya kazi pamoja ili kukutana na mahitaji ya watu hawa. Kufanya hivyo pia kutaonyesha umoja, ambao ndio utume wa msingi na kusudi la kanisa.

c. *Makanisa tofauti, na makanisa ya dini tofauti, yanapaswa kufanya kazi pamoja na kuwasaidia masikini na wahitaji.*

(1) Makanisa mengi yenyewe ni masikini. Hata hivyo, wakati makanisa tofauti yanafanya kazi pamoja na kukusanya nguvu zao pamoja na rasilimali zao pamoja, kiwango kikubwa na kizuri zaidi kinaweza kutimizwa ambacho hakuna kanisa lolote binafsi lingeweza kufanya au kuwa nacho. Kufanya kazi pamoja pia kunazuia kurudia mambo na kupoteza gharama zisizo na sababu.

(2) Uhitaji wa makanisa kufanya kazi pamoja ni muhimu katika namna nyingi. Kwa mfano, wakati watu wanabadilika kutoka Uislamu, wanaweza kukataliwa, wanaweza

kutishiwa au kufukuzwa na familia zao. Makanisa yanapaswa yawe na uwezo wa kuwapatia chakula, mavazi, mahali pa kujihifadhi, fedha, elimu, na ajira kuwasaidia hao walioamua kubadilika. Ikiwa tutafanya hivyo, tunaonyesha upendo na uwezo wa Kristo; ikiwa hatufanyi hivyo, tunaonyesha kwamba, tofauti na Waislamu wanaotoa vitu hivi kwa wale waliosilimu, imani yetu inakuwa imekufa (**Yak 2:14-26**).

**E.** ***Matokeo yanayoweza kuja wakati kanisa linatimiza wajibu wake kuwahudumia masikini na wahitaji***

1. Wakati kanisa linatimiza wajibu wake kuwahudumia masikini na wenye mahitaji kwa ujumla:
    a. Mungu hufurahi, kwa sababu kuwahudumia masikini na wahitaji ni sehemu ya dini iliyo safi, ni aina ya huduma inayofanana na dhabihu ya Agano la Kale na kanisa litakuwa linaonyesha imani yake katika Yesu Kristo **(2 Wakor 9:1, 12-13; Wafil 4:18; Waeb 13:16; Yak 1:27; 2:14-18; 1 Yoh 3:17-18).**
    b. Mungu atatuhudumia kwa mahitaji ya vitu ikiwa tutamuweka yeye mbele, na kuwa waaminifu **(Zab 41:1-3; Mith 3:9-10; 11:24-25; 28:27; Mal 3:8-12; Math 6:33; Marko 10:28-31; Luka 6:38; Wagal 6:6-7; 2 Wakor 9:6-11;** ona pia **Mith 22:16, 22-23).**
2. Tunapowahudumia waamini wenzetu walio masikini na wenye shida:
    a. Hatutaiona ile aibu inayotokana na *kushindwa* kutimiza wajibu wetu (**2 Wakor 9:1-4**);
    b. Shukurani, sifa, na utukufu kwa Mungu hujitokeza (**2 Wakor 9:11-15**).
    c. Mungu hutoa neema na furaha maalum kwa mtoaji (**2 Wakor 8:1-2; 9:8**).
    d. *Kuwahudumia ndugu waamini masikini na wenye mahitaji hulijenga kanisa zima, kwa sababu, tendo hilo:*
        (1) Huwategemeza watakatifu kimwili na kiroho (**2 Wakor 9:12**);
        (2) Huwawezesha watakatifu kusaidiana wenyewe; huleta usawa kati ya waamini ambao mwanzoni walikuwa masikini na sasa wana rasilimali kuwasaidia waamini wengine ambao baadaye wangeangukia katika kundi la masikini na wahitaji (**2 Wakor 8:13-15**);
        (3) Huliunganisha kanisa pamoja (**2 Wakor 9:14**);
        (4) Huwavuvia watakatifu kusaidiana (**2 Wakor 9:2**).

## NUKUU ZILIZOTOLEWA


Adeleye, Femi. *Preachers of a Different Gospel.* Kampala, Uganda: International Fellowship of Evangelical Students.

Adeyemo, Tokunboh, ed. 2006. *Africa Bible Commentary.* Nairobi, Kenya: WordAlive.

Aristides. c.124. *Apology.* Online: http://www.earlychristianwritings.com/text/aristides-kay.html.

Arthur, Kay. 1994. *How to Study Your Bible.* Eugene, OR: Harvest House.

Belleville, Linda. 1986. "'Under Law': Structural Analysis and the Pauline Concept of Law in Galatians 3:21-4:11." *Journal for the Study of the New Testament* 26: 53-78.

Betz, Hans Dieter. 1985. *2 Corinthians 8 and 9* (Hermeneia). Philadelphia: Fortress.

Blanchard, Kenneth, and Spencer Johnson. 1982. *The One Minute Manager.* New York: William Morrow.

Blomberg, Craig. 1990. *Interpreting the Parables.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

_______. 1999. *Neither Poverty nor Riches* (NSBT 7). Nottingham, England: Apollos.

Bruenning, David. n.d. *International Pastors and Christian Leaders Seminar.* Neenah, WI: International Christian Assistance; International Children's Fund.

_______. n.d. *Successful Christian Living.* Neenah, WI: International Christian Assistance; International Children's Fund, Inc.

Capps, Charles. 2008. "God's System for Your Success." Online: http://charlescapps.com/cc_1st_qutr_05.html.

Carson, D. A. 1991. *The Gospel According to John* (Pillar). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Chapman, Gary. 1992. *The Five Love Languages.* Chicago: Northfield.

_______. 2009. *The Five Love Languages Singles Edition.* Chicago: Northfield.

_______. 2010. *The Five Love Languages of Teenagers.* Chicago: Northfield.

Chapman, Gary, and Ross Campbell. 1997. *The Five Love Languages of Children.* Chicago: Northfield.

Chapman, Gary, and Paul White. 2011. *The Five Love Languages of Appreciation in the Workplace.* Chicago: Northfield.

Covey, Stephen. 1989. *The 7 Habits of Highly Effective People.* New York: Fireside.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature.* Chicago: The University of Chicago Press.

*Didache.* c.90. Online: http://www.ccel.org/ccel/richardson/fathers.viii.i.iii.html.

Dollar, Creflo. 2008. "Your Inheritance of Wealth and Riches" (July 2008). Accessed 28 July 2008 at: http://www.creflodollarministries.org/Public/Bible/Article.aspx?id=303.

Doriani, Daniel. 1996. *Getting the Message.* Philllipsburg, NJ: P&R.

_______. 2001. *Putting the Truth to Work.* Philllipsburg, NJ: P&R.

Editorial. 2001. "The Prosperity Gospel: An *AJET* Editorial." *Africa Journal of Evangelical Theology* 20: 1-2.

Fee, Gordon. 1984. "The 'Gospel' of Prosperity—an Alien Gospel." *Reformation Today* 82: 39-43.

France, R. T. 1992. "Faith." In *Dictionary of Jesus and the Gospels,* ed. Joel Green, Scot McKnight, and I. Howard Marshall, 223-26. Downers Grove, IL: InterVarsity.

Global Handwashing Day. 2008. "Background." Accessed 28 October 2008 at: http://www.globalhandwashingday.org/Background.asp.

Hodges, Melvin. 1953. *The Indigenous Church.* Springfield, MO: Gospel.

Hoekema, Anthony. 1986. *Created in God's Image.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Hummel, Charles. 1967. *Tyranny of the Urgent.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Hurowitz, Victor. 2002. "*akl* in Malachi 3:11—Caterpillar." *Journal of Biblical Literature* 121: 327-336.

Hussein, Bedru. 1998. *Stewardship in the Self-Supporting Church.* Mwanza, Tanzania: Inland.

Irenaeus. c.175-180. *Against Heresies.* Online: http://www.ccel.org/ccel/schaff/anf01.ix.vi.xiv.html.

Jamieson, Robert, A. R. Fausset, and David Brown. 1961. *Commentary on the Whole Bible.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Johnson, Dennis. 2007. *Him We Proclaim.* Phillipsburg, NJ: P&R.

Julian the Apostate. c.360-363. *Letter to Arsacius.* Online: http://www.thenagain.info/Classes/Sources/Julian.html.

Justin Martyr. c.150-155. *First Apology.* Online: http://www.ccel.org/ccel/richardson/fathers.x.ii.iii.html.

Kenneth Copeland Ministries. 2008. "Finances: Foundational Teachings." Accessed 28 July 2008 at: http://www.kcm.org/real/index.php?p=finances_teachings_01.

Knight III, George. 1992. *The Pastoral Epistles* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Koukl, Gregory. 2001. *Never Read a Bible Verse.* Online: http://www.str.org/site/News2?page=NewsArticle&id=5466.

Lakein, Alan. 1989. *How to Get Control of Your Time and Your Life.* New York: Signet.

Lehrer, Steve. 2006. *New Covenant Theology: Questions Answered.* Steve Lehrer.

Lewis, C. S. 1980. *The Weight of Glory.* New York: Macmillan.

Lucian of Samosata. c.165. *Death of Peregrinus.* Online: http://www.tertullian.org/rpearse/lucian/peregrinus.htm.

Lysaught, M. Therese. 2005. "Practicing the Order of Widows: A New Call for an Old Vocation." *Christian Bioethics* 11: 51-68.

MacDonald, William. 1975. *True Discipleship.* Kansas City, KS: Walterick.

Mathetes. c.130-200. *Epistle to Diognetus.* Online: http://www.earlychristianwritings.com/text/diognetus-roberts.html.

Ngundu, Onesimus. 2006. "Revelation." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1543-79. Nairobi: WordAlive.

Obiero, Daniel Oguso. 1995. *Christian Giving.* Nairobi: O.A.I.C./T.E.E.

"Pallisa District sets penalties to fight cholera spread." 2008, June 26. *Daily Monitor.* 12.

Peck, John, and Charles Strohmer. 2000. *Uncommon Sense.* Sevierville, TN: The Wise Press.

Piper, John. 2003. *Let the Nations Be Glad!,* 2nd ed. Grand Rapids, MI: Baker Academic.

_______. 2007. "Prosperity Preaching: Deceitful and Deadly." Online: http://www.desiringgod.org/ResourceLibrary/TasteAndSee/ByDate/2007/1993_Prosperity_Preaching_Deceitful_and_Deadly/.

_______. 2009. *Finally Alive.* Geanies House, Fearn, Ross-shire, Scotland: Christian Focus.

Rayburn, Robert. 1989. "Hebrews." In *Evangelical Commentary on the Bible,* ed. Walter Elwell, 1124-49. Grand Rapids, MI: Baker.

Ronsvalle, John, and Sylvia Ronsvalle. 2002. *The State of Church Giving Through 2000,* 12th ed. Champaign, IL: empty tomb, inc. Online: http://www.emptytomb.org/scg002Sol.pdf.

_______. 2005. *The State of Church Giving Through 2003,* 15th ed. Champaign, IL: empty tomb, inc. Online: http://www.emptytomb.org/SCG03Priorities.pdf.

Sarles, Ken. 1986. "A Theological Evaluation of the Prosperity Gospel." *Bibliotheca Sacra* 143: 329-52.

Schaeffer, Francis. 1982. *The Complete Works of Francis A. Schaeffer.* 5 vols. Westchester, IL: Crossway.

Schowalter, Daniel. 1993. "Faith." In *The Oxford Companion to the Bible,* ed. Bruce Metzger and Michael Coogan, 222-23. New York: Oxford University Press.

Tertullian. c.197-200. *Apology.* Online: http://www.earlychristianwritings.com/text/tertullian01.html.

Theroux, Paul. 2003. *Dark Star Safari.* Boston: Houghton Mifflin.

Travis, Stephen. 1982. *I Believe in the Second Coming of Jesus.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Trench, Richard. 1989 (reprint). *SYohonyms of the New Testament.* Grand Rapids, MI: Baker. Online: http://faculty.gordon.edu/hu/bi/Ted_Hildebrandt/New_Testament_Greek/Text/Trench-SYohonyms.pdf.

Willard, Dallas. 1997. *The Divine Conspiracy.* New York: HarperSanFrancisco.

Wolvaardt, Bennie. 2005. *How to Interpret the Bible: A Do-It-Yourself Manual.* London: Veritas College.

Zodhiates, Spiros. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament,* rev. ed. Chattanooga, TN: AMG.

**KUHUSU MWANDISHI**



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada ya kwanza elimu ya siasa (B.A. in political science) kutoka Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, ambapo alitunukiwa shahada ya heshima kutokana na kufaulu kwa viwango vya juu, mnamo mwaka wa 1974, akajumuika na Phi Beta Kappa ambayo ni taasisi ya heshima katika kijamii. Baadae akapata J.D. ambayo ni shahada ya juu ya sheria kutoka Shule ya sheria, Cornell magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akajumuishwa kwenye "Order of the Coif legal honor society" ambayo ni taasisi inayoheshimika katika jamii inayofanya kazi za kisheria. Akaitumia miaka 28 iliyofuata akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye kama mmiliki mwenza wa Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Akawa muamini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake katika Thiolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu (Master of Divinity) katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya mwaka 2007 – 2013 alikuwa mkurugenzi wa Afrika Masahariki wa huduma ya "Equipping Pastors International (EPI)" Na sasa Jonathan ni mkurugenzi wa huduma ya kuwawezesha viongozi wa kanisa Afrika Mashariki "Equipping Church Leaders East Africa. (ECLEA)": **www.eclea.net.** Kwa ujumla, kazi zake za mafundisho aliyoandika ya masomo ya Bibilia, yanapatikana kwenye: **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na anuani hii: **jonathanmenn@yahoo.com**.